**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

# MAPITIO YA HALI YA UCHUMI 2024 NA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO

**2024/2025**

**KITABU CHA KWANZA**

**TUME YA MIPANGO ZANZIBAR**

**JUNE, 2025**

## YALIYOMO

**ORODHA YA VIFUPISHO................................................................. xii**
**UTANGULIZI ................................................................................ 1**
**SURA YA KWANZA.......................................................................... 3**
**1.0 HALI YA UCHUMI ...................................................................... 3**
1.1 Uchumi wa Dunia ................................................................................ 3
1.2 Uchumi wa Nchi Zilizoendelea ........................................................... 4
1.3 Uchumi wa Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi ................ 4
1.4 Hali ya Uchumi wa Bara la Afrika........................................................ 6
1.4.1 Uchumi wa Afrika ........................................................................ 6
1.4.2 Uchumi wa Nchi za Visiwa Vilivyo Barani Afrika .......................... 8
1.4.4 Uchumi wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki........................ 12
1.4.5 Nchi zenye Uhusiano wa Kibiashara na Zanzibar (Zanzibar Trading Partners)............................................................................ 14
1.5 Hali ya Mfumko wa Bei.................................................................... 15
1.5.1 Mfumko wa Bei wa Dunia ........................................................... 15
1.5.2 Mfumko wa Bei kwa Nchi Zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara.. 16
1.5.3 Mfumko wa bei wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki............ 16
1.5.4 Mfumko wa bei kwa Nchi zenye Uhusiano wa Kibiashara na Zanzibar (Zanzibar Trading Partners) ........................................... 19
1.5.5 Mwenendo wa Bei kwa baadhi ya bidhaa katika Soko la Dunia ... 21
**SURA YA PILI.................................................................................. 23**
**2.0 HALI YA UCHUMI WA ZANZIBAR............................................... 23**
2.1 Pato la Taifa na Ukuaji wa Uchumi .................................................... 23
2.2 Pato la Mwananchi............................................................................ 24
2.3 Mwenendo wa Mfumko wa Bei Zanzibar .......................................... 25
2.4 Mwenendo wa Thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Sarafu nyengine duniani................................................................................ 27
a. Dola ya Kimarekani. ........................................................................ 27
2. 5 Mwenendo wa Uingiaji wa Watalii Zanzibar...................................... 28
2.6 Ukuaji wa Sekta katika Pato la Taifa ................................................. 29
2.6.1 Sekta ya Huduma ....................................................................... 29
2.6.2 Sekta ya Viwanda....................................................................... 31
2.6.3 Sekta ya Kilimo........................................................................... 32

2.7 Mchango wa Sekta katika Pato la Taifa ................................................ 33
2.7.1 Sekta ya Huduma.......................................................................... 33
2.7.2 Sekta ya Viwanda ........................................................................ 34
2.7.3 Sekta ya Kilimo ........................................................................... 34
2.8 Ukuzaji Rasilimali ............................................................................ 42
2.8.1 Nafasi za Ajira Kutoka Miradi ya Sekta Binafsi Iliyosajiliwa na Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) ......................... 43
2.8.2 Mgawanyo wa Miradi ya Wazawa na Wageni Iliyosajiliwa na ZIPA.......................................................................................... 44
2.8.3 Mgawanyo wa Miradi Iliyosajiliwa na ZIPA Kulingana na Mabara ....45
2.9 Hali ya Upatikanaji wa Ajira.............................................................. 46
**SURA YA TATU ................................................................................ 47**
**3.0 SEKTA YA NJE ............................................................................. 47**
3.1 Usafirishaji wa Bidhaa Nje ya Nchi.................................................... 47
3.1.1 Usafirishaji wa Mazao Makuu ya Biashara (Karafuu na Mwani)...... 47
3.2 Uagiziaji wa Bidhaa Kutoka Nje ya Nchi............................................ 49
3.3 Urari wa Biashara ............................................................................ 50
3.4 Uhaulishaji wa Bidhaa baina ya Zanzibar na Tanzania Bara................ 51
**SURA YA NNE .................................................................................. 52**
**5.0 SEKTA YA FEDHA......................................................................... 52**
5.1 Sekta Ndogo ya Benki ...................................................................... 52
5.1.1 Benki Kuu ya Tanzania (BoT)......................................................... 52
5.1.2 Huduma za Kibenki......................................................................... 54
5.1.3 Amana............................................................................................ 54
5.1.4 Mikopo ........................................................................................... 55
5.1.5 Mwenendo wa Riba za Benki......................................................... 56
5.1.6 Wakala wa Huduma za Kibenki ..................................................... 57
5.1.7 Mwenendo wa Viwango vya Ubadilishaji wa Fedha za Kigeni (Exchange Rate Movement)......................................................... 57
5.2 Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) ..................................................... 58
5.2.1 Utekelezaji wa Bajeti Julai 2024 hadi Machi 2025. ....................... 58
5.2.3 Malengo ya PBZ kwa Mwaka 2025................................................ 59
5.2.2 Miradi ya PBZ kwa Mwaka 2025. .................................................. 60
5.2.3 Changamoto na Utatuzi.................................................................. 61
5.3 Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) .......................... 61
5.3.1 Usajili wa Watoa Huduma za Bima................................................ 61

5.3.2 Mfumo wa Kusimamia na Kudhibiti Soko .................................... 62
5.3.3 Msuluhishi wa migogoro ya bima (Ombudsman) ........................ 63
5.3.4 Hali ya soko la huduma za Bima Zanzibar. ................................ 63
5.3.5 Mafanikio ....................................................................................... 63
5.3.6 Matarajio ....................................................................................... 65
5.4 Shirika la Bima la Zanzibar ................................................................ 70
5.4.1 Majukumu Makuu ya Shirika la Bima Zanzibar .......................... 70
5.4.2 Ofisi za Shirika ............................................................................... 71
5.4.3 Utekelezaji Halisi wa Kazi za Shirika kwa Kipindi cha Julai / Machi 2025 ....................................................................................... 71
5.4.4 Mafanikio yaliyopatikana kwa Shirika katika Sekta ya Fedha .... 71
**5.5 MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR (ZSSF)............ 73**
5.6 Idara ya Maendeleo ya Ushirika .......................................................... 81
5.6.1 Maendeleo ya Ushirika Zanzibar..................................................... 81
5.6.2 Mafanikio ......................................................................................... 85
5.6.3 Changamoto Zinazozikabili SACCOS za Zanzibar ....................... 86
5.6.4 Matarajio na Muelekeo kwa Sekta ya Fedha Machi 2025.............. 87
5.6.5 Mpango wa Utekelezaji kwa mwaka wa Fedha 2025/2026 .......... .88
**SURA YA TANO.................................................................................. 89**
**5.0 SEKTA YA MIUNDOMBINU.......................................................... 89**
5.1 Wakala wa Barabara............................................................................ 89
5.1.1 Mchanganuo wa Matumizi ya Fedha Kwa Ujenzi Wa Barabara Kwa Mwaka Wa Fedha (Julai 2024-Machi 2025). ....................... 91
5.3 Nishati ya Umeme................................................................................ 94
5.4 Mamlaka ya Maji Zanzibar.................................................................. 95
5.4.1 Usimamizi na Uendelezaji Rasilimali Maji na Utatuzi wa Changamoto za Maji. ........................................................................... 96
5.4.2 Huduma ya Maji Vijijini ................................................................ 96
**SURA YA SITA ................................................................................. 100**
**6.0 SEKTA YA ELIMU ......................................................................... 100**
6.1 Elimu na Mafunzo ya Amali ........................................................... 100
6.1.1 Idadi ya Wanafunzi: Maandalizi, Msingi, Kati na Sekondari kwa Skuli za Serikali .............................................................................. 101
6.1.2 Idadi ya Wanafunzi: Maandalizi, Msingi, Kati na Sekondari kwa Skuli za Binafsi ............................................................................... 103

6.1.3 Idadi ya Wanafunzi wa Skuli za Sekondari kwa Jinsia kwa Skuli za Serikali na Binafsi. ........................................................ 104
6.2 Idadi ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ............................................ 106
6.2.1 Idadi ya Mikopo iliyotolewa ........................................................ 106
6.2.2 Mwenendo wa Utoaji wa Mikopo na Utaratibu wa Kurejesha Mikopo ........................................................................................ 107
6.2.3 Ukusanyaji wa marejesho ya mikopo .......................................... 107
6.2.4 Urejeshaji wa Mikopo ya Elimu ya Juu ...................................... 108
6.2.5 Mapendekezo ya Kutatua Changamoto za Urejeshaji Mkopo wa Elimu ya Juu; .............................................................................. 109
6.2.6 Mikakati ya Bodi Juu ya Urejeshajiwa Mikopo kwa Wanufaika. 109
**SURA YA SABA ............................................................................111**
**7.0 SEKTA YA AFYA .....................................................................111**
7.1 Wataalamu wa afya .........................................................................111
7.1.2 Idadi ya Vituo vya Afya na Wagonjwa .........................................112
7.2 Huduma kwa Kinamama Wajawazito na Vizazi Hai ...........................113
7.2.1 Wilaya na Idadi ya Vizazi hai ......................................................113
7.2.2 Idadi ya Kinamama Wajawazito Waliojifungua Kwa Njia ya Upasuaji, Kawaida na Mimba Zilizoharibika. .............................114
7.2.3 Lishe ya Mama na Mtoto ............................................................115
7.4 Mpango wa Damu Salama ..............................................................116
7.5 Vifaa Tiba na Magonjwa Kumi Yaliyoripotiwa Mara kwa Mara 2023/2024 .......................................................................................116
7.6 Huduma za Upasuaji Mkubwa ..........................................................117
7.7 Idadi ya Vifo kwa Wagonjwa ............................................................117
7.8 Mpango wa Kumaliza Malaria Nchini. ..............................................117
7.8.1 Dawa Zinazotumika Kutibu Malaria Nchini .................................118
7.8.2 Madaraja ya Dawa za Kutibia Malaria Nchini ..............................119
7.8.3 Mikakati ya Kupambana na Malaria Zanzibar 2020-2024. ...........119
7.8.4 Kazi Kuu Zilizofanywa na Programu katika Kupambana na Malaria Zanzibar mwaka 2020-2024 ...........................................119
7.8.5 Idadi ya Nyumba Zilizopuliziwa Dawa ....................................... 120
7.9 Maradhi ya Kuambukiza .................................................................. 121
7.10 Hali ya Madawa ya kulevya Zanzibar ............................................. 121

7.10.1 Idadi ya Nyumba na Wakaazi Walioathirika na Uraibu wa Madawa ya Kulevya (Sober Houses) ........................................ 122
7.10.2 Idadi ya Wakaazi Kwenye Nyumba za Kurekebishia Tabia....... 123
7.11 Sekta ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, .................. 124
7.11.1 Idadi ya Wazee na Watoto Yatima Kwenye Nyumba za Hifadhi 124
7.12 Hali ya Watu wenye Mahitaji Maalumu Zanzibar ............................ 125
7.12.1 Mikakati ya Wizara Kuwawezesha Watu Wenye Mahitaji Maalum.................................................................................. 125
7.13 Hali ya Wanawake na Watoto. ........................................................ 126
7.13.1 Wilaya Zilizoongonza kwa Visa vya Unyanyasaji wa Kijinsia 2024 ................................................................................ 127
7.13.2 Matokeo/Visa ya Unyanyasaji wa Kijinsia Vilivyoripotiwa ...... 127
7.13.3 Uhalifu Dhidi ya Watu na Mali ................................................. 128
7.13.4 Makosa ya Jinai ........................................................................ 128
7.13.5 Ajali za Barabarani ................................................................... 129
7.13.6 Kesi Zilizofikishwa Mahakama ya Vijana (watoto).................. 129
**SURA YA NANE ............................................................................ 131**
**8.0 MAENDELEO YA KIUCHUMI NA KIJAMII ZANZIBAR MWAKA 2024.............................................................................. 131**
**SURA YA TISA................................................................................ 133**
**9.0 UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2024/2025........... 133**
9.1 Mapato ya Serikali ............................................................................ 133
9.1.1 Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani ................................................ 133
9.1.2 Ukusanyaji wa Mapato Kitaasisi................................................. 133
9.1.3 Mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo............................ 134
9.2 Matumizi ya Serikali 2024/2025. .................................................. 134
9.2.1 Matumizi ya Kazi za Kawaida .................................................... 134
9.2.2 Mishahara .................................................................................... 134
9.2.3 Matumizi Mengineyo .................................................................. 134
9.2.4 Matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali ....................................... 134
9.2.5 Matumizi ya Kazi za Maendeleo.................................................. 135
9.3 Deni la Taifa....................................................................................... 135

**SURA YA KUMI .......................................................................................... 136**
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MIRADI YA KIMKAKATI KWA KIPINDI CHA JULAI 2024 HADI MACHI 2025 ........................................................................................... 136
**SURA YA KUMI NA MOJA .......................................................................... 156**
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2024 HADI MACHI 2025 ...... 156
11.2 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU NA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA JULAI 2024 HADI MACHI 2025 KWA KILA WIZARA........................................................................................ 157

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| ABS | Asset-Backed Securities |
| AfDB | African Development Bank (Benki ya Maendeleo ya Afrika) |
| ISA | International Standars on Auditing |
| BADEA | Arab Bank for Economic Development in Africa |
| BOA | Bank of Africa |
| BMEJZ | Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar |
| CCECC | China Civil Engineering Construction Corporation |
| CRDB | Cooperative and Rural Development Bank |
| CRJE | China Railway Jianchang Engineering |
| EU | European Union (Umoja wa Ulaya) |
| GBS | General Budget Support (Misaada ya Kibajeti) |
| GIZ | German Society for International Cooperation |
| HESLB | Higher Education Students Loan Board (Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Tanzania) |
| HIV | Human Immune Virus |
| IMF | International Monetary Fund (Shirika la Fedha la Kimataifa) |
| JKU | Jeshi la Kujenga Uchumi |
| KIST | Karume Institute of Science and Technology |
| KfW | German Development Bank |
| KMKM | Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo |
| MRDT | Malaria Rapid Diagnostic Test (Uchunguzi wa Haraka wa Malaria) |
| NHIF | National Health Insurance Fund (Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ) |
| NBC | National Bank of Commerce (Benki ya Taifa ya Biashara) |
| NMB | National Microfinance Bank Limited |
| OPEC | Organization of the Petroleum Exporting Countries (Umoja wa Nchi Zinazozalisha na Kusafirisha Mafuta kwa wingi Duniani) |
| PBZ | People Bank of Zanzibar (Benki ya Watu wa Zanzibar) |
| RBS | Risk Based Supervision (Mfumo unaoangazia Vihatarishi) |
| RINA | Registro Italiano Navale |
| SDGs | Sustainable Development Goals |
| SNR | Sema na Rais |
| SMT | Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| SMZ | Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar |

| | |
|---|---|
| TASAF | Tanzania Social Action Fund |
| TCB | Tanzania Commercial Bank (Benki ya Biashara Tanzania) |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TZS | Tanzania Shilings (Shilingi ya Tanzania) |
| TIRA | Tanzania Insurance Regulatory Authority (Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania) |
| UKIMWI | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| UN-WOMEN | United Nation for Women |
| UNEP | United Nation Environment Programme |
| ZAWA | Zanzibar Water Authority (Mamlaka ya Maji Zanzibar) |
| ZADEP | Zanzibar Development Plan (Mpango wa Maendeleo Zanzibar) |
| ZECO | Zanzibar Electricity Corporation (Shirikia la Umeme Zanzibar) |
| ZF DEVCO | Zanzibar Ferry Development Company |
| ZIPA | Zanzibar Investment Promotion Authority (Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar) |
| ZIC | Zanzibar Insurance Cooperation (Shirika la Bima la Zanzibar) |
| ZOLAS | Zanzibar Online Local Application System |
| ZRA | Zanzibar Revenue Authority (Mamlaka ya Mapato Zanzibar) |
| ZSSF | Zanzibar Social Security Fund (Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar) |

# UTANGULIZI

Miongoni mwa madhumuni makuu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuandaa sera madhubuti za mipango ya maendeleo zenye kuchochea ukuaji wa uchumi endelevu wenye kujumuisha wananchi katika shughuli za uzalishaji mali na kuinua hali zao. Kwa mwaka 2024 Serikali iliendelea na kasi ya kuleta maendeleo endelevu yenye lengo la kuimarisha ustawi wa wananchi kiuchumi na kijamii pamoja na kusimamia misingi ya utawala bora kama ilivyoainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Zanzibar (ZDV 2050) na kutafsiriwa na Mpango Mkuu wa Maendeleo wa muda mfupi wa Zanzibar (ZADEP 2021-2026) pamoja na Mipango mengine ya Kitaifa ikiongozwa na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 - 2025 na Hotuba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi wakati akizindua Baraza la Kumi la Wawakilishi mnamo mwezi wa Novemba 2020. Aidha, Mpango huu pia umezingatia Sera, Mipango na Mikakati ya kufikia Malengo ya Dira za Kisekta, Kikanda na Kimataifa kama vile Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ya mwaka 2050; Dira ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) ya mwaka 2050; Ajenda ya Maendeleo ya Afrika ya mwaka 2063; na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) ya mwaka 2030.

Mwenendo wa ukuaji wa uchumi wa Dunia mwaka 2024 umekua kwa kasi ya wastani wa asilimia 3.2, ikilinganishwa na kasi ya ukuaji wa asilimia 3.1 mwaka 2023. Uchumi wa nchi Zilizoendelea umefikia ukuaji wa wastani wa asilimia 1.7 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 1.6 mwaka 2023. Uchumi wa Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia kiuchumi umefikia ukuaji wa wastani wa asilimia 4.2 mwaka 2024, ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 4.3 mwaka 2023.

Aidha, mwenendo wa ukuaji wa uchumi wa Zanzibar umeendelea kuimarika na kufikia wastani wa asilimia 7.1 mwaka 2024 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.4 mwaka 2023. Pato halisi la Taifa (GDP at constant price) limefikia thamani ya TZS 4026.4 bilioni mwaka 2024 kutoka thamani ya TZS 3,758.8 bilioni mwaka 2023. Hata hivyo, Pato la Taifa kwa bei ya soko (GDP at current price) limeongezeka na kufikia thamani ya TZS 6572.6 bilioni mwaka 2024 kutoka thamani ya TZS 6,041.3 bilioni mwaka 2023.

Kuongezeka kwa Pato la Taifa ni kiashiria cha kuimarika kwa uchumi wa Zanzibar ikiwa ni matokeo ya juhudi na weledi wa Serikali katika kubuni na kutekeleza miradi ya maendeleo, kuweka mazingira mazuri ya kuwavutia wawekezaji, kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za kiuchumi na kijamii, kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani na kusimamia nidhamu ya matumizi bora ya rasilimali fedha.

Kwa Mwaka 2024, Kasi ya mfumuko wa bei imepungua kufikia wastani wa asilimia 5.1 kutoka wastani wa asilimia 6.9 mwaka 2023. Kupungua kwa kasi ya mfumko wa bei kumetokana na kushuka kwa bei za bidhaa za chakula na zisizo za chakula katika soko la dunia. Serikali inaendelea na juhudi za kufatilia na kusimamia mwenendo wa bei za bidhaa na huduma, ikiwemo kupunguza ushuru na msamaha wa kodi kwa bidhaa muhimu za chakula zinazoingizwa nchini, kutoa bei elekezi za bidhaa za chakula na vifaa vya ujenzi, kuanzishwa kwa Mfuko wa Kuhimili Uchumi (Economic Stabilization Fund) ili kuimarisha uchumi na kupunguza upandaji wa bei za bidhaa ikiwemo mafuta. Juhudi hizo zimepelekea wananchi kupata huduma muhimu na zimeweza kupunguza kasi ya mfumko wa bei nchini na kuendelea kuwa na kasi ya mfumko wa bei wa kiwango cha tarakimu moja.

Katika juhudi za kufanikisha Mpango wa Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetekeleza miradi mikubwa ya kimkakati sambamba na utekelezaji wa miradi ya kijamii ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano, afya, elimu na programu ndogo zenye lengo la kuwajengea uwezo na mazingira bora wananchi wenye kipato cha chini na mahitaji maalum, juu ya utoaji huduma za kibiashara, kilimo, uvuvi, utalii na ujasiriamali kwa ajili ya kuinua vipato vyao.

## SURA YA KWANZA

# 1.0 HALI YA UCHUMI

## 1.1 Uchumi wa Dunia

Kwa mujibu wa ripoti ya Mtazamo wa Uchumi wa Duniani "World Economic Outlook" (WEO) ya mwezi wa Januari, 2025. Uchumi wa Dunia umekuwa kwa kasi ya wastani wa asilimia 3.2 mwaka 2024 ikilinganishwa na kasi ya ukuaji wa wastani wa asilimia 3.1 mwaka 2023 Ukuaji wa uchumi wa Dunia hujumuisha nchi Zilizoendelea, Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi zikiwemo nchi zilizoko Jangwa la Sahara ambazo kikawaida zina mwenendo tofauti katika ukuaji wa uchumi wake. Ukuaji huo umetokana na kuendelea kuimarika kwa masoko ya fedha na mitaji duniani iliyopelekea kupungua kwa viwango vya gharama za riba za mikopo na kuengezeka kwa riba za uwekezaji

Ukuaji wa uchumi kwa **Nchi Zilizoendelea** umefikia wastani wa asilimia 1.7 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 1.6 mwaka 2023 kutokana na kuongezeka kwa biashara za kimataifa za viwandani zenye uwakala na umiliki kutoka katika nchi hizo na kuongezeka kwa thamani ya uwekezaji katika masoko ya mitaji.

Uchumi wa **Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia kiuchumi** umefikia wastani wa asilimia 4.2 mwaka 2024, ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 4.1 mwaka 2023. Kwa upande wa Nchi za Afrika, kasi ya ukuaji wa uchumi imefikia wastani wa asilimia 4.0 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 3.1 mwaka 2023. Ukuaji huo umetokana na kuongezeka kwa usambazaji wa huduma za nishati ya umeme na gesi nchini Afrika Kusini na kuongezeka kwa uzalishaji wa mafuta nchini Nigeria.

**Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara,** kasi ya ukuaji uchumi mwaka 2024 imefikia wastani wa asilimia 3.8 kutoka wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2023, hali ya kuimarika kumetokana na unafuu wa sera za udhibiti wa fedha za kigeni hasa Dola ya Marekani kulikopelekea kuimarika kwa sarafu za nchi hizo.

Kasi ya Ukuaji Uchumi kwa Nchi za Afrika Mashariki imefikia wastani wa asilimia 5.1 mwaka 2024, kutoka wastani wa asilimia 5.0 mwaka 2023. Ukuaji huo ni kutokana na ongezeko la uzalishaji na usafirishaji wa mafuta katika ukanda

wa Afrika Mashariki. Aidha, kuongezeka kwa thamani ya usafirishaji wa mazao na bidhaa kwa nchi ya Sudan ya Kusini, pamoja na kuongezeka kwa mitaji ya uwekezaji na kuimarika kwa masoko ya hisa nchini Kenya kumesababisha kwa kiasi kikubwa ukuaji huo.

### 1.2 Uchumi wa Nchi Zilizoendelea

Kwa mwaka 2024, uchumi wa nchi zilizoendelea umeimarika na kufika wastani wa asilimia 1.7 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 1.6 mwaka 2023. Ukuaji huo umetokana na kuongezeka kwa biashara za kimatifa za viwandani zenye uwakala na umiliki kutoka katika nchi hizo, kuongezeka kwa thamani ya uwekezaji katika masoko ya mitaji, kuongezeka kwa usafirishaji wa bidhaa zenye kutumia teknologia za nishati za umeme, gesi na nguvu za jua kama vila mashine, gari na vifaa vya TEHAMA. Ukuaji wa uchumi wa nchi zilizoendelea umetokana zaidi na kuimarika kwa uchumi wa nchi za Marekani, ambayo kasi ya ukuaji uchumi imefikia wastani wa asilimia 2.8 mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 2.5 mwaka 2023. Nchi ya Japani, kasi ya ukuaji ilifikia wastani wa asilimia (0.2) mwaka 2024, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 1.9 mwaka 2023. Jumuia ya Ulaya, kasi ya ukuaji uchumi ilifikia wastani wa asilimia 0.8 mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 0.4 mwaka 2023. Uingereza, kasi ya ukuaji uchumi ilifikia wastani wa asilimia 0.9 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 0.5 mwaka 2023.


### 1.3 Uchumi wa Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi

Hizi ni nchi zenye ushawishi mkubwa katika kuleta mageuzi ya kiuchumi na kichocheo cha ukuaji wa uchumi duniani. Miongoni mwa nchi hizo ni Brazil, Urusi, India, China na Afrika ya Kusini. Kwa mwaka 2024, ukuaji wa uchumi kwa nchi hizi umefikia wastani wa asilimia 4.2 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.1 mwaka 2023. Kwa upande wa nchi ya **India**, kasi ya ukuaji wa uchumi imefikia wastani wa asilimia 6.5 mwaka 2024, kutoka wastani wa asilimia 6.7 mwaka 2023, hali hii imetokana na kupungua kwa usafirishaji wa bidhaa kutoka viwandani.

Nchi ya **China** kwa mwaka 2024, kasi ya ukuaji uchumi imefikia wastani wa asilimia 4.8 kutoka wastani wa asilimia 5.2 mwaka 2023. Kasi hii ya ukuaji wa uchumi imetokana na kupungua kwa biashara za uuzaji na ukodishaji wa majengo na kuyumba kwa bei za masoko ya hisa.

Kwa upande wa nchi ya **Urusi**, kasi ya ukuaji wa uchumi imeongezeka kufikia wastani wa asilimia 3.8 mwaka 2024, kutoka wastani wa asilimia 3.6 mwaka 2023. Hii ni kutokana na kuogezeka kwa matumizi ya bajeti ya serikali katika kuimarisha viwanda vya uzalishaji silaha za kivita, kupungua kwa tatizo la ajira na kuongezeka kwa mishahara katika Taasisi za umma. Nchi ya **Brazil** kasi ya ukuaji wa uchumi imeongezeka na kufikia wastani wa asilimia 3.7 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 2.9 mwaka 2023. Ukuaji huo umechochewa na kuimarika kwa sekta ya kilimo baada ya ukame mrefu katika maeneo ya kaskazini hadi kusini mashariki mwa nchi hiyo na kuimarika kwa biashara za kimatifa zikiwemo bidhaa za kilimo na sukari, ***(Mchoro Nambari 1).***

**Mchoro Nambari 1: Ukuaji wa Uchumi wa Dunia, nchi Zilizoendelea , Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi 2022-2024.**




***Chanzo: Ripoti ya Mtazamo wa Uchumi wa Dunia na OECD, 2024.***

## 1.4 Hali ya Uchumi wa Bara la Afrika

### 1.4.1 Uchumi wa Afrika


Uchumi wa Bara la Afrika umekua kwa kasi ya wastani wa asilimia 4.0 mwaka 2024, kutoka wastani wa asilimia 3.1 mwaka 2023 ***(Mchoro Nambari 2)***. Kwa Kanda ya Kaskazini mwa Bara la Afrika, uchumi umefikia wastani wa asilimia 3.6 mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.1 mwaka 2023; Kanda ya Kusini imefikia wastani wa asilimia 2.2 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 1.6 mwaka 2023; Kanda ya Magharibi ukuaji wa uchumi umefikia wastani wa asilimia 4.2 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 3.6 mwaka 2023; Kanda ya Afrika Mashariki ukuaji wa uchumi umefikia wastani wa asilimia 5.1 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 5.0 mwaka 2023. Kanda ya Afrika ya Kati imefikia wastani wa asilimia 4.1 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 4.3 mwaka 2023, Upungufu huo umetokana na kupungua kwa usafirishaji wa bidhaa za mafuta na gesi kwa nchi zinazozalisha mafuta; kuharibika kwa miundombinu ya kusafirisha mafuta nchini **Sudan ya Kaskazini**; na kuongezeka kwa athari za mabadiliko ya tabianchi ambazo zimeathiri uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo na kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ukuaji wa uchumi umefikia wastani wa asilimia 3.8 mwaka 2024 kutoka ukuaji wa wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2023. ***(Jadweli nambari 1).***

**Jadweli Nambari 1: Ukuaji Halisi wa Uchumi kwa Kanda za Afrika**

| KANDA ZA AFRIKA | UKUAJI HALISI (ASILIMIA) | |
|---|---|---|
| | 2023 | 2024 |
| **Afrika** | 3.1 | 4.0 |
| **Kanda ya Kusini** | 1.6 | 2.2 |
| **Kanda ya Kaskazini** | 4.1 | 3.6 |
| **Kanda ya Magharibi** | 3.6 | 4.2 |
| **Kanda ya Mashariki** | 1.5 | 4.9 |
| **Kanda ya Kati** | 4.3 | 4.1 |

***Chanzo: Hali Halisi na Mwelekeo wa Uchumi wa Afrika, (AfDB) 2025***

**Mchoro Nambari 2: Wastani wa Kasi ya Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi za Afrika mwaka (2020 - 2024).**




***Chanzo: Uchumi wa Afrika, (AfDB) 2025***

Kwa mwaka 2024, nchi za Afrika ambazo uchumi wake ulikuwa kwa Kasi Kubwa:

***a) Niger***

Niger ni miongoni mwa nchi za Afrika ambazo uchumi wake hutegemea usafirishaji wa mafuta ghafi. Kwa mwaka 2024, kasi ya ukuaji uchumi wa Niger imekua kwa wastani wa asilimia 10.4 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 2.5 mwaka 2023. Kasi ya ukuaji huo imetokana na kuondolewa kwa vikwazo vya kiuchumi vilivyowekwa na Jumuia ya Uchumi ya Umoja wa Nchi za Africa na Magharibi (ECOWAS). Hatua hii imepelekea kuimarika kwa biashara za usafirishaji mafuta na kurejea masoko ya kifedha ambayo yalifungwa na sasa kuendelea na utoaji wa huduma.

***b) Senegal***

Kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi ya Senegal imefikia wastani wa asilimia 9.3 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 4.3 mwaka 2023. Kasi hii ya ukuaji uchumi imetokana na uchimbaji wa mafuta (Hydrocarbon) na madini pamoja na kukamilika kwa miradi ya usafiri na mawasiliano.

***c) Tunisia***

Ukuaji wa uchumi wa nchi ya Tunisia ulifikia wastani wa asilimia 2.1 mwaka 2024, kutoka wastani wa asilimia 0.4 mwaka 2023. Hii imetokana na kuimarika kwa uchumi wa nchi hiyo baada ya kuanza kupungua kwa kiwango cha madeni, kuongezeka kwa mauzo ya huduma za kitalii na uhaulishaji wa fedha za kigeni kutoka kwa wazawa (Diaspora) kutoka nchi za nje.

Kwa mwaka 2024, miongoni mwa nchi za Afrika zilizokuwa na Kasi Ndogo ya Ukuaji wa Uchumi

***(a) Namibia***

Kasi ya ukuaji wa uchumi imefikia wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 4.2 mwaka 2023. Upungufu huo umetokana na kuanguka kwa sekta ya kilimo na ukame kulikopeleka kupungua kwa upatikanaji wa maji na kuathiri shughuli za uchimbaji madini.

***(b) Zambia***

Zambia ni maarufu katika uchimbaji na usafirishaji wa shaba duniani. Kwa mwaka 2024, uchumi wa Zambia umekua kwa kasi ndogo ya wastani wa asilimia hasi ya 4.5 kutoka wastani wa asilimia hasi ya 5.2 mwaka 2023. Hali hii imetokana na kushuka kwa bei ya Shaba katika soko la dunia na mabadiliko ya tabianchi yalioathiri kilimo cha umwagiliaji maji.

***(c) Zimbabwe***

Kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi hii imepungua na kufikia wastani wa asilimia 2.0 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 5.0 mwaka 2023 kutokana na kuendelea kwa zuio la mauzo ya bidhaa za kilimo katika nchi za Ulaya sambamba na kushuka kwa bei za mazao ya biashara hasa tumbaku katika soko la dunia.

### 1.4.2 Uchumi wa Nchi za Visiwa Vilivyo Barani Afrika

Zanzibar ni miongoni mwa nchi zenye uchumi wa visiwa *(Island Economies)*. Kutathmini mwenendo wa uchumi kwa nchi zenye uchumi kama wa Zanzibar Barani Afrika, ni muhimu sana katika kubaini fursa za kiuchumi na kubuni sera madhubuti za uchumi shindanishi. Visiwa kama Mauritius, Seychelles, Comoro

na Madagascar ni maarifu sana Barani Afrika na Duniani katika ushindani wa sekta ya utalii na biashara za viungo ambazo pia ni sekta tegemezi kwa uchumi wa Zanzibar.

Kwa mwaka 2024 uchumi wa Visiwa uliripotiwa kama ifuatavyo:

***a. Mauritius***

Kwa mwaka 2024, kasi ya ukuaji uchumi imefikia wastani wa asilimia 4.9 kutoka wastani wa asilimia 7.0 mwaka 2023. Kasi ndogo ya ukuaji wa uchumi ilisabishwa na kuanguka kwa sekta ya utalii pamoja na kuyumba kwa thamani ya sarafu ya nchi hiyo.

***b. Seychelles***

Kasi ya ukuaji uchumi imekuwa kufikia wastani wa asilimia 4.0 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 2.5 mwaka 2023. Sababu za kuimarika kwa uchumi wa nchi hiyo ni kutokana na kuimarika kwa thamani ya sarafu Rupee, baada ya kupungua kwa gharama za uagizaji bidhaa nje ya nchi na kuongezeka kwa mauzo ya huduma zitokanazo na utalii.

***c. Comoro***

Visiwa vya Comoro ni moja ya visiwa ambavyo vina mahusiano ya kibiashara na kiutamaduni na visiwa vya Zanzibar. Kwa mwaka 2024, uchumi wake umekua na kufikia wastani wa asilimia 4.0 kutoka wastani wa asilimia 3.1 mwaka 2023. Kasi ya ukuaji wa uchumi kwa visiwa vya Comoro ilitokana na ongezeko la uwekezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na uhaulishaji wa fedha za kigeni (Remittance) kutoka kwa wazawa wa Comoro wainaoishi nje ya nchi.


***d. Madagascar***

Kasi ya ukuaji uchumi kwa nchi ya Madagascar imekua kwa wastani wa asilimia 4.5 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 4.4 mwaka 2023. Ukuaji huo umetokana na kuimarika kwa sekta ya usafirishaji wa madini ya kimkakati (Graphite, Nickel na Cobalt) sambamba na kuimarika kwa soko la utalii.

Kwa kuzingatia kasi ya mwenendo wa ukuaji uchumi wa visiwa hivi, Zanzibar imendelea kuwa na kasi zaidi ya ukuaji uchumi ikilinganisha na visiwa vyengine vya barani Afrika ***(Mchoro Nambari 3)***. Visiwa hivyo vinaushindani mkubwa

na Zanzibar katika masoko ya kimataifa ya biashara za utalii. Juhudi na weledi wa kubuni sera na mikakati ya kuwavutia wawekezaji kuekeza katika miradi mikubwa ya hoteli za kitalii pamoja na miradi ya miundombinu ya mawasiliano na huduma za kijamii ikiwemo afya kumepelekea kuongezeka kwa idadi ya watalii wa Kimataifa na kukuza uchumi wa Zanzibar.

**Mchoro Nambari 3: Wastani wa Kasi ya Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi za Visiwa Vilivyo Barani Afrika ikiwemo Zanzibar kwa mwaka (2023-2024).**




*Chanzo: Uchumi wa Afrika, (AfDB) 2025*

| Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi za Uchumi wa Visiwa Afrika | 2023 (Asilimia) | 2024 (Asilimia) |
|---|---|---|
| **Nchi za Uchumi wa Visiwa** | | |
| Comoro | 3.9 | 3.1 |
| Mauritius | 7.0 | 4.9 |
| Madagasca | 4.4 | 4.5 |
| Seychelles | 2.5 | 4.0 |
| **Zanzibar** | 7.4 | 7.1 |

*Chanzo: Uchumi wa Afrika, (AfDB) na OCGS, 2025*

### 1.4.3 Uchumi wa baadhi ya Nchi Zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara

Kwa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara kasi ya ukuaji uchumi kwa mwaka 2024 imefikia wastani wa asilimia 3.8 kutoka wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2023, hii imetokana na kupunguzwa kwa sera za udhibiti wa fedha za kigeni hasa Dola ya Marekani kulikopelekea kuimarika kwa sarafu za nchi hizo na kupungua kwa gharama za ulipaji riba za madeni sambamba na kuimarika kwa masoko ya utalii na mitaji ya uwekezaji. Mwenendo wa ukuaji uchumi kwa baadhi ya nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ni kama ifutatvyo:

***a) Malawi***

Nchi ya Malawi uchumi wake hutegemea kilimo ambao kwa mwaka 2024 umekua kwa kasi ya wastani wa asilimia 3.3 kutoka wastani wa asilimia 1.5 mwaka 2023. Ukuaji huo umetokana na kurejea kwa shughuli za uzalishaji katika sekta ya kilimo baada kutokea kwa ukame na vimbunga.

***b) Equatorial Guinea***

Kasi ya ukuaji uchumi imefikia wastani wa asilimia 5.0 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 5.7 mwaka 2023. Kupungua kwa kasi ya ukuaji uchumi wa nchi hii imetokana na kupungua kwa uzalishaji wa mafuta kutokana na kuchakaa kwa miundombinu ya visima vya mafuta, kupungua kwa mapato yatokanayo na mauzo ya mafuta.

***c) Djibouti***

Kwa mwaka 2024, ukuaji wa uchumi wa nchi ya Djibouti umefikia wastani wa asilimia 6.2 kutoka wastani wa asilimia 7.3 mwaka 2023. Hii ni kutokana na kupungua kwa biashara za kimataifa baina ya ukanda wa Mashariki ya Kati kutokana na machafuko ya kisiasa na kupungua kwa shehena za mizigo kutoka Ethiopia.

**Jadweli Nambari 2: Mwenendo wa Uchumi kwa baadhi ya Nchi Zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara mwaka (2023 - 2024) (%)**

| Nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara | Ukuaji wa Uchumi kwa Asilimia | |
|---|---|---|
| | 2023 | 2023 |
| **Nchi zenye Kipato cha Kati** | | |
| Djibouti | 7.3 | 6.2 |
| Kenya | 5.2 | 5.4 |
| Namibia | 4.2 | 3.3 |
| Nigeria | 2.8 | 3.1 |
| Rwanda | 8.2 | 6.6 |
| Tanzania | 5.1 | 5.4 |
| | | |
| **Nchi zenye Kipato cha Chini** | | |
| Bukina Faso | 3.6 | 4.1 |
| Ethiopia | 7.1 | 6.7 |
| Malawi | 1.5 | 3.3 |
| Niger | 2.5 | 10.4 |
| Senegal | 4.3 | 9.3 |
| Zambia | 5.8 | 4.5 |

***Chanzo: Uchumi wa Afrika, (AfDB) na OCGS, 2025***

### 1.4.4 Uchumi wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki

Kasi ya ukuaji wa uchumi imefikia wastani wa asilimia 5.1 mwaka 2024, kutoka wastani wa asilimia 5.0 mwaka 2023. Ukuaji huo umetokana na kuongezeka kwa uwekezaji wa miundombinu kupitia sekta binafsi pamoja na kuimarika kwa shughuli za kitalii kwa baadhi ya nchi za ukanda huo zikiwemo Kenya na Tanzania.

#### *(a) Tanzania*

Uchumi wa Tanzania umekua kwa kasi ya wastani wa asilimia 5.4 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 5.1 mwaka 2023. Ukuaji wa uchumi umeendelea kuimarika zaidi baada ya kukamilika kwa uwekezaji mkubwa katika sekta za nishati hasa baada ya kuanza kwa matumizi katika mradi mkubwa wa bwawa la Umeme la Julius Nyerere, kukamilika kwa hatua ya kwanza kwa mradi wa usafiri wa treni ya mwendo kasi - Standard Gauge Railway (SGR) na kuimarika kwa miundombinu ya elimu, afya na mawasiliano ya barabara sambamba na kuongezeka kwa mitaji ya uwekezaji na kuimarika kwa sekta ya utalii.

***(b) Kenya***

Ukuaji wa uchumi wa nchi hii umefikia wastani wa asilimia 5.2 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 5.4 mwaka 2023. Ukuaji huo umetokana na kushuka kwa sekta ya uzalishaji viwandani sekta ya utalii.

***(c) Uganda***

Kasi ya ukuaji uchumi wa Uganda imekua na kufikia wastani wa asilimia 6.0 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 4.6 mwaka 2023. Kuongeza huko kumetokana na uwekezaji mkubwa katika sekta ya mafuta na gesi asilia ikiwemo uchimbaji wa visima vipya vya mafuta na ujenzi wa miundombinu ya kusafirishia mafuta.

***(d) Rwanda***

Kwa mwaka 2024, uchumi wa Rwanda umefikia wastani wa asilimia 6.6 kutoka wastani wa asilimia 8.2 mwaka 2023. Ukuaji huo mdogo wa uchumi imetokana na kupungua kwa mapato ya utalii hasa katika mikutano ya kimatifa na uhaulishaji wa fedha kutoka kwa wazawa wanaoishi nje ya nchi hiyo na kupungua kwa mitaji ya uwekezaji.

***(e) Burundi***

Uchumi wa Burundi umefikia wastani wa asilimia 4.6 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 2.8 mwaka 2023. Ukuaji huo umechangiwa na uwekezaji katika miundombinu ya usafiri, sekta ya madini na sekta za umma.

***(f) Sudani ya Kusini***

Uchumi wa nchi hii umefikia asilimia 5.0 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 0.4 mwaka 2023. Hali hii imetokana na kupungua kwa gharama za usafirishaji mafuta baada ya ukarabati na udhibiti wa miundombinu hiyo kutoka Sudan ya Kaskazini na kurejea kwa shughuli za kilimo baada ya athari za mabadiliko ya tabia nchi.


***(g) Jamhuri ya Demokrasia ya Congo***

Kwa mwaka 2024, uchumi wa nchi hii umefikia wastani wa asilimia 5.7 kutoka wastani wa asilimia 7.5 mwaka 2023. Ukuaji huo mdogo umetokana na kupungua kwa shughuli za biashara na uwekezaji na kuendelea kudorora kwa hali ya utulivu katika eneo la mashariki mwa nchi hiyo.

### *(h) Somalia*

Nchi hii hutegemea sana usafirishaji wa mifugo na samaki kwa asilimia 76 ya jumla ya bidhaa zinazosafirishwa nje. Kwa mwaka 2024, uchumi wa Somalia umefikia wastani wa asilimia 3.7 kutoka wastani wa asilimia 2.8 mwaka 2023. Kasi hii ya ukuaji uchumi imetokana na kurejea kwa shughuli za ufugaji na usafirishaji wa mifugo na samaki ***(Mchoro Nambari 3)***.

**Mchoro Nambari 4: Kasi ya Ukuaji wa Uchumi kwa nchi za Afrika Mashariki mwaka 2023 na 2024.**




***Chanzo: Uchumi wa Afrika, (AfDB) 2025***

## 1.4.5 Nchi zenye Uhusiano wa Kibiashara na Zanzibar (Zanzibar Trading Partners)

Ufatiliaji wa mwenendo wa uchumi kwa nchi za India, China, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), ni muhimu sana katika kuimarisha wigo wa biashara za kimataifa na kuinua hali za wanachi kiuchumi na kijamii. Kuimarika kwa uchumi kwa nchi hizi hupelekea kuongezeka kwa thamani ya mauzo ya fedha za kigeni kwa bidhaa mbalimbali tunazosafirisha kwenda katika nchi hizo kama vile viungo, karafuu, bidhaa zitokanazo na uchumi wa buluu, bidhaa za kilimo na mauzo yatokanayo na huduma za utalii. Vile vile kuyumba kwa uchumi wa nchi hizi hupelekea kupungua kwa misaada ya kibajeti na mitaji ya uwekezaji sambamba na kuongezeka kwa bei za bidhaa zinazoingia nchini kama vile nguo, mashine za uzalishaji viwandani, vifaa tiba, dawa za binadamu na huduma za kitabibu na matibabu. Mwenendo wa uchumi kwa nchi hizo ni kama ifuatavyo:

***a) India,***

Kwa mwaka 2024, kasi ya ukuaji wa uchumi imefikia wastani wa asilimia 6.5 kutoka wastani wa asilimia 6.7 mwaka 2023. Ukuaji huo umetokana na mabadiliko ya sera za biashara za kimataifa, zilizopelekea kupungua kwa usafirishaji wa bidhaa kutoka viwandani na ukosefu wa ajira.

***b) China***

Kwa mwaka 2024, kasi ya ukuaji uchumi kwa nchi ya China ilifikia wastani wa asilimia 4.8 kutoka wastani wa asilimia 5.2 mwaka 2023. Kasi hii ya ukuaji mdogo wa uchumi ilitokana na mabadiliko ya sera za biashara za kimataifa, kupungua kwa biashara za uzalishaji na ukodishaji wa majengo na kuyumba kwa bei za masoko ya hisa.

***c) Jumuiya ya Nchi za Falme za Kiarabu (U.A.E)***

Kasi ya ukuaji uchumi imefikia wastani wa asilimia 3.3 kwa mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 3.2 mwaka 2023. Kasi hii ya ukuaji wa uchumi imetokana na kuongezeka kwa uzalishaji mafuta baada ya agizo la kupunguza uzalishaji wa mafuta kwa nchi wanachama wa OPEC.

## 1.5 Hali ya Mfumko wa Bei

### 1.5.1 Mfumko wa Bei wa Dunia

Kasi ya mfumko wa bei duniani kwa mwaka 2024 imefikia wastani wa asilimia 5.9 kutoka wastani wa asilimia 6.8 mwaka 2023. Kupungua kwa mfumko wa bei duniani kumetokana na kupungua kwa bei za riba na masharti ya udhibiti sera za kifedha pamoja na sera ya kupunguza matumizi ya Dola ya marekani kama sarafu kuu kwa uhaulishaji wa biashara za kimataifa baina ya nchi wanachama wa BRICS. Hali hii imepelekea kupungua kwa bei za bidhaa na huduma katika soko la Dunia.


Kasi ya mfumko wa bei kwa **Nchi Zilizoendelea** imepunguwa kwa wastani wa asilimia 2.6 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 4.6 mwaka 2023. **Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia kiuchumi** zimefikia wastani wa asilimia 7.9 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 8.1 mwaka 2023. Kupungua kwa mfumuko wa bei kumetokana na utulivu wa bei za mafuta na kupungua kwa bei za chakula na bidhaa za viwandani. Aidha, hatua ya kuanza kutumika kwa sera

ya kupunguza matumizi ya dola ya Marekeni kama sarafu ya kuhaulisha bidhaa baina ya washirika wa biashara za kimataifa pia zimepelekea utulivu wa bei za bidhaa na huduma. ***(Mchoro nambari 4)***

### 1.5.2 Mfumko wa Bei kwa Nchi Zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara

Kasi ya mfumko wa bei katika ukanda wa nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara imeongezeka na kufikia wastani wa asilimia 18.1 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 17.6 mwaka 2023. Ongezeko hili limesababishwa na kupungua kwa uzalishaji wa vyakula kutokana na madiliko ya tabia nchi kama vile ukame na mafuriko katika nchi za Malawi, Jamhuri ya Afrika ya kati na Chad. Machafuko ya kisiasa nchini Ethiopia na vita katika nchi za Sudan, Jamhuri ya Demokrasia ya Congo imekua moja ya sababu ya kuongezeka kwa kasi ya mfumko wa bei katika eneo hilo.

**Mchoro Nambari 5: Kasi ya Mfumko wa Bei Duniani mwaka (2020 - 2024)**




***Chanzo: Ripoti ya Mtazamo wa Uchumi wa Dunia, 2025.***

### 1.5.3 Mfumko wa bei wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki

**Kasi ya Mfumko wa bei wa nchi nane (8) za Jumuiya ya Afrika Mashariki** (Tanzania, Kenya, Uganda, Burundi, Rwanda, Jamhuri ya Demokrasia ya Congo, Sudan ya Kusini na Somalia), imepungua na kufikia wastani wa asilimia 10.5 mwaka 2024, kutoka wastani wa asilimia 11.6 mwaka 2023. Hii imesababishwa

na kupungua kwa gharama za uagiziaji wa bidhaa kutokana na kuimarika kwa miundombinu ya usafiri na ufanisi wa bandari tegemezi za Dar es salaam - Tanzania na Mombasa - Kenya. ***(Mchoro nambari 6)***.

***(a) Tanzania***

Kasi ya mfumko wa bei kwa nchi ya Tanzania, imefikia asilimia 3.3 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.0 mwaka 2023. Kushuka kwa kasi ya mfumko wa bei kulichangiwa na utulivu wa bei za nishati ya mafuta, kuongezeka kwa mazao ya chakula na viwanda vidogo na vya kati vya kusarifu mazao ya chakula pamoja na kuimarika ufanisi wa miundombinu ya usafirishaji na bandari.

***(b) Kenya***

Mwaka 2024, mfumko wa bei kwa nchi ya Kenya umefikia wastani wa asilimia 6.2 kutoka wastani wa asilimia 7.7 mwaka 2023. Kushuka kwa mfumko wa bei kumetokana na kurejea kwa hali ya utulivu wa kisiasa kulikopelekea kupungua kwa gharama za uzalishaji na usafiri wa mazao ya chakula kutoka nchi jirani.

***(c) Uganda***

Mfumko wa bei umefikia wastani wa asilimia 5.0 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 5.4 mwaka 2023. Upungufu huo umetokana na kupungua kwa bei za usafiri wa ndani, kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya chakula na utulivu wa bei za mafuta na gesi. Hali hii imepekea kuhimili athari za kuyumba kwa thamani ya sarafu ya Uganda kutokana na kupungua kwa uagiziaji wa bidhaa nchini humo.

***(d) Rwanda***

Mwaka 2024, kasi ya mfumko wa bei nchini Rwanda, imepungua hadi kufikia wastani wa asilimia 7.0 kutoka wastani wa asilimia 14.0 mwaka 2023. Hii imetokana na hatua ya udhibiti wa mzunguko wa fedha, kupungua kwa gharama za uagiziaji wa bidha za chakula na zisizo za chakula na kuimarika kwa kilimo cha mazo ya chakula nchini humo. Aidha kuongezeka kwa ufanisi wa bandari tegemezi (Tanzania) na kushuka zaidi kwa bei za bidhaa zinazoagizwa nje ya nchi kupitia kwenye bandari hiyo.

***(e) Burundi***

Kwa nchi ya ya Burundi kasi ya mfumko wa bei imepungua kwa wastani wa asilimia 22.0 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 27.0 mwaka 2023. Kutokana na kuimarika kwa kilimo cha mazao ya chakula na kupungua gharama za uagiziaji wa bidhaa hizo nje ya nchi. Aidha kuimarika kwa miundombinu ya usafiri na ufanisi wa bandari tegemezi (Tanzania), kumechangia kupunguza gharama za uagiziaji na kupelekea kushuka kwa bei za bidhaa muhimu nchini humo.

***(e) Sudani ya Kusini***

Mfumko wa bei umefikia wastani wa asilimia 17.0 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 40.2 mwaka 2023. Hii imetokana na kuimarika kwa Pauni ya Sudani baada ya kurejea kwa udhibiti wa biashara ya usafirishaji wa nishati ya mafuta na kurejea kwa shughuli za kilimo cha mazao ya chakula baada ya athari za madiliko ya tabianchi.


***(f) Jamhuri ya Demokrasia ya Congo***

Athari za machafuko ya kisiasa na vita katika eneo la mashariki zimeendelea kuathiri kasi ya mfumko wa bei na uchumi wa Jamhuri ya Demokrasia ya Congo kwa kipindi kirefu. Hata hivyo, kwa mwaka 2024, mfumko wa bei wa nchi hiyo umepungua na kufikia wastani wa asilimia 17.8 kutoka wastani wa asilimia 19.9 mwaka 2023. Kushuka kwa mfumko wa bei kumetokana na kupungua kwa gharama za uagiziaji wa bidhaa nje ya nchi.

***(g) Somalia***

Mfumko wa bei umefikia wastani wa asilimia 4.8 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 6.1 mwaka 2023. Kupungua kwa kasi ya mfumko wa bei kwa nchi ya Somalia kumetokana na kurejea kwa shughuli za kilimo katika uzalishaji wa mazao ya chakula na ufugaji baada ya hali ya ukame katika miaka ya karibuni.

**Mchoro Nambari 6: Kasi ya Mfumko wa Bei kwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (2023-2024)**




***Chanzo: Ripoti ya Mtazamo wa Uchumi wa Dunia (IMF) na Afrika, (AfDB), 2025***

## 1.5.4 Mfumko wa bei kwa Nchi zenye Uhusiano wa Kibiashara na Zanzibar (Zanzibar Trading Partners)

Mashirikiano zaidi ya kibiashara baina ya Zanzibar na nchi za India, China na Umoja wa Falme za Kiarabu (U.A.E), huathiri moja kwa moja mwenendo wa kasi ya mfumko wa bei wa Zanzibar. Kupanda na kushuka kwa thamani ya sarafu za nchi hizi, hupunguza au kuzidisha gharama za uagiziaji wa bidhaa na huduma, na hatimae kuongeza au kupunguza kasi ya mfumko wa bei hapa Zanzibar. Katika mwaka 2024, hali ya mfumko wa bei kwa nchi washirika wa kibiashara iliripotiwa kama ifuatavyo;

### *(a) India*

Kwa mwaka 2024, kasi ya mfumko wa bei imepungua na kufikia wastani wa asilimia 4.4 kutoka wastani wa asilimia 5.4 mwaka 2023. Kupungua kwa mfumko wa bei kumetokana na kushuka kwa bei za vyakula hasa mboga mboga, nafaka na sukari pamoja na kupungua kwa bei za nyumba.


### *(b) Jumuiya ya Nchi za Falme za Kiarabu (U.A.E)*

Kasi ya mfumko wa bei kwa nchi za UAE imepanda na kufikia wastani wa asilimia 2.3 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 1.6 mwaka 2023. Hii imetokana na kuongezeka kwa bei za huduma za fedha na bima, na bidhaa zisizo za chakula kama vile pamba na nguo. Zanzibar ni muagiziaji wa bidhaa za nguo kutoka UAE, athari ya kupanda kwa mfumko wa bei hasa kwa bidhaa hizo kunapelekea ongezeko la bei za bidhaa hizo zinapofika hapa nchini kutokana na kuongezeka kwa gharama za uagiziaji.

### *(c) China*

Kasi ya mfumko wa bei imepanda na kufikia wastani wa asilimia 0.4 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 0.2 mwaka 2023. Hii ni kutokana na kuongezeka kwa bei za bidhaa zisizo za chakula kama vile nguo na vifaa vya mawasiliano, usafiri, huduma za makaazi na matibabu. ***(Mchoro nambari 7)***

**Mchoro Nambari 7: Mfumko wa Bei mwaka 2023 na 2024 kwa Nchi zenye Uhusiano wa Kibiashara na Zanzibar (Zanzibar Trading Partners)**




***Chanzo: Ripoti ya Mtazamo wa Uchumi wa Dunia, 2024***

### 1.5.5 Mwenendo wa Bei kwa baadhi ya bidhaa katika Soko la Dunia

Ufuatiliaji wa kina juu ya mwenendo wa baadhi ya bei za bidhaa muhimu katika soko la dunia ni hatua ya msingi hasa kwa nchi zenye uchumi wa visiwa kama Zanzibar. Hatua hii hurahisisha kubuni sera na mikakati ya kudhibiti mfumko wa bei ili kunusuru upandaji wa bei za bidhaa zinazoagizwa kuja katika soko la ndani. Moja ya juhudi za Serikali ya Zanzibar ni kuhakikisha kuwa mwananchi wa kipato cha chini anaweza kumudu gharama zake za maisha. Kwa kufanikisha hilo, Serikali imekua ikitoa misamaha nafuu ya ushuru kwa bei za vyakula muhimu vinavyoagizwa na wafanyabiashara hapa nchini. Licha ya Changamoto zinazojitokeza Duniani zikiwemo migogoro ya kisiasa na vita vinavyooendelea baina ya Urusi na Ukraine na Israel na Palesitina vinapelekea kuathiri usambazaji wa bidhaa za chakula na zisizo za chakula katika soko la duniani na kupelekea kupanda kwa bei za bidhaa muhimu. Kwa mwaka 2024 bei za bidhaa zenye matumizi makubwa na zinazouzwa zaidi katika soko la dunia ni kama ifuatavyo:

***i. Nishati ya Mafuta***

Bei ya nishati ya mafuta kwa mwaka 2024 ilifikia wastani wa Dola za Kimarekani 78.1 kwa pipa kutoka Dola za Kimarekani 80.8 kwa pipa mwaka 2023. Sawa na punguzo la asilimia 3.3. Kushuka kwa bei za mafuta duniani kumetokana na kuongezeka kwa uzalishaji, sambamba na mkakati wa baadhi ya nchi wanachama wa OPEC kupunguza matumizi ya Dola ya Marekani katika kuhaulisha biashara za kimataifa. Hatua hiyo pia imepelekea kupungua kwa gharama za usafirishaji na usambazaji wa mafuta ghafi.

***ii. Mchele***

Bei ya mchele kwa mwaka 2024, imepanda kufikia Dola za Kimarekani 588.4 kwa tani ikilinganishwa na Dola za Kimarekani 553.7 kwa tani mwaka 2023. Sawa na ongezeko la asilimia 6.2. Hii ni kutokana na kupungua kwa hifadhi ya bidhaa hiyo katika nchi zinazozalisha mchele kwa wingi duniani (Thailand na India), kuongezeka kwa gharama za pembejeo za kilimo na kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa hiyo duniani.

***iii. Unga wa Ngano***

Katika mwaka 2024, bei ya unga wa ngano katika soko la dunia ilishuka na kufikia wastani wa Dola za Kimarekani 229.0 kwa tani ikilinganishwa na wastani wa Dola za Kimarekani 257.7 kwa tani mwaka 2023. Sawa na upungufu wa asilimia 11.1. Hii ni kutokana kupungua kwa gharama za uzalishaji na usambazaji.

*iv. Sukari*

Mwaka 2024, bei ya sukari katika soko la dunia imepungua na kufikia wastani wa Dola za kimarekani 450.0 kwa tani ikilinganishwa na wastani wa Dola za Kimarekani 520.0 kwa tani mwaka 2023, sawa na punguzo la asilimia 13.5. Kupungua kwa bei ya sukari katika soko la dunia kumetokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa sukari katika nchi za Brazil na India ambao ni wazalishaji wakuu duniani. ***(Jadweli nambari 3)***.

**Jadweli Nambari 3: Mwenendo wa Bei kwa baadhi ya Bidhaa katika Soko la Dunia**

| BIDHAA | KIPIMO | 2023 Bei kwa (USD) | 2024 Bei kwa (USD) | TOFAUTI Aslimia (%) |
|---|---|---|---|---|
| Mchele | Tani | 553.7 | 588.4 | 6.27 |
| Unga wa Ngano | Tani | 257.7 | 229.0 | -11.14 |
| Sukari | Tani | 520.0 | 450.0 | -13.46 |
| Nishati ya Mafuta | Pipa | 78.1 | 80.8 | 3.46 |

***Chanzo: Takwimu za Bidhaa za Dunia 2025***


# SURA YA PILI

## 2.0 HALI YA UCHUMI WA ZANZIBAR

### 2.1 Pato la Taifa na Ukuaji wa Uchumi

Kwa mwaka 2024 kasi ya ukuaji wa Uchumi imeimarika na kupelekea kuongezeka kwa Pato halisi la Taifa (GDP at constant price) kufikia thamani ya TZS 4,026.4 bilioni kutoka thamani ya TZS 3,758.6 bilioni mwaka 2023. Aidha, Pato la Taifa kwa bei ya soko (GDP at current price) limeongezeka na kufikia thamani ya TZS 6,572.6 bilioni mwaka 2024 kutoka thamani ya TZS 6,041.3 bilioni mwaka 2023. Kwa mujibu wa takwimu hizo uchumi wa Zanzibar umeendelea kuimarika na kufikia ukuaji wa wastani wa asilimia 7.1 mwaka 2024. **(Mchoro nambari 8)**

**Mchoro Nambari 8: Kasi ya Ukuaji wa Uchumi mwaka (2020-2024)**




***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na kijamii Zanzibar, 2025***

Kuongezeka kwa Pato la Taifa na kuimarika kwa hali ya ukuaji wa uchumi kumetokana na mambo yafuatayo:-


i. Kuimarika kwa Sekta ya Kilimo, kwa kukua na kufikia wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 2.3 mwaka 2023. Ukuaji huu umetokana na ukuaji wa Sekta ndogo ya Mazao kwa asilimia 6.4 kutoka 2.8 mwaka 2023, shughuli za Uvuvi kufikia asilimia 14.2 kutoka asilimia 8.1 mwaka 2023;

ii. Kuongezeka kwa watalii waliotembelea Zanzibar kufikia watalii 736,755 mwaka 2024 kutoka watalii 638,498 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 15.4;
iii. Kuengezeka kwa miradi mipya ya uwekezaji kwa asilimia 13.0 kufikia miradi 131 yenye thamani ya TZS 1,887.7 bilioni iliyosajiliwa mwaka 2024 kutoka miradi 114 iliyosajiliwa mwaka 2023;
iv. Kuongezeka kwa shughuli za ujenzi, sekta ndogo ya Uchimbaji Mawe na Mchanga imeongezeka kwa asilimia 17.0 mwaka 2024 kutoka asilimia 10.4 mwaka 2023;
v. Kuongezeka kwa mapato ya ndani kufikia TZS 1,279.0 bilioni mwaka 2024/25 sawa na asilimia 97.1 ya makadirio ya kipindi hicho ukilinganisha na jumla ya TZS 1,075.9 bilioni zilizokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2023/2024,

## 2.2 Pato la Mwananchi

Kuongezeka kwa Pato la Taifa Zanzibar kumepelekea kuongezeka kwa kipato cha Mwananchi mmoja mmoja. Pato la mwananchi ni kiwango kinachoonesha wastani wa fedha anazopata mwananchi kwa mwaka. Kiwango hicho hukisiwa kwa kugawanywa Pato la Taifa na idadi ya watu wanaoishi katika nchi husika. Kwa mwaka 2024 Pato la Mwananchi limeongezeka na kufikia TZS 3.2 milioni sawa na Dola za Kimarekani 1,395 kutoka TZS 3.1 milioni sawa na Dola za Kimarekani 1,241 mwaka 2023, ***(Mchoro nambari 9)*****.**

**Mchoro Nambari 9: Idadi ya Watu Pamoja na Pato la Mwananchi kwa Thamani ya (TZS) na (USD) (2020 - 2024)**





*Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na kijamii Zanzibar, 2025*

## 2.3 Mwenendo wa Mfumko wa Bei Zanzibar

Kwa mwaka 2024, kasi ya mfumko wa bei imepungua na kufikia wastani wa asilimia 5.1 kutoka wastani wa asilimia 6.9 mwaka 2023. Kupungua huko kumetokana na kupungua kwa mfumko wa bei wa bidhaa za chakula na zisizo za chakula katika soko la ndani. Kwa mwaka 2024, bidhaa za chakula zimepungua na kufikia wastani wa asilimia 8.4 kutoka wastani wa asilimia 11.1 mwaka 2023, na bidhaa zisizo za chakula zimefikia wastani wa asilimia 2.6 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 4.0 mwaka 2023, ***(Mchoro nambari 10).***

**Mchoro Nambari 10: Kasi ya Mfumko wa Bei wa Zanzibar (2020-2024)**




*Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar, 2025*

Serikali inaendelea kuchukua hatua za kupunguza na kudhibiti kasi ya mfumko wa bei na kuhakikisha upatikanaji wa huduma na bidhaa muhimu kwa wananchi. Hatua zilizochukuliwa ni kama ifuatavyo:-

i. Kupunguza ushuru na kutoa misamaha ya kodi kwa bidhaa muhimu za chakula na zisizo za chakula zinazoingizwa nchini;
ii. Kuendelea kutoa bei elekezi na kusimamia bidhaa zinazoingia nchini zikiwemo bidhaa za chakula na vifaa vya ujenzi;
iii. Kupitia Benki Kuu ya Tanzania (BoT) inaendelea kufuatilia na kuchukua hatua za kudhibiti, kushuka kwa thamani ya sarafu ya Tanzania dhidi ya sarafu nyengine duniani;
iv. Kuimarisha ufanisi wa Bandari ya Malindi kwa ununuzi wa vifaa vya kisasa kwa ajili ya kupunguza muda wa kutoa mizigo bandarini;
v. Serikali kuimarisha na kujenga maghala na mifumo ya uhifadhi wa chakula ili kuwa na uhakika wa chakula nchini (Food Security) sambamba na kuendelea kutoa na kusimamia utoaji wa ruzuku kwa pembejeo za kilimo ili kuengeza uzalishaji wa mazao ya chakula;
vi. Kuanzishwa kwa Mfuko wa Kuhimili Uchumi (Economic Stabilization Fund) ili kuimarisha uchumi na kupunguza kasi ya mfumko wa bei;


vii. Uimarishaji wa miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji maji na usafirishaji wa mazao nchini.

## 2.4 Mwenendo wa Thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Sarafu nyengine duniani

### a. Dola ya Kimarekani.

Kwa mwaka 2024 thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Kimarekani imefikia wastani wa TZS 2,603.11 kwa dola moja ikilinganishwa na TZS 2,506.0 kwa dola moja mwaka 2023. Hii ni kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya mzunguko wa fedha za kigeni. Hata hivyo, kasi ya ushukaji wa thamani imepungua kufikia asilimia 3.8 mwaka 2024 kutoka asilimia 8.4 mwaka 2023. Benki Kuu ya Tanzania inaendelea kuchukua hatua za kuweka sarafu ya Tanzania katika hali ya utulivu ili kuongeza mzunguuko wa fedha kupitia uuzaji na usafirishaji wa madini, hususani uuzaji wa dhahabu na kuimarisha sera za kifedha. Aidha, Serikali inaendelea na kuimarisha hatua kadhaa zikiwemo kuweka sera madhubuti zinazoongeza uzalishaji wa ndani ili kupunguza uagiziaji pamoja na kuimarisha vivutio vya utalii.

**Mchoro Nambari 11: Thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola moja ya Kimarekani 2020-2024**





*Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania, 2025*

## 2. 5  Mwenendo wa Uingiaji wa Watalii Zanzibar

Kutokana na Serikali kuendelea kuimarisha sekta hii kwa kutumia mbinu tofauti. Sekta hii ya Utalii imekuwa ni sekta kiongozi kwa uchumi wa Zanzibar. Mwaka 2024, idadi ya watalii waliongia kupitia kiwanja cha ndege na bandari ya Zanzibar imeongezeka kwa asilimia 15.4 na kufikia watalii 736,755 kutoka watalii 638,498 mwaka 2023. Ongezeko hilo limepelekea kuongezeka kwa thamani ya mauzo yatokanayo na uhaulishaji wa huduma (Receipts from Service Account) yenye jumla ya dola za kimarekani 1,046.5 milioni kwa mwaka ulioishia Disemba 2024, kutoka dola za kimarekani 906 milioni mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 15.4. ***(Mchoro nambari 12***).  Jitihada zilizochukuliwa na Serikali kuimarhsa utalii ni pamoja na:

i. Kuitangaza Zanzibar kimataifa kupitia mawakala wa usafirishaji watalii pamoja na Mabalozi wa Tanzania nje ya nchi kupitia maonyesho na makongamano.
ii. Kuendelea kushajihisha uwekezaji wa miradi mikubwa ya hoteli za nyota tano;
iii. Kuhamasisha masoko mapya ya utalii na kuleta ndege zao moja kwa moja (Direct Flights) Zanzibar;
iv. Kutangaza utalii wa ndani kwa kuanzisha programu za kuonesha vivutio vya ndani na kushiriki maonesho ya kimataifa na ya kikanda ikiwemo matamasha, kongamano na warsha;
v. Kuendelea kuimarika kwa hali ya amani na utulivu nchini.

**Mchoro Nambari 12: Mwenendo wa Uingiaji wa Watalii Zanzibar (2020-2024)**




***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na kijamii Zanzibar, 2025.***

Nchi ambazo zimeongoza kwa kuleta watalii wengi mwaka 2024 ni **Italia** watalii 87,202 sawa na ongezeko la wastani wa asilimia 11.8. **Ujerumani** watalii 71,283 sawa na ongezeko la asilimia 9.7 **Ufaransa** watalii 69,557 sawa na ongezeko la asilimia 9.4. P**oland** watalii 51,644 sawa na ongezeko la wastani wa asilimia 11.5. Uingereza watalii 42,244 sawa na ongezeko la asilimia 5.7 na nchi nyengine za **Afrika** watalii 40,475 sawa na ongezeko la asilimia 5.5.


## 2.6 Ukuaji wa Sekta katika Pato la Taifa

### 2.6.1 Sekta ya Huduma

Sekta ya Huduma inajumuisha sekta ndogo za Elimu, Chakula na Vinywaji, Afya, Mawasiliano, Malazi, Sanaa, Burudani na Ubunifu, na nyenginezo. Sekta hii ni miongoni mwa sekta muhimu katika kuimarisha uchumi wa Zanzibar. Sekta ya Huduma imefikia wastani wa asilimia 9.0 mwaka 2024 ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 9.9 mwaka 2023. Ukuaji huo mdogo umesababishwa na kushuka kwa ukuaji wa sekta ndogo ya Fedha na Bima ambapo imefikia wastani wa asilimia 13.7 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 54.6 mwaka 2023. Sekta ndogo ya Sanaa, Burudani na Ubunifu imekua na kufikia wastani wa asilimia 8.5 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 33.8 mwaka 2023 ukuaji huo mdogo umesababishwa na pingamizi za shughuli za Sanaa na

burudani ikiwemo katazo la kupiga mziki katika maeneo mbali mbali, uhaba wa rasilimali fedha na nyenzo za kuendeleza uzalishaji wa kazi za Sanaa, uhaba wa wataalamu wa kufanya kazi za Sanaa na burudani, uhaba wa rasilimali fedha. Sekta ndogo ya Biashara na Ukarabati imekua kwa wastani wa asilimia 11.6 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 12.6 mwaka 2023. Sekta ndogo ya Huduma za Utawala imekua kwa wastani wa asilimia 5.9 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 17.0 mwaka 2023 .

**Mchoro Nambari 13: Ukuaji wa Sekta ya Huduma katika Pato la Taifa (%) (2020 -2024)**




| | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|
| Chakula na Vinywaji | -18.9 | 7.5 | 9 | 9.8 | 16.3 |
| Chakula na malazi | -12.7 | 6.6 | 11.7 | 8.2 | 13.7 |
| Malazi | -11.3 | 6.5 | 12.3 | 7.8 | 13.2 |
| Huduma ya Fedha na Bima | 2.2 | 9.9 | 3.7 | 54.6 | 13.7 |
| Biashara na Ukarabati | 7.4 | 14.9 | 4.2 | 12.6 | 11.6 |

Chakula na Vinywaji · Chakula na malazi · Malazi · Huduma ya Fedha na Bima · Biashara na Ukarabati

Kwa upande wa sekta zilizoonesha ukuaji mzuri kwa mwaka 2024 ni sekta ndogo ya Huduma ya Chakula na Vinywaji imefikia wastani wa asilimia 16.3 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 9.8 mwaka 2023, na sekta ndogo ya Malazi na Chakula imefikia wastani wa asilimia 13.7 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 8.2 mwaka 2023 kutokana na kuongezeka kwa wageni waliotembelea Zanzibar , sekta ndogo ya Malazi imekua kwa wastani wa asilimia 13.2 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 7.8 mwaka 2023, Sekta ndogo ya Elimu imekua na kufikia wastani wa asilimia 7.0 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 3.7 mwaka 2023, sekta ndogo ya Habari na Mawasiliano kwa mwaka 2024 imekua na kufikia wastani wa asilimia 4.9 kutoka wastani wa asilimia hasi 10.8 mwaka, sekta ndogo ya Utawala wa Umma kwa mwaka 2024 imekua na kufikia wastani wa asilimia 4.0 kutoka wastani wa asilimia 2.1 mwaka 2023, sekta ndogo ya Taaluma ya Sayansi na Ufundi kwa mwaka 2024 imekua kwa wastani wa asilimia


6.6 kutoka wastani wa asilimia 3.5 mwaka 2023, sekta ndogo ya ukodishwaji wa Majengo (Real estate activities) kwa mwaka 2024 imekua na kufikia wastani wa asilimia 7.3 kutoka wastani wa asilimia 7.2 mwaka 2023.

### 2.6.2 Sekta ya Viwanda

Sekta ya Viwanda imejumuisha sekta ndogo ya Uzalishaji Viwandani, Ujenzi, Uchimbaji Mawe na Mchanga, Umeme na Gesi, na nyenginezo. Mwaka 2024, sekta ya Viwanda imekua kwa kasi ndogo na kufikia wastani wa asilimia 5.7 kutoka wastani wa asilimia 6.6 mwaka 2023. Upungufu huu mdogo umesababishwa na kupungua kwa sekta ndogo ya Umeme na Gesi, ambapo kwa mwaka 2024 sekta hiyo imekua na kufikia wastani wa asilimia 11.2 kutoka wastani wa asilimia 12.4 mwaka 2023, Sekta ndogo ya Uzalishaji Viwanda kwa mwaka 2024 imekua kwa wastani wa asilimia 3.3 kutoka wastani wa asilimia 6.9 mwaka 2023.

Hata hivyo, sekta ndogo zilizoonesha ukuaji mzuri kwa mwaka 2024 ni, Sekta ndogo ya Uchimbaji Mawe na Mchanga, kwa mwaka 2024 sekta hii imekua na kufikia wastani wa asilimia 17.0 kutoka wastani wa asilimia 10.4 mwaka 2023, hii imetokana na ukuaji wa sekta ya ujenzi . Sekta ndogo ya Usambazaji Maji Safi na Maji Taka kwa mwaka 2024 imekua kwa wastani wa asilimia 6.3 kutoka wastani wa asilimia 4.6 na sekta ndogo ya Ujenzi kwa mwaka 2024 imekua na kufikia wastani wa asilimia 6.3 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 5.5 mwaka 2023. Hii imetokana na kuwepo kwa miradi mikubwa na miradi midogo inayoendelea kujengwa.

***Mchoro Nambari 14: Ukuaji wa Sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa (2020-2024)***




| | Umeme na gesi | Ujenzi | Uchimbaji mawe na mchanga | Uzalishaji viwandani | Usambazaji maji safi na maji taka |
|---|---|---|---|---|---|
| 2020 | -2.8 | 6.5 | -6 | 6.5 | 1.9 |
| 2021 | 8 | 8.9 | 9.9 | 1.1 | 6.9 |
| 2022 | 22.3 | 10.2 | 9.1 | 8.1 | 7 |
| 2023 | 12.4 | 5.5 | 10.4 | 6.9 | 4.6 |
| 2024 | 11.2 | 6.3 | 17 | 3.3 | 6.3 |

2020 2021 2022 2023 2024

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar, 2025***

### 2.6.3 Sekta ya Kilimo

Sekta ya Kilimo inajumuisha sekta ndogo za Misitu, Ufugaji, Uvuvi na Mazao. Sekta hii ni muhimu kwa Uchumi wa Zanzibar na ndio tegemeo kubwa la upatikanaji wa chakula nchini. Kwa mwaka 2024, sekta ya Kilimo imekua kwa kasi na kufikia wastani wa asilimia 3.3 kutoka wastani wa asilimia 2.3 mwaka 2023.

Ukuaji huo umetokana na kukua kwa sekta ndogo ya Uvuvi ambapo kwa mwaka 2024 sekta hii imekua na kufikia wastani wa asilimia 14.2 kutoka wastani wa asilimia 8.1 mwaka 2023, hali hii imesababishwa na utoaji wa elimu, mitaji na utafutaji wa masoko kwa wajasiriamali wa sekta ya uvuvi, uwezeshaji na uwekezaji katika uvuvi endelevu wa mwambao na bahari kuu ikiwemo kilimo cha mwani pamoja na ufugaji wa mazao ya bahari vile vile kuimarisha usimamizi wa maeneo ya hifadhi za bahari na kuzijengea uwezo kamati za uvuvi 102 Unguja na Pemba. ili kuongeza ufanisi katika shughuli za Uvuvi na kuanzisha maeneo mapya ya ufugaji wa pweza na samaki wa miambani.

Sekta ndogo ya Mazao imekua kwa wastani wa asilimia 6.4 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 2.8 mwaka 2023 , hali hii imetokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya mizizi ikiwemo viazi vikuu na vijimbi, mazao ya jamii ya kunde, nafaka ikiwemo mpunga wa umwagiliaji na mtama pamoja na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya mboga mboga na matunda.

Sekta ambazo ukuaji wake umepungua kwa mwaka 2024 ni sekta ndogo ya Ufugaji kufikia wastani wa asilimia hasi 10.8 kutoka asilimia hasi 4.3 mwaka 2023, hii imetokana na kupungua kwa mbuzi na kuku waliochinjwa, kuzuka kwa maradhi ya wanyama yaliyopelekea kushuka kwa sekta hiyo ya Mifugo. Katika jitihada za kudhibiti magonjwa ya Wanyama, jumla ya kuku 111,572 wamechanjwa dhidi ya magonjwa ya tofauti, mbwa 5,721 wamechanjwa dhidi ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa (Rabies) na ng'ombe 9,527 wamechanjwa dhidi ya ugonjwa wa chambavu (black quarter) na kimeta (nthrax) kwa Unguja na Pemba.

Sekta ndogo ya Misitu kwa mwaka 2024 imekua kwa wastani wa asilimia 0.1 kutoka wastani wa asilimia 6.4 mwaka 2023, hali hii imetokana na kuongezeka kwa mazao ya uzalishaji ikiwemo makaa, mapau, boriti, maguzo na fito.

## 2.7 Mchango wa Sekta katika Pato la Taifa

### 2.7.1 Sekta ya Huduma

Sekta ya Huduma ina mchango mkubwa zaidi katika kukuza uchumi wa Zanzibar kwa zaidi ya miongo miwili. Mchango wa sekta hii umeongezeka kufikia wastani wa asilimia 46.8 mwaka 2024 kutoka asilimia 46.6 mwaka 2023. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa sekta ndogo ya Huduma na Malazi ambayo imechangia kwa wastani wa asilimia 16.9 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 15.3 mwaka 2023, sekta ndogo ya Malazi imechangia wastani wa asilimia 13.9 mwaka 2024 kutoka wastani wa asilimia 15.3 mwaka 2023 , sekta ndogo ya Biashara na Ukarabati kwa mwaka 2024 imechangia wastani wa asilimia 6.1 kutoka wastani wa asilimia 5.6 mwaka 2023, kwa mwaka 2024 sekta ndogo ya Huduma ya Chakula na Vinywaji imechangia kwa wastani wa asilimia 3.0 kutoka wastani wa asilimia 2.4 mwaka 2023,na sekta ndogo ya Ukodishwaji wa Majengo kwa mwaka 2024 imechangia kwa wastani wa asilimia 7.2 kama ilivyochangia mwaka 2023.

Hata hivyo, sekta ambazo mchango wake umepungua ni sekta ndogo ya Bima na Fedha kwa mwaka 2024 imechangia wastani wa asilimia 5.7 kutoka wastani wa asilimia 6.2 mwaka 2023, sekta ndogo ya Utawala, kwa mwaka 2024 imechangia kwa wastani wa asilimia 4.4 kutoka wastani wa asilimia 4.5 mwaka 2023, sekta ndogo ya Usafirishaji na Uhifadhi kwa mwaka 2024 imechangia kwa wastani wa asilimia 2.5 kutoka wastani wa asilimia 2.6 mwaka 2023, sekta ndogo ya Elimu

kwa mwaka 2024 imechangia kwa wastani wa asilimia 2.0 kutoka wastani wa asilimia 2.2 mwaka 2023. sekta ndogo ya Ustawi wa Afya ya Jamii kwa mwaka 2024 imechangia wastani wa asilimia 0.8 kutoka wastani wa asilimia 0.9 mwaka 2023 na sekta ndogo ya Habari na Mawasiliano kwa mwaka 2024 imechangia wastani wa asilimia 0.7 kutoka wastani wa asilimia 1.4 mwaka 2023.

### 2.7.2 Sekta ya Viwanda


Kwa mwaka 2024 mchango wa sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa umefikia wastani wa asilimia 20.2 kutoka wastani wa asilimia 20.8 mwaka 2023. Sekta ndogo ambazo mchango wake umepungua ni sekta ndogo ya Umeme na Gesi ambapo kwa mwaka 2024 imechangia kwa wastani wa asilimia 1.0 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 1.1 mwaka 2023. Sekta ndogo ya uzalishaji viwandani kwa mwaka 2024 imechangia wastani wa asilimia 7.8 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 8.0 mwaka 2023 pia sekta ndogo ya Ujenzi imechangia wastani wa asilimia 10.0 mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 10.4 mwaka 2023.

Hata hivyo sekta ndogo ya Uchimbaji Mawe na Mchanga kwa mwaka 2024 imechangia kwa wastani wa asilimia 0.8 kama ilivyochangia mwaka 2023 na sekta ndogo ya Usambazaji Maji Safi na Maji Taka kwa mwaka 2024 imechangia kwa wastani wa asilimia 0.5 kama ilivyochangia mwaka 2023.

### 2.7.3 Sekta ya Kilimo

Kwa mwaka 2024 mchango wa sekta ya kilimo umefikia wastani wa asilimia 24.3 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 24.9 mwaka 2023. Mchango huu umetokana na kupungua kwa sekta ndogo ya Mazao ambayo imechangia wastani wa asilimia 6.8 mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 6.9 mwaka 2023 na sekta ndogo ya Ufugaji imechangia wastani wa asilimia 10.5 mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 12.8 mwaka 2023. Hata hivyo, sekta zilizochangia vizuri ni sekta ndogo ya Misitu ambayo ilichangia wastani wa asilimia 1.2 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 1.0 mwaka 2023 na sekta ndogo ya uvuvi imechangia wastani wa asilimia 5.7 mwaka 2024 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.1 mwaka 2023. ***(Mchoro nambari 15)***

**Mchoro Nambari 15: Mchango wa Sekta katika Pato la Taifa (2020-2024)**




***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar, 2025.***

**Sekta ndogo zilizo chini ya sekta ya Kilimo mchango wake ni kama ifuatavyo:**

### 2.7.3.1 Sekta ndogo ya Mazao

Sekta hii imejumuisha Uzalishaji wa mazao ya Chakula na mazao ya Biashara. Kwa upande wa uzalishaji wa mazao ya Chakula kwa mwaka 2024 ni kama ifuatavyo:-

***a) Zao la Mpunga.***

Kilimo cha mpunga Zanzibar ni kilimo kinachotegemea mvua za msimu na umwagiliaji maji. Kwa mwaka 2024, uzalishaji wa zao la mpunga unaotegemea mvua umepungua kufikia tani 29,767.5 zenye thamani ya TZS 32,463.7 milioni kutoka tani 36,362.4 zenye thamani ya TZS 39,480.8 milioni mwaka 2023. Hali hii imetokana na kupungua kwa mabonde ya uzalishaji mpunga kwa kutumia mvua kwenda katika kilimo cha umwagiliaji maji na kukosekana kwa mvua za kutosha. Aidha, eneo la uzalishaji wa mpunga wa kutegemea mvua limepungua na kufikia ekari 24,565.4 mwaka 2024 kutoka ekari 25,591.3 mwaka 2023.

Kwa upande wa zao la mpunga kwa njia ya umwagiliaji maji, uzalishaji umeongezeka na kufikia tani 11,634.5 zenye thamani ya TZS 15,653.8 milioni mwaka 2024 ikilinganishwa na tani 7,296.5 zenye thamani ya TZS 9,830.8 milioni mwaka 2023. Hali hii imetokana na kuongezeka kwa mabonde ya uzalishaji mpunga kwa kutumia mvua kwenda katika kilimo cha umwagiliaji

maji. Aidha, eneo la uzalishaji wa mpunga kwa kutumia umwagiliaji maji limeongezeka kufikia ekari 5,749.8 mwaka 2024 kutoka ekari 3,928.2 mwaka 2023.

### *(b) Zao la Muhogo*

Mwaka 2024 uzalishaji wa zao la muhogo umepungua na kufikia tani 117,871.7zenye thamani ya TZS 95,996.4 milioni ikilinganishwa na tani 220,411.8 zenye thamani ya TZS TZS 167,920.0 milioni mwaka 2023. Hii imetokana na kupungua kwa eneo la uzalishaji na kufikia ekari 20,080.4 mwaka 2024 kutoka ekari 37,548.9 mwaka 2023, pia wakulima kushajihika na kilimo cha viazi vikuu na kuachana na kilimo cha muhogo.

### *(C) Zao la Ndizi*

Mwaka 2024 uzalishaji wa ndizi umepungua na kufikia tani 62,808.3 zenye thamani ya TZS 90,360.1 milioni kutoka tani 74,514.1 zenye thamani ya TZS 107,195.5 milioni mwaka 2023.  Hali hii imetokana na kupungua kwa eneo la uzalishaji kufikia ekari 7,303.3 mwaka 2024 kutoka ekari 8,664.4 mwaka 2023, baadhi ya wakulima kutoka kwenye kilimo cha ndizi na kujiingiza kwenye kilimo cha mboga na matunda .

### *(d) Zao la Viazi Vikuu*

Kwa mwaka 2024 uzalishaji wa zao la viazi vikuu umeongezeka na kufikia tani 14,293.4 zenye thamani ya TZS 17,019.6 milioni kutoka tani 9,241.3 zenye thamani ya TZS 11,003.3 milioni mwaka 2023. Eneo la uzalishaji limeongezeka na kufikia ekari 2,876.7 mwaka 2024 kutoka ekari 1,848.3 mwaka 2023. Hali hii imesababishwa na wakulima wanaozalisha zao la muhogo kuamua kuzalisha zao la viazi vikuu.

### *(e) Zao la Njugu Nyasa*

Kwa mwaka 2024 uzalishaji wa zao la njugu nyasa umepungua na kufikia tani 519.4 zenye thamani ya TZS 1,193.4 milioni kutoka tani 698.0 zenye thamani ya TZS 1,500.2 milioni mwaka 2023. Eneo la uzalishaji limeongezeka na kufikia ekari 1,082.1 mwaka 2024 ikilinganishwa na ekari 1,454.3 mwaka 2023. Upungufu huu umetokana na wakulima kuamua kulima zao la njugu nyasa  na kupunguza ukulima wa  zao la viazi vikuu  kwa sababu ni zao la muda mrefu.

### *(f) Mboga mboga za Majani*

Mboga za Majani hujumuisha kilimo cha mazao ya mboga mboga na matunda kama vile matikiti, tungule, matango, mabilingani, bamia, pili pili na nyenginezo za aina hiyo. Mwaka 2024, uzalishaji wa mazao hayo umepungua na kufikia tani 80,044.2 kutoka tani 87,970.6 mwaka 2023. Jumla ya ekari 23,265.0 zimetumika katika ulimaji wa mazao mwaka 2024, ikilinganishwa na ekari 21,379.8 mwaka 2023. Kupungua kwa uzalishaji huo mwaka 2024 kumechangiwa na mvua kubwa zilizoathiri mazao hayo pamoja na baadhi ya wakulima kutokufuata maelekezo kutoka kwa wataalamu wa kilimo wakati wa kupanda mazao hayo. ***(Jadweli Nambari 4.)***

**Jadweli Nambari 4: Eneo la Uzalishaji kwa ekari kwa mazao ya chakula (2020-2024)**

| Zao | Ekari | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
| Mpunga | 30,412.6 | 25,383.6 | 26,243.0 | 25,591.3 | 24,565.4 |
| Muhogo | 26,995.7 | 30,948.6 | 34,500.8 | 37,548.9 | 2,702.7 |
| Ndizi | 7,772.1 | 7,104.0 | 6,085.7 | 8,664.4 | 7,303.3 |
| Njugu nyasa | 642.3 | 775.0 | 1,300.5 | 1,454.3 | 1,082.1 |
| Viazi vikuu | 582.4 | 1,549.3 | 1,338.4 | 1,848.3 | 2,876.7 |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na kijamii Zanzibar, 2025.***

**Jadweli Nambari 5: Kiwango na Thamani ya Bidhaa za Chakula Zilizozalishwa (2020-2024) (TZS milioni)**

| Zao | 2020 | | 2021 | | 2022 | | 2023 | | 2024 | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Tani | Thamani | Tani | Thamani | Tani | Thamani | Tani | Thamani | Tani | Thamani |
| **Mpunga** | 35,886.8 | 35,229.0 | 25,511.0 | 25,369.1 | 23,683.0 | 24,069.4 | 36,362.4 | 39,480.8 | 29,767.5 | 32,463.7 |
| **Muhogo** | 158,464.9 | 108,677.8 | 181,668.0 | 126,210.5 | 202,519.5 | 143,792.0 | 220,411.8 | 167,920.0 | 117,871.7 | 95,996.4 |
| **Ndizi** | 66,839.6 | 86,559.0 | 61,094.4 | 80,147.4 | 52,337.3 | 70,169.8 | 74,514.1 | 107,195.5 | 62,808.3 | 90,360.1 |
| **Viazi vikuu** | 2,911.8 | 3,121.0 | 7,746.3 | 8,410.8 | 6,692.0 | 7,425.9 | 9,241.3 | 11,003.3 | 7,758.6 | 17,019.6 |
| **Njugu nyasa** | 308.3 | 596.0 | 372.0 | 729.0 | 624.2 | 1,250.2 | 698.0 | 1,500.2 | 519.4 | 1,193.4 |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar, 2025.***

#### 2.7.3.2 Hatua zinazochukuliwa na Serikali za Kuendeleza sekta ya Kilimo

Serikali inaendelea kuchukua hatua za kuendeleza na kukuza kilimo ili kuongeza uzalishaji na kuhakikisha upatikanaji wa chakula, hatua zilizochukuliwa ni pamoja na:-

***a) Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji***

Kukamilisha miundombinu ya umwagiliaji maji katika mabonde saba (7) yenye ukubwa wa hekta 1,354; ikiwemo bonde la Kilombero (hekta 292), Cheju A' (hekta 315) na Cheju B' (hekta 301), Kibokwa (hekta 147), Kinyasini (hekta 184), Chaani (hekta 71) na Mlemele (hekta 44). Miundombinu hii imeongeza uzalishaji tija katika uzalishaji wa mpunga kutoka wastani wa tani 3 - 5 kwa hekta hadi tani 8 - 11 kwa hekta kwa mwaka. Matarajio ni kufikia tani 15 kwa mwaka.

***b) Kuimarishwa Mfuko wa Pembejeo Mwaka 2024/2025***

Jumla ya Aina tisa (9) za mbegu mpya za mpunga zimefanyiwa majaribio katika mabonde sita (6) ya Cheju, Kibonde mzungu na Uzini kwa Unguja, na mabonde ya Kwalempona, Tungamaa na Mlemele kwa Pemba. Lengo ni kuangalia ustahamilivu wa maradhi ya umanjano yanayojuilikana kitaalamu kwa jina la 'Rice Yellow Mottle Virus Diseases - (RYMV)' na maradhi ya ukungu yanayojulikana kwa jina la 'Rice blast'. Tathmini iliyowashirikisha wakulima katika maeneo 6 (3 Unguja na 3 Pemba), kwa misimu miwili (Masika na Vuli, 2024), imeonesha kuwa kati ya aina kumi (10) za mbegu za mpunga zilizotumika, aina 3 zilifanya vizuri ambazo ni ZARIC3, ZARIC5 na IR16A-3838 zenye uzazi mkubwa na kustahamili magonjwa ya umanjano na ukungu.

***c) Kuendelezwa Huduma za Kilimo na Uhakika wa Chakula:*** Kukamilika kwa Mpango wa Mageuzi ya Sekta ya Kilimo unaokusudia kuanzisha vituo vya wakulima kila wilaya ambapo elimu na mbinu za kisasa za kilimo zitatolewa ili kuongeza ufanisi katika sekta zote za kilimo. Mpango huo unategemewa kuleta mabadiliko katika sekta ya kilimo kwa kushirikisha Mikoa, Wilaya, mashirika na kampuni binafsi katika kuendeleza shughuli za kilimo na mifugo. Lengo kuu la Mpango ni kukibadilisha kilimo cha Zanzibar kutoka kilimo cha kujikimu na kuwa kilimo cha biashara ambacho kitaweza kwenda sambamba na mahitaji ya masoko ya ndani, yakiwemo ya utalii, na nje ya nchi.

Maghala mawili (2) ya kuhifadhia chakula yaliyopo Malindi (New ferry na Malindi Njiwa wengi) yamekarabatiwa kwa lengo la kuhifadhi akiba ya chakula nchini.

***d) Kilimo cha Mazao ya Biashara kuendelezwa:*** Mazao makuu ya biashara kwa Uchumi wa Zanzibar ni karafuu na mwani. Kwa mwaka 2024, mavuno ya zao la Karafuu yamepungua na kufikia tani 1,167.4 zenye thamani ya TZS 17,250.7 milioni ikilinganishwa na tani 2,654.70 zenye thamani ya TZS 37,980.6 milioni mwaka 2023.Upungufu huu umesababishwa na kuendelea kwa kushuka msimu wa uzalishaji wa zao hilo.

Kwa upande wa mavuno ya zao la mwani mwaka 2024, ujumla uzalishaji umeongezeka na kufikia tani 19,716.0 zenye thamani ya TZS 16,144.6 milioni kutoka tani 16,652.9 zenye thamani ya TZS 16,514.8 milioni mwaka 2023. Hali hii imetokana na kuwawezesha wakulima wa mwani kwa kuwapatia nyenzo (kamba, taitai na boti) na masoko. Hivyo, kuwashajihisha wakulima kuongeza maeneo ya uzalishaji na kuboresha mbinu za kazi. Jumla ya wakulima 3,000 wamepatiwa mafunzo katika mwaka wa fedha 2024/2025, ambapo wengi wao wameanza kutumia mbinu ya kisasa na iliyoboreshwa ya double loop method, ambayo ni rafiki kwa mazingira na yenye tija zaidi na ongezeko la ushiriki wa wadau mbalimbali na Taasisi zisizo za Serikali kama Zanzibar Maisha Bora Foundation, The Nature Conservancy, Milele Foundation, IRDP Mwanza na Mavuno Lab katika kutoa vifaa, mafunzo, na ufuatiliaji wa karibu kwa wakulima wa mwani umechangia kwa kiasi kikubwa kuinua ufanisi na kuongeza ari ya uzalishaji. Aidha, Ushirikiano huu baina ya Serikali na wadau umeibua mabadiliko chanya na kuwa kichocheo kikuu cha ongezeko la uzalishaji wa mwani Zanzibar.

**Jadweli Nambari 6: Uzalishaji wa mazao ya Karafuu na Mwani (2020-2024) (TZS milioni)**

| Zao | 2020 | | 2021 | | 2022 | | 2023 | | 2024 | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Tani | Thamani | Tani | Thamani | Tani | Thamani | Tani | Thamani | Tani | Thamani |
| **Karafuu** | 3,072.1 | 42,954.2 | 7,840.8 | 102,030.8 | 4,734.1 | 63,145.9 | 2,654.70 | 37,980.6 | 1,167.4 | 17,250.7 |
| **Mwani** | 8,784.6 | 5,387.1 | 10,530.8 | 6,402.8 | 12,593.7 | 10,054.4 | 16,652.9 | 16,514.8 | 19,716.0 | 16,144.6 |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar, 2025.***

*2.7.3.3 Sekta Ndogo ya Mifugo*

Kwa mwaka 2024, jumla ya idadi ya ng'ombe waliochinjwa imeongezeka na kufikia 31,953 ikilinganishwa na ng'ombe 29,851 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 7.04. Kwa upande wa kuku waliochinjwa mwaka 2024 wamefikia jumla ya kuku 1,085,856 ikilinganishwa na idadi ya kuku 1,161,238 waliochinjwa mwaka 2023 sawa na upungufu wa asilimia hasi ya 6.49. Idadi ya mbuzi waliochinjwa mwaka 2024 imepungua na kufikia mbuzi 11,282 ikilinganishwa na mbuzi 13,704 waliochinjwa mwaka 2023 sawa na upungufu wa asilimia hasi ya 17.6. Idadi ya kondoo waliochinjwa mwaka 2024 imeongezeka na kufikia kondoo 795 ikilinganishwa na kondoo 273 waliochinjwa mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 191.2. Kwa ujumla, ongezeko hilo ni kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya nyama ya ng'ombe na nyama ya kondoo.

*2.7.3.4 Sekta Ndogo ya Uvuvi.*

Mwaka 2024, upatikanaji wa samaki umefikia tani 78,943 thamani ya TZS 618,183 milioni kutoka thamani ya TZS 569,080 milioni mwaka 2023. Sawa na asilimia 8.6. Aidha, katika kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi Wizara inaendelea na utoaji wa elimu, kuhamasisha matumizi ya mbinu bora za uvuvi ambazo ni rafiki kwa mazingira ikiwa ni pamoja na kuendeleza sekta ya ufugaji wa mazao ya baharini.

*2.7.3.5 Sekta ndogo ya Misitu*

Misitu ni rasilimali muhimu kwa uchumi Zanzibar. Serikali inaendelea na mikakati ya kutunza na kuhifadhi misitu ya asili ili kupunguza athari za tabianchi. Bidhaa za misitu zilizouzwa kwa mwaka 2024 ni kama ifuatavyo: -

Jumla ya Boriti 3,200 zenye thamani ya TZS 3,955 milioni zimeuzwa mwaka 2024 ikilinganishwa na boriti 2,053.5 zenye thamani ya TZS 225.9 milioni mwaka 2023, nguzo 2,333 zenye thamani ya TZS 389 milioni zimeuzwa mwaka 2024 ikilinganishwa na nguzo 1,091.7 zenye thamani ya TZS 54.6 milioni zilizouzwa mwaka 2023, mapau 2,455 yenye thamani ya TZS 982 milioni yameuzwa mwaka 2024 ikilinganishwa na mapau 2,084.8 yenye thamani ya TZS 225.9 milioni mwaka 2023, jumla ya mizigo ya kuni 21,002 yenye thamani ya TZS 1,050 milioni yameuzwa mwaka 2024 ikilinganishwa na mizigo ya kuni 25,909.7 yenye thamani ya TZS 113.2 milioni yaliyouzwa mwaka 2023,

fito 1,201, zenye thamani ya TZS 200 milioni zimeuzwa kwa mwaka 2024 ikilinganishwa na fito 1,091.7 zenye thamani ya TZS 5.5 milioni zilizouzwa mwaka 2023 na kwa upande wa makaa jumla ya tani 2,207 zenye thamani ya TZS 2,759 milioni zimeuzwa mwaka 2024 ikilinganishwa na tani 2,128.2 zenye thamani ya TZS 1,702.6 milioni mwaka 2023.

### *2.8 Ukuzaji Rasilimali*

Ukuzaji rasilimali nchini unachangia Ukuaji wa Uchumi, Sekta hii inachangia ongezeko la upatikanaji wa ajira, ukusanyaji wa mapato, uingiaji wa fedha za kigeni, uimarishaji wa miundombinu, ujenzi wa nyumba za biashara/mali zisizohamishika. Kwa mwaka 2024, Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) imesajili jumla ya miradi 131 yenye thamani ya TZS 1.8 trilioni kutoka miradi 114 yenye thamani ya TZS 4.6 trilioni mwaka 2023 sawa na asilimia hasi 59.5 ya thamani ya miradi hiyo. Kupungua kwa thamani ya miradi hio kumechangiwa na kupungua kwa thamani ya miradi iliyowekezwa mwaka 2024. Kwa mwaka 2024, miradi yenye thamani kubwa zaidi iliyowekezwa nchini ni miradi ya nyumba za biashara/mali zisizohamishika (Real Estate) yenye thamani ya TZS 902.6 bilioni ikifuatiwa na miradi ya hoteli na migahawa (Accommodation and Food Services) yenye thamani ya TZS 553.1 bilioni. *(Jadweli Nambari 7)*.

**Jadweli Nambari 7: Idadi ya Miradi na Thamani Iliyoidhinishwa na ZIPA Kufikia mwaka 2024**

| ORODHA YA MIRADI | 2022 | | 2023 | | 2024 | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Miradi | TZS Mil | Miradi | TZS Mil | Miradi | TZS Mil |
| Kilimo , Misitu na Uvuvi | 7 | 44,021 | 3 | 139,512 | 7 | 44,945 |
| Uzalishaji Viwandani | 8 | 34,907 | 7 | 1,030,080 | 8 | 194,144 |
| Umeme na Gesi | 3 | 1,827,227 | 5 | 1,495,920 | 1 | 747 |
| Shughuli za Usimamizi wa Taka Taka | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | - |
| Shughuli za Ujenzi | 7 | 91,644 | 1 | 24,480 | 0 | - |
| Biashara za (jumla na reja reja), pamoja na Vyombo vya Moto | 3 | 8,774 | 4 | 13,968 | 5 | 103,887 |
| Usafiri na Uhifadhi | 1 | 17,087 | 1 | 9,600 | 3 | 44,322 |
| Huduma za Malazi na Migahawa | 27 | 525,482 | 44 | 1,248,666 | 56 | 553,165 |
| Huduma za Fedha na Bima | 3 | 1,738,677 | 1 | 4,800 | 0 | - |
| Habari na Mawasiliano | 1 | 46,180 | 0 | 0 | 0 | - |
| Huduma za Ukodishaji wa Nyumba za Biashara | 25 | 193,363 | 33 | 286,909 | 37 | 902,686 |
| Shughuli za Kiutawala | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | - |
| Elimu | 1 | 693 | 0 | 0 | 1 | 249 |
| Huduma za Afya na Kazi za Kijamii | 2 | 12,700 | 2 | 6,840 | 5 | 11,579 |
| Sanaa na Michezo | 3 | 5,195 | 11 | 380,475 | 6 | 7,844 |
| Huduma Nyenginezo | 2 | 4,119 | 2 | 4,800 | 2 | 14,193 |
| **Jumla** | **93** | **4,550,069** | **114** | **4,646,050** | **131** | **1,877,760** |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar, 2025***

### 2.8.1 Nafasi za Ajira Kutoka Miradi ya Sekta Binafsi Iliyosajiliwa na Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA)

Sekta binafsi imekuwa na mchango mkubwa katika kuongeza uzalishaji wa ndani, upatikanaji wa ajira, ukusanyaji wa mapato, uingiaji wa fedha za kigeni, uimarishaji wa miundombinu na kukuza hali za uchumi kwa wananchi. Kwa mwaka 2024, miradi 131 iliyosajiliwa na ZIPA imechangia upatikanaji wa ajira mpya 4,109 kutoka ajira 6,146 mwaka 2023 sawa na asilimia hasi 33.1. Hii ni kutokana na uwepo wa uhitaji mdogo wa ajira mpya katika miradi ya mahoteli na migahawa, umeme na gesi, ujenzi, habari na mawasiliano, na nyumba za biashara.

Aidha; kwa mwaka 2024, miradi mipya iliyochangia ajira nyingi zaidi kuliko miradi mengine ni miradi ya hoteli na migahawa kufikia ajira mpya 1,834, ikifuatiwa na miradi ya uwekezaji wa nyumba za biashara (Real Estate) kufikia ajira mpya 933, ikifuatiwa na miradi ya kilimo, misitu na uvuvi kufikia ajira mpya 454. ***(Jadweli nambari 8).***

**Jadweli Nambari 8: Idadi ya Ajira Zilizopatikana kutoka Miradi ya Uwekezaji ZIPA (2020-2024)**

| MIRADI | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kilimo , Misitu na Uvuvi | 24 | 496 | 446 | 65 | 454 |
| Uzalishaji Viwandani | 179 | 2,779 | 206 | 100 | 176 |
| Umeme na Gesi | 12 | 0 | 100 | 120 | 0 |
| Shughuli za Usimamizi wa Taka Taka | 0 | 30 | 0 | 0 | 0 |
| Shughuli za Ujenzi | 0 | 520 | 383 | 70 | 0 |
| Biashara za (jumla na reja reja), pamoja na Vyombo vya Moto | 23 | 40 | 127 | 39 | 201 |
| Usafiri na Uhifadhi | 35 | 266 | 400 | 15 | 318 |
| Huduma za Malazi na Migahawa | 809 | 2,043 | 1,240 | 4,442 | 1,834 |
| Huduma za Fedha na Bima | 20 | 19 | 0 | 20 | 0 |
| Habari na Mawasiliano | 0 | 0 | 30 | 0 | 0 |
| Huduma za Ukodishaji wa Nyumba za Biashara | 50 | 234 | 903 | 1,019 | 933 |
| Shughuli za Kiutawala | 0 | 20 | 0 | 0 | 0 |
| Elimu | 80 | 215 | 20 | 0 | 10 |
| Huduma za Afya na Kazi za Kijamii | 0 | 900 | 20 | 25 | 130 |
| Sanaa na Michezo | 24 | 190 | 95 | 204 | 38 |
| Huduma Nyenginezo | 0 | 39 | 0 | 27 | 15 |
| **Jumla** | **1,256** | **7,791** | **3,970** | **6,146** | **4,109** |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar, 2025***

### 2.8.2 Mgawanyo wa Miradi ya Wazawa na Wageni Iliyosajiliwa na ZIPA

Kwa mwaka 2024, kati ya miradi 131 yenye thamani ya TZS 1.8 trilioni iliyoidhinishwa na ZIPA, jumla ya miradi 26 yenye thamani ya TZS 520.2 bilioni sawa na asilimia 20 imemilikiwa na Wazawa, na miradi 105 yenye thamani ya TZS 1.3 trilioni sawa na asilimia 80 imemilikiwa na Wageni. ***(Jadweli Nambari 9).***

**Jadweli Nambari 9: Mchanganuo wa Umiliki wa Miradi na Thamani Iliyoidhinishwa na ZIPA kufikia mwaka 2024**

| Umiliki | Idadi ya Miradi (2021) | Thamani TZS (000,000) | Idadi ya Miradi (2022) | Thamani TZS (000,000) | Idadi ya Miradi (2023) | Thamani TZS (000,000) | Idadi ya Miradi (2024) | Thamani TZS (000,000) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Wazawa | 28 | 200,584 | 35 | 216,512 | 28 | 226,075 | 26 | 520,201 |
| Wageni | 69 | 2,413,064 | 58 | 4,333,557 | 86 | 4,419,975 | 105 | 1,357,559 |
| **Jumla** | **97** | **2,613,648** | **93** | **4,550,069** | **114** | **4,646,050** | **131** | **1,877,760** |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar, 2025***

### 2.8.3 Mgawanyo wa Miradi Iliyosajiliwa na ZIPA Kulingana na Mabara

Kwa mwaka 2024, kati ya miradi 131, jumla ya miradi 47 ni kutoka Bara la Amerika, miradi 42 kutoka Bara la Australia, Miradi 36 ni kutoka Bara la Afrika, na miradi 6 kutoka Bara la Asia.

Aidha, mikakati na juhudi za uhamasishaji wa uwekezaji zinaendelea kufanyika ili kuwahamasisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuwekeza miradi yao hapa nchini kwa lengo la kuimarisha hali ya uchumi na kijamii. Miongoni mwa fursa na faida za uwekezaji ni kama ifuatavyo:

a. Kuongeza ukusanyaji wa mapato ya Serikali yanayosaidia utekelezaji wa mipango endelevu ya kiuchumi na kijamii Zanzibar;
b. Kuongeza fursa za ajira mpya hususani kwa vijana na wanawake.
c. Kuimarisha uhusiano mwema wa kidiplomasia baina ya Zanzibar na mataifa mengine yanayowekeza nchini;
d. Uingizwaji wa teknolojia za kisasa pamoja na kujifunza ujuzi kutoka kwa wataalamu wa nchi zinazowekeza Zanzibar; na
e. Upatikanaji wa huduma bora za kijamii zikiwemo afya, elimu, sanaa na michezo, huduma za watu wenye uhitaji maalumu, huduma za makaazi na miundombinu nchini.

Aidha, kushiriki katika matamasha na mikutano ya kimataifa, uhamasishaji kwa watalii wanaotembelea Zanzibar, pamoja na usambazaji wa matangazo ya biashara na uwekezaji ya ndani na nje ya nchi ni miongoni mwa mikakati inayosaidia kuwavutia wawekezaji nchini. ***(Jadweli Nambari 10).***

**Jadweli Nambari 10: Mgawanyo wa Miradi iliyosajiliwa kwa Mabara (2020-2024)**

| Mabara | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|
| **Afrika** | 15 | 38 | 37 | 38 | 36 |
| **Ulaya** | 13 | 36 | 33 | 44 | 0 |
| **Asia** | 3 | 13 | 17 | 25 | 6 |
| **Amerika** | 3 | 9 | 4 | 7 | 47 |
| **Australia** | 0 | 1 | 2 | 0 | 42 |
| **Jumla** | **34** | **97** | **93** | **114** | **131** |

*Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar, 2025*

## 2.9 Hali ya Upatikanaji wa Ajira

Kwa mwaka 2023/2024, jumla ya ajira mpya zilizosajiliwa kutoka Serikalini, Mashirika ya Serikali na Sekta Binafsi zimefikia ajira 83,430 (Wanaume 43,629 na Wanawake 39,801) ikilinganishwa na ajira 82,225 (Wanaume 43,643 na Wanawake 38,582) zilizosajiliwa mwaka 2022/2023 sawa na ongezeko la asilimia 1.4. Kuongezeka kwa ajira mpya kumetokana na kuongezeka kwa uhitaji mkubwa wa wafanyakazi katika sekta ya Elimu ambayo imechangia upatikanaji wa ajira mpya 25,017 ikifuatiwa na Sekta ya Utawala wa Umma iliyotoa ajira mpya 11,726 kwa mwaka 2023/24. ***(Jadweli Nambari 11)*.**

**Jadweli Nambari 11: Mchanganuo wa Ajira Mpya kwa Sekta na Jinsia (2018/19 – 2023/24)**

| Sekta | Jinsia | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Serikali** | Wanaume | 14,562 | 15,545 | 16,190 | 15,541 | 15,603 | 15,786 |
| | Wanawake | 17,753 | 19,888 | 22,556 | 21,648 | 22,264 | 22,498 |
| | **Jumla ndogo** | **32,315** | **35,433** | **38,746** | **37,189** | **37,867** | **38,284** |
| **Mashirika ya Serikali** | Wanaume | 4,395 | 4,306 | 4,526 | 4,522 | 4,442 | 5,224 |
| | Wanawake | 2,085 | 2,153 | 2,476 | 2,365 | 2,411 | 3,206 |
| | **Jumla ndogo** | **6,480** | **6,459** | **7,002** | **6,887** | **6,853** | **8,430** |
| **Binafsi** | Wanaume | 16,031 | 17,102 | 14,141 | 15,947 | 23,598 | 22,619 |
| | Wanawake | 7,978 | 8,101 | 6,767 | 8,609 | 13,907 | 14,097 |
| | **Jumla ndogo** | **24,009** | **25,203** | **20,908** | **24,556** | **37,505** | **36,716** |
| **Jumla** | Wanaume | 34,988 | 36,953 | 34,857 | 36,010 | 43,643 | 43,629 |
| | Wanawake | 27,816 | 30,142 | 31,799 | 32,622 | 38,582 | 39,801 |
| | **Jumla Kuu** | **62,804** | **67,095** | **66,656** | **68,632** | **82,225** | **83,430** |

*Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar, 2025*

# SURA YA TATU

## 3.0 SEKTA YA NJE

Sekta hii ina mchango mkubwa katika kukuza Pato la Taifa. Sekta hii hukuza uchumi wa nchi kwa kutoa fursa za ajira, kuongeza upatikanaji wa fedha za kigeni, uzalishaji na kuongeza thamani ya bidhaa za viwanda pamoja na kuongeza mapato ya Serikali. Zanzibar ni miongoni mwa nchi za visiwa vilivyopiga hatua kubwa ya ushindani wa kibiashara na kufanikiwa kujenga urafiki mwema wa kibiashara kwa usafirishaji na uagiziaji wa bidhaa. Miongoni mwa mataifa ambayo Zanzibar inayo mahusiano mazuri ya kibiashara ni kama vile China, India, Japan, U.A.E, Singapore, Congo na nyenginezo.


### 3.1 Usafirishaji wa Bidhaa Nje ya Nchi

Kwa mwaka 2024, usafirishaji wa bidhaa kwenda nje ya nchi umefikia thamani ya TZS 105.2 bilioni kutoka thamani ya TZS 109.2 bilioni mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 3.6. Nchi zilizoongoza katika thamani ya usafirishaji wa bidhaa kwa mwaka 2024 ni India kwa thamani ya TZS 30.9 bilioni, Singapore kwa thamani ya TZS 14.1 bilioni na Uganda kwa thamani ya TZS 10.2 bilioni. Mazao makuu ya biashara yaliyosafirishwa kutoka Zanzibar ni zao la karafuu na mwani, pamoja na mazao mengine kama majongoo bahari (sea cucumbers), viungo (spices) na dagaa.

#### 3.1.1 Usafirishaji wa Mazao Makuu ya Biashara (Karafuu na Mwani)

Kwa mwaka 2024, usafirishaji wa zao la karafuu umefikia jumla ya tani 1,974.4 zenye thamani ya TZS 30.7 bilioni kutoka tani 3,197.3 zenye thamani ya TZS 47.0 bilioni mwaka 2023 sawa na upungufu wa thamani kwa asilimia 34.7. Kupungua kwa usafirishaji wa zao la karafuu kumechangiwa na mabadiliko ya msimu wa zao hilo.

**Mchoro Namba 16: Tani na Thamani ya Usafirishaji wa Zao la Karafuu 2020-2024 TZS Mil**





| | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|
| Thamani TZS Mil | 38,370.90 | 115,358.70 | 118,287.30 | 47,081.10 | 30,737.30 |
| Tani | 3,506.80 | 6,775.50 | 6,452.80 | 3,197.30 | 1,974.40 |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar, 2025***

Kwa mwaka 2024, usafirishaji wa zao la mwani umefikia tani 7,089.5 zenye thamani ya TZS 10.7 bilioni kutoka tani 11,737.3 zenye thamani ya TZS 19.2 bilioni mwaka 2023 sawa na upungufu wa thamani kwa asilimia 44.1. Hii imechangiwa na mabadiliko ya thamani ya sarafu ya Dola ya Kimarekani mwaka 2024 jambo lililosababisha kwa baadhi ya Kampuni kupunguza usafirishaji wa mwani (kwa kiwango kikubwa) kuepuka hasara inayoweza kutokea katika biashara hiyo. Aidha, ushindani wa uzalishaji wa zao la mwani kwa baadhi ya nchi kama Indonesia na China kumechangia kupungua kwa usafirishaji wa mwani. ***(Mchoro Nambari 17)***.

**Mchoro Nambari 17: Tani na Thamani ya Usafirishaji wa Zao la Mwani 2020-2024 TZS Mil.**




| | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|
| Thamani TZS Mil | 11,700.10 | 11,960.70 | 16,010.20 | 19,233.20 | 10,738.70 |
| Tani | 11,382.60 | 12,611.10 | 13,972.50 | 11,737.30 | 7,089.50 |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar, 2025***

### 3.2 Uagiziaji wa Bidhaa Kutoka Nje ya Nchi

Thamani ya Uagiziaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi imefikia TZS 1.6 trilioni mwaka 2024 kutoka thamani ya TZS 1.5 trilioni mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 9.8. Kwa mwaka 2024, Zanzibar imefanya uagiziaji na nchi za Falme za Kiarabu (U.A.E) wenye thamani ya TZS 829.7 bilioni, ikifuatiwa na nchi ya China wenye thamani ya TZS 203.2 bilioni, India wenye thamani ya TZS 103.8 bilioni, Pakistani wenye thamani ya TZS 74.6 bilioni, na nchi nyenginezo.

Bidhaa zilizoingia nchini ni pamoja na mashine, vifaa vya viwandani na zana za kilimo (Capital Goods) zenye thamani ya TZS 377.9 bilioni. Aidha, bidhaa za nishati ya mafuta pamoja na mali ghafi za viwandani (Intermediate Goods) zenye thamani ya TZS 871.2 bilioni, na bidhaa za matumizi ya kila siku kama vyakula na nguo (Consumer Goods) zenye thamani ya TZS 400.0 bilioni.

Uagiziaji wa bidhaa za chakula: **Mchele** umefikia tani 65,788 kwa mwaka 2024 kutoka tani 133,727 mwaka 2023, kupungua kwa uagiziaji wa mchele nchini kumetokana na uhaulishwaji mkubwa wa mchele unaolimwa Tanzania Bara. **Sukari** uagiziaji umefikia tani 43,662 mwaka 2024 ikilinganishwa na tani 36,910 za mwaka 2023; na unga wa **Ngano** umefikia tani 29,464 mwaka 2024 kutoka tani 4,070 mwaka 2023 kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa hizo hapa nchini. Kwa upande wa uagiziaji wa bidhaa zisizo za chakula: **Nishati na gesi** zimeongezeka kwa mwaka 2024; mafuta ya petroli yamefikia lita 113,284,726 kutoka lita 110,852,126 mwaka 2023, dizeli imefikia lita 75,197,228 mwaka 2024 kutoka lita 71,759,929 mwaka 2023. Uagiziaji wa **mafuta ya taa** umefikia lita 1,958,918 mwaka 2024 kutoka lita 2,876,641 mwaka 2023 kutokana na kupungua kwa utumiaji wake hapa nchini, uhamasishaji na utumiaji mkubwa wa nishati za umeme na gesi salama za kupikia zinaendelea kupunguza uhitaji wa matumizi ya mafuta ya taa visiwani Zanzibar. ***(Jadweli Nambari 12).***

**Jadweli Nambari 12: Uagiziaji wa Bidhaa Kuu za Chakula kwa Mwaka (2020 – 2024)**


| Tani | | | |
|---|---|---|---|
| **Mwaka** | **Mchele** | **Sukari** | **Unga wa Ngano** |
| **2020** | 104,804 | 34,299 | 7,967 |
| **2021** | 36,161 | 26,630 | 5,424 |
| **2022** | 81,460 | 32,122 | 38,885 |
| **2023** | 133,727 | 36,910 | 4,070 |
| **2024** | 65,788 | 43,662 | 29,464 |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar, (OCGS) 2025***

## 3.3 Urari wa Biashara

Kwa mwaka 2024, nakisi ya biashara imeongezeka kufikia thamani ya TZS 1.5 trilioni kutoka thamani ya TZS 1.3 trilioni mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 10.8, hali hii ni kutokana na kuongezeka kwa uagiziaji mkubwa wa bidhaa kutoka nje ya nchi. Aidha, usafirishaji wa mazao makuu ya biashara ambayo ni karafuu na mwani, pamoja na majongoo bahari, dagaa kavu na bidhaa za viungo (spices) zimesaidia kupunguza nakisi hiyo ambayo ingeweza kuwa kubwa zaidi endapo hakukuwa na usafirishaji wa mazao hayo. Ushajihishaji kwa wananchi wetu kukuza na kuimarisha uzalishaji wa ndani pamoja na kununua zaidi bidhaa zinazozalishwa nchini badala ya zile zinazozalishwa nje ya nchi zitasaidia katika kupunguza nakisi ya biashara nchini. ***(Mchoro Nambari 18).***

**Mchoro Nambari 18: Unaonesha Thamani ya Usafirishaji, Uagiziaji na Urari wa Biashara kwa mwaka (2020-2024).**





***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar, 2025***

### 3.4 Uhaulishaji wa Bidhaa baina ya Zanzibar na Tanzania Bara

Kwa mwaka 2024, uhaulishaji wa bidhaa kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara umeongezeka kufikia thamani ya TZS 280.8 bilioni kutoka thamani ya TZS 159.7 bilioni mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 75.8. Aidha, uhaulishaji wa bidhaa kutoka Tanzania Bara kuja Zanzibar pia umeongezeka kufikia thamani ya TZS 549.6 bilioni mwaka 2024 kutoka thamani ya TZS 431.5 bilioni mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 27.3. Kuimarika kwa masoko, uzalishaji na upatikanaji wa bidhaa muhimu za chakula na zisizo za chakula kwa nchi hizi mbili, kumechangia ukuaji wa uhaulishaji baina ya Zanzibar na Bara. Miongoni mwa bidhaa zilizohaulishwa kwenda Tanzania Bara ni Mafuta ya kupikia, Vitenge, Mwani, Majongoo bahari, Viungo (spices); na kwa bidhaa zilizohaulishwa kuja Zanzibar ni Mchele, Chakula cha Mifugo, Chokaa, Vitunguu Maji na Thomu, Tangawizi, Mbatata, Keroti, Vinywaji vyenye Vileo, Unga wa Ngano, Mbao, Samani (furnitures), Mbolea, Magodoro, Mkaa, na vyenginevyo, ***(Mchoro Nambari 19)***.

**Mchoro Nambari 19: Uhaulishaji wa bidhaa baina ya Zanzibar na Tanzania Bara (2020-2024), TZS Mil.**




*Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar, 2025*

## SURA YA NNE

## 5.0 SEKTA YA FEDHA

Sekta ya Fedha inajumuisha huduma za Mabenki, Bima, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Soko la Mitaji na Dhamana, Mifumo ya malipo na huduma ndogo ndogo za fedha (Microfinance). Sekta hii ni sekta muhimu katika ukuaji wa uchumi wa nchi na kupunguza umaskini. Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango kupitia Idara ya Sera za Kodi na Fedha ina jukumu la kusimamia maendeleo ya Sekta ya Fedha Zanzibar na kuhakikisha Sekta hii inakua imara, endelevu na yenye kusaidia katika kukuza uchumi wa nchi na kupunguza umasikini wa kipato kwa wananchi. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2024/2025 Utekelezaji wa Sekta ya Fedha ulikua kama ifuatavyo;

### 5.1 Sekta Ndogo ya Benki

Sekta ndogo ya benki ni moja kati ya sekta muhimu katika ukuaji wa uchumi wa nchi. Sekta hii imejumuisha Benki Kuu ya Tanzania ikiwa ndio msimamizi mkuu wa shughuli za fedha nchini; benki za biashara; mawakala wa huduma za kibenki na mitandao ya simu. Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025, Julai 2024 - Machi 2025, sekta hii iliendelea kuimarika na hivyo kuchangia katika ukuaji wa Pato la Taifa la Zanzibar kwa wastani wa asilimia 4.1.

#### 5.1.1 Benki Kuu ya Tanzania (BoT)

Benki Kuu ya Tanzania ina jukumu la kuandaa, kusimamia na kutathmini utekelezaji wa Sera ya Fedha inayolenga kudhibiti mfumko wa bei na kujenga mfumo imara wa sekta ya fedha inayozingatia ukuaji endelevu wa uchumi. Benki Kuu pia, husimamia mabenki na taasisi za fedha, kutoa ushauri kwa Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) katika masuala ya uchumi na fedha, kusimamia na kudhibiti mifumo ya malipo nchini, kutengeneza na kusambaza noti na sarafu, kuhifadhi akiba ya fedha za kigeni na kutoa huduma za kibenki kwa Serikali na benki za biashara. Katika kipindi cha Julai 2024 - Machi 2025, Benki Kuu imeendelea kutekeleza majukumu yaliyoanishwa hapo juu kama ifuatavyo: -

##### 5.1.1.1 Kuandaa na Kutekeleza Sera ya Fedha

Utekelezaji wa Sera ya Fedha kwa mwaka 2024/25 umekuwa wa mafanikio makubwa kwani hadi kufikia robo ya tatu, Benki Kuu iliendelea kutekeleza Sera ya Fedha kwa kutumia mfumo wa riba ambapo kutokana na mafanikio

yaliyopatikana Benki Kuu iliamua kuendelea kutumia riba ya asilimia sita (6) mpaka Disemba, 2024. Mabadiliko ya utekelezaji wa Sera ya Fedha kwa kutumia mfumo wa riba badala ya ujazi wa fedha umechangia kupungua kwa mfumko wa bei hadi kufikia asilimia 5.1 katika kipindi cha April 2024 hadi Machi 2025 kutoka asilimia 6.2 kipindi kama hicho mwaka 2023/24.

Benki Kuu ilitekeleza Sera ya fedha kwa lengo la kudumisha kiwango cha riba cha mikopo kati ya mabenki kwa muda wa siku saba (7) ndani ya kiwango cha asilimia nne (4) hadi nane (8), kulingana na kiwango cha riba cha Benki Kuu kilichowekwa kuwa asilimia sita (6) kwa robo ya mwaka iliyoishia Machi 2025. Utekelezaji wa Sera ya fedha ulifanikiwa kuimarisha matarajio ya mfumko wa bei chini ya lengo la muda wa kati la asilimia tano (5). Ujazi wa fedha katika uchumi uliendelea kuwa wa kutosha, huku kiwango cha riba cha siku saba (7) kati ya mabenki kikisalia ndani ya mpaka wa asilimia nne (4) hadi nane (8).

#### 5.1.1.2 Kusambaza Noti na Sarafu

Benki Kuu imeendelea kutimiza jukumu lake la kusambaza fedha (noti na sarafu) ili kutosheleza mahitaji ya uchumi bila kusababisha mabadiliko ya kasi ya upandaji wa bei za bidhaa na huduma (yaani mfumko wa bei). Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Benki Kuu ilisambaza jumla ya TZS 1,395.00 bilioni, kati ya hizo TZS 1,301.77 bilioni zilisambazwa kupitia Ofisi ya Unguja na TZS 93.23 bilioni kupitia Kituo cha Pemba, ***(Jadweli nambari 13).***

**Jadweli Nambari 13: Fedha (Shilingi) Zilizosambazwa Zanzibar: Julai 2023 - Machi 2024, *TZS***

| | Kituo cha Unguja | Kituo cha Pemba | Jumla |
|---|---|---|---|
| Noti | 1,289.2 | 93.2 | 1,382.4 |
| Sarafu | 12.6 | 0.0 | 12.6 |
| **Jumla** | **1,301.8** | **93.2** | **1,395.0** |

***Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania***

#### 5.1.1.3 Nakisi ya Fedha za Kigeni

#### Fedha za Kigeni za Nchi

Benki Kuu ni mtunzaji wa hazina ya fedha za kigeni kwa kuzingatia malengo ya usalama, ukwasi, faida na usimamizi wa madeni ya nje. Hadi kufikia Machi 2025, akiba ya fedha za kigeni iliongezeka hadi kufikia dola milioni 5,693.2,

ikilinganishwa na dola milioni 5,327.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Hifadhi itatosheleza kuagiza bidhaa kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi 4.6 ikilinganishwa na makadirio ya miezi 4.0 kwa nchi ya Tanzania na makadirio ya miezi 4.5 kwa nchi za Afrika Mashariki.

#### 5.1.1.4 Utoaji wa Huduma za Kibenki kwa Serikali na Mabenki

Huduma za kibenki zinazotolewa ni kutunza fedha za Serikali na taasisi zake pamoja na kufanya malipo kwa Serikali. Kutoa mikopo ya muda mfupi kwa Serikali kwa kutumia huduma yake ya overdraft. Kutunza Amana za benki za biashara hapa nchini zikiwemo amana za kisheria (statutory minimum reserve requirement) zinazotakiwa kuwekwa Benki Kuu pamoja na kiasi cha Amana kinachohitajika kwa ajili ya malipo au matumizi ya kila siku (Clearing balances). Benki Kuu inaendelea kuwa mhifadhi na mlipaji mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Taasisi za Jamhuri ya Muungano zilizopo Zanzibar pamoja na kutoa huduma za kibenki kwa Benki za Biashara zilizopo Zanzibar.

### 5.1.2 Huduma za Kibenki

Huduma za kibenki Zanzibar zinaendelea kuimarika zikichagizwa zaidi na kukua kwa teknolojia, utumiaji wa njia mbadala wa kufikisha huduma kwa wateja ikiwa ni pamoja na Mawakala wa benki (agent banking). Hadi kufikia Machi 2025, idadi ya benki zilizokuwa zikitoa huduma zilikuwa 14, huku idadi ya matawi ya benki yamefikia 43, ambapo Pemba ilikuwa na matawi 10 na Unguja ikiwa na matawi 33 . Idadi ya ATM zikiwa 118. Idadi ya Mawakala wa benki wakiwa 6,379 wakijumuisha mawakala 2,999 waliokuwa Pemba na mawakala 3,380 waliopo Unguja. Maduka ya kubadili fedha za kigeni (Bureau de Change) yalikuwa nane (8), yenye matawi 28. Benki zote za biashara zilitoa huduma ya kubadili fedha za kigeni.

### 5.1.3 Amana

Hadi kufikia Disemba, 2024, Amana katika benki ziliongezeka hadi kufikia shilingi 3,021.2 bilioni kutoka shilingi 2,183.9 bilioni kwa kipindi kama hicho mwaka uliopita . PBZ ilikuwa na asilimia 53.3 ya Amana zote; ikifuatiwa na benki za NMB, CRDB, NBC, na ABSA (BARCLAYS) ambazo kwa pamoja zilizochangia asilimia 33.2 ya amana zote.

**Jadweli Nambari 14: Amana katika benki** *TZS Bilioni*

| | Amana Zinazohitajika Muda wowote (Demand Deposits) | Amana za Muda Maalum (Time Deposit) | Amana za Akiba (Savings) | Amana Nyinginezo (Others) | Jumla ya Amana zote |
|---|---|---|---|---|---|
| Dec-21 | 652.3 | 174.5 | 334.2 | 47.4 | 1,208.4 |
| Mar-22 | 836.5 | 248.1 | 428.7 | 51.4 | 1,564.8 |
| Jun-22 | 756.2 | 268.9 | 354.4 | 53.3 | 1,432.6 |
| Sept-22 | 267.6 | 337.9 | 338.0 | 85.5 | 1,029.0 |
| Dec-22 | 306.2 | 270.4 | 375.6 | 643.8 | 1,596.0 |
| Mar-23 | 973.4 | 327.5 | 396.0 | 41.5 | 1,738.4 |
| Jun-23 | 491.2 | 265.3 | 380.7 | 842.8 | 1,980.1 |
| Sept-23 | 1,233.4 | 484.6 | 390.5 | 75.5 | 2,184.0 |
| Dec-23 | 765.6 | 597.1 | 534.7 | 1,099.7 | 2,997.1 |
| Mar-24 | 1,256.2 | 780.8 | 652.0 | 170.8 | 2,859.7 |
| Jun-24 | 1,359.3 | 794.2 | 457.2 | 182.8 | 2,793.5 |
| Sept-24 | 2,101.9 | 602.5 | 544.3 | 1.3 | 3,250.0 |
| Dec-24 | 1,509.5 | 786.4 | 544.1 | 181.2 | 3,021.2 |

**Chanzo: Benki za Biashara**

### 5.1.4 Mikopo

Mikopo ni sehemu kubwa ya rasilimali za benki ambazo zinatokana na Amana za wateja. Kwa kipindi cha Julai 2024 - Machi 2025 thamani ya mikopo iliyotolewa imepungua kwa asilimia moja (1) na kufikia shilingi 2,171.3 bilioni. Mikopo binafsi (ambayo zaidi inalenga wafanyakazi wa muda mrefu au wenye mikataba) ilichukua asilimia 41.8 ya mikopo yote iliyotolewa katika kipindi cha Disemba 2024, ikifuatiwa na sekta za kilimo, biashara, utalii na Sekta nyingine ambazo kwa pamoja zilipata asilimia 40.5 ya Mikopo iliyotolewa. Aidha, mikopo inayotolewa katika Sekta ya utalii iliongezeka kwa asilimia 51.2 hadi kufikia TZS 119.03 bilioni iliyotolewa Disemba 2024.

**Jadweli Nambari 15: Sekta zilizonufaika na mikopo,** *TZS (Milioni)*

| Sekta | 2023/2024 Dec-23 | 2024/2025 Dec-24 | % Mgawanyo 2024/2025 |
|---|---|---|---|
| Mikopo Binafsi | 844.5 | 907.1 | 41.8 |
| Nyinginezo | 546.5 | 428.4 | 19.7 |
| Kilimo | 341.2 | 368.4 | 17.0 |
| Biashara | 196.9 | 197.1 | 9.1 |
| Utalii | 162.1 | 119.0 | 5.5 |
| Mawasiliano | 19.8 | 56.1 | 2.6 |
| Viwandani | 35.3 | 48.1 | 2.2 |
| Ujenzi | 35.7 | 45.4 | 2.1 |
| Taasisi za Fedha | 6.4 | 1.7 | 0.1 |
| **Jumla** | **2188.4** | **2171.3** | |

***Chanzo: Benki za Biashara***

### 5.1.5 Mwenendo wa Riba za Benki

Viwango vya riba za mikopo inayotolewa na benki havikuwa na mabadiliko katika mwaka 2024/25. Wastani wa riba za jumla za mikopo ulikuwa asilimia 15.5 sawa na asilimia 15.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Aidha, wastani wa riba za Amana uliongezeka na kufikia asilimia 2.90 kutoka asilimia 2.29 kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Kuongezeka kwa riba za mikopo ni kutoka na maboresho ya sekta ya fedha, ambapo Benki Kuu imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kwa lengo la kufanya maboresho yatakayopelekea kuendelea kupungua kwa riba za mikopo na kuongeza tija katika uzalishaji mali nchini.

**Jedweli Nambari 16: Mwenendo wa Riba za Benki kwa mwezi, July 2024 – Machi 2025**


***Asilimia***

| | Jul-24 | Aug-24 | Sept-24 | Oct-24 | Nov-24 | Dec-24 | Jan-25 | Feb-25 | Mar-25 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Riba ya Amana( Savings deposit rate) | 2.9 | 3.0 | 2.8 | 2.8 | 2.7 | 2.8 | 3.0 | 3.0 | 2.9 |
| Riba ya Jumla ya amana ya Muda Maalum( Overall time deposit) | 8.1 | 8.0 | 8.2 | 8.3 | 8.2 | 8.3 | 8.3 | 8.1 | 8.0 |
| Riba ya amana ya mwaka (I Year deposit rate) | 9.0 | 8.8 | 9.1 | 10.4 | 9.6 | 9.6 | 10.1 | 9.5 | 8.1 |
| Riba ya amana ya maelewano( Negotiated deposit rate) | 10.0 | 10.1 | 9.9 | 10.3 | 10.1 | 10.4 | 11.8 | 11.4 | 10.3 |
| Riba ya Jumla ya Mikopo(Overall lending rate) | 15.3 | 15.3 | 15.5 | 15.7 | 15.7 | 15.7 | 15.7 | 15.1 | 15.5 |
| Riba ya mikopo ya muda mfupi hadi mwaka 1 (Short term lending rate up to 1 year) | 15.7 | 15.5 | 15.7 | 16.1 | 15.6 | 15.7 | 15.7 | 15.8 | 15.8 |
| Riba ya mikopo ya maelewano (Negotiated lendig rate) | 12.8 | 12.8 | 12.9 | 12.9 | 12.8 | 12.8 | 12.8 | 13.4 | 12.9 |
| Riba ya dhamana za serikali za siku 364 (364 T Bills yield) | 8.8 | 10.6 | 11.0 | 11.7 | 12.8 | 13.0 | 12.6 | 12.0 | 10.1 |
| Riba za dhamana za serikali kwa ujumla(Overall treasure bills) | 8.8 | 10.6 | 10.9 | 11.6 | 12.7 | 13.0 | 12.5 | 11.9 | 10.1 |
| Riba ya siku moja baina ya mabenki (Overnight interbank rates) | 6.8 | 7.6 | 7.9 | 7.7 | 7.7 | 7.1 | 7.7 | 7.9 | 7.9 |

***Chanzo: Benki za Biashara***

**Mchoro Nambari 21: Wastani wa riba za Benki kwa mwezi, Julai 2024 - Machi 2025**

*Asilimia*




***Chanzo: Benki za Biashara***

### 5.1.6 Wakala wa Huduma za Kibenki

Hadi kufikia mwezi Machi 2025, idadi ya mawakala wa benki (agent banking) ilikuwa 6,379 sawa na asilimia 4.4 ya mawakala wote Tanzania. Pemba mawakala 2,999 na Unguja mawakala 3,380. Thamani ya miamala iliongezeka zaidi kwenye kuweka na kutoa. Kwa upande wa kuweka thamani ya miamala iliongezeka hadi kufikia TZS 921.04 bilioni ukilinganisha na TZS 761.24 bilioni mwaka 2023/24. Na kwa utoaji, thamani ya miamala iliongezeka hadi kufikia TZS 370.8 bilioni kutoka TZS 277.32 billion mwaka 2023/24. ***(Jadweli nambari 17).***

**Jadweli Nambari 17: Wakala wa Benki, Zanzibar**

| KUWEKA | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Disemba, 2023 | | | | Disemba, 2024 | |
| | Idadi ya Mawakala | Idadi ya Miamala | Thamani ya Miamala | Idadi ya Mawakala | Idadi ya Miamala | Thamani ya Miamala |
| **Zanzibar** | 4,503 | 908,669 | 761,241,708,302.4 | 6,379 | 1,216,022 | 921,039,682,231.8 |
| **Jumla** | 4,503 | 908,669 | 761,241,708,302.4 | 6,379 | 1,216,022 | 921,039,682,231.8 |
| **KUTOA** | | | | | | |
| | Disemba, 2023 | | | | Disemba, 2024 | |
| | Idadi ya Mawakala | Idadi ya Miamala | Thamani ya Miamala | Idadi ya Mawakala | Idadi ya Miamala | Thamani ya Miamala |
| **Zanzibar** | 4,503 | 702,445 | 277,319,020,037.6 | 6,379 | 885,110 | 370,783,743,011.7 |
| **Jumla** | 4,503 | 702,445 | 277,319,020,037.6 | 6,379 | 885,110 | 370,783,743,011.7 |

***Chanzo****: Benki Kuu ya Tanzania*

### 5.1.7 Mwenendo wa Viwango vya Ubadilishaji wa Fedha za Kigeni (Exchange Rate Movement)

Kwa kipindi cha Machi 25, shilingi ya Tanzania iliendelea kuwa tulivu dhidi ya dola ya Marekani, ikibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,624.70 kwa dola ya Marekani, ikilinganishwa na shilingi 2,544.54 kwa dola ya Marekani kwa mwezi uliopita na Shilingi 2,560.29 katika kipindi kama hicho mwaka 24, sawa na kupungua kwa thamani ya asilimia 2.5 kwa shilingi ya Tanzania ikilinginishwa na dola ya Marekani. Aidha, Shilingi inaendelea kuimarika kutokana na uwepo wa akiba ya kutosha ya fedha za kigeni, mfumko mdogo wa bei nchini ukilinganishwa na nchi washirika wa kibiashara, na nakisi ndogo ya urari wa bidhaa, huduma na uhamisho wa mali nchi za nje. Hali hii pia ilichangiwa na hatua zilizochukuliwa katika kuongeza utulivu katika soko la fedha za kigeni nchini.

### 5.2 Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ)

#### 5.2.1 Utekelezaji wa Bajeti Julai 2024 hadi Machi 2025.

Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, mapato halisi ya PBZ yameendelea kuongezeka kufikia TZS 161,534 milioni ikiwa ni sawa na asilimia 93 ya mapato yaliokadiriwa yaTZS 173,439 milioni. Ongezeko hilo limesababishwa na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na riba za mikopo, faida kwa mikopo ya huduma za benki ya kiislam na mapato yanayotokana na huduma za kielektroniki (Huduma za ATM, wakala, mobile banking, PBZ app, internet banking). Mapato hayo ni ongezeko la asilimia 23 ukilinganisha na mapato ya TZS 131,615 milioni katika kipindi kama hicho cha Julai 2023 hadi Machi 2024.

Matumizi ya benki kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 yalifikia TZS. 88,725 milioni ambayo ni asilimia 12 pungufu ya makadirio ya bajeti ya TZS 100,671 milioni. Upungufu huo umetokana na kutomalizika kwa baadhi ya miradi kama vile ujenzi wa tawi la Arusha na kituo cha kutolea huduma cha Konde- Pemba ambayo matumizi yake yalipangwa yaanze katika kipindi hicho. Miradi itamalizika ndani ya mwaka 2025. Matumizi hayo ni ongezeko la asilimia 64 ya TZS 53,947 milioni ya matumizi katika kipindi kama hicho cha Julai 2023 hadi Machi 2024.

Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, faida halisi ya benki ilifikia TZS 72,809 milioni ikiwa ni sawa na asilimia 100 na kufikia lengo la kiwango kilichokadiriwa cha TZS 72,768 milioni.

Hadi kufikia Machi 2025 benki ilikuwa na jumla ya rasilimali za TZS 2,602,807 Milioni ikiwa ni sawa na asilimia 83 ya kiwango kilichokadiriwa cha TZS 3,148,954 milion. Hivyo kuifanya PBZ kuendelea kuwa miongoni mwa benki kubwa hapa Tanzania. Amana za wateja hadi Machi 2025 zilifikia TZS 2,083,277 milioni ikiwa ni sawa na asilimia 80 ya kiwango kilichokadiriwa cha TZS 2,612,888 milioni. Hadi kufikia Machi 2025, mikopo kutoka katika sekta mbalimbali imefikia TZS 1,222 bilioni ambayo ni sawa na asilimia 78 ya makadirio ya TZS 1,566 bilioni. Mtaji wa benki hadi mwezi wa Machi 2025 umefikia TZS 236 bilioni ikiwa ni asilimia 84 ya kiwango kilichokadiriwa cha TZS 281 bilioni. Mtaji wa benki umekua kwa asilimia 30 kutoka TZS 181,394 milioni kwa Machi 2024. PBZ imeendelea kuwa miongoni mwa walipa kodi wakubwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Katika kipindi cha miezi tisa cha Julai 2024 hadi Machi 2025, benki imefanikiwa kulipa jumla ya kodi ya TZS

34 bilioni kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA). Ulipaji huo ni ongezeko la asilimia 14 ukilinganisha na kiwango cha TZS 30 bilioni kilicholipwa katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024.

Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, PBZ ilifanikiwa kulipa Gawio kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar la TZS 7 Bilioni ikiwa ni gawio linalotokana na faida iliyopatikana mwaka 2023.

Benki ya Watu wa Zanzibar inaendelea kusogeza mitandao yake ya utoaji huduma huko Tanzania Bara na katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, PBZ imefanikiwa kufungua matawi matatu (3) katika mikoa ya Morogoro, Mbeya na Mwanza na hivyo kuifanya PBZ kuwa na jumla ya matawi 20 hadi Machi 2025. Vilevile benki imefanikiwa kufungua kituo kimoja cha kutolea huduma cha Kinyasini.

Aidha, katika kipindi cha miezi tisa (9), mawakala 390 waliongezeka na hivyo kufanya mawakala wa PBZ hadi Machi 2025 kufikia 1,627. PBZ imeweza kuweka mashine za kutolea fedha (ATM) mpya nne (4) na kufanya idadi ya ATM zote za PBZ hadi Machi 2025 kufikia 49.

PBZ ndani ya kipindi hicho cha miezi tisa (9) imefanikiwa kuboresha mfumo wa benki kiganjani wa PBZ APP ambayo imeweza kumrahisishia mteja kupata huduma zaidi kama vile: kulipa malipo ya serikali, kununua vifurushi vya ving'amuzi vya televisheni, kulipia umeme (Luku na Tukuza), kulipia bili ya maji ya ZAWA na DAWASA, kulipia usafiri wa SGR, kuwekeza katika hati fungani ya SUKUK na nyenginezo.

Benki ya Watu wa Zanzibar imepewa kazi ya uwakala na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kupitia Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kutoa Hati Fungani inayofuata misingi ya Sheria za kiislam inayoitwa "SUKUK" . Fedha zilizopatikana kupitia Hati Fungani hizo zitaiwezesha Serikali kuwekeza katika miradi ya Maendeleo ya Zanzibar.

**5.2.3 Malengo ya PBZ kwa Mwaka 2025**.

Katika kutekeleza bajeti yake ya mwaka 2025, PBZ inakadiria kufikia viwango vifuatavyo:

a. Mapato ya benki yanakadiriwa kuongezeka kwa asilimia 38 kutoka TZS 201,368 milioni na kufikia TZS 277,196 milioni. Ongezeko hilo litatokana na ongezeko la riba kwa kuongeza utoaji wa mikopo, pia

kupitia mapato yasiyo ya riba ya faida ya uwezeshaji wa huduma za benki ya kiislam, na mapato yatokanayo na huduma za kielektroniki;

b. Matumizi yanakadiriwa kuongezeka kwa asilimia 43 kutoka TZS 109,282 milioni na kufikia TZS 156,738 milioni, Ongezeko hilo litatokana na gharama mbalimbali za matawi mapya na vituo vipya vya kutolea huduma, pamoja na matumizi ya kuboresha mifumo mbalimbali ya kibenki;
c. Faida ya benki inakadiriwa kuongezeka kwa asilimia 31 kutoka TZS 92,086 milioni na kufikia faida ya TZS 120,458 milioni;
d. Raslimali za benki zinakadiriwa kuongezeka kwa asilimia 26 kutoka TZS 2,505,361 milioni na kufikia TZS 3,150,543 milioni;
e. Amana za wateja zinakadiriwa kuongezeka kwa asilimia 34 kutoka TZS 1,952,671 milioni na kufikia TZS 2,612,888 milioni. Ongezeko hilo litatokana na wateja wapya katika matawi mapya yanayofunguliwa huko Tanzania Bara;
f. Jumla ya mikopo ya kawaida na inayofuata sharia ya kiislam imekadiriwa kukuwa kwa asilimia 29 kutoka TZS 1,212,895 milioni na kufikia TZS 1,566,157;
g. Mtaji wa benki unakadiriwa kukuwa na utafikia TZS 307,419 milioni ikiwani sawa na ongezeko la asilimia 24.

### 5.2.2 Miradi ya PBZ kwa Mwaka 2025.

a. PBZ inaendelea na ujenzi wa matawi katika mikoa ya Arusha, Tanga na Ubungo katika mkoa wa Dar es salaam.
b. PBZ inaendelea kufanya ujenzi wa vituo vya kutolea huduma (service centres) katika maeneo ya Pemba (ZSTC Madungu na Konde), na inatarajia kufanya ujenzi wa vituo vya kutolea huduma kwa Unguja (Kiwengwa na Kwa Nyanya Market, na Tunduma).
c. PBZ kwa mwaka 2025 imepanga kuweka mashine za kutolea fedha ATM katika maeneo ya KVZ-Mtoni, Jumbi, Dunga, Kizimkazi/Jambiani, Wingwi Mapofu na Mkokotoni.
d. PBZ inatarajia kuboresha miundombinu ya tehama kwa kununua switchi yake (Financial Switch) ambayo itarahisisha na kuiongezea mapato benki kwenye huduma za mashine za kutolea fedha (ATM).
e. Kutokana na maelekezo ya mamlaka ya mkoa wa Dar es salaam kufanya biashara katika eneo la Kariakoo kwa masaa 24, PBZ imeshaanza zoezi

hilo kwa tawi lake la Kariakoo na inategemea kuimarisha miundo mbinu hitajika ili iwe endelevu.

### 5.2.3 Changamoto na Utatuzi

**Jadweli Nambari 18. Changamoto na Utatuzi**

| Nam | CHANGAMOTO | UTATUZI |
|---|---|---|
| 1. | Kuwa na mtaji mdogo unaozuia benki kuingia katika ushindani wa kutoa mikopo mikubwa zaidi na kujiendeleza kibiashara (kufungua matawi) kwa haraka. | Serikali tayari ishatoa kibali kwa PBZ kutafuta mwekezaji wa kimkakati (strategic investor), na mchakato umeshaanza.<br>Mwekezaji atakaepatikana anatarajiwa kuongeza mtaji pamoja na ujuzi utakaosaidia benki kujiendesha kisasa na kuboresha huduma zake. |
| 2. | Kutokuwepo kwa (Kanuni) regulations zinazosimamia uendeshaji wa benki zinazofata misingi ya kiislamu. Hali hii inapelekea Benki ya Kiislam kukosa miongozo ya kiuendeshaji wake. | Benki Kuu ya Tanzania ipo katika hatua za kutoa Kanuni kwa benki zinazofuata misingi ya kiislamu. |

## 5.3 Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA)

Kwa mujibu wa Sheria ya Bima Sura 394, shughuli za Mamlaka hufanyika Tanzania Bara na Visiwani. TIRA inaongozwa na Kamishna wa Bima ambaye ndie Mtendaji Mkuu wa Mamlaka chini ya uongozi wa Bodi ya Bima ya Taifa (National Insurance Board). Kamishna wa Bima anasaidiwa na Naibu Kamishna wa Bima ambaye anaongoza shughuli za Mamlaka kwa upande wa Zanzibar.
Majukumu mahsusi ya Mamlaka ni: kusajili na kutoa leseni kwa watoa huduma za bima; kusimamia mwenendo, ustahimilivu, uendelevu na ukwasi kwa watoa huduma za Bima; Kulinda maslahi ya wateja, walaji na wanufaika wa huduma na bidhaa za bima; Kuendeleza soko la bima; Kutoa elimu kwa umma na kuishauri Serikali kuhusu masuala ya Bima.

### 5.3.1 Usajili wa Watoa Huduma za Bima

Mamlaka inaendelea kusajili watoa huduma za bima mbalimbali nchini ikiwemo kampuni za bima mtawanyo wa ndani na nje, Wataalamu wa Ushauri wa Bima Mtawanyo (Re Insurance Brokers) wa ndani na nje, wauza Bima Kidijitali (Insurance Digital Platform), Watathmini Bima (Insurance Actuaries firms), Wachunguzi Binafsi na Maafisa wauza Bima. Watoa huduma za bima (hawa hawana matawi/ofisi hapa Zanzibar). Aidha, watoa huduma za bima 117 ambao

ndio wanaofanya shughuli zao hapa Zanzibar, sawa na asilimia 7 ya idadi ya watoa huduma hao waliosajiliwa nchini.

Kati ya Kampuni za bima 38 zilizosajiliwa, Kampuni 18 ndio zina matawi/ ofisi zao hapa Zanzibar sawa na asilimia 47 ya Kampuni zote za bima nchini. Aidha Kampuni ya kwanza yenye kutoa huduma za bima kwa misingi ya Sharia imesajiliwa Zanzibar (Takaful) ambayo makao makuu yapo Zanzibar. ***(Jadweli nambari 19.)***

**Jedwali Nambari 19: Ulingano wa watoa huduma za bima Tanzania**.

| **Na.** | **Watoa huduma za Bima** | **Idadi** | | **% ya Jumla** |
|---|---|---|---|---|
| | | **Tanzania** | **Zanzibar** | |
| 1 | Kampuni za Bima | 38 | 18 | 47% |
| 2 | Washauri wa bima/Madalali | 144 | 2 | 1% |
| 3 | Mawakala wa bima | 1,402 | 86 | 6% |
| 4 | Benkiwakala | 36 | 6 | 17% |
| 5 | Wakadiria hasara | 56 | 0 | 0% |
| 6 | Kampuni ya TAKAFUL | 2 | 1 | 50% |
| 7 | Watoa huduma za Afya (Health services providers) | 17 | 4 | 24% |
| **Jumla** | | **1,695** | **117** | 7% |

Vilevile kuna ongezeko la kampuni za bima 18 zinazotoa huduma za bima hadi kufikia Machi 2025 sawa na ongezeko la asilimia 47. Hii ikiashiria kua zipo fursa kubwa za kutoa huduma za bima visiwani Zanzibar.

### 5.3.2 Mfumo wa Kusimamia na Kudhibiti Soko

Katika kuhakikisha soko la bima linakua imara, thabiti na kutoa huduma kwa mujibu wa Sheria, Mamlaka ina mfumo unaojulikana kama TIRA RBS unatumika kusajili watendaji wote wa bima zikiwemo kampuni na madalali wa bima, kuwasilisha hesabu, kuchambua na kutoa taarifa mbalimbali zinazohusu utendaji wa soko la bima nchini. Pia ipo mifumo mengine ya TEHAMA inayotumika na Mamlaka kama; TIRA-ORS, TIRA-MIS, mifumo ambayo inasomana na baadhi ya mifumo mengine ya Serikali kama; NIDA, TRA, BRLA, ZRA, BPRA, Polisi n.k. Mifumo hii pia imeunganishwa na mifumo ya kampuni zote za bima nchini. Lengo na madhumuni ya mifumo hii ni; kupokea na kuchakata taarifa za mwenendo na bishara ya bima ikiwemo; usajili wa watoa huduma za bima, uwasilishaji wa taarifa za biashara ya bima, upokeaji wa malalamiko kuhusu bima, uhakiki na uhalali wa bidhaa za bima na uchakataji wa taarifa za bima.

### 5.3.3 Msuluhishi wa migogoro ya bima (Ombudsman)

Ofisi ya Msuluhishi wa Migogoro ya Bima ni Taasisi inayojitegemea iliyoanzishwa chini ya sheria ya Bima ya Mwaka 2009 Sura ya 394. Lengo la kuanzisha ofisi hii ni kutatua migogoro baina ya wateja wa Bima na kampuni za Bima kupitia njia za usuluhishi nje ya utaratibu wa kawaida wa kimahakama. Shughuli za usuluhishi, kwa upande wa Zanzibar hufanywa na Mamlaka ya Usimamizi wa bima ofisi ya Zanzibar. Maafisa kutoka ofisi ya Msuluhishi wa Migogoro ya Bima watafika Zanzibar iwapo kuna haja ya kufanya hivyo ili kushirikiana na watendaji wa Mamlaka waliopo Zanzibar. Malalamiko yote yatakayofikia kuwa migogoro hupelekwa kwenye Kamati ya Utekelezaji wa Sheriana itakaposhindikana hupelekwa katika ofisi ya Msuluhishi wa Migogoro ya bima.

### 5.3.4 Hali ya soko la huduma za Bima Zanzibar.

Hali ya soko la Bima kwa upande wa Zanzibar kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 imeimarika. Biashara ya bima imekua na kufikia asilimia 271 kutokana na ongezeko la watoa huduma ya bima kufikia kampuni 18 hapa Zanzibar, kufikia kuandikisha bima zenye thamani ya TZS 75.9 bilioni kwa Mikataba ya bima 1,447,986 ambapo Jumla ya TZS 5.4 bilioni zililipwa kama fidia kwa wahanga 4,082.

### 5.3.5 Mafanikio

1. Tasnia ya Bima kushiriki katika uchumi wa Gesi na Mafuta kwa kuanzishwa kwa Muungano wa Kampuni za Bima za Utoaji wa Bima za Mafuta na Gesi (Oil and Gas Consortium).
2. Kuanzishwa kwa muungano wa kampuni za utoaji wa bima za kilimo (Agriculture Insurance consortium);
3. Taasisi kuendelea kufanya marekebisho katika Sheria ya Bima Sura Na. 394 na Kanuni zake, pamoja na kuandaa Kanuni Mpya za Bima kwa lengo la kuboresha mfumo wa usimamizi na uendelezaji wa bima nchini;
4. Kulinda haki ya mteja wa bima kwa kuwepo na mkakati kabambe wa kushughulikia kero na malalamiko kwa wananchi, kwa kuandaa semina kwa ofisi za kanda na Zanzibar katika ulipaji wa madai;
5. Kuanzishwa kwa aina mpya za bidhaa za bima ambapo jumla ya bidhaa 17 zimeanzishwa kwenye soko la bima kukidhi mahitaji ya wananchi hususan wa kipato cha chini. Bidhaa hizi ni pamoja na huduma za bima

kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo na wa kati na bidhaa za kilimo na uvuvi;

6. Uunganishwaji wa mifumo ya TEHAMA ya usimamizi wa bima kati ya TIRA na Mamlaka nyengine za Serikali Mfumo wa TEHAMA wa bima ulioundwa na TIRA - TIRAMIS umeunganishwa na mifumo ya Mamlaka ya Kodi Tanzania (TRA), Jeshi la Polisi Tanzania (TPF), na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA). Aidha, Mamlaka inatarajia kuunganisha mifumo yake ya TEHAMA na Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani (ZARTSA) ili kuhakikisha kuwa vyombo vya moto vinakatiwa bima kama Sheria inavyoelekeza na kuweza kukinga dhidi ya majanga ya barabarani;
7. Kuongezeka kwa wigo wa Bima za lazima ili kujumuisha masoko ya umma, majengo ya biashara, vyombo vya kusafiria majini na uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi;
8. Kufunguliwa kwa ofisi mbili za Kanda ambazo ni Kanda ya Unguja Kusini itahudumia Mikoa mitatu Unguja kati, Mjini Magharibi na Kaskazini, kwa upande wa Pemba itahudumia Mkoa wa Kaskazini na Kusini. Soko kuendelea kukua na kulipa madai kwa wananchi.
9. Matumizi ya bima kwa Serikali ya SMZ. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekua mstari wa mbele katika kutumia huduma za bima kulinda mali na rasilimali zake muhimu. Serikali imeendelea kutumia bima kwa ajili ya kulinda majengo ya Umma, Magari ya Serikali, na Miradi ya maendeleo, hii inapelekea kupunguza athari za majanga na gharama za matengenezo. Mpango wa Bima za lazima umeimarisha uwajibikaji katika ulinzi wa mali za Serikali, hivyo, kuongeza ufanisi wa usimamizi kwa rasilimali za Umma. Aidha, Ofisi ya Zanzibar ilifanya tathmini kuhusu matumizi ya bima katika taasisi za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na kubaini kuwa kuna matumizi makubwa kwenye bima za vyombo vya Moto na Bima ya Afya kutokana na kuwa bima hizo ni za lazima. Hii inaonesha kuwa Serikali inaendelea kutumia huduma za bima kwa ufanisi ili kulinda mali zake na kuimarisha ustawi wa rasilimali za Taifa;
10. Kuendelea kutoa Elimu endelevu ya Bima kwa Umma katika jitihada za kuimarisha utoaji wa elimu ya Bima kwa Umma, mbinu mbalimbali zimeendelea kutumika ikiwemo kutoa elimu kupitia warsha na matamasha mbalimbali yaliyofanyika Zanzibar kwa mwaka 2024. Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), kwa kushirikiana na wadau wa

bima, ilifanya mikutano ya hadhara, semina kwa watumishi wa Taasisi za SMZ, semina za wajasiriamali, na vipindi vya redio na televisheni, ambavyo vililenga kuongeza uelewa wa bima kwa wananchi na Taasisi. Zaidi ya watu milioni mbili (2) walipata elimu ya bima;

11. Kushiriki Maonesho ya biashara na Sherehe za Maadhimisho ya miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mamlaka iliweza kushiriki katika maonesho ya 11 ya biashara ya kimataifa yaliyofanyika Dimani, kuanzia tarehe 01 hadi 15 Januari, 2025. Maonesho hayo yalihusisha taasisi za Serikali, Kampuni binafsi, na wajasiriamali, na yalilenga kuonesha bidhaa na huduma zinazotolewa na Taasisi hizo zinazopatikana Tanzania Bara na Zanzibar kwa lengo la kutoa fursa kwa wananchi kupata elimu ya bima. Mamlaka iliweza kutoa elimu ya bima kwa Taasisi, wajasiriamali na wananchi kwa ujumla waliotembelea kwenye banda la TIRA, zaidi ya wananchi 200 walipata elimu ya bima;
12. Utekelezaji wa Bima ya Safari (Travel insurance) Shirika la Bima la Zanzibar (ZIC) kupitia bidhaa mpya ya Bima ya Safari (Inbound Travel) ambayo ilianza kutekelezwa tarehe 24 Julai 2024, limeendelea kufanya maboresho katika upatikanaji wa huduma hiyo kwa watalii na wageni wanaoingia Zanzibar hivyo kupunguza changamoto zilizojitokeza awali wakati wa utekelezaji. Bidhaa hiyo inalenga kutoa kinga ya bima kwa wageni na watalii wote wanaoingia Zanzibar kutoka nje ya nchi. Huduma hiyo inaendelea kuwapa watalii na wageni uhakika wa kinga dhidi ya majanga mbalimbali wakati wakiwa Zanzibar. Utekelezaji wa bima ya safari kwa watalii na wageni wanaoingia Zanzibar imechangia kuongeza mapato ya Sekta ndogo ya bima na kuchochea ukuaji wa Sekta ya Utalii Zanzibar.

### 5.3.6 Matarajio

1. Kukamilishwa kwa Sera ya Bima ya Taifa (National Insurance Policy - NIP);
2. Kuendelea na uunganishwaji wa mifumo ya TEHAMA ya usimamizi wa bima kati ya TIRA na Taasisi nyengine za Serikali (kama vile TASAC, TPA, NIDA, ZRA, Idara ya Usafirishaji na Mawasiliano Zanzibar, NSSF, ZSSF, NHIF, CHF, na WCF) ili kuongeza tija na ufanisi ndani ya sekta ndogo ya bima na pia kupunguza gharama za usimamizi;

3. Kuanzishwa kwa Bodi ya Wataalam kwenye Tasnia za Bima, bodi hiyo itaitwa Insurance, Social Protection, and Actuarial Board – ISPAB. Lengo la bodi ni kuongeza fursa za kutambulika na tija kwa wanataaluma husika;
4. Kukamilisha kwa Kanuni za Bima za Lazima. TIRA kama msimamizi wa Bima inaendelea kukamilisha kanuni za Bima za lazima katika maeneo ya; Majengo ya Biashara, Masoko ya Umma, Bidhaa zinazotoka nje, Vyombo vya Usafiri wa Majini kama vile Meli, Boti na Feri au Vivuko.

   Aidha, Mamlaka kwa kushirikiana na wadau mbali mbali itaendelea na utekelezaji wa matakwa ya Mpango Mkuu wa Serikali wa Kuendeleza Sekta ya Fedha (FSDMP) ikiwemo, kutekeleza mkakati wa kitaifa wa elimu ya Bima; kutekeleza mkakati wa kitaifa wa Bima jumuishi na kuweka na kutekeleza mfumo madhubuti wa kushughulikia madai, malipo na malalamiko ya wateja.

**Jadweli Nambari 20: Hali ya soko la huduma za Bima Zanzibar kwa bidhaa za Bima Julai 2024 – Machi 2025**

| Na m | Bidhaa | Jumla ya Ada za Bima | | Ziada/ Pungufu |
|---|---|---|---|---|
| | | 2024 | 2025 | |
| 1 | Moto | 7,386,350,736 | 7,507,726,608 | 2% |
| 2 | Ufundi | 1,550,245,214 | 1,029,653,584 | -34% |
| 3 | Majini | 2,320,611,686 | 2,311,522,306 | 0% |
| 4 | Vyombovya Moto | 4,482,731,375 | 5,513,984,518 | 23% |
| 5 | Mchanganyiko | 1,972,629,851 | 34,413,734,241 | 1645% |
| 6 | Anga | 804,041,867 | 969,414,318 | 21% |
| 7 | Afya | 3,400,000 | 25,739,391 | 0% |
| 8 | Nyenginezo | 1,777,503,743 | 24,145,474,129 | 1258% |
| 9 | Maisha | 155,531,446 | 20,206,971 | -87% |
| | **Jumla** | **20,453,045,918** | **75,937,456,066** | **271%** |

***Chanzo: Kampuni za Bima zilizopo Zanzibar***

**Jadweli Nambari 21: Hali ya soko la huduma za Bima Zanzibar kwa Kampuni Julai 2024 – Machi 2025**

| Nam. | Makampuni ya Bima | Thamani ya Bima za kawaida | Idadi ya mikataba ya Bima za kawaida | Thamani ya Bima za maisha | Idadi ya mikataba ya Bima za maisha | Jumla ya thamaniya Bima | Jumla ya mikataba ya Bima |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | BUMACO | 462,706,977 | 3,061 | - | - | 462,706,977 | 3,061 |
| 2 | HERITAGE | 1,368,861,000 | 3,615 | - | - | 1,368,861,000 | 3,615 |
| 3 | JUBILEE Allianz | 8,848,821,694 | 2,314 | - | - | 8,848,821,694 | 2,314 |
| 4 | MAYFAIR | 480,348,609 | 679 | - | - | 480,348,609 | 679 |
| 5 | NIC | 264,620,434 | 309 | 19,246,971 | 397 | 283,867,405 | 706 |
| 6 | MUA | 1,100,984,815 | 392 | - | - | 1,100,984,815 | 392 |
| 7 | SANLAM LIFE | - | - | 960,000 | 8 | 960,000 | 8 |
| 8 | STRATEGIES | 387,389,327 | 1,474 | - | - | 387,389,327 | 1,474 |
| 9 | UAP/NEW TAN | 95,959,147 | 260 | - | - | 95,959,147 | 260 |
| 10 | ZIC | 57,084,342,383 | 1,385,684 | - | - | 57,084,342,383 | 1,385,684 |
| 11 | ICEA LION | 444,294,585 | 509 | - | - | 444,294,585 | 509 |
| 12 | RELIANCE | 84,001,386 | 156 | - | - | 84,001,386 | 156 |
| 13 | MILEMBE | 9,586,600 | 67 | - | - | 9,586,600 | 67 |
| 14 | FIRST ASSURANCE | 1,153,740,982 | 1,869 | - | - | 1,153,740,982 | 1,869 |
| 15 | GA INSURANCE | 134,329,141 | 979 | - | - | 134,329,141 | 979 |
| 16 | MO ASSURANCE | 99,642,309 | 563 | - | - | 99,642,309 | 563 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 17 | TANZINDIA | - | - | - | - | - | - |
| 18 | ZIC TAKAFUL | 3,897,619,708 | 45,650 | - | - | 3,897,619,708 | 45,650 |
| | **JUMLA** | **75,917,249,095** | **1,447,581** | **20,206,971** | **405** | **75,937,456,066** | **1,447,986** |

***Chanzo: Kampuni za Bima zilizopo Zanzibar***

**Jadweli Nambari 22: Hali ya malipo ya fidia ya Majanga ya Bima Zanzibar Kuanzia Julai 2024 hadi Machi, 2025**

| Nam. | Makampuni ya Bima | Thamani ya fidia za majanga ya Bima za kawaida | Idadi ya fidia za Bima za kawaida | Thamani ya fidia za majangaya Bima za maisha | Idadi ya fidia za Bima za maisha | Jumla ya thamani yafidia za majangaya Bima | Jumla idadi ya fidia za Bima |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | BUMACO | 13,446,750 | 3 | - | - | 13,446,750 | 3 |
| 2 | HERITAGE | 795,618,000 | 40 | - | - | 795,618,000 | 40 |
| 3 | JUBILEE Alliance | 753,974,482 | 74 | - | - | 753,974,482 | 74 |
| 4 | MAYFAIR | - | - | - | - | - | - |
| 5 | NIC | - | - | 32,237,789 | 27 | 32,237,789 | 27 |
| 6 | MUA | - | - | - | - | - | - |
| 7 | SANLAM LIFE | - | - | 343,762,784 | 2,054 | 343,762,784 | 2,054 |
| 8 | STRATEGIES | 12,159,900 | 3 | - | - | 12,159,900 | 3 |
| 9 | UAP/NEWTAN | - | - | - | - | - | - |
| 10 | ZIC | 3,243,210,689 | 1,848 | - | - | 3,243,210,689 | 1,848 |
| 11 | ICEA LION | 84,085,522 | 16 | - | - | 84,085,522 | 16 |
| 12 | RELIANCE | 1,888,047 | 3 | - | - | 1,888,047 | 3 |
| 13 | MILEMBE | - | - | - | - | - | - |
| 14 | FIRST ASSURANCE | 3 | 1 | - | - | 3 | 1 |
| 15 | GA INSURANCE | 3 | | - | - | 3 | - |
| 16 | MO ASSURANCE | - | - | - | - | - | - |
| 17 | TANZINDIA | - | - | - | - | - | - |
| 18 | ZIC TAKAFUL | 118,539,682 | 13 | - | - | 118,539,682 | 13 |
| | **JUMLA** | **5,022,923,077** | **2,001** | **376,000,573** | **2,081** | **5,398,923,651** | **4,082** |

## 5.4 Shirika la Bima la Zanzibar

Shirika la Bima la Zanzibar lilianzishwa mwezi wa June mwaka 1969 ni miongoni mwa Mashirika yanayomilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa asilimia 100 likiwa chini ya Afisi ya Rais Fedha na Mipango Zanzibar.

Katika kufanikisha Maendeleo ya Sekta ya Bima na Sekta ya Fedha Zanzibar na Tanzania kwa ujumla Shirika la Bima la Zanzibar linaendelea kutoa huduma zake kwa Wananchi kupitia ofisi zake ziliopo Zanzibar (Unguja na Pemba) na ofisi za matawi zilizopo Tanzania Bara pamoja na maeneo mbalimbali kupitia kwa ofisi za mawakala na madalali.

Kwa hivi sasa Shirika linafanya kazi zake chini ya Sheria ya Msajili wa Hazina Namba 6 yamwaka 2021. Vilevile, Shirika la Bima la Zanzibar linasimamiwa na Sheria ya Bima namba 10 ya mwaka 2009 katika utekelezaji wa utoaji wa huduma zake chini ya usimamizi wa Kamishina wa Bima Tanzania.

Shirika linazidi kuonyesha muelekeo mzuri wa mabadiliko kwa kuongeza mapato yake, kupunguza gharama za uwendeshaji na kufanya uwekezaji wenye tija.

### 5.4.1 Majukumu Makuu ya Shirika la Bima Zanzibar

Kutokana na "Legal Notice No. 11 of 1969." iliyoanzisha Shirika na kupewa Mamlaka ya utekelezaji wa majukumu yafuatayo: -

i. Kusimamia mapato ya Shirika kutokana na vyanzo mbali mbali vya mapato. Mapato hayo yanajumuisha bima za magari, Bima za moto, Bima za meli, pamoja na mapato yatokanayo na uwekezaji;
ii. Kusimamia mali za Shirika kupitia usimamizi wa ununuzi, utunzaji na uondoaji wa mali za Shirika kwa mujibu wa Sheria za Ununuzi;
iii. Kusimamia utekelezaji wa Bajeti kwa kila mwaka wa fedha, huduma za Uhasibu na ukaguzi wa ndani na ukaguzi wa nje;
iv. Shirika linasimamia maendeleo ya Sekta ya Bima Tanzania kwa kushirikiana na wadau wote;
v. Kusimamia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano TEHAMA kupitia mifumo inayohusisha kudhibiti mapato na matumizi ya Shirika;
vi. Kutoa huduma ya kinga za Bima za aina mbalimbali kwa jamii hapa Nchini.

### 5.4.2 Ofisi za Shirika

Shirika lina jumla ya wafanyakazi 182 na jumla ya Mawakala na Madalali 151 na linafanya kazi zake kwa kupitia ofisi ya Makao Makuu Mpirani Zanzibar, ofisi ya Tawi Amani Unguja, Kanda Pwani- Dar es salaam, Kanda ya Ziwa Mwanza, Kanda ya kati Dodoma, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya, Kanda ya Kaskazini Arusha, Kanda ya Kusini Mtwara, Ofisi ya Pemba, Ofisi ya mauzo Tanga, Ofisi ya mauzo Kahama na Ofisi ya mauzo Posta Dar es salaam.

### 5.4.3 Utekelezaji Halisi wa Kazi za Shirika kwa Kipindi cha Julai / Machi 2025

**a. Mapato**

Kwa kipindi cha Julai-Machi 2025, Shirika limekusanya mapato jumla ya TZS 82.3 bilioni yanayotokana na vianzio vyake vya mauzo ya Bima pamoja na faida zinazotokana na Uwekezaji, ambayo ni sawa na asilimia 142 ya makadirio ya kukusanya TZS 57.8 bilioni katika kipindi cha tathmini. Ongezeko hilo la asilimia 42 limetokana na mapato yanayotokana na uwanzishwaji wa Bima ya Lazima "Inbound Travelling Insurance" kwa wageni wanaoingia Zanzibar.

**b. Matumizi**

Matumizi ya Shirika kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2025, yamegawika kama ifuatavyo:

i. **TZS 7.2 bilioni** zilitumika kwa ajili ya gharama za uwendeshaji wa ofisi (Management Expenses) sawa na asilimia 75 ya makadirio ya matumizi katika kipindi cha tathmini ambayo ni TZS 9.6 bilioni.
ii. **TZS 6.7 bilioni** zimetumika kulipa madai mbalimbali ya wateja wake waliopata ajali na kutimiza matakwa ya Sheria za bima ambayo ni sawa na asilimia 80 ya makadirio ya TZS 8.4 bilioni katika kipindi cha tathmini.
iii. **TZS 2.8 bilioni** zimetumika pia kulipa ujira kwa Mawakala na Madalali wanaofanya biashara ya bima kwa niaba ya Shirika. Malipo hayo ni sawa na asilimia 68 ya makadirio ya TZS 4.1 bilioni katika kipindi cha tathmini.

### 5.4.4 Mafanikio yaliyopatikana kwa Shirika katika Sekta ya Fedha

Katika kipindi Julai-Machi 2025, Shirika la Bima la Zanzibar limeweza kupata mafanikio yafuatayo: -

I. Uwezo wa Shirika katika maeneo mbalimbali umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka kwa kutoa huduma bora kwa Wananchi kwa lengo la kujiongezea mapato ambapo kwa sasa Shirika lina jumla ya Ofisi 11 pamoja na mawakala na madalali 151 Nchi nzima.

II. Shirika limeweza kupanda katika viwango vya soko la bima Tanzania "Market Share" kutoka nafasi ya 8 mwaka 2023 hadi nafasi ya 6 mwaka 2024 kati ya Makampuni 30 yaliyopo katika soko la Bima Tanzania, hali hizo zimetokana na jitihada na mikakati mbalimbali inayo chukiliwa na Shirika katika kuhakikisha linakuwa, na vilevile kupandisha nafasi yake pamoja na ushindani uliopo na Makampuni mengine ya Bima Tanzania.

III. Shirika limeweza kulipa madai ya aina mbalimbali ya halali na yaliyohakikiwa kwa wateja wake kwa wakati na kuzidi kuonyesha uwaminifu kwa wateja wake katika kukatia kinga za Bima mali zao.

IV. Shirika kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Zanzibar na Tanzania Bara limeweza kutoa taaluma kuhusiana na masuala ya usalama barabarani kwa kuandaa makongamano mbalimbali lengo likiwa ni kupunguza majanga mbalimbali ya ajali kwa Wananchi.

V. Kuanzishwa kwa bima ya lazima kwa wageni wote wanaofika Zanzibar (Inbound Travel Insurance) ambayo inatoa kinga dhidi ya majanga na dharura pindi yakitokea ndani ya siku (92) popote pale Zanzibar na Tanzania. Ambapo jumla ya wageni 442,705 walifanikiwa kukata bima katika kipindi hicho.

VI. Shirika limefanikiwa kuongeza wigo wa Biashara ya Bima kwa mashirikiano ya kimkakati na Mabenki mbalimbali katika mfumo wa (Bank Assurance) kama vile Shirika la Posta Tanzania, NMB Bank, CRDB Bank, EXIM Bank, TCB Bank, DCB Bank, NBC Bank, BOA Bank, Mwalimu Commercial Bank, MUKOBA Bank na PBZ Bank. Lengo ni kuongeza mapato ya Shirika.

VII. Kuimarisha mifumo ya TEHAMA katika kuimarisha utendaji kazi wa Shirika kama ifuatavyo:

a. Kubadilisha mfumo wa kufanya kazi kwa kutumia karatasi na kuhamia kutoa huduma Kidijitali.

b. Kuunganisha mifumo yake na Mamlaka za Bima (TIRA), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), Pamoja na Mabenki kama vile CRDB, PBZ, NMB, KCB, EXIM, TCB, NBC, Zan Malipo, n.k.

c. Kutoa huduma kwa kupitia mitandao ya simu kama vile Vodacom M-Pesa, Mix by YAS na Selcom Money pamoja na kuanzisha program za simu za mikononi za "Mobile app" na program ya kusajili kidigitali huduma za Bima ya lazimaya Msafiri (Inbound Travel Insurance) kwa wageni wote wanaoingia Zanzibar.

### 5.5 MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR (ZSSF)

Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Mfuko ulitekeleza majukumu yake ya kulipia mafao, kufanya uwekezaji na matumizi ya Shughuli za uendeshaji za Mfuko na pia ulipitisha makisio ya mapato yatokanayo na vyanzo vikuu viwili ambavyo ni Michango ya Wanachama na Mapato Yatokanayo na Uwekezaji.

Ripoti inaonesha utekelezaji wa bajeti ya Mfuko kwa kipindi cha Julai hadi Machi, mwaka 2024/2025. Utekelezaji huo utakuwa kwa upande wa makadirio ya Mapato na Matumizi kama ifuatavyo: -

#### 1.0 Mapato ya Mfuko

Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2024/2025, Mfuko ulikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 246.34 bilioni**. Mapato hayo yalitegemewa kutoka katika vyanzo vikuu viwili (2), ikiwa ni **TZS 154.28 bilioni** ni michango ya wanachama na **TZS 92.06 bilioni** ni mapato yatokanayo na uwekezaji. Kati ya makadirio hayo, jumla ya **TZS 195.90 bilioni** zilikusanywa ikiwa sawa na asilimia **80.** Kati ya hizo, **TZS 117.18 bilioni** ni michango ya wanachama na **TZS 78.72 bilioni**, ni mapato ya uwekezaji. Mchanganuo wa michango ya wanachama na mapato ya uwekezaji ni kama ufuatavyo:

#### 1.1 Michango ya Wanachama

Kwa kipindi cha kuanzia Julai hadi Machi 2024/2025 Mfuko ulipanga kukusanya TZS 154.28 bilioni kutoka kwa michango ya wanachama kati ya hizo Mfuko ulikusanya **TZS 117.18 bilioni** sawa na asilimia **76** ya ufanisi, ikilinganishwa na **TZS 111.45 bilioni**, Julai hadi Machi 2023/2024 sawa na ongezeko la asilimia **5.**

**Mchanganuo wa Michango ya Wanachama kama ifuatavyo: -**

i. Kwa kipindi cha kuanzia Julai hadi Machi 2024/2025 Mfuko ulikusanya jumla ya **TZS 146.00 bilioni**, kutoka Mfuko wa lazima sawa na asilimia

**76** ya makadirio ya **TZS 111.24 bilioni**, ikilinganisha na **TZS 106.02 bilioni**, kipindi cha Julai hadi Machi 2023/2024, sawa na ongezeko la asilimia **4**.

ii. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2024/2025, Mfuko ulikusanya jumla ya **TZS 31.09 milioni** kutokana na adhabu, sawa na asilimia 57 ya makadirio ya **TZS 54.51 milioni** ikilinganishwa **TZS 34.82 milioni**, katika kipindi cha Julai hadi Machi 2023/2024, sawa upungufu wa asilimia **11**.

iii. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2024/2025, Mfuko ulikusanya jumla ya **TZS 422.52 milioni** kutokana na Mfuko wa Hiari, sawa na asilimia **91** ya makadirio ya **TZS 466.63 milioni**, ikilinganishwa na **TZS 292.16 milioni**, katika kipindi cha Julai hadi Machi 2023/2024, sawa na ongezeko la asilimia **45**.

iv. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2024/2025, Mfuko ulikusanya jumla ya TZS 5.48 bilioni kutokana michango ya Skimu ya Fidia sawa na asilimia 75 ya makadirio ya TZS 7.30 bilioni ikilinganishwa na TZS 5.11 bilioni, katika kipindi cha Julai hadi Machi 2023/2024, sawa na ongezeko la asilimia 7.

v. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2024/2025, Mfuko ulipanga kukusanya **TZS 461.02 milioni** kutokana na Hifadhi ya Jamii kwa Misingi ya Sharia. Hadi kufikia Machi 2025, Mfuko haujaanza kukusanya michango kutokana na Bima hiyo.

### *1.2 Mapato ya Uwekezaji*

Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2024/2025, Mfuko ulikusanya jumla ya uwekezaji **TZS78.72 bilioni** kutokana na mapato ya uwekezaji sawa na asilimia 86 ya makadirio ya **TZS 92.06 bilion**i, ikilinganishwa na TZS 66.15 bilioni katika kipindi cha Julai hadi Machi 2023/2024 sawa na ongezeko la asilimia **19**.

### *1.3 Thamani ya Uwekezaji hadi Kufikia Machi 2025*

Uwekezaji wa Mfuko unajumuisha uwekezaji wa mabenki, hati fungani za Serikali na makampuni, hisa, uwekezaji wa majengo na mikopo. Hadi kufikia Machi 31 2025, thamani ya uwekezaji wa Mfuko iliongezeka kufikia **TZS 1.165 trilioni** ikinganisha na **TZS 958.9 bilioni** mwaka 2023/24, sawa na asilimia **21**. Hii ni kutokana na kuongezeka kwa Uwekezaji na Mapato yatokanayo na uwekezaji.

### *2.0 Matumizi ya mfuko*

Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2024/2025, Mfuko ulipanga kutumia jumla ya **TZS 358.99 bilioni** ikiwa **TZS 85.55 bilioni** kwa ajili ya kulipia mafao, **TZS 260.63 bilioni** kwa ajili ya uwekezaji, **TZS1.28 bilioni** kwa ajili ya kusimamia miradi na **TZS 11.53 bilioni** kwa ajili ya kugharamia shughuli za uendeshaji. Kiasi cha **TZS 331.55 bilioni** zilitumika sawa na asilimia **92**, ikiwa **TZS 69.27 bilioni** kwa ajili ya kulipia mafao, **TZS 252.96 bilion**i kwa ajili ya uwekezaji, TZS 1.26 bilioni kwa ajili ya kusimamia miradi na **TZS 7.6 bilioni** kwa ajili ya kugharamia shughuli za uendeshaji.

### *2.1 Gharama za Uendeshaji*

Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2024/2025, Mfuko ulipanga kutumia jumala ya **TZS 11.53 bilioni** kwa gharama za uendeshaji. Kati ya hizo, zimetumika jumla ya **TZS 7.60 bilioni** sawa na asilimia **66** ya makadirio, ikilinganishwa **TZS 7.17 bilion**i katika kipindi kama hicho cha Julai hadi Machi 2023/2024, sawa na ongezeko la asilimia **6.** Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa gharama za uendeshaji wa shughuli za ofisi.

### *2.2 Malipo ya Mafao kwa Wanachama*

Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2024/2025, Mfuko ulipanga kutumia **TZS 85.55 bilioni** kulipia mafao ya wanachama. Kati ya **TZS 69.27 bilioni** zilitumika sawa na asilimia **81** ya makadirio, ikilinganishwa na **TZS 57.33 bilioni** kipindi cha Julai hadi Machi 2023/2024 sawa na ongezeka la asilimia **21**. Hili linatokana kuongezeka kwa kima cha chini cha pencheni ambapo inaathiri utekelezaji wa bajeti, ongezeko la idadi ya wastaafu na marejesho kwa wageni wanaondoka nchini katika kipindi hicho.

### *2.3 Gharama za uwekezaji na Usimamizi wa Miradi*

Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2024/2025, Mfuko ulipanga kuwekeza jumla ya **TZS 260.63 bilion**i, kati ya hizo, Mfuko uliekeza **TZS 252.96 bilioni** sawa na asilimia **97** ya makadirio, ikilinganishwa na **TZS 180.55 bilioni** katika kipindi kama hicho cha Julai hadi Machi 2023/2024, sawa na ongezeko la asilimia **40.** Ongezeko hilo, linatokana na kuongezeka kwa uwekezaji.

Aidha, kwa upande wa gharama za usimamizi wa miradi na uwekezaji, Mfuko ulipanga kutumia **TZS 1.28 bilioni** kati ya hizo **TZS 1.26 bilioni** zilitumika,

sawa na asilimia 98 ya makadirio, ikilinganishwa na **TZS 1.15 bilioni** katika kipindi kama hicho mwaka 2023/2024 sawa na ongezeko la asilimia **10**. Hii ni kutokana na kuongezeka kwa gharama za usimamizi wa miradi.

**Taarifa Nyengine za Utekelezaji kwa Mfuko wa ZSSF**

Taarifa nyengine za utekelezaji wa Mfuko katika kipindi cha Julai hadi Machi 2024/2025 ni kama ifuatavyo: -

i. Hadi kufikia Julai hadi Machi 2024/2025, Mfuko ulikua na jumla ya **Waajiri 3,327** ikilinganishwa na jumla **waajiri 3,029 243** Julai hadi Machi mwaka 2023/2024. Jumla ya waajiri wapya 245 walisajiliwa kwa kipindi cha Julai hadi Machi mwaka 2024/2025, sawa na asilimia 87 ya makisio ya kuwasajili **waajiri 283**, ikilinganishwa na wajiriwa **wapya 237** katika kipindi kama hicho cha Julai hadi Machi 2023/2024, sawa na asilimia **98**.

ii. Mfuko umesajili **waajiriwa 11,500** sawa na asilimia **56** ya makadirio ya kuwasajili waajiriwa 20,713 na kufikia jumla ya **waajiriwa 153,351** ikilinganishwa na **8,827** kutoka makadirio ya waajiriwa 13,988 sawa na asilimia **63** na kufikia **128,995** Julai hadi Machi 2023/2024.

iii. Mfuko wa Hiari umesajili wanachama wapya **794** na kufikia **13,364** sawa na asilimia 41 ya makisio ya kuwasajili wanachama **1,923**, ikilinganishwa na Wanachama **326**, waliofikia 1**2,618** sawa na asilimia 23 ya makisio ya kuwasajili wanachama **1,400**, mwaka uliopita katika kipindi cha Julai hadi Machi 2023/2024.

iv. Mfuko wa Hifadhi ya jamii Zanzibar unaendelea kukusanya michango ya asilimia moja (1%) kutoka kwa waajiri kuhusiana na Fao la kuumia kazini.

v. Kwa upande wa mradi wa ujenzi wa nyumba za gharama nafuu iliyopo Mombasa Zanzibar, majengo 14 yanaendelea kujengwa na utekelezaji umefikia asilimia 99, kazi zinazoendelea kwa sasa ni marekebisho madogo madogo kwa majengo yote ya mradi kutengeneza mtaro wa kutoa maji ya mvua pia mkandarasi anamalizia miundombinu ya umeme kwa majengo yote. Mradi huo tayari umeshawekewa jiwe la msingi na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi tarehe 24, Oktoba 2023.

vi. Kwa upande wa mradi wa ujenzi wa maegesho ya gari Malindi, kwa sasa mradi huo umekamilika na utekelezaji umefikia asilimia 100. Mradi huo umefunguliwa rasmi na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi tarehe 20, Disemba 2024.

vii. Kwa upande wa mradi wa kituo cha mabasi Kijangwani, kwa sasa mradi huo umekamilika na utekelezaji umefikia asilimia 100. Mradi huo umefunguliwa rasmi na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi tarehe 03, Januari 2025.

viii. Ujenzi wa mradi wa Michezo na Biashara Mbweni, mradi wa michezo na biashara tayari umekamilika na mkandarasi anaendelea na hatua za marekebisho ya "Slag" kwa hatua zote mbili ili kupelekea kukamilika kwa mradi huo na utekelezaji umefikia asilimia **99**. Mradi huo tayari umezinduliwa rasmi na Mstaafu Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi tarehe 02, Januari 2025.

ix. Ujenzi wa Kituo cha kisasa cha Mabasi Malindi, mkataba wa kazi baina ya Mshauri elekezi na Mfuko ameshakamilisha michoro ya mwisho na taratibu za kumpata Mkandarasi zinaendelea.

x. Kuendelea na ujenzi wa Soko la Mombasa. Mradi huu umefikia asilimia **55**. Mkandarasi anaendelea na hatua za ujenzi wa sakafu (Ground Floor) ya ndani na kujenga vizimba na tofali kwa baadhi ya maeneo katika ghorofa ya kwanza. Mradi huo umeshawekewa jiwe la msingi na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mhe. Hemed Suleiman Abdulla tarehe 29, Disemba 2024.

## 3.0 MAFANIKIO NA CHANGAMOTO KWA KIPINDI CHA JULAI 2024 HADI MACHI 2025 KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

## 3.1 MAFANIKIO

### 3.1.1 Utekelezaji Ilani 2020-2025

Katika Ibara ya 220 Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2020 – 2025 Mfuko umetekeleza Ilani kwa asilimia 95, katika maeneo yafuatayo: -

i. **Kusimamia utekelezaji wa Sera na Sheria ya Hifadhi ya Jamii kwa manufaa ya wananchi wote na Taifa kwa ujumla**.

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar, unaendelea kusimamia utekelezaji wa Sera na Sheria ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2014 ambayo ilipelekea kufanyika marekebisho ya Sheria ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi na kuongeza Mafao mawili (Fao la Upotevu wa Ajira na Fao la Kuumia Kazini). Sambamba na hayo, Mfuko unaendelea kutoa elimu kwa wananchi wote kupitia vyombo vya habari juu ya utekelezaji wa Sera na Sheria za Mfuko.

ii. **Kujenga Majengo ya Makaazi na Biashara katika eneo la Mombasa Unguja**

Mfuko unaendelea na ujenzi wa Mradi wa Majengo ya makazi na Biashara katika eneo la Mombasa Unguja, Mradi huo utakua na nyumba 276 za gharama nafuu na Maduka ya biashara 42 na utekelezaji umefikia asilimia 99.

iii. **Kuongeza kiwango cha usajili wa wanachama hadi kufikia asilimia 50 ya wanaoweza kufanya kazi.**

Mfuko ulipanga kusajili waajiriwa 20,713 na kufanikiwa kusajili waajiriwa 11,500 ikiwa ni sawa na asilimia 56 ya malengo ya kusajili wanachama wanaoweza kufanya kazi. Kwa mujibu wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, hadi kufikia Machi 2025. Idadi ya wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar ni 153,351 sawa na asilimia 34.

iv. Kufungua Ofisi za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii katika Mikoa ya Zanzibar

Mfuko umeshafungua Ofisi za Mikoa, ambapo kwa Mkoa wa Kusini Ofisi ya Mfuko ipo katika Jengo la Halmashauri Wilaya ya Kusini (Kitogani) na kwa upande wa Kaskazini Ofisi ya Mfuko ipo Kinduni katika Jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini B Mkoa wa Kaskazini Unguja, Mfuko unaendelea kutafuta eneo kwa ajili ya Ofisi ya Mkoa wa Kaskazini Pemba.

v. **Kuanzisha Mafao mapya kama vile Mafao ya Matibabu na kupunguza muda wa kulipa Mafao katika kipindi cha wiki mbili**

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar umefanikiwa kuongeza mafao mawili mapya kama ilivyoelekezwa kwenye Ilani ikiwemo Fao la kuumia kazini na Fao la upotevu wa ajira. Kwa upande wa Fao la Matibabu,

Serikali imeandaa utaratibu maalum kwa kuanzisha Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar.

Kwa kushirikiana na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali Zanzibar (CAG), Mfuko umetengeneza Mfumo maalum wa kielektroniki wa mchakato wa upitiaji wa Mafaili ya wastaafu. Mfumo huo umefanikisha kupunguza taratibu za ulipaji wa Mafao kutoka siku 30 hadi siku 14.

### 3.1.2 Mafanikio kwa ujumla

**i. Utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Ongezeko la kima cha chini cha Pencheni**:
Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar umefanya malipo kwa ongezeko la pensheni kutoka TZS 90,000 hadi kufikia TZS 180,000 kuanzia mwezi Julai 2023. Hii ikiwa ni kutekeleza ahadi ya Mh. Rais aliyoitoa katika Sherehe za Mei Mosi 2023 huko Nungwi.

**ii. Uimarishaji Utendaji kazi**
Mfuko umeimarisha usimamizi na utendaji kazi na kuongeza ufanisi wa watendaji kwa kuweka utaratibu maalum wa kuwapima uwezo wa utendaji kazi zao. Hatua hii, imeweza kuongeza uwazi na uwajibikaji katika kutekeleza majukumu ya Mfuko na kufanikisha kufikiwa kwa malengo. Mfuko umeanzisha mfumo wa kielektroniki wa Rasilimali watu kwa ajili ya kuwapima watendaji wake.

**iii. Uwekezaji**
Kutokana na Uwekezaji mzuri unaoendelea kufanyika kumepelekea kuongezeka kwa Mapato ya uwekezaji na Ukusanyaji wa Michango. Mfuko umeendelea kuimarika uhimilivu wake na kuongezeka uwezo wa kulipa Mafao kwa miaka 25 ijayo bila ya kuyumba.

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar unaendelea kuongeza juhudi katika utafutaji wa fursa za uwekezaji zenye faida, tija na salama kwa ajili ya michango ya wanachama ndani na nje ya nchi kwa mustakabali mpana wa uhimilivu wa Mfuko. Thamani ya Mfuko imeongezeka kutoka **TZS 958.9 bilioni** katika kipindi cha Machi 2024 hadi kufikia **TZS 1.098.6 trilioni** katika kipindi cha Machi 2025, ikiwa ni ongezeko la **TZS 139.7 bilioni** ikiwa ni ongezeko la wastani wa asilimia **15**.

**iv. Mifumo ya Tehama**

Kuanzishwa kwa mifumo mipya ya mawasiliano na TEHAMA kwa lengo la kuboresha utendaji kazi na kurahisisha huduma kwa wanachama wetu, mifumo ambayo imesaidia wafanyakazi wetu kujipima utendaji kazi na ufanisi wa huduma wanazozitoa, pia mifumo hiyo imesaidia wanachama wetu kupata taarifa fupi kupitia simu zao za mkononi ikiwemo kujua mienendo ya michango yao na pia kupata taarifa mbali mbali zinazohusiana na Mfuko. Mifumo hiyo kama ifuatavyo: -

- Mfumo wa ukusanyaji michango – (Employers' Portal)
- Mfumo wa Uhakiki kwa wastaafu – (Mobile App)
- Mfumo wa Utunzaji na utafuataji wa nyaraka kwa kutumia makabati ya kielektroniki (Electronic Document Management System)
- Mfumo maalum wa kielektroniki wa mchakato wa upitiaji wa Mafaili ya wastaafu – (Fumis CAG).
- Mfumo wa Fao la Upotevu wa Ajira – (Fumis Labor Commission).

**v. Ushirikiano kwa taasisi za Kikanda na Kimataifa**

Mfuko kuimarisha ushirikiano na taasisi za fedha, taasisi zinazoshughulika na hifadhi ya jamii za kikanda na za nje ya nchi. Mfuko umeshasaini Hati ya Makubaliano (MoU) na Mfuko wa Fidia kwa wafanyakazi Tanzania (WCF) na Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma Tanzania (PSSSF). Aidha, Mfuko unaendelea kushirikiana na Taasisi za Hifadhi ya Jamii za Kimataifa ASSA na ISA (International Standars on Auditing).

**vi. Kuogezeka Ukwasi wa Mfuko.**

Kutokana na utofauti baina ya dhima, mapato ya uwekezaji na rasilimali unazomiliki, Mfuko umendelea kuongeza ukwasi wake na unaweza kumudu kulipa mafao kwa wanachama wake bila ya wasiwasi wowote. Aidha Mfuko unalipa pencheni kwa wastaafu kila ifikapo tarehe 15 ya kila mwezi ili kuwapunguzia wazee msongamano katika Mabenki.

## 4.0 CHANGAMOTO

Pamoja na mafanikio makubwa yaliopatikana, changamoto zilizojitokeza ni hizi zifuatazo:

i. Kukosa utayari wa kufuata Sheria za Hifadhi ya Jamii kwa baadhi ya waajiri na waajiriwa hali inayopelekea kutokuwajibika katika uchangiaji na usajili wa waajiriwa wao.

ii. Kushuka kwa viwango vya faida katika uwekezaji wa soko la fedha duniani.
iii. Kukosekana kwa sera za uwekezaji wa nyumba za gharama nafuu na sera za kikodi kwa wawekezaji na kunapelekea Mfuko kushindwa kutimiza malengo yake ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu kwa wananchi.

**5.0 Hatua za Kuondoa Changamoto Zilizojitokeza**

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar umepanga kufanya yafuatayo ili kuondoa changamoto zilizojitokeza: -

i. Kuendelea kutoa elimu kwa waajiri na waajiriwa pamoja na wachangiaji wa hiari juu ya umuhimu wa kujisajili na kuchangia.
ii. Kuwachukulia hatua kwa waajiri wanaokiuka Sheria.
iii. Kuendelea kutafuta fursa za uwekezaji zenye tija pamoja na kuongeza juhudi katika utafutaji wa masoko yenye faida ndani na nje ya nchi kwa mustakabali mpana wa uhimilivu wa Mfuko.
iv. Kuendelea na mazungumzo na Serikali na mamlaka husika juu ya uanzishwaji wa sera ya uwekezaji wa nyumba za gharama nafuu ili kuwezesha taasisi za Serikali kushiriki katika uwekezaji huo kwa lengo la kuwasaidia wananchi wenye kipato cha chini ili kumudu gharama za makazi.

***5.6 Idara ya Maendeleo ya Ushirika***

Idara ya Maendeleo ya Ushirika Zanzibar ipo chini ya Afisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji - Zanzibar. Idara hii ina dhamana ya kusimamia maendeleo na shughuli za Vyama vya Ushirika Zanzibar. Idara imeanzishwa rasmi mwaka 1980, kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Zanzibar Nambari 3 ya mwaka 1979. Kwa sasa Idara ya Maendeleo ya Ushirika inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Nambari 15 ya mwaka 2018, Sera ya Maendeleo ya Ushirika 2014 na kanuni mbili (Kanuni ya SACCOS na kanuni ya Vyama vya Uzalishaji) za mwaka 2019.

**5.6.1 Maendeleo ya Ushirika Zanzibar**

1. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Idara ya Maendeleo ya Ushirika, pamoja na mambo mengine imefanikiwa kutekeleza yafuatayo: -
   i. Imesajili Vyama vya Ushirika 1,352 (Unguja 735; Pemba 617), kati ya hivyo SACCOS 2 vyama vya uzalishaji na utoaji huduma 1,350. Vyama

hivi vinafanya miradi ya Biashara ndogo ndogo, ufugaji wa ngo'mbe, kuuza mbao, biashara ya duka, kupamba na uchoraji, uchongaji, kudarizi, uvuvi, kilimo mchanganyiko, fundi gereji na Ufugaji kuku. Zoezi hili limeongeza idadi ya vyama vilivyosajiliwa kufikia 7,621 (Unguja 3,697; Pemba 3,924).

ii. Imekagua hesabu za Vyama vya Ushirika 211 (Unguja 106 na Pemba 105). Kaguzi hizo zimeonyesha dosari mbali mbali zikiwemo uhaba wa elimu juu ya uendeshaji na usimamizi wa Vyama, (ukosefu wa bajeti na mpango kazi, usimamizi wa fedha na mbinu za kubuni miradi ya uzalishaji). Idara imejipanga kutoa mafunzo na ushauri juu ya dosari zilizoonekana kupitia ukaguzi uliofanywa.

iii. Imefanya ukaguzi wa kawaida; imefuatilia uendeshaji wa shughuli za Vyama, utunzaji wa vitabu, ufuatwaji wa Sheria katika Vyama vya Ushirika na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Vyama 444 (Pemba 295; Unguja 149) sawa na asilimia 44.4% ya utekelezaji. Aidha jumla ya SACCOS saba (7) Zimekata leseni zikiwemo Mawasu SACCOS, Makuli Multipurpose, Dhowshed SACCOS, Melinne SACCOS, BoT SACCOS, Boresha Maisha yako SACCOS na Johari SACCOS.

iv. Imetoa mafunzo juu ya mabadiliko ya mtazamo, kujitambua, dhana ya Ushirika, Uongozi na utawala bora kwenye ushirika, muundo na uongozi wa ushirika, Dhana ya SACCOS.Jumla ya washiriki 8,837 (wanawake 6,940; wanaume 1,897) kutoka vyama 1,812 (Unguja; 570: Pemba 1,242) walipatiwa mafunzo hayo. Sawa na asilimia 55 ya utekelezaji ambapo Idara ilijipangia kutoa mafunzo hayo kwa wanachama na watendaji 16,000 kwenye vyama vya ushirika 2,300.

v. Idara imeadhimisha siku ya Ushirika Duniani ambapo kwa mwaka huu kilele cha maadhimisho hayo kilifanyika siku ya Jumamosi tarehe 6/7/2024 katika viwanja vya Skuli ya Jadida Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba. Maadhimisho hayo yaliambatana na Kongamano la Wanaushirika, usafi wa Mazingira katika maeneo ya hospitali ya Kinyasini Wilaya ya Wete Pemba, uchangiaji wa damu salama pamoja na dua ya kuwaombea waasisi, viongozi na wanaushirika wote waliotangulia mbele ya haki. Kauli mbiu ilikua ***"Ushirika hujenga Mustakabali bora kwa wote".***

v. Aidha, Kongamano lilifanyika siku ya Jumatano tarehe 4/07/2024 katika Ukumbi wa Baraza la Wawakilishi Wete Pemba, kongamano hilo lilishirikisha wawakilishi kutoka kwenye Vyama vya Ushirika vya Uzalishaji na SACCOS za Unguja na Pemba, wakiwemo ZASFICU, Muungano wa Vyama vya Ushirika Zanzibar (CUZA), Benki kuu ya Tanzania (BoT), na Maafisa kutoka Idara ya Maendeleo ya Ushirika. Kongamano hili lilitoa fursa kwa washiriki kujifunza mambo mengi yakiwemo umuhimu wa elimu na mafunzo ya Ushirika, chimbuko na mageuzi ya Ushirika nchini Tanzania kwa kupitia uzoefu wa Ushirika wa Nchi mbalimbali, mageuzi kwenye Vyama vya Ushirika. Jumla ya washiriki 253 (165 Wanawake na 88 wanaume) walishiriki na Kauli Mbiu ya kongamano hilo ilikuwa ni ***"Mifumo ya kidigitali katika kuendesha mageuzi ya Ushirika".***

vi. Idara imeshiriki katika maonesho ya siku ya chakula duniani yaliyofanyika katika viwanja vya Chamanangwe, Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba, ambapo wanaushirika, vikundi pamoja na wajasiriamali mbali mbali walitembelea banda letu na kujipatia taaluma pamoja na ushauri, kwa upande wa Vyama vya Ushirika vilivyotembelea banda letu vilieleza kwamba vinakabiliwa na changamoto ya masoko na nembo ya ubora ambapo walipatiwa ushauri na kuunganishwa na Taasisi husika.

vii. Kuviunganisha Vyama vya Ushirika na Asasi za Fedha; Idara imeviunganisha vyama 225 (Unguja 139) CRDB 59, PBZ 55, TADB 9, NMB 1 na Equity 15); (Pemba 86) PBZ 18, CRDB 16, TCB 52) na Kufungua Hesabu zao katika Benki hizo lengo ni kurahisisha upatikanaji wa mikopo pia kuwa na usalama wa kuhifadhi fedha za wanachama.

viii. Idara imesimamia Mikutano kwa Vyama vya Ushirika, Jumla ya vyama 35 vilifanya Mikutano hiyo. Aidha Mikutano hiyo ilikuwa ni Mikutano Mikuu ya mwaka, na ya Uchaguzi. Lengo la mikutano hiyo ni kuidhinisha Bajeti na Mipango kazi, kupokea ripoti mbali mbali za kamati ya Uongozi pamoja na ripoti ya Mkaguzi, kujadili utekelezaji wa shughuli za Ushirika, kuchangamkia fursa za uzalishaji, kuthibitisha wanachama wapya na kuwatoa wanachama na viongozi waliokosa sifa za kuwa wanachama na kuchagua Viongozi wapya wa Vyama vya Ushirika, kuboresha usimamizi wa ushirika, kuboresha mashirikiano na vyama vyengine vya kifedha kwa lengo la kupata huduma za fedha

kutoka kwenye ushirika huo. Jumla ya washiriki wa mikutano hiyo ni 4,485 wakiwemo wanawake 2,555 na wanaume 1,930. Aidha, idara imeshiriki katika Mikutano ya kamati ya Mikopo ya 4:4:2 kwa lengo la kutathmini miradi iliyokaguliwa ambayo imeombewa mikopo kwa hatua ya awali katika Wilaya ambazo zimeanza kutoa mikopo hiyo.

ix. Idara imeshiriki katika kutatua Migogoro 10 (7 Unguja na 3 Pemba) chanzo cha migogoro hiyo ni kukiukwa kwa Sheria ndogo, madai ya haki za wanachama na utaratibu mbaya wa uendeshaji wa Vyama vya Ushirika, vyanzo hivi vya migogoro imepelekea kusimamishwa uanachama kiutokana na kukiuka taratibu za ushirika. Vyama vilivyohusika na migogoro hiyo ni Jitihada njema SACCOS, Makuli multipurpose na Ushirika wa Tusisahau vilivyopo Shehia ya Malindi, Mkokotoni SACCOS - Shehia ya Mkokotoni, Nguvu ya Chukwani, Twins Coop. Maungani, Hatubaguani Mtofaani kwa Unguja; Ushirika wa Mola Tubariki Shehia ya Kilindi Chake Chake, ushirika wa Fukara hanashauri uliopo shumba Mjini na Ushirika wa Hakina Shaka uliopo Mtambwe Wete. Matokeo, migogoro hiyo imeweza kusuluhishwa kwa kuwaita Viongozi na wanachama kwa lengo la kupata suluhisho na kupewa Elimu na wanachama kupatiwa haki zao.

x. Kwa kushirikiana na Wataalam wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi Idara imefanya Utafiti wa Mageuzi ya Vyama vya Ushirika. Lengo la Utafiti ni kujua hali halisi ya Ushirika Nchini, mafanikio, changamoto na fursa zilizopo ili kupata taarifa ya kuiwezesha Serikali kwa lengo la kufanya Mageuzi ya Sekta ya Ushirika nchini. Zoezi hili limejumuisha sampuli ya Vyama 352 kutoka Shehia 131 (61 Unguja na 70 Pemba). Aidha ripoti ya utafiti na mikakati ya utekelezaji tayari imeshakamilika na imeshakabidhiwa uongozi wa Wizara na baadhi ya mikakati hiyo imeingizwa kwenye bajeti ya mwaka 2025 kwa ajili ya utekeleza.

xi. Idara imeratibu upatikanaji wa ziara za mafunzo kwa Vyama 2 ambavyo ni Ushirika wa Jambo nia Mzuri Makunduchi na Furahia Wanawake uliopo Paje. Vyama hivyo vilibahatika kushiriki katika Maonyesho ya Bidhaa na Tamaduni za Kitaifa yaliyofanyika Wilaya ya Songea Mkoa wa Ruvuma. Pia vyama 4 vilipata msaada wa malighafi (usumba) kwa uzalishaji wa madometi. Vyama hivyo ni Jambo Nia, Tufahamiane, Imani yetu na Tusibabaishwe vyote kutoka katika Wilaya ya Kusini Unguja.

Ziara za kujenga ya ushirikiano baina ya Zanzibar na Tanzania Bara kwa Idara ya Maendeleo ya Ushirika na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) imefanyika. Ziara hiyo ilifanyika Dodoma lengo ni kubadilishana uzoefu katika kutekeleza shughuli za ushirika nchini na kuvifanya vyama vya ushirika kuimarika. Aidha, Idara ya Maendeleo ya Ushirika ilipata fursa ya kujifunza mfumo wa usimamizi wa vyama vya ushirika (MUVU), katika ziara hiyo wajumbe kutoka Zanzibar walipata fursa ya kuvitembelea vyama vya Ushirika vinne (4) zikiwemo SACCOS mbili (UDOM SACCOS na K.K.T SACCOS) pamoja na AMCOS mbili ambazo ni CHABUMA AMCOS ambayo inajishughulisha na kilimo cha Zabibu na Chinangari BBT AMCOS inajishughulisha na kilimo cha mboga mboga. Aidha, Idara ilipata fursa ya kutembelea Shirika la Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika Tanzania (COASCO) ambalo linakagua hesabu za Vyama vya Ushirika vya aina zote, shirika hili la uakaguzi lina kagua linakagua kwa kutumia mfumo maalum unaojulikana kwa jina la "COAMIS", mfumo umerahisisha kazi na muda wa ukaguzi, umepunguza gharama za kazi ya ukaguzi na umeongeza mapato ya kazi ya ukaguzi. Aidha, COASCO imeonyesha utayari wa kufanya kazi na Idara kwenye utoaji wa mafunzo kwa Wakaguzi wa hesabu za Vyama vya Ushirika wa Idara. Vile vile, Idara ya Maendeleo ya Ushirika imesaini makubaliano ya ushirikiano na Tume ya Maendeleo ya Ushirika

### 5.6.2 Mafanikio

Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: -

i. Idara imefanikiwa kufanya Utafiti wa Mageuzi ya Vyama vya Ushirika. Lengo la Utafiti ni kujua hali halisi ya Ushirika Nchini, mafanikio, changamoto na fursa zilizopo ili kupata taarifa ya kuiwezesha Serikali kwa lengo la kufanya Mageuzi ya Sekta ya Ushirika nchini. Aidha ripoti ya utafiti na mikakati ya utekelezaji tayari imeshakamilika na imeshakabidhiwa uongozi wa Wizara na baadhi ya mikakati hiyo imeingizwa kwenye bajeti ya mwaka 2025 kwa ajili ya utekeleza.

ii. Kukua kwa Demokrasia katika SACCOS; kwa sasa SACCOS zimepata muamko na kufanya uchaguzi wa kuchagua viongozi wapya ambao wataendeleza shughuli za ushirika zinaendesha Mikutano yao na wanachama wanapata fursa ya kuhoji na kupata maelezo ya kutosha juu ya shughuli zinazoandaliwa na SACCOS zao kupitia Mikutano Mikuu.

Hii ni kutokana na kufuatwa kwa sheria na kanuni za ushirika na pia taaluma za Ushirika kwa wanachama na viongozi wa SACCOS.

iii. Matumizi ya mifumo "System": Baadhi ya SACCOS tayari zinatumia mifumo ya kuweka taarifa zao. SACCOS zenyewe ni BoT SACCOS, Uwezeshaji SACCOS, Beach Porter SACCOS, Watanga SACCOS, Melinne SACCOS. Afya SACCOS na Elimu SACCOS Tanzania kwa lengo la kuimarisha na kukuza sekta ya Ushirika nchini, makubaliano hayo yaliwekwa saini tarehe 13 Machi, 2025.

**Changamoto:**

**i. Uhaba wa vitendea kazi:** Idara kwa sasa inatumia vitendea kazi vya zamani ambavyo ni chakavu haviendani na mabadiliko yaliyopo.

**ii. Uhaba wa wafanyakazi katika kitengo cha Usimamizi wa Vyama vya ushirika:** Idara kwa sasa imebakiwa na mtendaji mmoja tu katika kitengo cha Usimamizi wa vyama vya ushirika kutokana na kustaafu kwa wafanyakazi na uhamisho wa watendaji ambao walikua katika kitengo hicho.

**5.6.3 Changamoto Zinazozikabili SACCOS za Zanzibar**

i. Utekelezaji wa Sheria; Baadhi ya SACCOS hawatekelezi sheria hivyo kupelekea kutokezea migogoro kwenye vyama vyao na ukiukwaji wa utkelezaji wa majukumu yao. Katika kulitatua hili Idara inaendelea kutoa taaluma ya Sheria na kanuni za ushirika ili kupunguza migogoro kwenye vyama vyetu.

ii. Ujuzi wa utumiaji wa vitabu vya Hesabu; SACCOS nyingi za Vijini hazina ujuzi wa kutosha katika kutumia vitabu vya hesabu, hali hii inapelekea vyama hivyo kukosa kumbukumbu za hesabu. Katika kulitatua hili Idara tayari imeanzisha programu za mafunzo ambazo zimejumuisha somo la uwekaji wa kumbukumbu na namna ya kurikodi taarifa za fedha kwenye vyama vya ushirika.

iii. Kuibua mbinu za uwekezaji (taaluma ya Ujasiriamali); baadhi ya vyama vya ushirika havina taaluma ya ujasiriamali hali hii inapelekea kukosa kuwa na vyanzo ambavyo vitawasaidia wanachama na ushirika kwa ujumla. Katika kulitatua hili Idara tayari imeanzisha programu za mafunzo ambazo zimejumuisha somo la Wajasiriamali katika vyama vya ushirika.

iv. Ucheleweshaji wa taarifa za SACCOS; Baadhi ya SACCOS zinachelewesha taarifa za mwenendo wa Ushirika wao hii hupelekea kutokupatikana kwa taarifa za Portfolio ndani ya wakati.

v. Baadhi ya Vyama kutokufungua Akaunti benki, Baadhi ya vyama vya ushirika hasa vya uzalishaji vinaweka fedha kwenye visanduku jambo ambalo linahatarisha usalama wa fedha za ushirika.

vi. Baadhi ya Vyama kutokutumika kwa vitabu sahihi vya uandishi wa kumbukumbu za hesabu, hasa vyama vya uzalisahji ambapo hutumia madaftari ya kawaida. Hii pia inapelekea baadhi ya taarifa za hesabu kupotea.

vii. Kutokuwa na Bajeti: Baadhi ya vyama vya ushirika haviweki bajeti ya matumizi kwa mwaka unaofuata na pia wanatumia kinyume a bajeti yaani wanazo lakini hawazitumii. Hii inapelekea kutumia gharama kubwa za uzalishajiambapo tija inayopatikana ni ndogo au kupelekea hasara.

viii. Uhaba wa vitendea kazi: Idara kwa sasa inatumia vitendea kazi vya zamani ambavyo ni chakavu haviendani na mabadiliko yaliyopo. Idara ina Gari na Vespa ambazo pia zishakua chakavu. Katika kutatua changamoto hii Idara imejipanga kufanya manunuzi ya gari moja na honda mbili kwa shughuli za ufuatiliaji wa vyama, Idara itanunua kompyuta 4 ili kurahishisha shughuli za kiutendaji za kiofisi.

ix. Uhaba wa wafanyakazi kasa katika kitengo cha Usimamizi wa Vyama vya ushirika: Idara kwa sasa imebakiwa na mtendaji mmoja tu katika kitengo cha Usimamizi wa vyama vya ushirika kutokana na kustaafu kwa wafanyakazi na uhamisho wa watednaji ambao walikua katika kitengo hichi. Katika kulitafutia ufumbuzi suala hili idara kupitia Idara ya Utumishi na Uendeshaji (ORKUU) imepeleka maombi ya wafanyakazi wapya kada ya Wakaguzi na Maafisa Ushirika katika Wizara ya Utumishi wa UMMA.

### 5.6.4 Matarajio na Muelekeo kwa Sekta ya Fedha Machi 2025.

i. Kuwa na Mfumo wa Msimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU) ambao utarahishisha shughuli za ushrika Nchini;

ii. Kuwa na Sheria na Kanuni za Vyama vya Ushirika zilizofanyiwa mapitio;

iii. Tuwe na SACCOS zilizo imara kupitia Uhakiki maalum kwa Vyama vya SACCOS Zanzibar;

iv. Kutoa Mafunzo kwa Wanachama, Viongozi na Watendaji wa SACCOS.

### 5.6.5 Mpango wa Utekelezaji kwa mwaka wa Fedha 2025/2026.

Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Programu ya Usimamizi na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika imejipanga kufanya mambo yafuatayo:

i. Kufanya usajili vyama 2000 Unguja na Pemba;
ii. Kufanya ukaguzi wa hesabu kwa vyama 500 (Unguja na Pemba);
iii. Kufanya ufuatiliji na ukaguzi wa kawaida kwa vyama 1000 Unguja na Pemba;
iv. Kutoa mafunzo kwa wanachama 1800 na watendaji 9000 wa Vyama vya Ushirika;
v. Kufanya mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Ushirika Zanzibar 2014, Sheria ya Vyama vya Ushirika Namba 15 ya mwaka 2018, na Kanuni za Vyama vya Ushirika 2019;
vi. Kukuimarisha mashirikiano baina ya Idara ya maendeleo ya ushirika, Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) na Chuo cha Ushrika Moshi (MoCU).

# SURA YA TANO

## 5.0 SEKTA YA MIUNDOMBINU

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea na juhudi za kuimarisha miundombinu ya nchi ili kurahisisha upatikanaji wa huduma muhimu kwa wananchi wake. Sekta ya miundombinu ni miongoni mwa kichocheo kikubwa cha ukuaji wa uchumi wa nchi, maendeleo ya jamii na kukuza uwekezaji katika sekta mbalimbali kama vile biashara na utalii. Sekta hii ni muhimu katika upatikananji wa huduma muhimu kwa wananchi pamoja na kuchangia Pato la Tifa.

### 5.1 Wakala wa Barabara

Hii ni Taasisi yenye kujitegemea ambayo imeundwa kwa Sheria Nambari 11 kifungu Nambari 3 (1) ya mwaka 2019. Taasisi hii imetokana na mageuzi yaliyofanywa ya muundo wa Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara (UUB) kwa lengo la kuimarisha huduma zinazotolewa na taasisi hiyo. Hata hivyo, Serikali iliiwezesha Wakala wa barabara kwa kuwapatia za vifaa vipya na rasilimali watu ilikuingia katika soko la ushindani na mapato yanayopatikana katika biashara na shughuli zinazofanywa na wakala, yanatumika kuendeshea kazi zao za kila siku.

Mwaka 2024 Zanzibar ina barabara zenye urefu wa kilomita 1,622.97 kati ya hizo zenye lami ni kilomita 1,023.42 na zisizo na lami ni kilomita 599.55. Barabara Kuu ni kilomita 358.31, Barabara za Vijijini kilomita 572.23 barabara za Mijini ni kilomita 128.83 na barabara za Ndani ni kilomita 563.55 (Jadweli nambari 23).

**Jadweli Nambari 23: Mchanganuo wa Barabara za Zanzibar kwa mwaka 2024**

| Aina za Barabara | Urefu (km) | Zenye Hali Nzuri | | Zilizo Afadhali | | Zenye Hali Mbaya | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | km | Asilimia (%) | km | Asilimia (%) | km | Asilimia (%) |
| Barabara Kuu za Lami | 358.31 | 240.24 | 67.05 | 28.72 | 8.01 | 89.35 | 24.94 |
| Barabara Kuu zisizokua na lami | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 |
| Barabara za Vijijini zenye lami | 386.02 | 277.30 | 71.84 | 16.36 | 4.23 | 92.36 | 23.93 |
| Barabara za Vijijini zisizokua na lami | 186.32 | 41.53 | 22.30 | 75.71 | 40.66 | 68.97 | 37.034 |
| Barabara za Mjini zenye lami | 87.50 | 73.28 | 83.75 | 14.22 | 16.25 | 0.00 | 0.00 |
| Barabara za Mjini zisizokua na lami | 41.33 | 0.00 | 0.00 | 17.64 | 42.68 | 23.69 | 57.32 |
| Barabara za ndani zenye lami | 191.54 | 126.89 | 66.25 | 21.44 | 11.19 | 43.21 | 22.56 |
| Barabara za Ndani zisizokua na lami | 372.01 | 92.67 | 24.91 | 136.57 | 36.71 | 142.77 | 38.38 |
| **Jumla (km)** | **1,622.92** | **851.91** | **52.47** | **310.66** | **19.14** | **460.35** | **28.37** |

***Chanzo:* *Wakala wa Barabara, 2025***

### 5.1.1 Mchanganuo wa Matumizi ya Fedha Kwa Ujenzi Wa Barabara Kwa Mwaka Wa Fedha (Julai 2024-Machi 2025).

Kwa kipindi cha Julai 2024 – Machi 25, jumla ya TZS 11.1 bilioni zimetumika kwa ajili ya kufanya ukarabati katika maeneo mbali mbali kwa matengenezo ya muda maalum kama vile Ujenzi wa Barabara mbalimbali za ndani zenye urefu wa km 6.7 kwa kiwango cha lami, Ujenzi wa barabara ya Mchangani (Dunga) - Msikitini kilomita 1.1 kwa kiwango cha lami, Ujenzi wa barabara ya Mgelema- Wambaa yenye urefu wa kilomita 4.2 kwa Kiwango cha Lami. ***(Jadweli nambari 24).***

**Jadweli Nambari 24: Mchanganuo wa Matumizi ya Fedha kwa Ujenzi wa Barabara kwa Mwaka wa Fedha Unguja na Pemba, (2024/2025)**

| | AINA YA KAZI | KILOMITA | GHARAMA (FEDHA), MILIONI |
|---|---|---|---|
| | Ujenzi wa Barabara mbalimbali za ndani zenye urefu wa km 6.7 kwa kiwango cha lami<br>Chuo kikuu cha Abrahman Al Sumait<br>Mwakaje (selemu) – Mbuzini<br>Barabara ya Chuo cha Karume (KIST)<br>Barabara ya Mahakama Kuu Tunguu – Istiqama<br>Barabara ya Kisauni – Mbuyuni | **6.7** | **2,257.04** |
| | Ujenzi wa Barabara ya Mchangani (Dunga) - Msikitini km 1.1 kwa kiwango cha lami | 1.1 | **706.14** |
| | Ujenzi wa barabara za ndani za Kizimkazi zenye jumla ya urefu wa kilomita 6.59 kwa kiwango cha lami<br>Barabara inayounganisha barabara kuu na viwanja vya mpira wa miguu<br>Barabara inayounganisha barabara kuu na Hospital<br>Barabara ya Hospital-Sports stadium (Mgombewa)<br>Barabara inayotoka Msikiti ya Kihistoria -Mama Samia<br>Barabara ya Hema roundabout- Machomwe<br>Barabara ya Tawi la CCM Dimbani CCM-Kituo cha kuuza mafuta<br>Barabara inayounganisha barabara kuu na kiwanja cha kufurahishia Watoto | **6.59** | **5,472.32** |
| | Ujenzi wa Barabara ya Mgelema- Wambaa yenye urefu wa kilomita 4.2 kwa Kiwango cha Lami | 4.2 | **2,120.00** |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Ujenzi wa barabara za ndani kwa kiwango cha kifusi kwa hatua ya kwanza km 3 kwa kiwango cha kifusi,<br>Mahuduthi-Sipwese<br>Kirimdomo-Kihogoni<br>Chwaka ndogo<br>Mtamba na Kitondooni | 3.0 | **193.15** |
| | Matengenezo ya dharura (Emergence work) Unguja na Pemba;<br>matengenezo kwa kiwango cha kifusi barabara ya Kicha-Chwaka km 1.8<br>matengenezo ya kalavati iliyokatika Mambosasa Minanasini | 1.8 | **90.00** |
| | Matengenezo ya Kawaida ya Barabara viraka (Routine patchwork); -<br>Uzibaji wa Mashimo kwenye barabara zilizojengwa kwa lami Unguja<br>Uzibaji wa Mashimo kwenye barabara zilizojengwa kwa lami Pemba | Mita za mraba 8,945<br><br>Mita za mraba16,213 | **280.00** |

***Chanzo : Wakala wa Bara Bara Zanzibar 2025***

## 5.3 Nishati ya Umeme.

Nishati ya umeme ni nyenzo muhimu katika kufikia maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Nishati hutumika kwa shughuli mbalimbali zikiwemo miradi ya uwekezaji, viwandani na majumbani. Idadi ya wateja waliounganishwa na huduma ya umeme katika gridi ya taifa imepungua na kufikia wateja 32,547 mwaka 2024 ikilinganishwa na wateja 35,838 mwaka 2023 sawa na upungufu wa asilimia hasi 2.1 Upungufu huo ni kutokana na kukamilika kwa baadhi ya miradi ya ujenzi na uwekezaji. ***(Jadweli nambari 25)***.

**Jadweli Nambari 25: Idadi ya Wateja Wapya Waliounganishwa na Gridi ya Taifa Zanzibar (2020 – 2024).**

| Eneo | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | Asilimia (%) ya ukuaji kwa mwaka 2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Unguja | 12,900 | 25,346 | 23,046 | 31,053 | 27,796 | -11.7 |
| Pemba | 2,526 | 7,703 | 4,974 | 4,785 | 4,751 | -0.71 |
| Zanzibar | 15,426 | 3,349 | 2,820 | 35,838 | 32,547 | -10.1 |

***Chanzo: Shirika la Umeme Zanzibar, 2025***

Kiwango cha umeme kilichosambazwa kimeongezeka na kufikia 671,732 kWh mwaka 2024 kutoka 560,702 kWh mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 19.8 Thamani ya mauzo ya umeme katika kipindi hicho imeongezeka na kufikia TZS 195,517 bilioni mwaka 2024 kutoka TZS 158,448 bilioni mwaka 2023. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa huduma za upatikanaji wa umeme katika mahoteli, viwandani na majumbani. (Jadweli nambari 26 na 27).

**Jadweli nambari 26: Kiwango cha Umeme kilichosambazwa (2020-2024) (KWH "000")**

| MAELEZO | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|
| Majumbani (Z 0) | 205 | 13 | 25 | 27 | 37 |
| Majumbani na Biashara (Z1) | 4,763 | 2,494 | 1,710 | 1,853 | 1513 |
| ViwandaVidogovidogo (Z 2) | 9,713 | 8,914 | 13,070 | 21,516 | 21,307 |
| Viwanda vya Kati na Vikubwa (Z3) | 109,447 | 142,154 | 162,707 | 182,799 | 206,380 |
| TUKUZA | 255,085 | 286,136 | 323,763 | 354,507 | 442,495 |
| **Jumla** | **379,213** | **439,711** | **501,275** | **560,702** | **671,732** |

***Chanzo: Shirika la Umeme Zanzibar, 2025***

**Jadweli Nambari 27: Thamani ya Umeme Uliosambazwa (2020 – 2024) (TZS Milioni)**

| MAELEZO | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|
| Majumbani (Z 0) | 43.0 | 2.9 | 7.7 | 7.9 | 10 |
| Majumbani na Biashara (Z1) | 2,124 | 698 | 479 | 520 | 903 |
| ViwandaVidogovidogo (Z 2) | 2,198 | 2,038 | 2,773 | 4,306 | 4230 |
| Viwanda vya Kati na Vikubwa (Z3) | 20,348 | 24,263 | 28,284 | 31571 | 38,291 |
| TUKUZA | 95,182 | 97,997 | 110,291 | 122,043 | 152,083 |
| **Jumla** | **119,895** | **124,999** | **141,835** | **158,448** | **195,517** |

***Chanzo: Shirika la Umeme Zanzibar, 2025***

## 5.4 Mamlaka ya Maji Zanzibar

Maji ni nishati muhimu kwa maisha ya wanadamu. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikitilia mkazo katika kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi wa Zanzibar na kuendelea kuvitunza na kuhifadhi vyanzo vya asili vya maji. Hili ni moja ya lengo la Serikali ya kuwaondolea wananchi changamoto za upatikanaji wa huduma muhimu ya maji safi na salama nakuimarisha maendeleo katika jamii. Kwa mwaka 2024 visima vinavyozalisha maji vimeongezeka na kufikia jumla ya visima 389 kutoka visima 309 mwaka 2023. Hii ni kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu na makaazi na kupelekea kuongezeka uchimbwaji wa visima katika maeneo hayo. ***(Jadweli nambari 28)***

**Jadweli Nambari 28: Visima Vinavyozalisha Maji na Kutoa Huduma (2020 – 2024)**

| Mkoa | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kaskazini Unguja | 49 | 46 | 46 | 47 | 51 |
| KusiniUnguja | 53 | 48 | 44 | 44 | 59 |
| MjiniMaghribi | 85 | 81 | 81 | 82 | 132 |
| Kaskazini Pemba | 48 | 48 | 49 | 53 | 53 |
| Kusini Pemba | 81 | 70 | 81 | 83 | 94 |
| **Total** | **316** | **293** | **301** | **309** | **389** |

***Chanzo: Mamlaka ya Maji Zanzibar, 2025***

### 5.4.1 Usimamizi na Uendelezaji Rasilimali Maji na Utatuzi wa Changamoto za Maji.

Mamlaka ya Maji Zanzibar bado ipo kwenye hatua za kutatua tatizo la uvamizi na uharibifu katika maeneo ya vianzio vya maji na kufanya shughuli ambazo hazistahiki katika sehemu hizo kama vile kilimo, ufugaji, ujenzi wa nyumba za makaazi. Wanachi wanazidi kupata uelewa juu ya umuhimu wa kutunza vyanzo vya maji na kushirikiana na Serikali katika kuunga mkono hatua za Mamlaka ya Maji ya kuvitunza vyanzo hivyo. Kwa mwaka 2024, imeibuka migogoro 398 inayohusiana na maeneo ya uzalishaji wa maji, kati ya hiyo migogoro 298 imetatuliwa na 100 bado inaendelea kupatiwa ufumbuzi. Aidha, Mamlaka ya Maji Zanzibar inaendelea kuchukua juhudi za kutatua migogoro iliyobakia. ***(Jadweli nambari 29).***

**Jadweli Nambari 29: Migogoro ya Watumiaji Maji Iliyopatiwa Ufumbuzi (2020-2024)**

| Hali ya migogoro | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|
| Migogoro iliyomalizika | 0 | 3 | 5 | 120 | 298 |
| Migogoro inayoendelea | 0 | 6 | 2 | 2 | 100 |
| **Jumla** | **0** | **9** | **7** | **122** | **398** |

***Chanzo: Mamlaka ya Maji Zanzibar, 2025***

### 5.4.2 Huduma ya Maji Vijijini

Mamlaka ya Maji Zanzibar kwa mwaka 2024, imeweza kusimamia na kuendelea kusambaza huduma ya maji safi na salama ili kurahisisha shughuli za maendeleo Unguja na Pemba. Hata hivyo, miradi (8) ya usambazaji maji imetekelezwa katika kipindi cha mwaka 2024 sawa na miradi (5) iliyotekelezwa mwaka 2023. Katika miradi hiyo, mradi (1) umetekelezwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na miradi (7) imetekelezwa chini ya ufadhili wa Washirika wa Maendeleo. Huu ni mwendelezo wa nia njema ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kuhakikisha kila mwananchi anapata maji safi na salama, ***(Jadweli nambari 30).***

**Jadweli Nambari 30: Idadi ya Miradi ya Maji na Wafadhili (2020-2024)**

| Aina ya Ufadhili | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|
| Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar | 1 | 1 | 1 | 2 | 1 |
| Washirika wa Maendeleo | 2 | 1 | 1 | 3 | 7 |
| **Jumla** | **3** | **2** | **2** | **5** | **8** |

***Chanzo: Mamlaka ya Maji Zanzibar, 2025***

**Jadweli Nambari 31: Juhudi, Huduma, na Mchanganuo na Taarifa ya Utekelezaji wa Huduma ya Maji Mkoa wa Mjini kwa mwaka 2024**

| Na. | TAARIFA | MAELEZO |
|---|---|---|
| 1. | Juhudi zinazochukuliwa kuwafikia wasiopata huduma ya maji. | Mamlaka ya Maji Zanzibar kwa mwaka *2024* ilifanya juhudi za kusambaza huduma kwa kutekeleza Miradi ya maji kwa maeneo ambayo huduma ya maji haijafika au hakuna mtandao wa maji.<br>Jumla ya Skimu ***6*** (Skimu ya Kidutani, Skimu ya Maungani, Simu ya Dimani, Skimu ya Masingini, Skimu ya Dole na Skimu ya Mfenesini) za Mkoa wa Mjini kupitia **Mradi wa Uhaulishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar** uliyotekelezwa kwa Mkopo wa Benki ya Exim India **USD milioni 92.18.**<br>Vilevile; jumla ya **Shehia 36** zikiwemo (Dimani, Maungani, Masingini, Mfenesini, Kwarara, Fumba, Kijichi n.k) zinaendelea kunufaika na mradi husika. |
| 2. | Huduma za maji Mkoa Mjini 2024. | Mamlaka ya Maji Zanzibar kwa mwaka 2024 Kwa upande wa Mkoa wa Mjini imelaza jumla **kilomita 403.06** kupitia *Mradi wa Uhaulishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar* pamoja na juhudi za kazi za kawaida za Mamlaka ya Maji Zanzibar ambapo jumla ya **mita 26,302**.<br>Hivyo; kufanya jumla ya **kilomita 429.362** kwa mwaka *2024***.** |
| 3. | Mchanganuo/mfumo wa usambazaji maji Mjini | Mamlaka ya Maji Zanzibar inaendelea kutoa huduma kupitia mifumo miwili mikuu.<br>• Usukumaji wa moja kwa moja (Direct Pumping) na<br>• Mifumo ya kuhifadhi maji kwenye matangi (Storage Tanks).<br>Kwa mwaka *2024* Mkoa wa Mjini Magharibi, jumla ya matangi ***13*** (Dole-**2**, Kwarara-Kidutani – **3**, Masingini – **2**, Dimani – **2**, Maungani - **2** na Mfenesini – **2**) yamejengwa kwa lengo la kusambaza huduma ya maji kwa ufanisi zaidi badala ya kutumia mfumo wa usukumaji wa moja kwa moja (Direct Pumping) kunakopelekea kuharibika kwa pampu mara kwa mara. |

***Chanzo: Mamlaka ya maji Zanzibar (Land Water) 2025***

Serikali inaendelea na mikakati ya kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi wa Zanzibar kwa lengo la kuwaondolea usumbufu wanachi wake kupata huduma hiyo kwa wakati na uhakika kwa Serikali na washirika wa Maendeleo Exim Bank, India Dola za Kimarekani 92.18 milioni. Vilevile; jumla ya Shehia 36 zikiwemo (Dimani, Maungani, Masingini, Mfenesini, Kwarara, Fumba, Kijichi ) zinaendelea kunufaika na Mamlaka ya Maji Zanzibar inaendelea kutoa huduma kupitia mifumo miwili mikuu.

A. Usukumaji wa moja kwa moja (Direct Pumping); na
B. Mifumo ya kuhifadhi maji kwenye matangi (Storage Tanks). Mifumo hiyo husaidia kupeleka maji kwenye matangi jumla ya matangi 13 (Dole-2, Kwarara-Kidutani – 3, Masingini – 2, Dimani – 2, Maungani - 2 na Mfenesini – 2) yamejengwa kwa lengo la kusambaza huduma ya maji kwa ufanisi zaidi.

**Jadweli Nambari 32: Idadi ya Miradi Mipya ya Maji Vijijini (2020-2024)**

| Miradi | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|
| Maendeleo ya miundo mbinu ya maji | 3 | 9 | 1 | 2 | 0 |
| Uchimbaji wa visima | 1 | 0 | 28 | 0 | 0 |
| Usafishaji maji | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **4** | **9** | **29** | **2** | **0** |

***Chanzo: Mamlaka ya Maji Zanzibar, 2025***

Vile vile kwa mwaka 2024, Mamlaka ya Maji Zanzibar imeweza kuzalisha na kusambaza maji jumla ya **Cubic Meter 223.7** milioni na kukusanya TZS 3,317 bilioni kwa mikoa yote ya Unguja na Pemba. Uzalishaji huo wa maji ni upungufu wa asilimia 18.9 ya mahitaji yote ya maji ya **Cubic Meter 276** milioni.

**Jadweli Nambari 33: Ukusanyaji Mapato, Uzalishaji na Usambazaji Maji (2024)**

| Mwaka | Jumla ya uzalishaji wa maji *(Milion Cubic meter)* | Makadirio ya mahitaji ya maji Milioni *(Cubic meter)* | Upungufu katika mahitaji ya maji *(percent)* | Ukusanyaji wa mapato |
|---|---|---|---|---|
| **2020** | 42.3 | 60.7 | 30.40 | 2,407 |
| **2021** | 131.8 | 240.7 | 45.20 | 2,613 |
| **2022** | 108.5 | 188.6 | 42.4 | 2,271 |
| **2023** | 192 | 276 | 30 | 2,127 |
| **2024** | 223.7 | 276 | 18.9 | 3,317 |

***Chanzo: Mamlaka ya Maji Zanzibar, 2025***

# SURA YA SITA

## 6.0 SEKTA YA ELIMU

### 6.1 Elimu na Mafunzo ya Amali

Uwekezaji katika rasilimali watu ni jambo muhimu linaloendelea kutiliwa mkazo kitaifa na kimataifa. Elimu inaanza tokea elimu ya msingi na kuendelea na elimu ni haki ya msingi ya binaadamu katika kukuza na kuendeleza maendeleo ya uchumi wa nchi. Serikali inaendelea kuwekeza katika sekta ya elimu kwa ujenzi wa skuli mpya zenye vifaa vya kisasa vya maabara na kushajihisha wanafunzi kwa kuendelea kuwapa hamasa pale wanapofaulu kwa madaraja ya juu na kuondoa michango ya wanafunzi. Kuwekeza katika sekta ya elimu kunalihakikishia Taifa kuwa na wataalamu na kuweza kutatua changamoto za maendeleo za sasa na baadae.

Kwa mwaka 2024 idadi ya Skuli za Maandalizi zimepungua kufikia skuli 349 kutoka skuli 599 mwaka 2023, (kati ya Skuli hizo, Serikali ina jumla ya skuli 67 mwaka 2024 kutoka skuli 56 mwaka 2023 na skuli Binafsi ni 282 mwaka 2024 kutoka skuli 543 mwaka 2023 sawa na upungufu wa asilimia 41.7. Hii inatokana na baadhi ya skuli kupandishwa daraja na baadhi ya skuli binafsi kufutiwa usajili kutokana na kutokufikiwa kwa vigezo.

Skuli za Msingi mwaka 2024 zimefikia 627 kutoka skuli 576 mwaka 2023, ambapo (mwaka 2024 skuli za Serikali zimefikia 328 kutoka skuli 326 mwaka 2023) na skuli Binafsi mwaka 2024 zimefikia skuli 299 kutoka skuli 250 mwaka 2023.

Skuli za Sekondari mwaka 2024 zimepungua na kufikia skuli 236 kutoka skuli 245 mwaka 2023 (jumla ya skuli za Serikali ni 217 kwa mwaka 2024 kutoka skuli 216 mwaka 2023 na skuli Binafsi ni 19 mwaka 2024 kutoka skuli 29 mwaka 2023). Vyuo vya Amali (13), Taasisi nne (4) na Vyuo Vikuu ni vitatu (3). Idadi ya wanafunzi waliopata fursa ya kujiunga na elimu ya Maandalizi mwaka 2024 imeongezeka na kufikia wanafunzi 103,581 kutoka wanafunzi 102,908 mwaka 2023. Hii inatokana na wazazi wengi kuwapeleka watoto wao kuanza skuli za msingi moja kwa moja. Hata hivyo, idadi ya wanafunzi wanaoendelea na masomo katika skuli za Msingi za Serikali na Binafsi kwa mwaka 2024 imeongezeka na kufikia wanafunzi 391,388 kutoka wanafunzi 380,638 sawa na ongezeko la asilimia 3. Hii inatokana na uhamasishaji uliopelekea mwamko kwa

wazazi uliosabaibishwa na utoaji wa elimu kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

### 6.1.1 Idadi ya Wanafunzi: Maandalizi, Msingi, Kati na Sekondari kwa Skuli za Serikali

Kwa mwaka 2024 jumla ya wanafunzi 111,273 wameandikishwa katika skuli za Maandalizi na Msingi za Serikali kutoka wanafunzi 109,046 walioandikishwa kwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 2.0. Kwa upande wa skuli za Maandalizi za Serikali kwa mwaka 2024 zimepungua na kufikia 62,974 kutoka wanafunzi 63,732 mwaka 2023 sawa na upungufu wa asilimia 1.1. Kati ya hao, wanafunzi wa kiume kwa mwaka 2024 ni 31,573 kutoka wanafunzi 31,596 mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 0 na wanafunzi wa kike kwa mwaka 2024 ni 31,401 kutoka wanafunzi 32,136 mwaka 2023 sawa na upungufu wa asilimia 2.2.

Idadi ya wanafunzi wapya walioandikishwa darasa la kwanza katika skuli za Msingi za Serikali na Binafsi kwa mwaka 2024 imeongezeka na kufikia wanafunzi 48,299 ikilinganishwa na wanafunzi 45,314 waliondikishwa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 6.5. Kati ya hao wanafunzi wa kiume ni 24,795 kutoka wanafunzi 23,436 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 5.7, na wanafunzi wa kike ni 23,504 kutoka wanafunzi 21,878 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 7.4.  Hii ni kutokana na kuongezeka kwa uhamasishaji unaofanywa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na ukaribu wa skuli hizo kwa jamii.

Jumla ya wanafunzi katika skuli za Msingi za Serikali kwa mwaka 2020 -2024 imeongezeka na kufikia 391,388 kutoka wanafunzi 324,457 kwa mwaka 2019-2023 sawa na ongezeko la asilimia 20.6. Aidha, wanafunzi wa kiume wamefikia 197,294 kutoka wanafunzi 164,088 sawa na ongezeko la asilimia 20.2, wanafunzi wa kike wamefikia 194,094 kutoka wanafunzi 160,369 sawa na ongezeko la asilimia 21.

Idadi ya wanafunzi katika skuli za Sekondari (kuanzia Kidato cha Kwanza hadi cha Nne) kwa mwaka 2024 imeongezeka na kufikia wanafunzi 104,987 kutoka wanafunzi 92,510 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 13.4. Ambapo idadi ya wanafunzi wa kike imeongezeka na kufikia 57,124 kutoka wanafunzi 50,936 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 12.1 na idadi ya wanafunzi

wa kiume pia imeongezeka na kufikia 47,863 kutoka wanafunzi 41,574 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 15.1.

Idadi ya wanafunzi waliofaulu Kidato cha Pili kwa mwaka 2024 imepungua na kufikia wanafunzi 18,934 kutoka wanafunzi 27,571 mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 31, ambapo wanafunzi wa kiume ni 8,905 mwaka 2024 kutoka wanafunzi 11, 806 mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 24.5, na wanafunzi wa kike ni 10,029 mwaka 2024 kutoka wanafunzi 15,765 mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 36.

Kwa upande wa Kidato cha nne mwaka 2024, idadi ya wanafunzi waliofaulu imeongezeka na kufikia 21,338 kutoka wanafunzi 20,800 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 2.5, kati ya hao wanafunzi wa kiume ni 8,680 kutoka wanafunzi 8,469 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 2.4, na wanafunzi wakike ni 12,658 kutoka wanafunzi 12,331 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 2.6. Hii ni kutokana na mikakati na juhudi zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali pamoja na Wizara katika kuhakikisha elimu inakua nchini, pamoja kuweka mazingira mazuri ya kujifunzia ikiwemo mitandao ya kijamii ***(Jadweli nambari 34).***

**Jadweli Nambari 34: Idadi ya Wanafunzi wa Skuli za Sekondari za Serikali Kidato cha I-IV (2020-2024)**

| **Mwaka** | | **Kidato** | | | | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Jinsia** | **I** | **II** | **III** | **IV** | |
| 2020 | Wanaume | 15,385 | 14,958 | 11,021 | 8,796 | 50,159 |
| | Wanawake | 16,636 | 16,965 | 15,039 | 12,817 | 61,457 |
| | **Jumla** | **32,021** | **31,923** | **26,059** | **21,613** | **111,616** |
| 2021 | Wanaume | 15,445 | 14,964 | 10,688 | 8,897 | 49,994 |
| | Wanawake | 16,710 | 16,260 | 15,051 | 12,693 | 60,714 |
| | **Jumla** | **32,155** | **31,224** | **25,739** | **21,590** | **110,708** |
| 2022 | Wanaume | 7,610 | 13,670 | 8,922 | 9,206 | 39,408 |
| | Wanawake | 11,075 | 14,960 | 12,261 | 12,902 | 51,198 |
| | **Jumla** | **18,685** | **28,630** | **21,183** | **22,108** | **90,606** |
| 2023 | Wanaume | 12,841 | 9,138 | 10,658 | 8,937 | 41,574 |
| | Wanawake | 11,547 | 12,068 | 14,292 | 13,029 | 50,936 |
| | **Jumla** | **24,388** | **21,206** | **24,950** | **21,966** | **92,510** |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2024 | Wanaume | 18,739 | 11,571 | 7,747 | 9,806 | 47,863 |
| | Wanawake | 20,962 | 11,134 | 11,506 | 13,522 | 57,124 |
| | **Jumla** | **39,701** | **22,705** | **19,253** | **23,328** | **104,987** |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar, 2025***

### 6.1.2 Idadi ya Wanafunzi: Maandalizi, Msingi, Kati na Sekondari kwa Skuli za Binafsi

Kwa mwaka 2024 idadi ya wanafunzi walioandikishwa katika skuli za Maandalizi kwa skuli binafsi imeongezeka na kufikia 40,607 kutoka wanafunzi 39,176 kwa mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 3.6 ambapo wanafunzi wa kiume wamefikia 20,422 kutoka wanafunzi 19,492 kwa mwaka 2023, wanafunzi wa kike wamefikia 20,185 kutoka wanafunzi 19,684 kwa mwaka 2023.

Kwa mwaka 2024 Idadi ya wanafunzi kwa skuli za Msingi imeongezeka na kufikia 63,888 kutoka wanafunzi 56,181 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 13.7. Kati ya hao wanafunzi wa kiume wamefikia 31,702 mwaka 2024 kutoka 27,886 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 13.6 na wanafunzi wa kike wamefikia 32,186 mwaka 2024 kutoka 28,295 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 13.7.

Idadi ya wanafunzi katika skuli za Sekondari (Kidato cha Kwanza hadi cha Nne) kwa mwaka 2024 imeongezeka na kufikia wanafunzi 11,647 kutoka wanafunzi 11,030 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 5.5. Ambapo idadi ya wanafunzi wa kike imeongezeka na kufikia 6,174 kutoka wanafunzi 5,811 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 6.2 na idadi ya wanafunzi wa kiume pia imeongezeka na kufikia 5,473 kutoka wanafunzi 5,212 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 5. ***(Jadweli namba 35)***.

**Jadweli Nambari 35: Idadi ya Wanafunzi wa Skuli za Sekondari za Binafsi Kidato I-IV (2020-2024)**

| Mwaka | Kidato | | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Jinsia | I | II | III | IV | |
| 2020 | Wanaume | 1,609 | 1,402 | 1,553 | 1,359 | 5,923 |
| | Wanawake | 1,748 | 1,617 | 1,823 | 1,766 | 6,954 |
| | **Jumla** | **3,357** | **3,019** | **3,376** | **3,125** | **12,877** |
| 2021 | Wanaume | 1,608 | 1,501 | 1,403 | 1,282 | 5,794 |
| | Wanawake | 1,665 | 1,527 | 1,837 | 1,602 | 6,631 |
| | **Jumla** | **3,273** | **3,028** | **3,240** | **2,884** | **12,425** |
| 2022 | Wanaume | 1,590 | 1,522 | 1,586 | 1,227 | 5,925 |
| | Wanawake | 1,742 | 1,613 | 1,769 | 1,634 | 6,758 |
| | **Jumla** | **3,332** | **3,135** | **3,355** | **2,861** | **12,683** |
| 2023 | Wanaume | 605 | 1,517 | 1,672 | 1,418 | 5,212 |
| | Wanawake | 475 | 1,766 | 1,898 | 1,672 | 5,811 |
| | **Jumla** | **1,080** | **3,283** | **3,570** | **3,090** | **11,023** |
| 2024 | Wanaume | 1,696 | 557 | 1,620 | 1,600 | 5,473 |
| | Wanawake | 1,919 | 517 | 1,891 | 1,847 | 6,174 |
| | **Jumla** | **3,615** | **1,074** | **3,511** | **3,447** | **11,647** |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar, 2025***

### 6.1.3 Idadi ya Wanafunzi wa Skuli za Sekondari kwa Jinsia kwa Skuli za Serikali na Binafsi.

Idadi ya wanafunzi wa Kidato cha Kwanza kwa mwaka 2024 imeongezeka na kufikia wanafunzi 43,316 kutoka wanafunzi 25,468 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 70, ambapo skuli za Serikali ni wanafunzi 39,701 kutoka wanafunzi 24,388 na skuli Binafsi ni wanafunzi 3,615 kutoka wanafunzi 1,080. Wanafunzi wa kidato cha Pili kwa mwaka 2024 imepungua na kufikia wanafunzi 23,779 kutoka wanafunzi 24,489 mwaka 2023 kati ya hao wakiume ni 12,128 mwaka 2024 kutoka wanafunzi 10,655 mwaka 2023 na wanafunzi wa kike ni 11,651 mwaka 2024 kutoka wanafunzi 13,834 mwaka 2023 sawa na upungufu wa asilimia 15.7.

Aidha, wanafunzi wa Kidato cha Nne kwa mwaka 2024 imeongezeka na kufikia 26,775 kutoka wanafunzi 25,056 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia

7, ambapo kwa mwaka 2024 wanafunzi wakiume wamefikia 11,406 kutoka wanafunzi 10,355 mwaka 2023 na wa kike ni 15,369 kutoka wanafunzi 14,701 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 4.5.

Kwa upande wa Kidato cha Tano mwaka 2024, idadi imeongezeka na kufikia wanafunzi 5,530 kutoka wanafunzi 3,831 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 44, kati ya hao wanafunzi wakiume kwa mwaka 2024 ni 2,483 kutoka wanafunzi 1,898 mwaka 2023, na wakike kwa mwaka 2024 ni 3,047 kutoka wanafunzi 1,933 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 57. Kwa upande wa Kitado cha Sita kwa mwaka 2024 idadi ya wanafunzi imeongezeka na kufikia 3,476 kutoka wanafunzi 2,681 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 29.6, Kati ya hao wanaume ni 1,710 kutoka 1,317 mwaka 2023 na wanawake ni 1,766 kutoka wanafunzi 1,364 mwaka 2023. Hii inatokana na uwepo wa mazingira mazuri ya kujisomea ikiwemo vifaa vya kisasa, walimu wenye sifa na matumizi mazuri ya mitandao ya kijamii. ***(Jadweli nambari 36).***

**Jadweli Nambari 36: Idadi ya Wanafunzi wa Shule za Sekondari kwa Jinsia na Kiwango: Kidato I-VI (2020-2024)**

| Mwaka | Jinsia | Kidato | | | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | I | II | III | IV | V | VI | |
| 2020 | Wanaume | 16,994 | 16,358 | 12,573 | 10,155 | 1,557 | 1,267 | 58,904 |
| | Wanawake | 18,384 | 18,584 | 16,862 | 14,583 | 1,578 | 1,277 | 71,268 |
| | **Jumla** | **35,378** | **34,942** | **29,435** | **24,738** | **3,135** | **2,544** | **130,172** |
| 2021 | Wanaume | 17,053 | 16,465 | 12,091 | 10,179 | 1,953 | 1,250 | 58,991 |
| | Wanawake | 18,375 | 17,787 | 16,888 | 14,295 | 2,090 | 1,403 | 70,838 |
| | **Jumla** | **35,428** | **34,252** | **28,979** | **24,474** | **4,043** | **2,653** | **129,809** |
| 2022 | Wanaume | 9,200 | 15,192 | 10,508 | 10,433 | 1,511 | 1,715 | 38,051 |
| | Wanawake | 12,817 | 16,573 | 14,030 | 14,536 | 1,467 | 1,891 | 61,314 |
| | **Jumla** | **22,017** | **31,765** | **24,538** | **24,969** | **2,978** | **3,606** | **109,873** |
| 2023 | Wanaume | 13,446 | 10,655 | 12,330 | 10,355 | 1,898 | 1,317 | 38,480 |
| | Wanawake | 12,022 | 13,834 | 16,190 | 14,701 | 1,933 | 1,364 | 60,613 |
| | **Jumla** | **25,468** | **24,489** | **28,520** | **25,056** | **3,831** | **2,681** | **110,045** |
| 2024 | **Wanaume** | 20,435 | 12,128 | 9,367 | 11,406 | 2,483 | 1,710 | 57,529 |
| | **Wanawake** | 22,881 | 11,651 | 13,397 | 15,369 | 3,047 | 1,766 | 68,111 |
| | **Jumla** | **43,316** | **23,779** | **22,764** | **26,775** | **5,530** | **3,476** | **125,640** |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar, 2025***

## 6.2 Idadi ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu

Zanzibar ina jumla ya Vyuo Vikuu 3, kati ya hivyo kimoja ni cha Serikali na Vyuo Vikuu 2 ni vya Binafsi. Idadi ya wanafunzi waliodahiliwa katika Vyuo Vikuu vya Serikali na Binafsi imeongezeka na kufikia wanafunzi 13,038 kwa mwaka wa masomo 2024/25 kutoka wanafunzi 11,277 kwa mwaka wa masomo 2023/2024 sawa na ongezeko la asilimia 15.6, ambapo wanaume ni 5,061 kutoka wanafunzi 4,545, na wanawake ni 7,977 kutoka 6,732, hii inatokana na miundombinu ya kujifunzia ikiwemo majengo ya kisasa yenye vifaa vya kisasa vya kujifundishia pamoja na juhudi za Serikali kutoa mikopo kwa wahitaji.

Idadi ya wanafunzi waliodahiliwa katika Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA) imepungua na kufikia 6,714 kwa mwaka wa masomo 2024/25 kutoka 6,807 kwa mwaka wa masomo 2023/2024 sawa na upungufu wa asilimia 1.3. Idadi ya wanafunzi wanawake imefikia 4,127 mwaka 2024/25 kutoka wanafunzi 4,074 mwaka 2023/2024 na wanaume imefikia 2,587 kutoka wanafunzi 1,335 mwaka 2023/2024.

Kwa upande wa Vyuo Vikuu Binafsi, idadi ya wanafunzi waliodahiliwa imeongezeka na kufikia wanafunzi 6,324 mwaka 2024/25 kutoka wanafunzi 4,470 kwa mwaka 2023/2024 sawa na ongezeko la asilimia 41.4. Kati ya hao wanawake ni 3,850 kwa mwaka 2024/25 kutoka 2,658 kwa mwaka 2023/2024 sawa na ongezeko la asilimia 45, na wanaume ni 2,474 kwa mwaka 2024/25 kutoka 1,812 kwa mwaka 2023/2024 sawa na ongezeko la asilimia 36.5

### 6.2.1 Idadi ya Mikopo iliyotolewa

Kwa mwaka wa masomo 2024/2025 jumla ya wanafunzi waliiomba mkopo kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar ni 7,183 kutoka wanafunzi 4,526 kwa mwaka wa masomo 2023/24, kati ya hao wanaume ni 3,216 kutoka wanafunzi 1,848, na wanawake ni 3,967 kutoka wanafunzi 2,678,

Aidha, kwa mwaka wa masomo 2024/25, Bodi ya Mikopo Zanzibar ilifanikiwa kutoa mikopo kwa wanufaika 4,629 kutoka wanufaika 2,502 kwa mwaka wa masomo 2023/2024 kati ya hao wanaume ni 1,839 kutoka 1,127 na wanawake ni 2,790 kutoka 1,375. Hali hii imesababishwa na kuongezeka kwa ufaulu wa wanafunzi na Bodi kuanza kuwapa mikopo wanafunzi wa elimu ya ngazi ya diploma. ***(Jadweli nambari 37)***.

**Jadweli Nambari 37: Idadi ya Wanafunzi wa Vyuo Vikuu Walioomba na Waliopata Mkopo Kutoka Bodi ya Mikopo Mwaka 2023/24 na 2024/25**

| **Walioomba Mkopo** | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **2023/24** | | | **2024/25** | | |
| Wanaume | Wanawake | **Jumla** | Wanaume | Wanawake | **Jumla** |
| 1,848 | 2,678 | **4,526** | 3,216 | 3,967 | **7,183** |
| **Waliopata Mkopo** | | | | | |
| **2023/24** | | | **2024/25** | | |
| Wanaume | Wanawake | **Jumla** | Wanaume | Wanawake | **Jumla** |
| 1,127 | 1,375 | **2,502** | 1,839 | 2,790 | **4,629** |
| **Wanaoendelea na kunufaika na Mkopo** | | | | | |
| **2023/24** | | | **2024/25** | | |
| Wanaume | Wanawake | **Jumla** | Wanaume | Wanawake | **Jumla** |
| 1,795 | 1,840 | **3,635** | 3,627 | 5,299 | **8,926** |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar, 2025***

### 6.2.2 Mwenendo wa Utoaji wa Mikopo na Utaratibu wa Kurejesha Mikopo

Utoaji wa mikopo ya elimu ya juu Zanzibar ulianza mwaka wa fedha 2006/2007 na hadi kufikia Machi mwaka wa fedha 2024/25 jumla ya TZS 147.4 bilioni zilishatumika kwa utoaji wa mikopo hiyo kwa wanafunzi 25,652 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2023/2024 jumla ya TZS 115.4 bilioni zilitumika kwa utoaji wa mikopo kwa wanufaika 18,454. Bajeti ya utoaji mikopo kwa mwaka wa fedha 2024/25 ni TZS 30.5 bilioni kwa wanafunzi 7,367 (3,070 wapya na 4,297 wanaondelea) ukilinganisha na mwaka wa fedha 2023/24 kwa bajeti ya TZS 29.05 bilioni kwa wanafunzi 6,060 (wapya 2,425 na wanaoendelea ni 3,635).

Aidha, katika utaratibu wa urejeshaji wa mikopo mnufaika hutakiwa kuanza kulipa mkopo wake miaka miwili tangu kumaliza masomo yake na kupata ajira. Mkopo huo hulipwa kwa kiwango maalum cha malipo kwa mwezi na mnufaika hulipa deni hilo bila ya nyongeza yoyote (Riba).

### 6.2.3 Ukusanyaji wa marejesho ya mikopo

Urejeshaji wa mikopo ya elimu ya Juu Zanzibar ulianza mwaka wa fedha 2011/12 (mwezi Februari 2012) kwa kipindi cha miaka (6) tangu kuanza utoaji wa mikopo; na hadi mwezi Machi 2023 wadaiwa 5,453 walikuwa wameanza kurejesha mikopo yao na jumla ya deni lao ni TZS 37.3 bilioni. Aidha, hadi Machi 2025 jumla ya TZS 27.9 bilioni zimekusanywa kutoka wa wanufaika

hao 5,453 na kati yao wanufaika 1,813 wamemaliza kulipa mikopo yao. Aidha, kwa kipindi cha miezi tisa ya mwaka wa fedha 2024/2025 (Julai 2024 – Machi 2025) jumla ya TZS 3.3 bilioni za marejesho ya mikopo zimekusanywa sawa na asilimia 82 ya lengo la mwaka.

### 6.2.4 Urejeshaji wa Mikopo ya Elimu ya Juu

Changamoto katika urejeshaji wa mikopo ya elimu ya juu, miongoni mwa hizo ni;

a) Kutokua tayari kwa wanafunzi walionufaika na mikopo kurejesha mikopo yao kwa hiari pale muda wa kurejesha mkopo unapofikia;
b) Kwa vile mnufaika hukopeshwa kiwango kikubwa kwa muda mfupi na kulipa deni lake kwa kipindi kirefu, kasi ya makusanyo ya marejesho hailingani na ongezeko la fedha zinazohitajika kukopeshwa kila mwaka. Kwa mfano muhitimu aliyekopeshwa TZS 8,000,000 kwa kipindi cha masomo ya miaka mitatu hulipa deni lake hilo kidogo kidogo baada ya kumaliza masomo kwa kipindi cha miaka minane (8);
c) Kuwepo kwa wanufaika wenye madeni makubwa ambao imekuwa vigumu kulipa madeni kupitia mishahara yao na kuweza kumaliza kwa wakati.
d) Kuwepo kwa wadaiwa wanaostaafu kazi kabla ya kumaliza kulipa madeni yao ya mkopo wa elimu ya juu. Kwa sasa utaratibu hauruhusu kukata kiinua mgongo cha mstaafu aliyekopea mafao yake kutoka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar kulipa deni la mkopo wa elimu ya juu;
e) Kuwepo wanufaika wanaochukuwa likizo bila malipo kabla ya kumaliza kulipa madeni yao na kupelekea marejesho ya mikopo yao ya kila mwezi kusita;
f) Ugumu wa kuwatambua na kupata marejesho ya mkopo kutoka kwa wanufaika wanaofanya kazi katika baadhi ya Taasisi za SMT;
g) Ugumu wa kupata orodha za waajiriwa wapya wa Taasisi za Serikali ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kuhakiki majina ya wanufaika wa mikopo; na
h) Ugumu wa kupata marejesho ya mikopo kutoka kwa wafanyakazi wa Sekta Binafsi. Mara nyingi waajiri wao huwa hawako tayari kutoa mashirikiano.

### 6.2.5 Mapendekezo ya Kutatua Changamoto za Urejeshaji Mkopo wa Elimu ya Juu;

a) Elimu iendelee kutolewa kwa jamii juu ya umuhimu na wajibu wa kurejesha mikopo ya Elimu ya Juu;

b) Waajiri wote (Serikalini na Taasisi Binafsi) waendelee kupewa elimu juu ya wajibu wa kutekeleza Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar (BMEJZ) na Sheria ya Utumishi wa Umma inayowataka kuwasilisha BMEJZ orodha za wafanyakazi wapya wanaowaajiri;

c) Kuwepo na ufuatiliaji wa kutosha wa makubaliano kati ya BMEJZ ya HESLB ya kubadilishana taarifa za waajiriwa katika Taasisi za Muungano na Taasisi za SMZ ili kuwatambua wanufaika wa mkopo wa BMEJZ wanaofanya kazi katika Taasisi za Muungano;

d) Makubaliano ya hiari ya kupokea mikato ya mikopo ya wafanyakazi wa Taasisi za SMT kupitia Hazina-SMT yafikiwe ili kuondoa changamoto ya kuchelewa kupokea mikato ya taasisi kwa wakati;

e) Ziwepo njia mbadala za kubadilishana taarifa na Taasisi nyengine ili kuwapata wanufaika wa mkopo kama vile uhakiki wa wanufaika wa mikopo wakati wa kutoa leseni za aina mbalimbali, kuomba mikopo katika Taasisi za Fedha na wakati wa kuomba hati ya kusafiria; na

f) Mkopo wa elimu ya juu uwe ni mkato wa lazima (compulsory deduction) kama ilivyo mikato ya kodi ya mapato na mifuko ya hifadhi ya jamii ili kusiwe na kikwazo cha thuluthi moja.

### 6.2.6 Mikakati ya Bodi Juu ya Urejeshajiwa Mikopo kwa Wanufaika

i. Kuunganisha mfumo wa (ZOLAS) na mifumo mengine ya Serikali ili kuwabaini walipo wanufaika ambao hawajaanza kulipa mikopo yao. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 BMWEJZ itakamilisha uunganishaji wa mfumo wa ZOLAS na Mfumo wa Rasilimali Watu na Mishahara wa SMZ unaosimamiwa na Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora. Aidha, katika mwaka wa fedha 2024/2025, bajeti imetengwa kwa ajili ya kuunganisha mifumo ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Tanzania (HESLB);

ii. Sheria Namba 2/2024 ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Zanzibar imeweka mazingira ya kuwafuatilia kwa karibu wanufaika wanaohitimu;

iii. Sheria Namba 2/2024 ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Zanzibar imeweka mazingira ya kuwashajihisha wanufaika kulipa mikopo yao kwa kuweka punguzo maalum kwa watakaolipa vizuri mikopo yao;

iv. Kupeleka barua za kuomba majina ya wahitimu wa elimu ya juu katika Taasisi mbalimbali za Serikali na Binafsi;

v. Kuendelea na ziara za uhakiki kwa kuwatafuta wafanyakazi waliokopa katika Taasisi mbalimbali kwa kushirikiana na waajiri;

vi. Kuwatumia wadhamini wa wadaiwa katika kuwatafuta waliowadhamini na kuwataka waanze kurejesha mikopo yao;

vii. Kuwashajiisha wahitimu kuwa Wazalendo kwa kurejesha mikopo yao kwa hiyari kupitia vyombo vya habari na makongamano; na

viii. Kufanya kazi kwa mashirikiano na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Tanzania (HESLB) kwa kubadilishana taarifa za wajiriwa katika Taasisi za Serikali na Binafsi na kufanya ziara za pamoja kwenye Taasisi.

## SURA YA SABA

### 7.0 SEKTA YA AFYA

Serikali ya Zanzibar inaendelea kuboresha sekta ya afya, na kutoa fursa kwa wawekezaji kutoka nje na ndani kwa lengo la kuhakikisha sekta hii inaimarika na inakuwa na rasilimali za kutosha kwa ajili ya maendeleo endelevu ya kiafya nchini. Sekta inaendelea na jitihada ya kuboresha huduma kwa lengo la kuimarisha utoaji wa huduma bora za Afya nchini uboreshaji huo umetokana na Wizara kuendelea na ujenzi, uboreshaji wa vituo vya afya na hospitali kote nchini kwa lengo la kuhakikisha kuwa huduma bora za afya zinapatikana karibu na wakazi wa vijijini na mijini.

Mikakati ya kufanya utanuzi na marekebisho kwa hospitali kuu ya Mnazi Mmoja inaendelea ili kuhudumia wagonjwa wengi na kuboresha ubora wa huduma. Serikali ina mipango endelevu ya kuwajengea uwezo na kuwaajiri wataalamu wenye fani na ujuzi maalumu, ikiwemo madaktari, wauguzi, na wataalamu wa afya ya akili. Lengo ni kukabiliana na uhaba wa wafanyakazi ili kuwa na nguvu kazi ya kutosha na kupunguza magonjwa mbali mbali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo.

Wizara inaendelea na kampeni za uhamasishaji wa afya ya umma pamoja na kuimarisha Teknolojia ya Afya (e-Health) ili kupunguza magonjwa nchini. Hii ni pamoja na kuanzisha mifumo ya kielektroniki kwa ajili ya kuhifadhi taarifa za wagonjwa na kurahisisha upatikanaji wa huduma za afya.

### 7.1 Wataalamu wa afya

Mwaka 2024, idadi ya madaktari bingwa wamefikia 83 kutoka 81 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 2.4, madaktari hawa wanaendelea kujitolea na kutoa huduma stahiki kwa wananchi ili kujenga jamii yenye afya bora kwa maendeleo Taifa. Ongezeko hilo limetokana na madaktari kurudi masomoni na kupata shahada za juu hadi kufikia ngazi ya kuwa madaktari bingwa (specialist). Kwa upande wa madaktari bingwa kutoka nje ya nchi wamefikia Madaktari 36 mwaka 2024 kutoka 12 mwaka 2023. Hii imetokana na mazingira salama na rafiki ya kufanyia kazi kwa madaktari wa kigeni nchini.

Mwaka 2024, Madaktari wa kawaida wameongezeka na kufikia 498 kutoka 478 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 4.1. Jumla ya Wauguzi 1,486

wanatoa huduma kwenye hospitali na vituo mbali mbali vya Afya nchini mwaka 2024 wameongezeka kutoka wauguzi 1,424 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 4.3. Mabwana na Mabibi afya wamepungua hadi kufikia 2024 mwaka 2024 ikilinganishwa na 227 mwaka 2023 sawa na upungufu wa asilimia hasi 1.3. Hii imetokana na baadhi ya watumishi kubadilisha kada. ***Jadweli nambari 38.***

**Jadweli Nambari 38. Idadi ya Watumishi wa Afya ya Umma 2020 – 2024**

| Watumishi wa Afya na Kada zao | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|
| Madaktari Bingwa. | 64 | 64 | 71 | 81 | 83 |
| Madaktari (Medical Doctors) | 270 | 310 | 343 | 478 | 498 |
| Madaktari wasaidizi (Assistance Medical Officers) | 49 | 35 | 45 | 38 | 28 |
| Madaktari wa meno (Dentist) | 77 | 76 | 82 | 86 | 91 |
| Klinik Afisa | 327 | 371 | 375 | 359 | 401 |
| Wauguzi | 1,342 | 1,521 | 1,384 | 1,424 | 1,486 |
| Wataalamu wa Maabara | 372 | 437 | 398 | 366 | 390 |
| Fundi madawa | 186 | 337 | 327 | 269 | 274 |
| Mabwana Afya | 341 | 444 | 171 | 227 | 224 |
| Radiographic/Medical Image | 41 | 28 | 31 | 24 | 27 |
| Matibabu ya mifupa | 8 | 4 | 5 | 6 | 6 |
| Matibabu ya macho | 10 | 6 | 13 | 5 | 7 |
| Kazi | 0 | 0 | 0 | 3 | 5 |
| Anesthesiologist | 29 | 25 | 15 | 19 | 20 |
| Tiba ya kimwili | 33 | 32 | 32 | 48 | 55 |
| **Total** | **3,179** | **3,690** | **3,256** | **3,433** | **3,595** |

***Chanzo: Repoti ya Muhtasari wa takwimu za kiuchumi na kijamii Zanzibar 2023/24***

### 7.1.2 Idadi ya Vituo vya Afya na Wagonjwa

Wizara ya Afya hupokea muongozo kutoka Shirika la Afya Duniani juu ya mwenendo wa Afya na kuhakikisha Afya za Wananchi zipo salama ili kujenga jamii yenye Afya bora kwa maendeleo endelevu, huduma hizo hutolewa kupitia ngazi za vituo mbali mbali vya Afya msingi na sekondari (PHCUs na PHCU+), hospitali za Wilaya na Mikoa na rufaa.

Vituo vya afya vimefikia 342 mwaka 2024 kutoka 365 mwaka 2023 (bila kujumuisha kliniki zinazotoa huduma moja), sawa na upungufu wa asilimia hasi 6.3. Upungufu huu ulitokana na kutowekwa katika mgawanyo au kubatilishwa kwa vituo 36 vya PHCU ili kurahisisha huduma na kuboresha ugawaji wa rasilimali. Vituo vya afya vya Sekondari na vya Elimu ya Juu viliendelea kuimarika, vikiwa na hospitali 10 za wilaya, hospitali 2 za mikoa, na vituo 3 vya elimu ya juu, ambapo vituo vya afya binafsi viliongezeka kwa asilimia 6.2.

Idadi ya wagonjwa waliotibiwa na kurudi majumbani mwaka 2024 imefikia 3,329,878 kutoka wagonjwa 1,921,043 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 73.3. Kati ya wagonjwa hao, wagonjwa 2,604,210 mwaka 2024 walisajiliwa vituo vya umma kutoka 1,445 mwaka 2023 na wagonjwa 535,860 walisajiliwa katika vituo binafsi mwaka 2024 kutoka 404,845 mwaka 2023. Kwa upande wa vituo vya mashirika vimesajili wagonjwa 167,801 mwaka 2024 kutoka wagonjwa 150,389 mwaka 2023. Idadi ya wagonjwa waliolazwa imepungua na kufikia 49,788 mwaka 2024 kutoka 54,623 mwaka 2023 sawa na asilimia hasi 8.8. Kwa hospitali za umma, idadi imepungua na kufikia 43,522 mwaka 2024 kutoka 47,125 mwaka 2023.

### 7.2 Huduma kwa Kinamama Wajawazito na Vizazi Hai

Idadi ya watoto waliozaliwa hai katika vituo vya afya Zanzibar imepungua na kufikia 53,540 mwaka 2024, kutoka 56,918 mwaka 2023 ikiwa sawa na upungufu wa asilimia hasi 5.9. Upungufu huo ni matokeo ya elimu ya uzazi wa mpango kwa wanajamii ambao imepelekea watu kupata uwelewa juu ya muda sahihi ya ubebaji wa mimba na umri sahihi wa wenza kupata watoto.

#### 7.2.1 Wilaya na Idadi ya Vizazi hai

Wilaya ya Mjini, imekuwa na idadi ndogo ya vizazi hai na kufikia 14,812 mwaka 2024 kutoka 22,777 mwaka 2023 sawa na upungufu wa asilimia 35.0. Upungufu huo umetokana na kinamama na kinababa kuhamasika kutumia uzazi wa mpango kwa Wilaya ya Mjini na Wazazi wengi kujifungulia kwenye vituo vya Afya vya Wilaya na Mikoa na kupunguza idadi ya vizazi hai vinavyorikodiwa Hospitali ya Mnazi mmoja. Wilaya ya Wete imefikia idadi ya vizazi hai 3,782 mwaka 2024 kutoka vizazi hai 4,227 mwaka 2023 sawa upungufu wa asilimia hasi 10.5 na Wilaya ya Chake Chake idadi ya vizazi hai imefikia 5,338 mwaka 2024 kutoka vizazi hai 5,513 mwaka 2023 sawa na upungufu wa asilimia hasi 3.2. Wilay ya Magharibi ‘A’ imefikia idadi ya vizazi hai 4,309 mwaka 2024 kutoka idadi ya vizazi 2,805 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 53.7 na Wilay ya Magharibi ‘B’ idadi ya vizazi hai imefikia 7,149 mwaka 2024 kutoka idadi 3,939 mwaka 2023 zilirekodi ongezeko la aslimia 81.5.

**Jadweli Nambari 39. Idadi ya Vizazi Hai kwa Wilaya za Zanzibar, 2020-2024**

| Wilaya | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kaskazini "A" | 4,432 | 4,590 | 5,112 | 5,600 | 5,171 |
| Kaskazini "B" | 576 | 532 | 512 | 648 | 761 |
| Kati | 1,104 | 1,010 | 1,154 | 1,830 | 3,118 |
| Kusini | 1,349 | 1,578 | 1,619 | 1,849 | 1,864 |
| Magharibi "A" | 928 | 1,580 | 1,819 | 2,805 | 4,309 |
| Magharibi "B" | 2,633 | 2,490 | 2,484 | 3,939 | 7,149 |
| Mjini | 19,551 | 23,013 | 23,669 | 22,777 | 14,812 |
| Chake chake | 4,994 | 5,673 | 5,381 | 5,513 | 5,338 |
| Micheweni | 3,786 | 4,140 | 3,900 | 4,359 | 4,102 |
| Mkoani | 2,915 | 3,298 | 3,027 | 3,371 | 3,134 |
| Wete | 4,439 | 4,188 | 3,961 | 4,227 | 3,782 |
| **Jumla** | **46,707** | **52,092** | **52,638** | **56,918** | **53,540** |

***Chanzo: Repoti ya Muhtasari wa takwimu za kiuchumi na kijamii Zanzibar 2023/24.***

### 7.2.2 Idadi ya Kinamama Wajawazito Waliojifungua Kwa Njia ya Upasuaji, Kawaida na Mimba Zilizoharibika.

Kwa mwaka 2024, jumla ya wazazi waliojifungua hospitalini wamefikia 60,248, kati ya hao 7,329 waliojifungua Kwa njia upasuaji na 52,919 kwa njia ya kawaida ikilinganisha na 49,680 walio jifungua mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 18.3. Mimba zilizoharibika zimepungua na kufikia 3,516, mwaka 2024 kutoka mimba 3,942 mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilima 10.8. Wizara ya Afya inaendelea na tafiti ili kuangalia sababu za kuongezeka kwa idadi ya kina mama wanaojifungua kwa njia ya upasuaji, sababu za kiujumla ni: kubeba mimba katika umri mdogo au umri mkubwa, watoto kuwa wakubwa tumboni, kuchelewa au kutokwenda kliniki mapema kwa kinamama wajawazito, wazazi kushindwa kujifungua kwa njia ya kawaida na watoto kufia matumboni mwa mama zao kabla ya kuzaliwa.

**Jadweli Nambari 40: Kinamama Wajawazito Waliojifungua kwa njia ya Upasuaji na Walioharibu Mimba (2020 – 2024)**

| | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya kina mama waliojifungua kwa njia ya upasuaji | 4,482 | 6,028 | 6,684 | 7,285 | 7,329 |
| Idadi ya mimba zilizoharibika | 1,481 | 2,913 | 5,611 | 3,942 | 3,516 |

***Chanzo: Repoti ya Muhtasari wa takwimu za kiuchumi na kijamii Zanzibar 2023/24***

### 7.2.3 Lishe ya Mama na Mtoto

Hali ya lishe ya mama na mtoto Zanzibar katika mwaka 2023/2024 imeendelea kuimarika, hii imetokana na jitihada za Wizara kuhamasisha wanajamii kula mlo bora kwa wakati. Juhudi za serikali na mashirika yasiyo ya Serikali (UNICEF, WFP, na WHO) kuendelea kuhakikisha kinamama wajawazito na watoto wanapata lishe bora. Mipango ya Zero Stunting Campaign inaendelezwa ili kupunguza athari za ukosefu wa lishe kwa watoto. Upatikanaji wa vyakula vya kutosha na virutubisho muhimu kama vile protini, vitamini, na madini, ni kipaumbele cha wizara na kuendelea kutoa madini ya folic acid na chumvi za iodini ni muhimu kwa maendeleo ya makuzi ya watoto na kinamama.

Mwaka 2024, jumla ya watoto 379,491, wamepatiwa matone ya Vitamini A na madini chuma kwenye vituo vya Afya kutoka 218,468 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 73.7.

Katika kuimarisha huduma za lishe kwa mama na watoto nchini. Serikali kupitia Wizara ya Afya inaendelea na kampeni maalumu ya ulishaji wa matone ya Vitamin "A" kwa watoto chini ya miezi 5 hadi 6 ili kuimarisha afya za watoto nchini. Mafanikio haya yamechangiwa na mashirikiano makubwa kutoka sekta za Serikali na jamii hususani Masheha na wahudumu wa afya wa kujitolea (CHVs). Kampeni hii imefanikiwa kuwapa watoto wengi matone hayo na kwa wakati Sawa na ongezeko la asilimia 62.8 kwa mwaka 2024 kutoka asilimia 38.3 kwa mwaka 2023, watoto wa Mikoa na Wilaya zote za Unguja na Pemba wamepatiwa matone hayo kwa wakati.

Wizara ya Afya pamoja na Shirika la Afya Duniani inaendelea kusimamia miongozo yake juu ya lishe ya mama na mtoto na kutoa maelekezo ya utekelezaji kwa kupitia na kukamilisha mkakati shirikishi wa lishe ambao unahusisha utekelezaji wa majukumu ya sekta zote. Mkakati huo una shajihisha mambo yafuatayo:

a) Lishe kwa wajawazito na watoto wadogo kwa wakati;
b) Kutoa elimu shirikishi kwa vikundi ambavyo vitahusika kwenye lishe ya mama na mtoto pamoja na elimu ya uzazi;
c) Kupunguza tatizo la lishe kwa watoto wa skuli;
d) Kupambana na tatizo la utapiamlo kwa watoto walioathirika; na
e) Kutoa elimu ya kupunguza matatizo ya lishe yanayotokana na taratibu za ulaji usiofaa na mitindo ya maisha, uzito uliozidi na kiribatumbo (Utapiamlo) kwa wanawake na wanaume.

## 7.4 Mpango wa Damu Salama

Damu ni rasilimali ya uhai kwenye maisha ya kila binaadamu. Bila ya damu salama hakuna uhai. Hivyo, upatikanaji wa damu salama kwa wahitaji ni sehemu ya jitihada za kuokoa maisha ya binaadamu. Benki ya damu inaendelea kukusanya, kuchunguza, kuhifadhi na kusambaza damu salama katika hospitali nchini. Wananchi wengi wamehamasika kuchangia damu kwa hiari kwa ajili ya kuokoa maisha yao na wananchi wenzao.

Mwaka 2024, kupitia Mpango wa Damu Salama, Wizara ya Afya imekusanya jumla ya chupa za damu 16,224, kutoka chupa 15,313 zilizokusanywa mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 6.0. Hii imetokana na jitihada ya Benki kuimarisha utoaji wa elimu na uhamasishaji kwa wananchi juu ya kuchangia damu kwa hiyari ili kuokoa maisha ya watu kupitia mabonanza, mikutano ya kidini na mikusanyiko mikubwa ya watu kwa lengo kuu la kuhakikisha uwepo wa damu ndani ya nchi. Licha ya mafanikio hayo, benki ya damu salama imekuwa na changamoto ambazo zinarudisha nyuma shughuli za ukusanyaji damu kwa wakati kulingana na mahitaji halisi kwa muda sahihi ili kuendana na mahitaji ya damu salama. ***(Jadweli nambari 41.).***

**Jadweli Nambari 41. Ukusanyaji wa Damu Kupitia Benki ya Damu2020-2024**

| Mwaka | Idadi ya Chupa |
|---|---|
| 2020 | 14,482 |
| 2021 | 15,206 |
| 2022 | 14,552 |
| 2023 | 15,313 |
| 2024 | 16,224 |

***Chanzo: Repoti ya Muhtasari wa takwimu za kiuchumi na kijamii Zanzibar 2023/24***

## 7.5 Vifaa Tiba na Magonjwa Kumi Yaliyoripotiwa Mara kwa Mara 2023/2024

Mwaka 2024, Vifaa tiba vya msingi vilirikodiwa kupanda kwa 22,007, sawa na asilimia 9.1 kutoka 20,165 mwaka 2023. Ugonjwa wa Upumuwaji wa Juu (Upper Respiratory Tract Infections) umeongezeka kwa kesi 304,571, sawa na asilimia 13.1 ikifuatiwa na homa ya baridi na kikohozi kwa asilimia 10.7 na Magonjwa Mengine ya Ngozi kwa asilimia 9, ikilinganishwa na kesi kama hizo kwa Mwaka 2023, Hali hii imetokana na mifumo mibaya ya ulaji kwa wananchi walio wengi pasipokufata taratibu za kiafya katika ulaji wa vyakula.

### 7.6 Huduma za Upasuaji Mkubwa

Serikali inaendelea kuchukua Jitihada za makusudi kuhakikisha huduma ya upasuaji mkubwa inapatikana nchini kwa lengo la kuboresha Afya za wananchi na kupunguza gharama kubwa ya upatikanaji wa huduma hii. Upasuaji wa uti wa mgongo na ubongo (Neurosurgery) kupitia kambi maalumu ya wataalamu wazawa na wakigeni kutoka nchini Hispania na Israel wanaendelea na kutoa matibabu ya upasuaji. Mwaka 2024, kitengo kimefanikiwa kuwapatia matibabu wagonjwa 73 Kutoka wagonjwa 252, mwaka 2023 sawa na upungufu wa asilimia hasi 71.0 Serikali kupitia Wizara ya Afya inaendelea na mikakati ya kuongeza juhudi za kitaalamu na kuongeza idadi ya wataalamu wa fani husika ili kudhibiti magonjwa hayo nchini.

### 7.7 Idadi ya Vifo kwa Wagonjwa

Mwaka 2024, idadi ya vifo kwa wagonjwa imeongezeka hadi kufikia vifo 2,262 kutoka 2,242 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 0.9. Ajali ya mishipa ya damu ya ubongo (Cerebrovascular; CVA), ni miongoni mwa sababu kuu ya vifo. Ugonjwa wa upungufu wa osijini (Asphyxia) ya kuzaliwa ilipanda hadi nafasi ya pili, kufikia 159 mwaka 2024 kutoka 127 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 25.1. Aidha, idadi ya vifo vitokanavyo na ugonjwa wa homa ya Nimonia vilipungua na kufikia vifo 86 mwaka 2024 kutoka 198 mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia hasi 56.5. Vifo vilivyotokana na upungufu mkubwa wa damu viliongezeka na kufikia 2,262 kati ya wagonjwa 49,788 waliolazwa mwaka 2024 kutoka 2,242 kati ya wagonjwa 54,623 waliolazwa mwaka 2023.

### 7.8 Mpango wa Kumaliza Malaria Nchini.

Zanzibar ikiwa ni sehemu ya dunia, inaendelea na mikakati ya kupambana na kudhibiti ugonjwa wa Malaria kwa kushirikiana na Mashirika ya Kimataifa, ili kuendelea na kampeni ya kuwafahamisha wananchi juu ya njia za kuzuia na kujikinga juu ya ugonjwa huo. Wakati Serikali ikiendelea na utoaji wa huduma za matibabu stahiki, hali ya ugonjwa imepungua kwa kiasi kikubwa, licha ya changamoto ambazo hupelekea kuzorotesha jitihada za kuondosha maradhi hayo, program (Zero Malaria Inaanza na Mimi na Wewe ), inaendelea na mikakati mbalimabali ili kufikia azimio la kumaliza malaria nchini.

Jumla ya wagonjwa 22,375 mwaka 2024 kutoka wagonjwa 18,283 mwaka 2023 walichunguzwa na kugunduliwa na vimelea vya malaria ikiwa sawa na ongezeko la asilimia 22.3. Aidha matokeo ya vifo vitokanavyo na malaria nchini

vimepungua kufikia 18 mwaka 2024 vikilinganishwa na vifo 29 mwaka 2023. Upungufu huo umetokana na jitihada za Wizara Afya kuelimisha Wananchi juu ya kujikinga na ugonjwa huo. ***(Jadweli nambari 42).***

**Jadweli Nambari 42. Hali ya Malaria nchini na idadi ya vifo 2020-2024**

| | Hali ya Malaria nchini | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Idadi ya wagonjwa wa malaria | 14,188 | 6,616 | 4,557 | 18,283 | 22,375 |
| 2 | Vifo vya malaria | 20 | 9 | 4 | 29 | 18 |

***Chanzo: Repoti ya Muhtasari wa takwimu za kiuchumi na kijamii Zanzibar 2023/24***

### Vituo Vinavyotumia MRDT na Darumini

Kwa mwaka 2024, vituo vinavyotumia darubini (MRDT) vimefikia 305 ikilinganishwa na vituo 169 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 80.5. Vipimo hivi vinatumika kwa ajili ya uchunguzi wa vimelea vya Malaria. Wizara kupitia Mpango wa Kudhibiti Malaria inafuatilia kujua maeneo gani yanayoripotiwa kuwa na wagonjwa wengi na kuchukua hatua za kutoa tiba na kinga kwa maeneo husika. ***Jadweli nambari 43***.

**Jadweli Nambari 43. Upimaji wa Malaria na Vituo Vinavyotumia MRDT na Darumini (Microscope) 2023/2024**

| **Zanzibar** | **Aina ya kipimo Vinavyo tumika Kupimia Malaria Nchini** | |
|---|---|---|
| | **MRDT** | **Darumini (Microscope)** |
| Unguja | 205 | 124 |
| Pemba | 100 | 36 |
| **JUMLA** | **305** | **160** |

***Chanzo : Wizara ya Afya Zanzibar ,2025***

### 7.8.1 Dawa Zinazotumika Kutibu Malaria Nchini

Kwa sasa dawa zilizothibitishwa na kupewa nafasi ya kwanza kutumika kwa kutibu ugonjwa wa malaria ni dawa zile zile ambazo zinaendelea kutumika nchini kama vile mchanganyiko wa "Artemisinin Based Combination Therapy (ACTs)"kiwango cha 0.25mg/kg na "Primaquinephosphate, Artemether Lumefantrine" na "primaquine" inatumika kama njia ya pili ya tiba ya kutibu ugonjwa wa malaria sugu, dawa hizi ziko katika mfumo wa vidonge nchi nzima. Kwa upande wa watoto kuanzia miezi 0-5 wanapatiwa dawa yenye viwango vya kitoto "Pediatric formular" hii ni kwa mujibu wa ushauri wa Shirika la Afya Duniani (WHO) kupitia Madaktari Bingwa wa watoto waliopendekeza utumiaji wa dawa hiyo. Serikali imepiga hatua kubwa katika kupambana na malaria hadi kufikia lengo la kiwango cha chini ya asilimia zero, Wizara inaendeleza mikakati

mbali mbali ya kudhibiti malaria, Zanzibar bila malaria inawezekana kupitia programu ya Zero Malaria na utoaji wa vyandarua kwa kaya mbali mbali nchini.

### 7.8.2 Madaraja ya Dawa za Kutibia Malaria Nchini

Wizra ya Afya imeweka muongozo wa kutibu Malaria nchini ili kutoa tathmini halisi ya kitabibu juu ya matumizi sahihi ya utumiaji dawa kwa Hospitali za Serikali na Binafsi ili kuepuka kutumia madawa yasiyofaa kwa kutibia ugonjwa huo kama ifuatavyo:-

- i Daraja la kwanza ni Artesunate +Amodiaqune (ASAQ)
- ii Daraja la pili ni Dihydroartemisin+Piperaquine (DHAP), Artemether+ Lumefantrine (ALU)
- iii Daraja la tatu ni Sindano ya Artesunate au Sindano ya Artemether

### 7.8.3 Mikakati ya Kupambana na Malaria Zanzibar 2020-2024

Utumiaji wa dawa za (Artesunate+Amodiaqune (ASAQ) Dihydroartemisin+Piperaquine (DHAP), Artemether+ Lumefantrine (ALU) na kwa homa kali ni Sindano ya Artesunate au Sindano ya Artemether.

- a. Upulizaji wa dawa (viatilifu) ya kuuwa mbu wa malaria majumbani
- b. Utumiaji wa vyandarua vyenye dawa ya Muda mrefu kwa ajili ya kuua na kufukuza mbu waenezao ugonjwa wa malaria
- c. Ufuatiliaji wa wagonjwa majumbani waliogundulika kuwa na ugonjwa wa malaria kwa lengo la kukata maambukizi ya malaria
- d. Utiaji wa viatilifu (dawa) katika mazalio ya mbu
- e. Utoaji wa elimu ya afya kwa jamii juu ya kujingika na ugonjwa wa malari.

### 7.8.4 Kazi Kuu Zilizofanywa na Programu katika Kupambana na Malaria Zanzibar mwaka 2020-2024

- i. Kuhakikisha wananchi wanapata elimu ya kutosha kwenye umuhimu wa utumiaji wa vyandarua vyenye dawa ya Muda mrefu kwa ajili ya kuua na kufukuza mbu waenezao ugonjwa wa malaria;
- ii. Uchunguzi wa vinasaba vya mbu waenezao Malaria;
- iii. Upulizaji wa dawa (viatilifu) ya kuuwa mbu wa malaria majumbani;
- iv. Ufuatiliaji wa wagonjwa majumbani waliogundulika kuwa na ugonjwa wa malaria kwa lengo la kukata maambukizi ya malaria;
- v. Utiaji wa Viatilifu (Dawa) katika mazalio ya mbu; na

vi. Kuwepo kwa kikosi kazi cha kukamata na kuchunguza mbu wanaosambaza malaria.

### 7.8.5 Idadi ya Nyumba Zilizopuliziwa Dawa

Wizara inaendelea na mikakati maalumu ya kupambana na kumaliza Malaria Zanzibar. Wananchi wanapewa elimu na kupata muamko mkubwa ili wakubali kupigiwa dawa kwa hiari baada ya kuelewa athari za ugonjwa huo. Kwa mwaka 2024 jumla ya nyumba zilizopuliziwa dawa zimepungua na kufikia 16,718 ikinganishwa na nyumba 54,004 mwaka 2023 sawa na upungufu wa asilimia 69.0. ***(Jadweli Nambari 44)***

**Jadweli Nambari 44. Idadi ya Nyumba Zilizopuliziwa Dawa 2024-2020**

| Mwaka | Lengo, Idadi ya Nyumba na Asilimia | Kaskazini Unguja | Kusini Unguja | Mjini Magharibi | Kaskazini Pemba | Kusini Pemba | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2020 | Lengo | 7,970 | 13,206 | 14,021 | 5,043 | 610 | 41,231 |
| | Nyumba | 8,204 | 14,021 | 15,673 | 5,911 | 723 | 44,532 |
| | Asilimia | 102.9 | 106.2 | 108.8 | 117.2 | 118.5 | 108.5 |
| 2021 | Lengo | 6,126 | 13,969 | 17,300 | 7,528 | 1,042 | 45,965 |
| | Nyumba | 6,561 | 13,958 | 17,008 | 7,695 | 1,094 | 46,316 |
| | Asilimia | 107.1 | 99.9 | 98.3 | 102.2 | 105 | 100.8 |
| 2022 | Lengo | 14 | 2,172 | 10,799 | 4,470 | 4,797 | 22,252 |
| | Nyumba | 14 | 2,117 | 10,291 | 4,356 | 4,692 | 21,470 |
| | Asilimia | 100 | 97.5 | 95.3 | 97.4 | 98 | 96.5 |
| 2023 | Lengo | 948 | 18,560 | 34,212 | 2,372 | 995 | 57,087 |
| | Nyumba | 923 | 17,494 | 32,262 | 2,344 | 981 | 54,004 |
| | Asilimia | 97.4 | 94.3 | 94 | 98.8 | 98.5 | 95 |
| 2024 | Lengo | 3,803 | 454 | 10,581 | 1,987 | 972 | 17,797 |
| | Nyumba | 3,658 | 450 | 9,762 | 1,928 | 920 | 16,718 |
| | Asilimia | 96.2 | 99.1 | 92.3 | 97.3 | 94.6 | 93.7 |

***Chanzo: Repoti ya Muhtasari wa takwimu za kiuchumi na kijamii Zanzibar 2023/24***

## 7.9 Maradhi ya Kuambukiza

Wizara ya Afya inaendelea kuelimisha na kuhamasisha jamii juu ya kutunza afya zao dhidi ya maradhi ya kuambukiza, ikiwemo kufanya uchunguzi wa afya mara kwa mara na kujenga tabia inayozingatia kanuni za afya. Wananchi wanaendelea kupata mwamko mkubwa wa kujua afya zao na kujikinga na maradhi yanayoambukiza, ikiwemo Ukimwi, Gonoria, Kaswende na Ukoma. Wananchi wengi hufika hospitalini na kujua afya zao kwa kufanya vipimo, kupatiwa dawa na ushauri pale wanapogundulika wamepata maambukizi ya magojwa hayo. Mwaka 2024, hali ya maambukizi mapya ya magonjwa ya virusi vya ukimwi imefikia 1,150 kutoka maambukizi 1,050 mwaka 2023 sawa na upungufu wa asilimia 9.5. Utoaji wa elimu ya kujitambua hasa kwa vijana wadogo kati ya umri wa miaka 18 hadi 35 umesaidia kupunguza maabukizi mapya ya maradhi ya kujamiyana.

Mwaka 2024, wagonjwa 1279, wamegundulika na ugonjwa wa Kifua kikuu kutoka 1,135 mwaka 2023.  Sawa na ongezeko la asilimia 12.6. Hii imetokana na muingiliano wa shughuli mbali mbali za kijamii. Juhudi za kuwaelimisha wananchi zinaendelea kutolewa kupitia Maafisa wa Afya nchi nzima kwa kuwapa wanajamii muamko juu ya kupunguza zaidi maambukizi ya magonjwa hayo nchini.  (Jadweli nambari 45).

**Jadweli nambari 45. Magonjwa ya kuambukiza 2023/2024**

| Mwaka | 2023 | 2024 |
|---|---|---|
| Chlamydia | 104 | 54 |
| Gonorria | 217 | 162 |
| Kaswende | 280 | 134 |
| Ukimwi | 1298 | 1180 |
| Kifua kikuu | 1,135 | 1279 |

***Chanzo: Wizara ya Afya Zanzibar 2023/2024***

## 7.10  Hali ya Madawa ya kulevya Zanzibar

Madawa ya kulevya ni janga la ulimwengu na huleta athari kwa maendeleo endelevu ya nchi na ulimwengu kwa ujumla. Zanzibar ikiwa ni sehemu ya Dunia nayo pia inakumbwa na janga hili ambalo huathiri nguvu kazi ya Taifa na kudhoofisha maendeleo nchini. Serikali inaendelea na mapambano dhidi ya madawa ya kulevya ili kuiweka jamii yenye afya njema kwa maslahi mapana ya maendeleo endelevu ya nchi yetu.

### 7.10.1 Idadi ya Nyumba na Wakaazi Walioathirika na Uraibu wa Madawa ya Kulevya (Sober Houses)

Mwaka 2024, jumla ya nyumba nne (4) za waathiriwa wa madawa ya kulevya za wanaume pekee ziliripotiwa. Hii ni sawa na nyumba za mwaka 2023. Jumla ya watumiaji 203 wa dawa za kulevya waliripotiwa mwaka 2024 ikilinganishwa na watumiaji 275 mwaka 2023 sawa na upungufu wa asilimia 26.2. Kati ya hao, makundi ya umri wa miaka 26-45, ndio waathirika wakubwa wa madawa ya kulevya.

Upungufu huo umetokana na jitihada za Serikali na Taasisi za kiraiya kupambana kikamilifu dhidi ya uingiaji na utumiaji wa dawa za kulevya sambamba na utoaji wa elimu juu ya athari za madawa ya kulevya kuanzia ngazi za chini za familia hadi ngazi ya Taifa. ***(Jadweli nambari 46).***

**Jadweli Nambari 46. Nyumba za Kurekebisha Tabia (Sober Houses by Location), 2020 – 2024**

| **Mwaka** | **Sehemu Zilizopo Nyumba** | **Nyumba za wanawake** | **Nyumba za wanawake** | **Jumla ya Nyumba** |
|---|---|---|---|---|
| 2020 | Unguja | 4 | 0 | 4 |
| | Pemba | 2 | 0 | 2 |
| | **Jumla** | 6 | 0 | 6 |
| 2021 | Unguja | 4 | 0 | 4 |
| | Pemba | 1 | 0 | 1 |
| | **Jumla** | 5 | 0 | 5 |
| 2022 | Unguja | 4 | 0 | 4 |
| | Pemba | 1 | 0 | 1 |
| | **Jumla** | 5 | 0 | 5 |
| 2023 | Unguja | 3 | 0 | 3 |
| | Pemba | 1 | 0 | 1 |
| | **Jumla** | **4** | **0** | **4** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 2024 | Unguja | 3 | 0 | 3 |
| | Pemba | 1 | 0 | 1 |
| | **Jumla** | **4** | **0** | **4** |

***Chanzo: Repoti ya Muhtasari wa takwimu za kiuchumi na kijamii Zanzibar 2023/24.***

### 7.10.2 Idadi ya Wakaazi Kwenye Nyumba za Kurekebishia Tabia

Idadi ya wakaazi kwenye nyumba za kurekebisha tabia imefikia wakaazi 203 Mwaka 2024 kutoka 275 Mwaka 2023 sawa upungufu wa asilimia 26.2, upungufu huo umesababishwa na ongezeko la elimu kwa jamii juu ya athari ya madawa ya kulevya na mikakati thabiti ya Serikali kupambana na waingizaji, wauzaji na watumiaji wa madawa, kwa kushirikiana na vitengo mbali mbali na asasi za kiraia. (***Jadweli Nambari 47)***.

**Jadweli Nambari 47. Idadi ya Wakaazi Katika Nyumba za Waathirika wa Madawa ya Kulevya Zanzibar (2024- 2020)**

**kwa Umri**

| Miaka /Umri makundi husika | | **15–25** | **26–35** | **36–45** | **46 +** | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2020 | M/me | 53 | 148 | 95 | 53 | 349 |
| | M/ke | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | **Jumla** | **53** | **148** | **95** | **53** | **349** |
| 2021 | M/me | 91 | 147 | 42 | 29 | 309 |
| | M/ke | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Jumla | 91 | 147 | 42 | 29 | 309 |
| 2022 | M/me | 33 | 73 | 32 | 28 | 166 |
| | M/ke | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | **Jumla** | **33** | **73** | **32** | **28** | **166** |
| 2023 | M/me | 58 | 99 | 75 | 43 | 275 |
| | m/ke | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | **Jumla** | **58** | **99** | **75** | **43** | **275** |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2024 | M/me | 75 | 64 | 40 | 24 | 203 |
| | M/ke | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | **Jumla** | **75** | **64** | **40** | **24** | **203** |

***Chanzo: Repoti ya Muhtasari wa takwimu za kiuchumi na kijamii Zanzibar 2023/24***

## 7.11 Sekta ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto,

Hii ni sekta inayo gusa jamii moja kwa moja, kwa lengo la kuhakikisha ustawi na usawa katika jamii pamoja na kupiga vita juu ya udhalilishaji dhidi ya wanawake, watoto na wazee.

Kwa mwaka 2023/2024 Sekta hii imetekeleza mambo yafuatayo: -

- i Kuimarisha uratibu wa ufikiwaji wa usawa wa kijinsia na kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia;
- ii Kuweka mazingira bora ya Ustawi wa Jamii, Watoto, Wazee na kusimamia malipo ya Pencheni Jamii.
- iii Kufuatilia mchakato wa kuwapatia Bima ya Afya kwa wazee wote nchini;
- iv |Kuimarisha hifadhi ya wazee, utoaji wa misaada ya kiustawi kwa wananchi wanaoishi katika mazingira magumu zaidi;
- v Kutoa elimu juu ya matumizi bora ya vinua mgongo kwa wazee wanao karibia kustaafu kazi;
- vi Kuimarisha mfumo wa hifadhi ya mtoto na kusimamia haki na wajibu wao.

### 7.11.1 Idadi ya Wazee na Watoto Yatima Kwenye Nyumba za Hifadhi

Mwaka 2024. Vituo vya Watoto Yatima vimeongezeka na kufikia 563, ikilinganishwa na 384 mwaka 2023. Kati ya hao, Wavulana 302. na wasichana 26. Hali hii inaonesha kuongezeka kwa idadi ya watoto waliokosa uangalizi wa familia. Aidha, idadi ya wazee walioandikishwa katika nyumba za hifadhi wamefikia 60 mwaka 2024 ikilinganishwa na 67 mwaka 2023. (***Jadweli nambari 48)***

**Jadweli Nambari 48. Idadi ya Wazee na Watoto Yatima Kwenye Nyumba za Hifadhi 2020-2024.**

| Vituo | Jinsia | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Vituo vya mayatima | Watoto wa kiume | 160 | 205 | 264 | 196 | 302 |
| | Watoto wa kike | 98 | 132 | 173 | 188 | 261 |
| | **Jumla** | **258** | **337** | **437** | **384** | **563** |
| Vituo Vya kutunzia Wazee | Wazee wa kike | 74 | 42 | 22 | 40 | 35 |
| | Wazee wa kiume | 60 | 29 | 37 | 27 | 25 |
| | **Jumla** | **134** | **71** | **59** | **67** | **60** |

***Chanzo: Wizara ya Maendeleo, Jinsia, Wanawake na Watoto 2020-2024.***

## 7.12 Hali ya Watu wenye Mahitaji Maalumu Zanzibar

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea na mikakati ya kuhakisha ustawi na ushirikishwaji wa makundi yote katika shughuli za uzalishaji na fursa mbalimbali za maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini. Takwimu zinaonyesha kuwa mwaka 2024, Zanzibar ina jumla ya watu 8,100, wenye mahitaji maalumu kati ya hao, Wanawake 3,838 na Wanaume 4,262. Kati ya watu wenye umri wa miaka 15 hadi 34 ndio umri unao ongoza kwa watu wenye mahitaji maalumu. ***(Jadweli Nambari 49.)***

### 7.12.1 Mikakati ya Wizara Kuwawezesha Watu Wenye Mahitaji Maalum

- i Kuwafadhili watu wenye Mahitaji Maalumu kupata fursa ya elimu, kuanzia ngazi za cheti na Diploma;
- ii Kuwasaidia matibabu ndani na nje ya nchi;
- iii Kuwapatia watu wenye Mahitaji Maalumu Vifaa saidizi kama vigari vya kutembelea, stiki, miwani nk; na
- iv Kuwasaidia kupata mikopo ya kifedha kupitia Mamlaka ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (ZEEA).

**Jadweli Nambari 49. Watu Wenye Ulemavu na Mahitaji Maalumu 2023/2024**

| **Aina za ulemavu** | W/ume | W/Mke | **Jumla** |
|---|---|---|---|
| Ulemavu wa kimwili | 1,711 | 1,290 | **3,001** |
| Ulemavu wa macho | 539 | 451 | **990** |
| Ulemavu wa maskio | 617 | 745 | **1,362** |
| Ulemavu wa akili | 586 | 489 | **1,075** |
| Ulemavu wa Ngozi | 45 | 59 | **104** |
| Ulemavu jumuishi | 722 | 768 | **1,490** |
| Ulemavu Mwengineo | 42 | 36 | **78** |
| **Jumla kuu** | **4,262** | **3,838** | **8,100** |

***Chanzo: Repoti ya Muhtasari wa takwimu za kiuchumi na kijamii Zanzibar 2023/24.***

## 7.13 Hali ya Wanawake na Watoto.

Ukatili dhidi ya wanawake na watoto ni ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu. Athari zake ni kati ya matokeo ya papo hapo hadi ya muda mrefu ya kimwili, kingono, kiakili na hata kupelekea kifo kwa wahanga.

Kwa mwaka 2024, matukio ya ukatili wa kijinsia yalipungua hadi kufikia 1,809 kutoka 1,954 mwaka 2023 sawa na upungufu wa asilimia 7.4. Ubakaji ulipungua asilimia 9.8, kulawiti asilimia 36.2, na kuingiliwa kwa asili kwa asilimia 21.1. Utekaji nyara asilimia 27.5, matukio ya kushambuliwa asilimia 32.9. Hii imetokana na jitihada kubwa ya Serikali kupambana na hali ya ukatili wa kijinsia ikiwemo kuanzishwa kwa madawati ya kijinsia nchi nzima. ***Jadweli nambari 50***.

**Jadweli Nambari 50. Idadi ya Matukio ya Ukatili wa Kijinsia Yaliyoripotiwa kwa Aina ya Ukatili; 2020 - 2024**

| **Aina za Ukatili wa kijinsia /Mwaka** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** |
|---|---|---|---|---|---|
| Ubakaji | 571 | 621 | 651 | 923 | 833 |
| Ulawiti | 102 | 177 | 200 | 246 | 157 |
| Udhihaki dhidi ya asili | 46 | 83 | 88 | 90 | 71 |
| Utekaji nyara | 150 | 95 | 84 | 109 | 139 |
| Shambulio la Matusi | 74 | 114 | 125 | 210 | 279 |
| Shambulio | 420 | 132 | 212 | 376 | 330 |
| **Makossa kwa ujumla** | **1,363** | **1,222** | **1,360** | **1,954** | **1,809** |

***Chanzo: Wizara ya wanawake na watoto-Zanzibar 2024/23.***

### 7.13.1 Wilaya Zilizoongonza kwa Visa vya Unyanyasaji wa Kijinsia 2024

Kaskazini "A" visa vilipungua kwa asilimia 39.8, ikifuatiwa na Kaskazini 'B' asilimia 33.6, Mjini asilimia 16.0, Magharibi 'B' asilimia 3.4, Chake Chake asilimia 4.6, na Micheweni asilimia 9.5. Zaidi ya waathirika wa ukatili huo ni umri wa miaka 15 hadi 17 ambapo jumla ya matukio 722 ni wasichana sawa na asilimia 57.5 na Wavulana 73 sawa na asilimia 27.0. Aidha, kati ya visa 298 ni Wasichana na 91 Wavulana wenye umri wa miaka 11 hadi 14. Vile vile kati ya visa 166 ni Wasichana na 86 ni Wavulana wenye umri wa miaka 6 hadi 10 na kati ya visa 69 ni Wasichana na 20 ni Wavulana wenye umri wa miaka 0 hadi 5. ***(Jadweli Nambari 51)***.

**Jadweli Nambari 51. Idadi ya Matukio ya Ukatili wa Kijinsia Yaliyoripotiwa kwa Wilaya, 2020-2024**

| Wilaya | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** |
|---|---|---|---|---|---|
| Kaskazini 'A' | 60 | 60 | 52 | 98 | 59 |
| Kaskazini 'B' | 73 | 80 | 59 | 113 | 75 |
| Kati | 97 | 101 | 110 | 94 | 97 |
| Kusini | 51 | 35 | 47 | 45 | 46 |
| Mjini | 297 | 169 | 279 | 457 | 384 |
| Magharibi 'A' | 199 | 290 | 253 | 433 | 429 |
| Magharibi 'B' | 273 | 182 | 288 | 417 | 431 |
| Wete | 80 | 111 | 115 | 93 | 77 |
| Micheweni | 41 | 53 | 39 | 42 | 46 |
| Chake Chake | 115 | 88 | 76 | 108 | 113 |
| Mkoani | 77 | 53 | 42 | 54 | 52 |
| **Jumla** | **1,363** | **1,222** | **1,360** | **1,954** | **1,809** |

***Chanzo: Zanzibar Toleo la Ukatili wa Kijinsia, 2024***

### 7.13.2 Matokeo/Visa ya Unyanyasaji wa Kijinsia Vilivyoripotiwa

Mwaka 2024, kumetokea jumla ya matokeo 1,809 vya unyanyasaji wa kijinsia. Kati ya matokeo hayo Wanawake ni 1,458 sawa na asilimia 80.7, Wanaume ni 351 sawa na asilimia 19.3. Mahali ambapo ubakaji ulifanyika mara kwa mara ni nyumbani kwa mbakaji, ambapo matukio ya ulawiti ni 157 sawa na asilimia 36.2, udhalilishaji ni 60 sawa na asilimia 38.2, Mashambulizi 330 sawa na asilimia

33.3 na utekaji-nyara110. Aidha, kati ya matokeo 290 vilikutwa na hatia, sawa na asilimia 16.0, huku kesi 352 zikiwa mahakamani ni sawa na asilimia 19.5. Idadi kubwa ya visa 882 ikiwa sawa na asilimia 48.8, vilikuwa chini ya uchunguzi wa polisi, matokeo 147 sawa na asilimia 8.1, yalifungwa na polisi, na visa 56 sawa na asilimia 3.1, yalipelekwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma.

### 7.13.3 Uhalifu Dhidi ya Watu na Mali

Mwaka 2024, makosa ya uhalifu dhidi ya mtu yamefikia jumla ya 202, yakionekana kupungua kutoka 208 mwaka 2023. Uhalifu dhidi ya mali umepungua kutoka kesi 9,345 mwaka 2023 kufikia kesi 2,313 mwaka 2024. Kesi za wizi zimepungua kutoka 7,075 mwaka 2023 hadi kesi 245 mwaka 2024. na visa vya ubakaji kwa wasichana (chini ya umri wa miaka 18) vilipungua kufikia visa 758, kutoka visa 824 mwaka 2023. Kesi za mauaji ziliongezeka kutoka 44 mwaka 2023 hadi kufikia 66 mwaka 2024. Hii ni kutokana na wananchi kuchukua Sheria mikononi mwao na kesi kutopelekwa kwenye vyombo vya Sheria.

### *7.13.4 Makosa ya Jinai*

Makosa ya Jinai mwaka 2024, yamepungua hadi kufikia 1,736 kutoka 2,049 mwaka 2023, sawa na upungufu wa asilimia 15.2. Hii imetokana na jitihada za Serikali kupambana na makosa ya uhalifu nchini. ***(Jadweli Nambari 52)***

**Jadweli Nambari 52: Makosa ya Jinai yaliyoripotiwa mwaka 2019-2023**

| Makossa ya jinai | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 |
|---|---|---|---|---|---|
| Mauwaji | 33 | 41 | 34 | 44 | 66 |
| Jaribio la kutaka kujiuwa | 0 | 4 | 22 | 40 | 0 |
| Ubakaji kwa umri wa miaka 18 na zaidi | 64 | 58 | 62 | 95 | 75 |
| Ubakaji kwa msichana (chini ya miaka 18) | 507 | 563 | 585 | 824 | 758 |
| Ubakaji kwa kikundi | 0 | 0 | 4 | 4 | 0 |
| Jaribio la Kubaka | 0 | 4 | 2 | 9 | 0 |
| Uliwati | 103 | 177 | 200 | 246 | 157 |
| Kuingilia kati dhidi ya Asili | 46 | 83 | 88 | 90 | 71 |
| Kuachwa kwa Mtoto | 0 | 1 | 3 | 2 | 0 |
| Kuiba mtoto | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Utekaji nyara | 150 | 95 | 84 | 109 | 0 |
| Mashambulizi | 458 | 939 | 125 | 376 | 330 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Shambulio la Aibu | 74 | 114 | 212 | 210 | 279 |
| Jumla | **1,438** | **2,079** | **1,421** | **2,049** | **1,736** |

***Chanzo: Repoti ya Muhtasari wa takwimu za kiuchumi na kijamii Zanzibar 2023/24***

### 7.13.5 Ajali za Barabarani

Mwaka 2024, idadi ya ajali za barabarani zilifikia 222, kutoka ajali 193 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 15.0. Idadi kubwa zaidi ya ajali zilitokea Kaskazini 'A' ajali 38, ikifuatiwa na Magharibi 'A' ajali 33 na Magharibi 'B' ajali 32, na Mkoani ajali 7. ***(Jadweli nambari 53.)***

**Jadweli Nambari 53: Ajali Zilizorekodiwa za Trafiki, 2020 – 2024**

| **Mwaka** | **2020** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** |
|---|---|---|---|---|---|
| Unguja | 256 | 165 | 137 | 143 | 178 |
| Pemba | 50 | 44 | 35 | 50 | 44 |
| **Jumla** | **306** | **209** | **172** | **193** | **222** |

***Chanzo: Repoti ya Muhtasari wa takwimu za kiuchumi na kijamii Zanzibar 2023/24***

**Makosa ya barabarani yaliyoripotiwa mwaka 2023 -2024**

Mwaka 2024, jumla ya makosa ya usalama barabarani yalifikia 53,934 kutoka 38,791 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 39.2. Kati ya jumla ya makosa hayo, 53,722 yalikuwa ni makosa madogo sawa na asilimia 99.5 na 212 yalikuwa makosa makubwa sawa na asilimia 0.5. Kwa mwaka 2024, Wilaya ya Magharibi "A" na "B" ilikuwa na asilimia 20.9 ambayo ni idadi kubwa zaidi ikilinganishwa na Wilaya nyingine.

**Waathirika wa ajali za barabarani**

Mwaka 2024, jumla ya waathirika wa ajali za barabarani ilifikia 413 kutoka 385 mwaka 2023, sawa na asilimia 7.3. Kati ya ajali hizo watu 189 walifariki (Wanaume 170 na Wanawake 19) ikilinganishwa na 224 (Wanaume 190 na Wanawake 34) mwaka 2023.

### 7.13.6 Kesi Zilizofikishwa Mahakama ya Vijana (watoto)

Jumla ya Kesi za Uhalifu zilizowasilishwa katika Mahakama za watoto zilikuwa 98, kati ya hizo 60 sawa na asilimia 61.2 zilikuwa zimeamuliwa na kesi 38 zilikuwa zikiwasilishwa mbele ya Mahakama. Idadi ya kesi zilizowasilishwa ilipungua kwa asilimia 19.0 kutoka 121 mwaka 2023 hadi 98 mwaka 2024. Idadi ya kesi zilizosuluhishwa ilipungua kwa asilimia 61.2 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 66.1 mwaka 2023. ***(Jadweli nambari 54).***

**Jadweli nambari 54. Jumla ya Kesi Zilizopelekwa Mahakamani na Kutolewa Mashauri.**

| Mwaka | Kesi Zilizowasilishwa | Kesi Zilizoamuliwa | Kesi Zinazosubiri mbele ya Mahakama |
|---|---|---|---|
| 2020 | 68 | 16 | 52 |
| 2021 | 154 | 60 | 94 |
| 2022 | 106 | 49 | 57 |
| 2023 | 121 | 80 | 41 |
| 2024 | 98 | 60 | 38 |

***Chanzo: Repoti ya Muhtasari wa takwimu za kiuchumi na kijamii Zanzibar 2023/24.***

# SURA YA NANE

## 8.0 MAENDELEO YA KIUCHUMI NA KIJAMII ZANZIBAR MWAKA 2024

Uchumi wa Zanzibar umekuwa kwa wastani wa asilimia 7.1 mwaka 2024, ukuaji huo umekwenda sambamba na maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Juhudi na weledi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kubuni sera na mikakati ya kuimarisha uchumi, zimeendelea kuwa kichecho cha kubadili changamoto za ukuaji wa uchumi kuwa fursa za maendeleo. Mwaka 2024, miongoni mwa viashiria vya moja kwa moja vya maendeleo ya kiuchumi na kijamii ni kama ifuatavyo:

i. Kuongezeka kwa idadi ya miradi ya uwekezaji kwa asilimia 15, kutoka miradi 114 mwaka 2023, kufikia miradi 131 yenye jumla ya thamani ya TZS 1,877.7 bilioni mwaka 2024;

ii. Kuongezeka kwa ajira mpya zilizosajiliwa kutoka Serikalini, Mashirika ya Serikali na Sekta Binafsi kwa asilimia 1.4 kutoka jumla ya ajira 82,225 (Wanaume 43,643 na Wanawake 38,582) mwaka 2022/2023, kufikia jumla ya ajira 83,430 (Wanaume 43,629 na Wanawake 39,801) mwaka 2023/2024;

iii. Kuimarika kwa sekta ndogo ya Mazao kwa asilimia 6.4 mwaka 2024 kutoka asilimia 2.8 mwaka 2023. Ukuaji huo umetokana na kuimarika kwa uhakika wa chakula kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa mpunga kwa njia ya umwagiliaji maji kufikia tani 11,634.5 zenye thamani ya TZS 15,653.8 milioni mwaka 2024, ikilinganishwa na tani 7,296.5 zenye thamani ya TZS 9,830.8 milioni mwaka 2023;

iv. Kuongezeka kwa kiwango cha usambazaji umeme kwa asilimia 16.5. kutoka kWh 560,702 mwaka 2023 kufikia kWh 671,732 mwaka 2024. Ongezeko hilo limekwenda sambamba na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na mauzo ya umeme kwa asilimia 23.3; kutoka TZS 158,448 bilioni mwaka 2023 hadi kufikia TZS 195,517 bilioni mwaka 2024;

v. Kuongezeka kwa shughuli za Uchumi wa Buluu na matumzi bora ya rasilimali za bahari, kumepelekea kuimarika kwa sekta ndogo ya Uvuvi kufikia asilimia 14.2 kutoka asilimia 8.1 mwaka 2023;

vi. Kuongezeka kwa idadi ya watalii wa kimataifa waliotembelea Zanzibar kwa asilimia 15.2 kutoka watalii 638,498 mwaka 2023, hadi kufikia watalii 736,755 mwaka 2024. Ongezeko hilo limepelekea kuongezeka kwa thamani ya mauzo yatokanayo na uhaulishaji wa huduma (Receipts from Service Account) kwa asilimia 15.4 kutoka jumla ya thamani ya Dola za Kimarekani 906.6 millioni kwa mwaka ulioishia Disemba 2023, hadi kufikia thamani ya Dola za Kimarekani 1,046.5 milioni kwa mwaka ulioishia Disemba 2024;

vii. Kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi waliofaulu kidato cha nne (4) kwa asilimia 2.6 kutoka wanafunzi 20,800 mwaka 2023 kufikia wanafunzi 21,338 mwaka 2024. Kati ya hao, Wanafunzi wa kiume ni 8,680 kutoka Wanafunzi 8,469 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 2.4 na wanafunzi wakike ni 12,658 kutoka Wanafunzi 12,331 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 2.6;

viii. Kuimarika kwa viwango vya miundombinu ya mawasiliano ya barabara (Stardard Road Networks) kwa kiwango cha lami zenye jumla ya urefu wa kilomita 1,023.42 kati ya kilomita 599.55 zisizo na lami;

ix. Kuongezeka kwa mapato ya ndani kufikia TZS 1,279.0 bilioni mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia 97.1 ya makadirio ukilinganisha na jumla ya TZS 1,075.1 bilioni zilizokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2023/2024. Aidha, kumejitokeza ukuaji wa mapato wa TZS 203. bilioni sawa na asilimia 18.9; na

x. Kuimarika kwa hali ya amani na utulivu hapa nchini.

## SURA YA TISA

## 9.0 UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2024/2025

### 9.1 Mapato ya Serikali

### 9.1.1 Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani

Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali ilikadiriwa kukusanya mapato kutokana na vyanzo vya ndani jumla ya TZS 1,719.0 bilioni sawa na asilimia 26.2 ya Pato la Taifa. Kati ya fedha hizo, jumla ya TZS 1,466.7 bilioni zilitarajiwa kukusanywa kutoka vyanzo vya kodi na TZS 252.3 bilioni kutokana na vyanzo visivyo vya kodi. Kati ya TZS 1,466.3 bilioni zitokanazo na kodi, Mamlaka ya Mapato Zanzibar ilitarajiwa kukusanya kiasi cha TZS 845.9 bilioni, Mamlaka ya Mapato Tanzania ilikadiriwa kukusanya TZS 600.1 bilioni na TZS 21 bilioni zilipangwa kukusanywa na Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kutokana na Kodi ya Mapato kwa wafanyakazi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania waliopo Zanzibar.

Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 mapato ya ndani yalifikia TZS 1,279.0 bilioni sawa na asilimia 97.1 ya makadirio ya kipindi hicho ukilinganisha na jumla ya TZS 1,075.9 bilioni zilizokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2023/2024, kumejitokeza ukuaji wa mapato wa TZS 203.1 bilioni sawa na asilimia 18.9. Kati ya makusanyo hayo, mapato kutokana na kodi yalifikia TZS 1,142.3 bilioni ambazo ni sawa na asilimia 102.3 ya makadirio. Mapato yasiyokuwa ya kodi yalifikia TZS 136.7 bilioni sawa na asilimia 54.2 ya makadirio.

### 9.1.2 Ukusanyaji wa Mapato Kitaasisi

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ilikusanya jumla ya TZS 471.0 bilioni sawa na asilimia 106 ya makadirio ya TZS 442.9 bilioni ikilinganishwa na ukusanyaji wa kipindi kama hicho kwa mwaka 2023/2024 ambapo jumla ya TZS 373.2 bilioni zilikusanywa, sawa na ongezeko la asilimia 26 . Aidha, Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) ilikusanya jumla ya TZS 655.5 bilioni sawa na asilimia 99.6 ya makadirio ya TZS 657.9 bilioni. Mapato ya ZRA kwa mwaka 2024/2025 yameongezeka kwa asilimia 17.2 ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka 2023/2024 ambapo jumla ya TZS 559.3 bilioni zilikusanywa. Mapato yasiyokuwa ya kodi yamefikia TZS 136.7 bilioni sawa na asilimia 68.2. ya makadirio ya TZS 200.4 bilioni.

### 9.1.3 Mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo

Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Julai 2024 hadi Machi 2025 Serikali ya Mapinduziya Zanzibar imepokea misaada ya kibajeti (GBS 4.5%) yenye thamani ya TZS 76.6 bilioni. Aidha, Ruzuku na Mikopo iliyopokelewa kwa ajili ya Miradi na Programu za Maendeleo imefikia TZS 353.0 bilioni sawa na asilimia 223.8 ya makadirio ya kipindi hicho ya TZS 157.8 bilioni.

## 9.2 Matumizi ya Serikali 2024/2025.

Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali ilikadiriwa kufanya matumizi ya jumla ya TZS 4,961.4 bilioni sawa na asilimia 75.5 ya Pato la Taifa. Kati ya fedha hizo, jumla ya TZS 1,698.3 bilioni ni matumizi ya kazi za kawaida na jumla ya TZS 2,951.1 bilioni ni matumizi ya kazi za Maendeleo. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 mwaka wa fedha 2024/2025 jumla ya TZS 2,186.3 bilioni zimekadiriwa kutumika. Kati ya matumizi hayo yaliyokadiriwa, TZS 1,159.9 bilioni ni kwa kazi za Kawaida na TZS 785,297 milioni ni kwa Kazi za Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2025, matumizi halisi yalifikia TZS 2,255.1 bilioni. Kati ya matumizi hayo TZS 1,081.9 bilioni sawa na asilimia 93.2 zilitumika kwa kazi za kawaida na TZS 1,010.3 bilioni sawa na asilimia 128.7 zilitumika kwa Kazi za Maendeleo.

### 9.2.1 Matumizi ya Kazi za Kawaida

Matumizi ya Kazi za Kawaida kwa kipindi cha (Julai, 2024 hadi Machi, 2025) mwaka wa Fedha 2024/2025 yalifikia jumla ya TZS 1,081.9 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 18.2 ikilinganishwa na matumizi ya kawaida ya kipindi kama hicho mwaka 2023/2024, ambapo jumla ya TZS 915.4 bilioni zilitumika.

### 9.2.2 Mishahara

Kati ya matumizi ya kazi za kawaida, matumizi ya Mishahara yalifikia TZS 489.1 bilioni katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 mwaka wa fedha 2024/2025 sawa na asilimia 100.3 ya makadirio ya kipindi hicho. Matumizi hayo ni sawa na ongezeko la asilimia 13.7 ikilinganishwa na kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024, ambapo jumla ya TZS 430.2 bilioni zililipwa.

### 9.2.3 Matumizi Mengineyo

Matumizi mengineyo ukitoa Mfuko Mkuu wa Serikali yamefikia TZS 214.1 bilioni sawa na asilimia 94.8 ya makadirio ya kipindi hicho, matumizi hayo ni sawa na ongezeko la asilimia 14.3 ikilinganishwa na matumizi mengineyo ya mwaka wa fedha 2023/2024 ya jumla ya TZS 187. 3 bilioni.

### 9.2.4 Matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025 matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali yalifikia TZS 284.6 bilioni sawa na asilimia 87.9 ya makadirio ya kipindi hicho. Matumizi hayo ni sawa na ongezezko la asilimia 32.4 ikilinganishwa na matumizi kama hayo katika mwaka wa fedha 2023/24, ambapo jumla ya TZS 214.9 bilioni zilitumika

### 9.2.5 Matumizi ya Kazi za Maendeleo.

Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 mwaka wa fedha 2024/2025, jumla ya matumizi ya Maendeleo yalikuwa TZS 1,010.3 sawa na asilimia 128.7 ya lengo la TZS 785.3 bilioni. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani zilikuwa TZS 858.4 bilioni, sawa na asilimia 136.8 ya makadirio, na fedha za nje zilikuwa ni TZS 151.9 bilioni sawa na asilimia 96.3 ya makadirio ya TZS 157.8 bilioni na TZS 162.8 ni Mfuko wa kulipia Madeni, sawa na asilimia 67.5 ya makadirio ya TZS 241.1 bilioni.

## 9.3 Deni la Taifa

Hadi Machi 2025, deni la Taifa la Zanzibar limefikia TZS 1,334.6 bilioni ikilinganishwa na TZS 934 bilioni katika kipindi kama hicho mwaka 2024, ikiwa ni ongezeko la asilimia 42.9. Mikopo hii ilitumika kugharamia miradi mbali mbali ya maendeleo. Aidha, kati ya jumla ya deni la TZS 1,334.6 bilioni la Serikali, TZS 1,319.4 ni deni la ndani na TZS 15.2 bilioni ni deni la nje.

## SURA YA KUMI

## MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MIRADI YA KIMKAKATI KWA KIPINDI CHA JULAI 2024 HADI MACHI 2025

### 10.1 UTANGULIZI

Kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2024/25, Serikali imegharamia utekelezaji wa miradi ya kimkakati katika maeneo mahsusi, Kuimarisha Uchumi wa Buluu; Miundombinu; Mageuzi ya kiuchumi; Huduma za Kijamii; pamoja na Utawala Bora na Uhimilivu kama yalivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo (ZADEP) 2020/21-2025/26. Maeneo haya yameainishwa kuwa utekelezaji wake utaleta matokeo chanya na kwa haraka zaidi, kwa kuongeza ukusanyaji wa mapato ya Serikali, upatikanaji wa ajira kwa wananchi, uwekezaji, ubora wa mazingira ya kufanyia kazi pamoja na kuimarisha hali za wananchi. Kupitia utekelezaji wa maeneo hayo, programu na miradi 23 imepangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2024/25.

Kwa mwaka 2024/2025 jumla ya TZS 2,086.72 bilioni zilipangwa kutumika ili kutekeleza programu na miradi ya kimkakati. Kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, Programu na Miradi ya Kimkakati imepangiwa kutumia jumla ya TZS 1,130.1 bilioni (TZS 577.3 bilioni kutoka Serikalini na TZS 552.8 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

Kwa kipindi cha miezi tisa Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya programu na miradi 20 imetekelezwa sawa na ongezeko la asilimia 43 ikilinganishwa na miradi 14 iliotekelezwa katika kipindi kama hiki 2023. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 691.62 bilioni sawa na asilimia 61 ya lengo la 1,130.1 bilioni zimepatikana (TZS 508.7 bilioni kutoka Serikalini sawa na asilimia 88 ya lengo na TZS 182.9 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo sawa na asilimia 33 ya lengo). Utekelezaji wa Programu na Miradi hiyo kwa maeneo mahsusi ni kama ifuatavyo:-

**i. Kutumia Fursa za Uchumi wa Buluu**

Kwa mwaka 2024/2025 eneo hili lilipangiwa kutekeleza programu moja (1) na miradi minne (4) ya maendeleo ambayo imepangiwa kugharimu kiasi cha TZS

453 bilioni kwa Uimarishaji wa Maeneo ya Kihistoria katika maeneo ya fukwe; Ujenzi wa bandari Jumuishi ya Mangapwani, Ujenzi wa Madiko na Masoko ya Kisasa ya Samaki, Ujenzi wa Bandari ya Maruhubi na Ununuzi wa Boti mbili za Serikali. Kwa kipindi cha miezi tisa Julai 2024 hadi Machi 2025, programu na miradi hiyo ilipangiwa kiasi cha TZS 256.5 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, TZS 163.2 bilioni sawa na asilimia 64 ya lengo la TZS 256.5 bilioni zimepatikana. Utekelezaji wa eneo hili ni kama ifuatavyo:

**a.Programu ya Uimarishaji wa Maeneo ya Kihistoria katika maeneo ya fukwe**

Programu ina lengo la kuendeleza Sekta ya Utalii kwa kuimarisha na kuyahifadhi maeneo ya kihistoria na kukuza utalii ambao utaongeza fursa za ajira, vivutio vya utalii na kuongeza Pato la Taifa. Programu hii imeanza mwaka wa fedha 2017/18 na inatarajiwa kukamilika mwaka 2024/25 kwa Awamu ya Kwanza.

Kwa mwaka 2024/2025, programu imepangiwa kiasi cha TZS 15.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, Programu ilipangiwa kutumia TZS 8.3 bilioni kwa ajili ya kufanya Uimarishaji katika maeneo ya Mtoni Palace Unguja na kufanya Uimarishaji katika Bandari ya Majahazi Chake-Chake Pemba. Hadi kufikia Machi, 2025 TZS 889.4 milioni sawa na asilimia 11 ya lengo zimetumika kwa kazi ya kujenga ukuta wa kuzuia athari za bahari katika eneo la Mangapwani pamoja na kuweka ardhi sawa kwa maeneo ya Mangapwani. Vile vile, katika eneo la Mji Mkongwe katika jengo la Ngome kongwe, kazi zinazoendelea ni kufanya matengenezo ya theatre, matengenezo ya vibaraza, bustani na kusafisha kuta za ndani na utekelezaji umefikia asilimia 77 ya kazi yote. Katika Uimarishaji wa maeneo ya kihistoria kwenye Kasri la Mtoni na Pango la Pete upo katika hatua ya manunuzi. Vile vile, Rasi Mkumbuu, shughuli zilizotekelezwa ni umaliziaji wa tarazo, kufanya fitting ya maji na umeme, kuweka madirisha, milango na kujenga jengo la kujisaidia (Toilet building), ujenzi wa hodhi na mnara umekamilika kwa asilimia 100. Aidha, ukarabati wa maeneo ya makaburi, kisima na msikiti umefikia asilimia 90, utengenezaji wa njia za kupita na sehemu ya maegesho ya vyombo vya moto pamoja na upandaji wa bustani umefikia asilimia 90. Katika kuimarisha maeneo ya kihistoria Fufuni na Kichokochwe pamoja na kufanya marekebisho katika eneo la bandari ya Majahazi liliopo Chake Chake Pemba, shughuli hizi zipo katika hatua za manunuzi.

Kukamilika kwa programu hii kutasaidia kuyahifadhi na kuyalinda maeneo ya kihistoria ya Zanzibar, kuongeza Pato la Taifa kwa kupitia ukusanyaji wa mapato katika maeneo hayo na kukuza sekta ya Utalii kwa kuongezeka vivutio vya utalii nchini.

**b. Mradi wa Ujenzi wa Madiko na Masoko ya Kisasa ya Samaki**

Mradi huu una lengo la kuwawezesha wavuvi kupata huduma za msingi za bandari na masoko kwa kuwajengea madiko na masoko ya kuhifadhia na kuuzia samaki yenye hadhi ya kisasa katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba. Mradi huu umeanza mwaka wa fedha 2023/24 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2025/2026. Kwa mwaka 2024/25 Mradi umekusudia kujenga madiko na masoko mawili ya kisasa ya samaki ambapo soko moja linajengwa katika eneo la Fungurefu Mkokotoni Unguja na jengine katika eneo la Mkoani Pemba.
Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 27.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, Mradi ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 14.9 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, TZS 12.7 bilioni sawa na asilimia 86 ya lengo zimepatikana. Fedha hizo zimetumika kwa utekelezaji wa kazi za ujenzi wa ukuta wa kuzungusha eneo la mradi lisiathiriwe na maji chumvi, ujenzi wa daraja kwa ajili ya kupita wananchi na kingo za maji umekamilika kwa Mkoani Pemba, kazi zinazoendelea ni Ujenzi wa jengo la biashara na ofisi ambapo upo katika hatua ya kuweka zege kwa ajili ya ghorofa ya pili. Aidha, ujenzi wa maeneo ya maduka, vyoo na ujenzi wa miundombinu ya barabara za ndani unaendelea. Kwa upande wa Unguja kazi inayoendelea ni kuanza kwa hatua za maandalizi ya ujenzi wa soko la kisasa la Samaki katika eneo la Fungurefu ambapo hatua za matayarisho ya ujenzi yamekamilika ikiwemo; michoro, BoQ na Mkandarasi ameshapatikana na ameshakabidhiwa eneo kwa ajili ya ujenzi.

Kukamilika kwa mradi huu kutawezesha wananchi kupata eneo lenye hadhi ya kisasa kwa ajili ya kuhifadhia na kuuzia samaki ambalo litahudumia wastani wa watu 20,000 kwa siku, litatoa ajira kwa wananchi, litaongeza thamani kwa samaki na kuwa kivutio cha watalii. Serikali itaongeza mapato yake ya ndani na kukuza kipato cha wananchi

**c. Mradi wa Ujenzi wa Bandari Jumuishi – Mangapwani;**

Dhamira ya Mradi huu ni kujenga bandari jumuishi (Multipurpose Port) ambayo inajumuisha ujenzi wa gati ya mizigo eneo la ushushaji na upakiaji wa mafuta na chelezo cha kukarabati meli. Serikali inatarajia kushirikiana na sekta binafsi katika ujenzi wa bandari hii. Mradi huu ulianza mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo kwa sasa Upembuzi Yakinifu (feasibility study) umekamilika ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mradi kwa hatua za maandalizi.

Kwa mwaka 2024/2025, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 257.54 bilioni (TZS 157.54 bilioni kutoka Serikalini na TZS 100.00 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 141.6 bilioni (TZS 86.6 bilioni kutoka Serikalini na TZS 55.0 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi, 2025 TZS 155.7 bilioni sawa na asilimia 110 kutoka Serikalini zimepatikana. Fedha hizo zimetumika kwa kazi ya ujenzi wa nyumba za fidia, ujenzi wa miundombinu ya barabara na kufikisha huduma ya Umeme na Maji kwa ajili ya uwekezaji wa Bandari hiyo. Ujenzi wa Barabara za ndani katika Bandari jumuishi yenye urefu wa kilomita 12 unaendelea. Jumla ya kilomita 5.8 zimeshawekwa lami na kilomita 6.2 zinasubiria malipo ya fidia ya mazao na nyumba ili kupisha ujenzi huo. Kazi zinazoendelea katika ujenzi wa Barabara hiyo ni pamoja na ujenzi wa misingi, kujenga eneo la kupita kwa miguu (Pedestrian walk) pamoja na uwekaji taa na kwa upande wa ujenzi wa bandari Awamu ya Kwanza, Mkandarasi wa Kampuni ya CHECC ya nchini CHINA amekabidhiwa eneo la ujenzi na kazi za utafiti wa udongo na bahari zinaendelea. Kukamilika kwa mradi huu kutasaidia kuinua uchumi wa Zanzibar pamoja na kutoa ajira kwa wananchi. Vile vile, kutasaidia kukuza na kuimarisha kibiashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara pamoja na Nchi za jirani ikiwemo Mombasa-Kenya na Ukanda wa Bahari ya Afrika Mashariki. Vile vile, kurahisisha usafirishaji wa mizigo kutoka lango kuu la bandari kuelekea maeneo mengine Zanzibar.

**d. Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Abiria Maruhubi;**

Mradi huu una lengo la kuimarisha huduma ya usafirishaji wa abiria na mizigo katika visiwa vya Unguja na Pemba na Maeneo mengine. Mradi unahusisha ujenzi wa gati ya abiria na gati ya mizigo (roro) katika eneo hilo. Mradi unatarajiwa kutekelezwa baina ya Serikali na Mwekezaji Binafsi Kampuni ya ZF DEVCO

kutoka Uholanzi na unatarajiwa kutekelezwa kwa muda wa miaka mitatu (3). Mradi umeanza mwaka wa fedha 2024/25 na umepangiwa kutumia kiasi cha TZS 127.50 bilioni kutoka kwa Mwekezaji Binafsi. Kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, Mradi umepangiwa kutumia kiasi cha TZS 70.1 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, kazi ya upimaji wa udongo imekamilika na Mkandarasi ameanza kuleta vifaa kwa ajili ya kuanza kazi. Aidha, kazi ya ufukiaji wa eneo la juu la bahari imeanza ili kuweka usawa (level).

Kukamilika kwa mradi huu kutasaidia kuimarisha usafirishaji wa abiria na mizigo ndani na nje ya nchi, kuongeza ajira na ustawi wa maisha kwa wananchi. Vile vile, kutasaidia kuondoa msongamano wa mizigo katika bandari ya Malindi, kuwa kivutio kwa wawekezaji, kukuza utalii wa Zanzibar na kuongezeka kwa Mapato ya Serikali. Mradi huu unatarajiwa kuimarisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii Zanzibar.

**e. Mradi wa Ununuzi wa Boti mbili za Serikali**

Mradi huu una lengo la kuimarisha usafirishaji wa abiria na mizigo kwa wananchi wa visiwa vya Unguja na Pemba kwa kupunguza changamoto za usafiri zinazoikabili Zanzibar. Mradi huu ulianza mwaka wa fedha 2024/2025 na umepangiwa kiasi cha TZS 26.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, Mradi huu ulipangiwa kutumia kiasi cha TZS 14.3 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 2.9 bilioni zimepatikana sawa na asilimia 20. Kazi ya Michoro imeandaliwa na tayari imewasilishwa kwa Kampuni ya RINA- Classification Society ya nchini Italy kwa ajili ya kuthibitishwa (Approval). Aidha, Mradi unatekelezwa na Shirika la Meli kwa mkopo wa Benki uliodhaminiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mkopo huo umegharimu jumla ya USD milioni 27. Malipo ya Awali yameshafanyika kwa Kampuni ya Synergy Shipbuilder ya India kwa ajili ya kazi ya ujenzi.

Kukamilika kwa mradi huu kutasaidia kuondosha changamoto za usafiri wa abiria na mizigo kwa wananchi wa visiwa vya Unguja na Pemba, kuongeza mapato ajira kwa vijana na Serikali.

**ii. Mazingira Wezeshi na Kuimarisha Miundombinu**

Kwa mwaka 2024/2025 eneo hili limepangiwa kutekeleza programu tatu na miradi mitatu ya maendeleo ambayo itagharimu jumla ya TZS 778.10 bilioni kwa

ujenzi wa barabara kuu, barabara za ndani, matengenezo ya barabara za mjini, ujenzi wa uwanja wa ndege wa Pemba, kufanya mabadiliko sekta ya nishati na ujenzi wa Kituo na Maegesho ya vyombo vya Usafiri kuhudumia Soko la Mwanakwerekwe. Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya TZS 428.0 bilioni zimepangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 250.0 bilioni sawa na asilimia 58 ya lengo la TZS 428.0 bilioni zimepatikana. Utekelezaji wa eneo hili ni kama ifuatavyo:-

**a. Programu ya Ujenzi wa Barabara Kuu**

Programu hii ni endelevu imeanza mwaka 2022/23 na ina lengo la kujenga barabara kwa kiwango cha lami, ujenzi wa mitaro pamoja na uwekaji wa taa na alama za barabarani Unguja na Pemba ambapo imejumuisha ujenzi wa barabara ya Tunguu-Makunduchi km 53; ujenzi kwa barabara ya Chake Chake-Mkoani km 43.5 na ujenzi wa barabara ya Fumba - Kisauni kilomita 12, ukamilishaji wa ujenzi wa barabara ya Wete –Chake Chake km 22.1, ukamilishaji wa barabara kwa kiwango cha lami km 42.95 ambazo ni barabara ya Jozani-Charawe-Ukongoroni km 23.3, Fuoni-Tunguu km 5.8, barabara ya Bungi km 0.5 na barabara za Nungwi km 13.35.

Kukamilika kwa programu hii itasaidia kuunganisha miji ya Zanzibar na maeneo mengine ya kiuchumi ikiwemo viwanja vya ndege na bandari na kuhuisha uchumi na uwekezaji.

Kwa mwaka 2024/2025, programu imepangiwa kiasi cha TZS 311.77 bilioni (TZS 115.54 bilioni kutoka Serikalini na TZS 196.23 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Programu hii imepangiwa kutumia TZS 171.5 bilioni (TZS 63.5 bilioni kutoka Serikalini na TZS 107.9 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 12.0 bilioni sawa na asilimia 7 zimepatikana (TZS 3.0 bilioni kutoka Serikalini na TZS 8.9 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Fedha hizo zimetumika kwa ajili ya kumlipa Mkandarasi MECCO katika Ujenzi wa Barabara ya Wete – Chake Chake (22.1km) urefu wa km 16 kuanzia Melitano mpaka Machengwe zimeshawekwa lami na km 3.6 zimeshawekwa kifusi katika matabaka mbali mbali kutoka Mzambarauni hadi Weni na baada ya ulipaji wa fidia kwa wananchi waliopisha mradi watakamilisha eneo lililobakia. Kwa barabara za Jozani-Charawe, Ukongoroni –Bwejuu km 23.3, Fuoni Tunguu km 5.8, barabara za Nungwi km 13.35 na barabara ya Bungi km 0.5 zimekamilika kwa asilimia 100.

Kukamilika kwa programu hii kutasaidia kuunganisha miji mikubwa na maeneo ya usafirishaji ikiwemo viwanja vya ndege na bandari pamoja na maeneo mengine ya Zanzibar ambayo itarahisisha na kushajihisha shughuli za uchumi na uwekezaji. Vile vile, kukamilika kwa barabara hizi kutapunguza ajali za barabarani, misongamano ya magari, uharibifu wa vyombo vya usafiri na kutuwama kwa maji.

**b. Programu ya Ujenzi wa Barabara za Ndani**

Programu hii ni endelevu imeanza mwaka 2022/2023 ina lengo la kuunganisha mitaa na maeneo mbalimbali na barabara kuu ili kuweza kupunguza msongamano katika barabara kuu pamoja na kuongeza haiba ya kupendezesha miji katika maeneo ya Zanzibar. Programu itahusisha ujenzi wa barabara za ndani zenye urefu wa kilomita 275.9 katika maeneo ya mijini na vijijini Unguja na Pemba. Kwa mwaka 2024/2025, Programu imepangiwa kutumia kiasi cha TZS 45.60 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 25.1 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, Jumla ya TZS 102.6 bilioni zimepatikana kutoka Serikalini sawa na asilimia 409 ya lengo la TZS 25.1 bilioni.

Kwa Unguja kazi za uwekaji wa kifusi kwa tabaka mbali mbali zimefanyika kwa barabara za Kilindini -Kilimajuu (1.44km) na Kilimajuu-Kigomani (4.0 km). Vile vile, barabara za Kichakani (Ghana)-Kichaka Mabundi (0.5 km), Ussi Kombo-Daniel Ali-Mnarani (2.52km), Mto wa Pwani-Fungurefu (2.0 km), Bwekunduni-Soko la Samaki (2.66km), Kitaruni - Kichaka - Mabundi - Mkarafuu Pakacha (2.14km), Mfurumatonga-Mlilile Skuli (2.84 km), Mfurumatonga-Mbuyu Popo (3.35km), Donge Mbiji-Chechele (2.0km), Masingini-Kijichi (8.0km) na Mwakaje-Mwachealale-Bumbwisudi (5.13km) zimeshawekwa lami.

Kwa upande wa barabara za Pemba, barabara ya Mgagadu – Kwautao km 5.6, Mzambarau Takao-Mchangamdogo km 6.13, Konde-Msuka km 4.1, Pembeni-Pandani km 3.34, Kengeja-Shamiani-Kiimbini Spar km 4.85 na Wawi Mesi-Mzambaraumboko km 6.4 hizi zote zimewekwa kifusi tabaka tofauti. Vile vile, barabara ya Chanjamjawiri – Pujini (Matale) km 4.65, Finyakicha km 8.93, Micheweni-Shumba Mjini-Bandarini km 2.99, Ukutini-Mtangani-Bandarini km 4.65 na Micheweni-Kiuyu-Maziwa Ng'ombe km 7.57 zimekamilika kwa kuwekwa lami na alama za barabarani kwa baadhi ya barabara za ndani umefanyika kwa asilimia 30.

Kukamilika kwa programu hii kutasaidia kuunganisha mitaa na vijiji 62 vya Unguja na Pemba, kupunguza msongamano katika barabara kuu, kuongeza haiba na kupendezesha miji, mitaa na vijiji. Pia, Programu itasaidia kurahisisha usafirishaji wa mizigo na kuimarisha ukuaji wa uchumi, kuongeza kipato cha mwananchi mmoja mmoja pamoja na kuimairika kwa sekta nyengine za kiuchumi zikiwemo sekta ya kilimo na biashara. Vile vile, barabara zinatarajiwa kupunguza ajali za barabarani, misongamano ya magari kwenye barabara kuu, uharibikaji wa vyombo vya usafiri na kutuwama kwa maji.

**c. Programu ya Matengenezo ya Barabara za Mjini**

Programu imeanza mwaka 2022/2023 na inatarajiwa kukamilika mwaka 2025/2026. Programu hii ina lengo la kuimarisha haiba ya mji wa Zanzibar kwa ujenzi wa barabara katika maeneo ya mjini. Programu inajumuisha ujenzi wa barabara kilomita 100.9 za mjini na uimarishaji wa barabara katika maeneo ya Mkoa wa Mjini Magharibi. Ujenzi wa barabara hizi utaongeza haiba na kupendezesha Mji wa Zanzibar na kusaidia kuimarika kwa sekta nyengine ikiwemo sekta ya usafirishaji, utalii na biashara. Kwa mwaka 2024/2025, programu imepangiwa kiasi cha TZS 112.09 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, Programu imepangiwa kutumia kiasi cha 61.7 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha TZS 42.9 bilioni sawa na asilimia 70 ya lengo zimetumika. Fedha hizo zimetumika kwa kazi ya ujenzi wa barabara na kuweka mitaro, alama na taa kwa barabara za Kiembesamaki Junction Amani – Mtoni, Uwanja wa ndege, Mpendae Planned area. Aidha, barabara za Mazizini –ZRB- Mombasa km 0.6 na kituo cha Polisi Ng'ambo – Mfereji wa Wima km 0.33, Mazizini kituo cha Polisi - Chukwani Jeshini km 4.61 zinaendelea kujengwa kwa kiwango cha lami. Kwa ujumla utekelezaji wa programu hii, jumla ya kilomita 31.63 zimejengwa kwa kiwango cha lami na jumla ya kilomita 29.42 zimejengwa kwa kiwango cha zege kwa barabara za njia moja na kwa barabara za njia mbili jumla ya kilomita 15.12 zimekamilika kwa kiwango cha lami.

Kwa upande wa barabara ya juu (Flyover) ya Mwanakwerekwe kazi inayoendelea kwa sasa ni ujenzi wa chelezo kwa pande zote mbili za daraja na ujenzi umefikia asilimia 90 na ujenzi wa flyover ya Amani hatua iliofikia ni kunyanyua nguzo zitakazobeba flyover. Aidha, ujenzi wa nguzo zilizobaki na chelezo kwa pande zote mbili utaendelea baada ya kuondoshwa kwa bomba la maji na malipo ya fidia kukamilika kwa wananchi.

Kukamilika kwa programu hii kutaongeza haiba na kupendezesha miji yetu na kusaidia kuimarika kwa sekta nyengine ikiwemo sekta ya usafirishaji, utalii, biashara na kuondoa msongamano pamoja na kupunguza ajali katika maeneo hayo.

**d. Mradi wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege- Pemba.**

Mradi huu una lengo la kuimarisha miundombinu ya usafirishaji wa abiria na mizigo kwa njia ya anga ili iweze kuwa katika viwango vya Kimataifa. Programu inahusisha ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba, ujenzi wa maegesho ya ndege, njia za kupitia ndege pamoja na sehemu za kukaa abiria.

Mradi huu ulianza mwaka 2023/2024 unatarajiwa kukamilika kwa Awamu ya kwanza mwaka 2027/28. Kwa mwaka 2024/2025, mradi umepangiwa jumla ya TZS 101.4 bilioni (TZS 9.50 bilioni kutoka Serikalini na TZS 91.89 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, Mradi huu umepangiwa kutumia kiasi cha TZS 55.8 bilioni. (TZS 5.2 bilioni kutoka Serikalini na TZS 50.5 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 13.2 bilioni sawa na asilimia 24 zimepatikana (TZS 2.5 bilioni kutoka Serikalini na TZS 10.7 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Fedha hizo zimetumika kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi 727 kupisha eneo la ujenzi wa Uwanja wa Ndege. Mkandarasi ameshaanza kufikisha vifaa na wataalam na kuendelea na hatua za manunuzi ya vifaa husika vya ujenzi na maabara. Pia, mkandarasi anaendelea na kazi za usanifu wa michoro ambapo tayari ameshawasilisha rasimu ya awali (inception report) kwa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi.

Kukamilika kwa programu hii kutasaidia kuifungua Pemba kiuchumi kwa kukaribisha mashirika ya ndege za Kimataifa, kukuza kibiashara na kiuwekezaji kwa kuongezeka kwa uingiaji wa watalii watakaotembelea Pemba na kupatikana kwa ajira rasmi.

**e) Mradi wa Kuifanyia Mabadiliko sekta ya Nishati (ZESTA)**

Mradi una lengo la kuimarisha miundombinu ya umeme na kuzijengea uwezo Taasisi zinazoshughulikia masuala ya nishati ili ziweze kuimarisha utoaji wa huduma za usambazaji wa umeme katika maeneo tofauti ya visiwa vya Unguja na Pemba. Mradi unatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo. Kwa mwaka 2024/2025, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 178.26

bilioni (TZS 4.0 bilioni kutoka Serikalini na TZS 174.26 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, Mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 98.0 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 79.5 bilioni sawa na asilimia 81 zimepatikana. Fedha hizo zimetumika kwa ujenzi wa ukuta na usafishaji wa eneo kwa ajili ya solar PV, Mkandarasi amekamilisha kupima njia ya umeme, maeneo yote ya ujenzi wa vibanda vya umeme yameshasafishwa na Mafunzo kwa wataalamu wa ZECO kwa ajili ya masuali ya malipo yameshafanyika.

**f) Mradi wa Ujenzi wa Kituo na Maegesho ya Vyombo vya Usafiri Soko la Mwanakwerekwe**

Mradi huu una lengo la kuimarisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi na wafanyabiashara kwa kujenga kituo cha maegesho ya vyombo vya usafiri na huduma nyengine za usafiri katika Soko la Mwanakwerekwe ili kuongeza ufanisi wa upatikanaji wa huduma kwa jamii, kupunguza msongamano wa vyombo na kuongeza Pato la Taifa. Aidha, mradi utatunza mazingira katika eneo la Bwawa la Mwanakwerekwe na kuleta mandhari nzuri zaidi. Kwa mwaka 2024/2025, mradi umepangiwa jumla ya TZS 29.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 16.0 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, Mradi upo katika hatua za awali za kufanya Upembuzi Yakinifu ikiwemo utafiti wa Mazingira na kuangalia sanyansi ya udongo na umbile la eneo husika (geotechnic survey and topographic).

**iii. Kuimarisha Mageuzi ya Kiuchumi**

Kwa mwaka 2024/2025 eneo hili lilipangiwa kutekeleza programu moja na miradi miwili ya maendeleo ambayo imegharimu jumla ya TZS 65.3 bilioni kwa Uimarishaji wa maeneo huru ya Uwekezaji, Uanzishaji na Uendelezaji wa Maeneo Maalum ya Viwanda na Uendelezaji wa Vituo vya Biashara na Maonesho Zanzibar. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 – Machi 2025) jumla ya TZS 35.9 bilioni zimepangwa. Hadi kufikia Machi 2025, TZS 4.1 bilioni sawa na asilimia 11 ya lengo la TZS 35.9 bilioni zimepatikana. Utekelezaji wa eneo hili ni kama ifuatavyo: -

**a. Programu ya Uimarishaji wa Maeneo Huru ya Uwekezaji.**

Programu hii ina lengo la kukuza maeneo huru ya uwekezaji yaliyoainishwa kwa uwekezaji ili kuwavutia Wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kwa kufikisha miundombinu muhimu kwa uwekezaji na biashara ikiwemo barabara, maji, umeme na mawasiliano. Programu hii ilianza mwaka wa fedha 2021/2022 na inatarajiwa kukamilika mwaka 2025/2026. Kwa mwaka 2024/2025, programu imepangiwa jumla ya TZS 15.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, Programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 8.3 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, kazi inayoendelea ni ukamilishaji wa tathmini ya ulipaji fidia. Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa barabara ameshapatikana na Mikataba tayari imeshasainiwa baina ya ZIPA kwa upande wa Serikali na Kampuni ya CRJE ltd kwa ujenzi wa km 35 za barabara za Zone B Micheweni, kwa Bara bara nyengine Zabuni tayari imeshatangazwa. Kukamilika kwa Programu hii kutasaidia kuwa na maeneo ya uwekezaji ambayo yatavutia wawekezaji kuja kuwekeza katika Nchi yetu na kupelekea kuongezeka kwa ajira na Pato la Taifa.

**b. Mradi wa Kuanzisha na Kuendeleza Maeneo Maalum ya Viwanda (Indurstrial Parks);**

Mradi una lengo la kuimarisha maeneo tengefu ya viwanda ili kurahisisha viwanda vidogo vidogo na vya kati viweze kuwa katika maeneo maalum yatakayosaidia kukuza uchumi na kutoa ajira. Mradi huu ulianza mwaka 2019/2020 na kwa mwaka 2024/2025, mradi umepangiwa jumla ya TZS 40.32 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 22.2 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 4.0 bilioni sawa na asilimia 17 ya lengo zimetumika. Fedha hizo zimetumika kwa kazi ya kufanya malipo kwa Kampuni ya China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC), ambae ni Mkandarasi wa ujenzi wa barabara za ndani katika eneo la Viwanda Dunga; Kufanya malipo kwa Kampuni ya Simba Developer, ambae ni Mkandarasi wa Ujenzi wa tangi la Maji katika eneo la Viwanda Dunga na Kufanya malipo kwa Kampuni ya MS/Nimeta, ambae ni Mshauri Elekezi wa kazi ya ujenzi wa miundombinu ya barabara na maji katika eneo la Viwanda Dunga. Ujenzi wa miundombinu ya barabara umefikia asilimia 100 na ujenzi wa tangi la maji umefikia asilimia 100. Vile vile, ujenzi wa ukuta katika eneo lilipojengwa tangi la maji umekamilika pamoja na kujenga uzio wa kisima na usambazaji wa mtandao wa bomba

(Construction of water network) umekamilika, na chumba cha mlinzi, Ujenzi wa ukuta wa waya katika visima unaendelea.

Kukamilika kwa Mradi huu kutasaidia kuimarisha uchumi wa Zanzibar kwa kuchochea uwekezaji wa ndani na nje. Maeneo haya yatatoa fursa ya kuanzisha viwanda vipya, kutoa ajira kwa wananchi, na kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa nchini. Pia, yatasaidia kupunguza utegemezi wa uagizaji wa bidhaa kutoka nje, hivyo kuongeza kukuza biashara za ndani na ushirikiano wa kiuchumi. Vile vile, ujenzi wa miundombinu ya kisasa katika maeneo haya kutafungua milango kwa ukuaji wa sekta nyengine, na kuweza kuinua kiwango cha maendeleo hapa Zanzibar.

**c. Mradi wa Kuendeleza Vituo vya Biashara na Maonesho Zanzibar**

Mradi una lengo la kutoa huduma za kuimarisha sekta ya biashara na viwanda na kukuza wafanyabiashara wadogo wadogo na wa kati. Mradi huu ulianza mwaka wa fedha 2020/2021. Kwa mwaka 2024/2025, mradi umepangiwa jumla ya TZS 10 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 5.5 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 349.0 milioni sawa na asilimia 6 ya lengo zimetumika. Fedha hizo zimetumika kwa kazi ya kufanya malipo kwa Jeshi la Kujenga Uchumi – JKU ikiwa ni malipo ya ujenzi wa miundombinu kwa jengo la utawala katika Kituo cha Maonesho Nyamanzi. Kazi ya uwekaji wa vioo katika ukumbi wa Dkt. Hussein Mwinyi imekamilika, kazi ya ufungaji wa kamera za CCTV imefanyika kwa baadhi ya maeneo pamoja na uwekaji wa mfumo wa mawasiliano ya mtandao wa internet katika eneo la ukumbi wa mikutano.

Kukamilika kwa Mradi huu kutasaidia kuimarisha biashara na kuvutia uwekezaji. Mradi huu utatoa fursa za masoko kwa wajasiriamali na wafanyabiashara wa ndani na wa kimataifa kuonesha bidhaa na huduma zao, hivyo kupanua masoko na kuongeza nafasi za ushirikiano wa kibiashara. Kituo hiki kitakuwa kiungo muhimu katika kuhamasisha maendeleo ya sekta ya biashara kwa kuwaweka pamoja wajasiriamali, wawekezaji na wadau wengine. Vile vile, mradi huu utasaidia kukuza utalii wa kibiashara na kuinua uchumi wa Zanzibar kwa ujumla kupitia mikutano, maonesho, na mawasiliano ya kibiashara ya Kimataifa.

**iv. Kukuza Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii**

Kwa mwaka 2024/2025 eneo hili limepangiwa kutekeleza programu nne na miradi miwili ya maendeleo ambayo imegharimu TZS 674.6 bilioni kwa

Uimarishaji wa Miundombinu ya Elimu, Ukarabati na Ujenzi wa Vituo vya Afya ya Msingi, Ujenzi wa Nyumba za Wafanyakazi katika Hospitali za Wilaya na Mikoa, Uimarishaji wa Huduma za Usambazaji Maji Safi na Salama Zanzibar, Ukarabati na Utanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, pamoja na Ujenzi wa Nyumba za Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025) jumla ya TZS 371.0 bilioni zimepangwa na hadi kufikia Machi 2025, TZS 226.3 bilioni sawa na asilimia 61 ya lengo la TZS 371.0 bilioni zimepatikana. Utekelezaji wa eneo hili ni kama ifuatavyo:-

**a. Programu ya Uimarishaji wa Miundombinu ya Elimu.**

Programu hii ina lengo la kuinua ubora wa elimu kwa kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunza kwa kuimarisha miundombinu ya sekta ya elimu kiujumla ili kuwawezesha wananchi kupata elimu bora na viwango vya ufanisi. Kwa mwaka 2024/2025, programu hii imepangiwa jumla ya TZS 417.5 bilioni (TZS 234.39 bilioni kutoka Serikalini na TZS 183.13 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

Kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, Programu hii imepangiwa kutumia jumla ya TZS 230.0 bilioni (TZS 129 bilioni kutoka Serikalini na TZS 101 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 148 bilioni ya lengo la TZS 230.0 bilioni zimepatikana sawa na asilimia 64 (TZS 94.4 bilioni kutoka Serikalini na TZS 53.4 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

Fedha hizo zimetumika kwa kazi ya kujenga madarasa 420, (Sekondari 120 na Msingi 300), Ujenzi wa madarasa ni kwa skuli za Kiuyu, Zawiyani, Kipangani, Makongeni na Mjini Wingwi, ujenzi upo katika hatua ya uezekaji na Skuli za Kibuyuni, Kibeni, Mgambo, Kisiwa panza, Chambani, Kiwani, Msuka, Ghana, Mjimbini, Kangani, Simai, Jojo, Maziwa ngombe, Mtemani, Micheweni, Shumba, Tumbe B, Kangani, na Chokocho ujenzi umefikia hatua ya umaliziaji kwa kuweka plasta, rangi na sakafu. Aidha, Skuli ya Kinyasini, Gamba na Kidoti ujenzi wa madarasa umekamilika. Kwa ujumla utekelezaji umefikia asilimia 50. Vile vile, kukamilisha madarasa 170 yalioanzishwa na wananchi (madarasa 100 Msingi na 70 Sekondari), Ujenzi wa madarasa upo katika hatua mbali mbali kwa kupiga plasta, sakafu, kuezeka na kupaka rangi, baadhi ya skuli hizo ni Mfenesini, Dimani, Ubago Uzini, Unguja Ukuu, Kibele, Koani, Uchukuni, Kiboje, Ndijani Msingi, Ndijani sekondari, Binguni, Kitogani, Miza wa Miza, Muungoni. Kwa ujumla utekelezaji wake umefikia asilimia 45.

Ujenzi wa uzio kwa Skuli ya Sekondari ya Hasnuu Makame upo hatua ya mwisho kupiga plasta na Skuli ya Mohammed Juma Pindua upo katika hatua ya ukamilishaji na utekelezaji wake umefikia asilimia 80.

Ujenzi wa Dakhalia katika skuli 11 utekelezaji wake unaendelea katika hatua mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kujenga misingi, kuta, kuezeka mapaa, kutia plasta kuweka marumaru na tarazo. Shughuli hizi zinaendelea katika skuli za Lumumba, Misufini, Kiwani, Paje Mtule, Fidel Castro, Maziwa Ng’ombe, Mikindani na Chwaka Tumbe, ujenzi kwa ujumla umefikia asilimia 60, Ujenzi wa Ofisi Kuu Pemba umefikia asilimia 60 na kazi zinazoendelea ni ujenzi wa tofali katika ghorofa ya mwisho na ukarabati wa majengo ya Ofisi za Wizara ya Elimu na Mfunzo ya Amali kwa Unguja utekelezaji wake umefikia asilimia 25 na kwa Pemba bado haujaanza.

Ukarabati wa skuli 100 (msingi 70 na sekondari 30) unaendelea katika hatua mbali mbali ziko ambazo zinazoendelea na zilizokamilika. Kwa skuli ambazo ukarabati wake umekamilika ni skuli za Kiembe Samaki, Chukwani, Kijito Upele, Regeza Mwendo, Nyerere, Kilima Hewa, Kidongo Chekundu, Chuini, Mfenesini na Mbuzini. Ukarabati wa skuli ambazo unaendelea kwa hatua ya kuezua mapaa na kuongeza urefu na kuezeka baadhi ya skuli hizo ni Mwanakwerekwe C, Uroa, Bambi, Uzini, Mwera, Charawe, Ukongoroni, Jendele, Chwaka, Ndijani, Kikungwi, Kiboje, Dunga, Kajengwa, Bwejuu, Kijigoni, Paje, Michamvi, Jambiani, Kikadini, Kitogani, Kiongoni, Fukuchani, Kijini, Gamba, Nungwi, Potoa, Chaani, Kinowe, Kiuyu, Konde “A”, Konde “B”, Makangale, Maziwang’ombe, Micheweni “A”, Micheweni “B”, Mkiang’ombe, Mnarani, Mtemani, Shumba, Wingwi, Msuka na utekelezaji wake kwa ujumla umefikia asilimia 65.

Uendelezaji wa vyuo vitano vya Amali utekelezaji wake upo katika hatua ya zabuni ya kumpata Mkandarasi kwa ajili ya kuanza ujenzi, Utanuzi wa Chuo cha Karume (KIST) utekelezaji upo katika hatua za kuandaa michoro ya kina (Details drawing) na Mshauri Elekezi yupo katika hatua za mwisho za kukamilisha kazi hiyo. Ujenzi wa skuli tatu (Skuli ya Gamba na Mfenesini kwa Unguja na Kifundi kwa Pemba) zenye Dakhalia kwa mashirikiano na BADEA upo katika hatua ya kukamilisha kwa kupaka rangi na kuweka land scape na utekelezaji wake kwa ujumla umefikia asilimia 90.

Kukamilika kwa programu hii kutasaidia kuingiza Idadi kubwa ya wanafunzi katika vyuo vya amali kwa kujenga ujuzi na kuwaandaa katika ajira, kupunguza

idadi ya wanafunzi darasani, kuongezeka kwa kiwango cha ufaulu, kuwa na Mazingira bora ya kusomea na kufundishia, kuongezeka kwa ajira za walimu pamoja na kuwa na mkondo mmoja tu wa masomo kwa siku.

**b. Programu ya Ukarabati na Ujenzi wa Vituo vya Afya ya Msingi;**

Programu hii ina lengo la kuimarisha afya kwa kuimarisha miundombinu ya vituo vya afya vya msingi ili viweze kutoa huduma za afya zenye viwango na kuimarisha afya ya jamii. Programu hii ilianza mwaka wa fedha 2023/24. Kwa mwaka 2024/2025, programu imepangiwa jumla ya TZS 35.00 bilioni kutoka Serikalini kwa kujenga vituo 10 vya Afya ya Msingi. Kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, Programu imepangiwa kutumia kiasi cha TZS 19.3 bilioni.

Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 17.8 bilioni kutoka Serikalini sawa na asilimia 92 ya lengo zimetumika. Fedha hizo zimetumika kwa kujenga vituo 10 ambavyo ni:- Kituo cha Afya Nungwi kipo katika hatua ya ujenzi wa kuta za ndani na kimefikia asilimia 26, Kituo cha Afya Mahonda ujenzi upo katika hatua ya ukamilishaji wa kuezeka na kupiga plasta kwa upande wa nje na umefikia asilimia 50, Kituo cha Afya Sebleni ujenzi upo katika hatua ya kumalizia na umefikia asilimia 55, Kituo cha Afya Tunguu ujenzi upo katika hatua ya kukamilisha na umefikia asilimia 55, Kituo cha Afya Magomeni Wakandarasi wapo katika hatua ya kukamilisha na umefikia asilimia 80 na kwa upande wa Pemba ni Kituo cha Afya Konde ujenzi upo katika hatua ya kuweka jamvi kwa ajili ya ghorofa ya kwanza na ujenzi umefikia asilimia 25, Kituo cha Afya Jadida ujenzi upo katika hatua ya kukamilisha kwa jengo moja na jengo la pili lipo katika kuweka nguzo kwa ajili ya ghorofa ya kwanza kwa ujumla ujenzi umefikia asilimia 63, Kituo cha Afya Mtambile ujenzi upo katika hatua ya msingi na umefikia asilimia 10, Kituo cha Afya Kiuyu Minungwini ujenzi upo katika hatua ya msingi na umefikia asilimia 20, Kituo cha Afya Vitongoji ujenzi upo katika hatua ya kuezeka na kazi zinazoendelea ni ujenzi wa uzio na kibanda cha jenereta na kwa ujumla umefikia asilimia 55 na Kituo cha Afya Chonga kipo katika hatua ya kupiga plasta na kuweka madirisha ghorofa ya chini na ujenzi umefikia asilimia 35.

Kukamilika kwa programu hii kutasaidia kuwa na vituo vyenye viwango ambavyo vitatoa huduma sahihi za matibabu kwa wananchi na kupelekea kuwa na nguvu kazi yenye afya bora na kuongezeka kwa ajira kwa madaktari na wataalamu wa afya.

**c. Programu ya Ujenzi wa Nyumba za Wafanyakazi katika Hospitali za Wilaya na Mkoa.**

Programu hii ina lengo la kuimarisha makaazi kwa madaktari ili waweze kufanya kazi katika mazingira mazuri yenye utulivu zaidi kwa kuongeza ufanisi na kuweza kupatikana katika Mazingira ya kazi muda wote hasa wakati wa dharura. Programu hii imeaanza mwaka wa fedha 2022/2023. Kwa mwaka 2024/2025, programu imepangiwa jumla ya TZS 6.48 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, Programu hii imepangiwa kutumia jumla ya TZS 3.6 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 8.3 bilioni kutoka Serikalini sawa na asilimia 234 ya lengo la kipindi hicho zimepatikana. Fedha hizo zimetumika kwa kazi ya ujenzi wa Nyumba za Wafanyakazi Katika Hospitali za Wilaya kwa Unguja na Pemba. Utekelezaji ni kama ifuatavyo:-

Nyumba za wafanyakazi Mwera Pongwe ujenzi upo katika hatua ya kukamilisha mfumo wa maji na umeme na kumalizia kazi za nje na umefikia asilimia 95, Kitogani ujenzi umekamilika kazi inayoendelea ni ufungaji wa lifti na umefikia asilimia 96, Pangatupu ujenzi upo katika hatua kukamilisha mfumo wa maji na umeme na umefikia asilimia 91 na kwa upande wa Pemba, nyumba za wafanyakazi Kinyasini ujenzi upo katika hatua ya ukamilishaji kwa kupiga rangi na kumalizia kazi za nje na umefikia asilimia 97 na Vitongoji ujenzi upo katika hatua ya kumwaga zege kwa ajili ya ghorofa ya kwanza na umefikia asilimia 52. Kukamilika kwa programu hii kutasaidia kuongezeka kwa huduma za afya, kupunguza msongamano wa wagonjwa katika hospitali kuu na kupatikana kwa madaktari wakati wa dharura.

**d. Programu ya Kuimarisha Huduma za Usambazaji Maji Safi na Salama Zanzibar.**

Programu hii ina lengo la kusimamia na kuhakikisha huduma za usambazaji maji safi na salama zinapatikana katika maeneo yote ya mijini na vijijini ili kuwawezesha wananchi kunufaika na huduma hiyo muhimu katika jamii. Programu ina miradi kama ifuatavyo: -

**i. Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar (INDIA)**

Mradi una lengo la kuimarisha miundombinu ya usambazaji maji safi na salama katika maeneo ya Wilaya ya Magharibi "A", (Mfenesini, Masingini na Kizimbani)

Magharibi “B” (Dimani na Kidutani) na Wilaya ya Kati (Jumbi- Mkorogo) pamoja na ujenzi wa jengo jipya la Ofisi ya Mamlaka ya Maji Zanzibar. Mradi huu ulianza mwaka wa fedha 2017/2018 na kukamilika 2023/24. Kwa mwaka 2024/2025, mradi umepangiwa jumla ya TZS 33.20 bilioni (TZS 10.15 bilioni kutoka Serikalini na TZS 23.05 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 18.3 bilioni (TZS 5.6 bilioni kutoka Serikalini na TZS 12.7 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 21.5 bilioni sawa na asilimia 118 zimepatikana (TZS 3.3 bilioni kutoka Serikalini na TZS 18.1 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Fedha hizo ni kwa ajili ya malipo ya Wakandarasi na Mshauri Elekezi kwa uangalizi wa mradi.

Kukamilika kwa mradi huu kutasaidia kuondoa tatizo la maji na wananchi kupata maji safi na salama.

**ii. Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maji Mkoa wa Mjini Magharibi (ZUWDIFP)**

Mradi huu una lengo la kuongeza uzalishaji wa maji katika maeneo ya Mkoa wa Mjini Magharibi ili kupunguza changamoto za upatikanaji wa huduma hiyo. Mradi utatekelezwa katika maeneo ya Welezo juu, Welezo Magharibi na Migombani. Mradi umeanza mwaka wa 2023/24. Kwa mwaka 2024/2025, mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 3.37 bilioni kutoka Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 1.9 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 1.38 bilioni sawa na asilimia 74 ya lengo zimepatikana. Fedha hizo zimetumika kwa malipo ya Mshauri Elekezi na maandalizi ya zabuni kwa ajili ya kumpata Mkandarasi yanaendelea.

**e. Mradi wa Ukarabati na Utanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja**

Mradi una lengo la kuimarisha huduma katika hospitali ya Mnazi Mmoja kwa kuweka miundombinu ya utoaji wa huduma za afya na ununuzi wa vifaa tiba vya kisasa. Serikali imepanga kufanya ukarabati mkubwa katika hospitali ya Mnazi Mmoja ili kuiwezesha kutoa huduma nzuri na zenye kukidhi viwango vya Kimataifa. Mradi ulianza mwaka wa fedha 2023/24. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 21 bilioni kutoka kwa Washirika wa

Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, Mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya TZS 11.6 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 90.2 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendelo sawa na asilimia 1 ya lengo zimepatikana. Fedha hizo zimetumika kwa gharama za uendeshaji wa ofisi (Mishahara ya watendaji wa kitengo cha Uratibu na uendeshaji wa mradi).

**f. Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Maendeleo.**

Mradi huu una lengo la kuweka mazingira mazuri ya makaazi kwa wananchi pamoja na kuweka haiba nzuri katika mandhari ya mji wa Zanzibar pamoja na kuwapatia wananchi wa Zanzibar makaazi yaliyo bora na kwa gharama nafuu. Mradi ulianza mwaka wa fedha 2024/25, na umepangiwa kutumia jumla ya TZS 40 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, Mradi ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 22.0 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 23 bilioni sawa na asilimia 103 ya lengo zimepatikana. Kazi zilizofanyika ni kufanya upembuzi yakinifu katika eneo linalotekelezwa mradi, kusafisha eneo la mradi, kukodi na kununua baadhi ya vifaa vya ujenzi, kujenga Ofisi kwa ajili ya kuwekea vifaa vya ujenzi na kuendelea na ujenzi wa uzio na utekelezaji umefikia asilimia 70.

Kukamilika kwa mradi huu kutasaidia kupunguza changamoto ya nyumba za makaazi na kukua kwa miji pamoja na kuongezeka kwa mapato ya Serikali.

**v. Kuimarisha Utawala Bora na Uhimili**

Kwa mwaka 2024/2025 eneo hili limepangiwa kutekeleza miradi mitatu ya maendeleo ambayo imegharimu jumla ya TZS 83.62 bilioni kwa Ujenzi wa Mji wa Serikali; Kuweka Zanzibar Salama na Ujenzi wa Mahakama za Wilaya na Mikoa. Kwa kipindi cha miezi tisa Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya TZS 46 bilioni zimepangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2025, TZS 27.3 bilioni sawa na asilimia 59 ya lengo zimepatikana. Utekelezaji wa eneo hili ni kama ifuatavyo: -

**a. Mradi wa kuimarisha ulinzi na usalama.**

Mradi una lengo la kuimarisha ulinzi na usalama ili kuweka mazingira salama kwa wananchi na wageni katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar. Vile vile, kuwa na miundombinu imara ya ulinzi na usalama. Zanzibar ni nchi inayopokea watalii kutoka katika mataifa mengi duniani, hivyo, usalama ni jambo muhimu kwa uchumi wa Zanzibar.

Kwa mwaka 2024/2025 mradi umepangiwa kiasi cha TZS 25 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, Mradi ulipangiwa kutumia kiasi cha TZS 13.8 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 17.4 bilioni sawa na asilimia 126 ya lengo zimepatikana. Fedha hizo zimetumika kwa kununua vitendea kazi kwa ajili matumizi ya Idara Maalum za SMZ ikiwemo sare za maafisa na wapiganaji, magari ya vikosi, vifaa vya ulinzi na usalama na Wizara tayari imeingia Mkataba na Mkandarasi wa Kampuni ya ROM SOLUTION kwa ajili ya mategenezo ya Kamera mradi wa Mji salama. Kukamilika kwa mradi huu kutasaidia kuimarisha utawala bora, ulinzi na usalama, kuongezeka kwa amani na utulivu uliopo nchini, kuongezeka kwa mapato ya Serikali kwa kuongezeka kwa Watalii watakaotembelea nchini, kuongeza ajira na kipato kwa wananchi.

**b. Mradi wa Ujenzi wa Mahakama za Wilaya na Mikoa**

Mradi una lengo la kujenga majengo mapya ya Mahakama ambayo yatasaidia kuweka mazingira mazuri zaidi na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za kisheria na upatikanaji wa haki. Mradi huu ulianza mwaka wa fedha 2023/24 na kwa mwaka 2024/2025, mradi umepangiwa jumla ya TZS 24.90 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 13.7 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 8.7 bilioni sawa na asilimia 63 ya lengo zimepatikana. Kazi zinaendelea kwa hatua za kukamilisha ujenzi kwa upande wa Unguja Mahakama ya Mkoa wa Mjini Magharibi upo katika hatua ya kufanya majaribio ya mifumo ya umeme na Tehama na kumalizia sehemu za milango ya kuingilia na kutokea, utekelezaji umefikia asilimia 94. Ujenzi wa Mahakama ya Mkoa wa Kaskazini katika eneo la Pale Kiongele upo katika hatua ya kufanya majaribio ya mifumo ya Tehama na umeme na kumalizia vibanda vya walinzi na kibanda cha kufua umeme pamoja na kumalizia sehemu ya nje, umefikia asilimia 93. Ujenzi wa Mahakama ya Mkoa wa Kusini katika eneo la Tunguu/Binguni upo katika hatua za kukamilisha kwa kufanya majaribio ya miundombinu ya umeme na Tehama pamoja na umaliziaji wa sehemu za kuingia na kutokea na ujenzi umefikia asilimia 96 na ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Magharibi B katika eneo la Kisakasaka upo katika hatua ya kukamilisha kwa kufanya majaribio ya mifumo ya umeme na Tehama na kumalizia sehemu za kuingilia na umefikia asilimia 93. Kwa upande wa Pemba Ujenzi unaendelea katika Mahakama ya Mkoa wa

Kaskazini eneo la Kinyasini upo hatua ya kukamilisha kwa vibanda vya walinzi, kibanda cha jenereta, mashimo ya vyoo na kuweka milango na umefikia asilimia 77, Mahakama ya Wilaya ya Micheweni katika eneo la Konde ujenzi upo katika hatua ya kuweka madirisha, kuweka poda, miundombinu ya maji na umeme pamoja na kuweka marumaru na ujenzi umefikia asilimia 70, Mahakama ya Wilaya ya Kusini katika eneo la Changaweni unaendelea katika hatua ya kuweka sawa nje, uwekaji wa marumaru, kumalizia ukuta kwa kupaka poda ndani na kumalizia plasta kwa nje pamoja na chumba cha kufulia umeme na ujenzi umefikia asilimia 62

Kukamilika kwa mradi huu kutasaidia kuwa na ufanisi zaidi katika utoaji huduma za kisheria pamoja na upatikanaji wa haki kwa wananchi.

**c. Ujenzi wa Mji wa Serikali**

Mradi una lengo la kujenga Ofisi za Serikali katika eneo la Kisakasaka. Kwa mwaka 2024/25, mradi umepangiwa jumla ya TZS 33.7 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025) jumla ya TZS 18.5 bilioni zimepangwa, hadi kufikia machi 2025, TZS 1.2 bilioni sawa na asilimia 7 zimeingizwa kutoka Serikalini. Jumla ya Kampuni saba tayari zimeshajitokeza kuingia ubia na Serikali kati ya hizo Kampuni tano zimeshafanya mazungumzo ya kina na Serikali na Kampuni mbili zinaendelea na mazungumzo. Aidha, Michoro ya Awali imeandaliwa pamoja na usafishaji wa eneo.

Kukamilika kwa mradi huu kutasaidia kuwa na mazingira mazuri ya kazi kwa watumishi wa Umma kwa matarajio ya kutoa huduma zenye viwango, ufanisi na kuongeza haiba ya mji wa Zanzibar.

## SURA YA KUMI NA MOJA

## MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2024 HADI MACHI 2025

### 11.1 UTANGULIZI

Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2024/25 ni mpango wa nne wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP 2021-2026) pamoja na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050. Mpango huo ulipanga kutekeleza programu na miradi ya maendeleo 97. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali imepanga kutumia jumla ya TZS 3,271.11 bilioni kwa kutekeleza shughuli za maendeleo ambapo TZS 3,263.07 bilioni kwa ajili ya Serikali Kuu na TZS 8.03 bilioni kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwa ni ongezeko la TZS 1749.12 bilioni sawa na asilimia 115 ikilinganishwa na Bajeti ya Maendeleo ya mwaka 2023/24 ya TZS 1,521.99 bilioni. Kati ya fedha hizo (TZS 3,263.07 bilioni), Serikali ilielekeza kutumia TZS 1,862.00 bilioni sawa na asilimia 57.06 ya Bajeti ya Maendeleo kutoka Serikalini na TZS 1401.07 bilioni (TZS 307.76 bilioni ni Ruzuku na TZS 1,093.31 ni Mkopo) sawa na asilimia 42.94 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Aidha, jumla ya TZS 2,086.72 bilioni sawa na asilimia 64 zimepangwa kutumika kwa Programu na Miradi ya Maendeleo ya Kimkakati na TZS 1,175.35 bilioni sawa na asilimia 36 ni kwa miradi mengineyo inayojumuisha miradi inayoendelea na ambayo Serikali ina dhima kwa Washirika wa Maendeleo.

Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 – Machi 2025), Serikali imepanga kutumia jumla ya TZS 1,794.96 bilioni ya fedha iliyopangwa kutumika kwa ajili ya Serikali kuu kwa kutekelezwa Programu na Miradi ya Maendeleo ambayo ni ongezeko la asilimia 44 ukilinganisha na mpango wa mwaka 2023/2024. Kati ya fedha hizo, Serikali ilipanga kutumia TZS 1,024.38 bilioni sawa na asilimia 57.07 ya bajeti ya Maendeleo kutoka fedha za ndani na TZS 770.59 bilioni sawa na asilimia 42.93 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kati ya fedha hizo (TZS 1,794.96 bilioni), TZS 1,130.09 bilioni zilipangwa kugharamia Programu na Miradi ya Kimkakati na yenye dhima na TZS 664.87 bilioni zilipangwa kutumika kwa Programu na Miradi mengineyo. Aidha, Jumla ya TZS 4.42 bilioni zilipangwa kutumika kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Programu na Miradi ya Maendeleo. Sura hii inaeleza Utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 kwa kila Wizara.

## 11.2 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU NA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA JULAI 2024 HADI MACHI 2025 KWA KILA WIZARA

Katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo, jumla ya Programu na Miradi 72 sawa na asilimia 74 kati ya programu na miradi 97 iliyopangwa iliingiziwa fedha kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025. Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, matumizi ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo yamefikia jumla ya TZS 934.54 bilioni sawa na asilimia 52 ya lengo la TZS 1,794.96 bilioni. Kati ya Fedha hizo TZS 657.17 bilioni sawa na asilimia 64 ya lengo la TZS 1,024.375 bilioni ni kutoka Serikalini na TZS 277.37 bilioni sawa na asilimia 36 ya lengo la TZS 770.59 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Sehemu hii inaeleza Utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 kwa kila Wizara kama ifuatavyo;

### 11.2.1 Ofisi ya Rais Ikulu

Ofisi ya Rais Ikulu ina jukumu la kusimamia majukumu ya kikatiba na kisheria ya Baraza la Mapinduzi ili kuhakikisha jamii inapata uelewa juu ya utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo na sera zinazotekelezwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Ofisi ya Rais Ikulu imetekeleza miradi mitatu kama ifuatavyo:-

**a. Mradi wa Uimarishaji wa Majengo ya Ikulu**

Mradi una lengo la kuimarisha majengo ya Ikulu ili kuwa na mazingira mazuri ya makaazi na mandhari za kupendeza kwa viongozi wa Serikali. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 2.50 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 1.38 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, hakuna kiasi cha fedha kilichotumika.

**b.Mradi wa Uimarishaji wa Mfumo wa Ulinzi na Usalama katika Makaazi ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi**

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha mifumo ya ulinzi na usalama katika majengo ya Ikulu na makaazi ya Mheshimiwa Raisi wa Zanzibar kwa

kuweka miundombinu ya mifumo iliyo imara katika makaazi hayo. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 1.60 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 880 milioni. Hadi kufikia Machi 2025, hakuna kiasi cha fedha kilichotolewa.

**c. Mradi wa Kuimarisha Mfumo wa Sema na Rais (SNR)**

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha mawasiliano baina ya wananchi na Mheshimiwa Rais katika mfumo wa Sema na Rais ili kuhakikisha wananchi wanapata fursa ya kuwasilisha changamoto zao kwa kupatiwa ufumbuzi. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 400 milioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 220 milioni. Hadi kufikia Machi 2025, hakuna kiasi cha fedha iliyotumika.

### 11.2.2 Ofisi ya Rais - Kazi, Uchumi na Uwekezaji

Ofisi hii ina jukumu la kuimarisha hali ya kijamii na kiuchumi ya wananchi wa Zanzibar kwa kutoa na kutumia fursa za kiuchumi zilizopo na zitakazokuja, kushajihisha utamaduni na uwezo wa ujasiriamali, kukuza uwekezaji wa ndani na nje, upatikanaji wa kazi za staha zenye kuzingatia Sheria na viwango vya kazi. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisi imepanga kutekeleza programu moja ya maendeleo.

**i.Programu ya Uimarishaji wa Maeneo Huru ya Uwekezaji**

Programu hii imeanzishwa mwaka 2021/2022 na inatarajiwa kukamilika mwaka 2025/2026 Programu ina lengo la kukuza maeneo huru ya uwekezaji kwa kuimarisha miundombinu ya barabara, maji, umeme na mawasiliano katika maeneo yote yaliyoainishwa kwa uwekezaji ili kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Kwa mwaka 2024/2025, Programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 15.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 8.25 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, hakuna kiasi cha fedha zilizotolewa lakini maandalizi ya mradi yameendelea kwa kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa barabara za Zone B Micheweni | Asilimia ya ujenzi iliyofikia. | 100 | 5 | 5 | Zabuni kwa ajili ya upelekaji wa miundombinu ya barabara yenye urefu wa 35 km katika eneo la mradi tayari imeshatangazwa, ripoti ya upembuzi yakinifu tayari imeshawasilishwa kwa uongozi kwa ajili ya kupata muongozo |
| Ulipaji wa fidia kwa maeneo yatakayoathirika na mradi | Idadi ya wananchi waliolipwa fidia. | 700 | 0 | 0 | Maombi ya Mtaalamu kwa ajili ya kufanya tathmini ya ulipaji wa fidia kwa wananchi yanafanyiwa kazi na Tume ya Mipango Zanzibar |
| Upelekaji wa miundombinu ya barabara, maji na umeme katika eneo la uwekezaji la Fumba | Asilimia ya ujenzi wa miundombinu iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa barabara ameshapatikana na mikataba tayari imeshasainiwa baina ya ZIPA kwa upande wa Serikali na kampuni ya CRJE (East Africa) Ltd |

### 11.2.2.1. Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar

Taasisi hii imeanzishwa kwa lengo la kuimarisha mazingira wezeshi ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ili kuongeza ajira kwa vijana na wajasiriamali, kuongeza tija katika uzalishaji na ufanisi wa masoko ya bidhaa za wafanyabiashara nchini. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Taasisi imepanga kutekeleza miradi mitatu (3) ya maendeleo.

**a. Mradi wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi**

Mradi umeanzishwa mwaka 2024/2025 na una lengo la kuinua kipato cha wajasiriamali, wazalishaji na wafanyabiashara kwa kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu ili kutoa ajira za staha, kukuza Pato la Taifa na kupunguza umasikini kwa jamii. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 32.0 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 17.6 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, hakuna kiasi cha fedha iliyotolewa.

**b. Kukuza Usawa wa Kijinsia Tanzania (Pamoja)**

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2024/2025 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2028/2029. Mradi una lengo la kukuza fursa za kiuchumi pamoja na kushughulikia masuala ya udhalilishaji wa wanawake na watoto. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 2.00 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 1.1 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, hakuna fedha iliyotolewa.

**c. Mradi wa Kuwasaidia Wajasiriamali Wadogo Wadogo, Wakati na Wakubwa.**

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2021/2022 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2025/2026 Mradi una lengo la kuwasaidia wajasiriamali (wadogo, wakati na wakubwa) waweze kuinua mitaji, kukuza vipato vyao na kuwasaidia waweze kujitegemea wakiwemo wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalum. Mradi huu unatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Abu dhabi kupitia Mfuko wa Khalifa (Khalifa Fund). Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 9.60 bilioni (TZS 4.50 bilioni kutoka Serikalini na TZS 5.10 bilioni kutoka kwa Washirika

wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 5.28 bilioni (TZS 2.48 bilioni kutoka Serikalini na TZS 2.81 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2025, hakuna fedha iliyopatikana lakini shughuli zifuatazo zilitekelezwa kupitia fedha zilizoingizwa mwaka 2022/2023 za mfuko wa Khalifa.

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wajasiriamali, wazalishaji na wafanya biashara | Idadi ya wanufaika waliopatiwa mikopo | 885 | 51 | 6 | Hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha TZS 1.07 bilioni ilitolewa, sawa na asilimia 15 ya mikopo iliyopangwa (TZS 6.99 bilioni). Mikopo hiyo imewanufaisha wanawake 26 na wanaume 25 |
| Kuratibu na kusimamia utoaji na urejeshwaji wa mikopo | Idadi ya mikopo iliyotolewa | 189 | 11 | 6 | Hadi kufikia Machi, 2025 mikopo hii imetolewa kupitia fedha zilizoingizwa mwaka 2022/2023 za mfuko wa Khalifa |
| | Thamani ya Mikopo iliyorejeshwa | 162 mil | 418 mil | 258 | Marejesho hayo yaliyokusanywa ni kutoka mikopo iliyotolewa kuanzia mwaka 2022/2023 ya programu hiyo. |

### 11.2.3 Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango

Ofisi ina majukumu ya kusimamia shughuli zote zinazohusiana na Mapato na Matumizi ya Serikali pamoja na kusimamia maendeleo ya Taasisi za kifedha zikiwemo benki. Ofisi hii pia ina wajibu wa kuishauri Serikali kuhusu masuala yanayohusu Mapato ya nchi ikiwemo ukusanyaji wa kodi, tozo na mapato yatokanayo na Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), Ofisi imetekeleza programu tatu (3) na mradi mmoja (1) wa maendeleo kama ifuatavyo: -

**i. Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali Zanzibar**

Programu hii imeanzishwa kwa lengo la kujenga na kukarabati Ofisi za Serikali katika maeneo yaliyopendekezwa. Programu itasaidia kutekeleza Mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa kuupanga mji wa Zanzibar na kuwa na mazingira mazuri kwa wafanyakazi ili kutoa huduma bora kwa wananchi na kuongeza haiba ya mji wa Zanzibar. Kwa mwaka 2024/2025, Programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 113.98 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 62.69 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha TZS 11.47 bilioni sawa na asilimia 30 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ukamilishaji na ujenzi wa Ofisi za Serikali ikiwemo Ofisi ya Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar, Tume ya Uchaguzi, Baraza la Wawakilishi, Ofisi ya Mufti, Skuli ya Sheria, Ofisi ya Tume ya Utangazaji Zanzibar, Ofisi na Studio za Redio na TV - Tunguu, Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, Shirika la Magazeti, Ofisi ya ZAECA, Mkurugenzi wa Mashtaka, Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Ukarabati wa Jengo la Ushindani Halali wa Biashara, Ofisi ya Maafa na Ghala, Ofisi | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa katika Ofisi ya Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar | 100 | 0 | 0 | Ujenzi unatarajiwa kuanza baada ya kukamilika kwa Nyaraka na Michoro ya jengo. |
| | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa katika Ofisi ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar | 100 | 95 | 95 | Jengo limeshapigwa plasta nje na ndani, miundombinu ya umeme, maji na TEHAMA tayari imeshawekwa pamoja na utiaji wa maru maru (tiles) |
| | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa katika Ofisi ya Baraza la Wawakilishi | 100 | 0 | 0 | Hatua za ujenzi kwa sasa zipo katika kutafuta eneo jengine la ujenzi na Baraza litakalojumuisha na huduma nyengine muhimu za Baraza. Barua imeshaandikwa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Mkaazi ya kupatiwa eneo. |
| | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa katika Ofisi ya Mufti | 100 | 100 | 100 | Ujenzi umeshakamilka |
| | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa katika Ofisi ya Skuli ya Sheria | 100 | 5 | 5 | Kiwanja cha ujenzi kimeshapatikana, uandaaji wa Michoro umeshafanyika na Mkandarasi ameshapatikana |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ya Nyaraka, Jengo la Ushirika, Jengo la Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji na Shirika la Nyumba | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa katika Ofisi ya Tume ya Utangazaji Zanzibar | 100 | 10 | 10 | Hati ya kiwanja ya eneo la ujenzi imeshapatikana, usafishaji wa eneo na upimaji wa udongo umefanyika na michoro imeshaandaliwa |
| | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa katika Ofisi na Studio za Redio na TV | 100 | 2 | 2 | Mshauri elekezi ameshapatikana na uandaaji wa Mikataba unaendelea |
| | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa katika Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali | 100 | 88 | 88 | Ujenzi upo katika hatua za mwisho kukamilika katika hatua ya upakaji wa rangi nje na ndani |
| | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa katika Ofisi ya Shirika la Magazeti | 100 | 65 | 65 | Ujenzi wa ofisi upo hatua ya kusimamisha nguzo na kumwaga zege katika ghorofa ya nne pamoja na kupiga plasta. Aidha, ujenzi wa msikiti na nyumba za wafanyakazi zipo katika hatua ya kupiga plasta nje na ndani na kuweka miundo mbinu ya umeme na maji pamoja na kuezeka |
| | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa katika Ofisi ya ZAECA | 100 | 2 | 2 | Ujenzi upo katika hatua ya uchimbaji wa misingi |
| | Asilimia ya ukarabati iliyofikiwa katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka | 100 | 99 | 99 | Ujenzi upo hatua ya ukamilishaji |
| | Asilimia ya ujenzi | 100 | 1 | 1 | Ujenzi umefikia katika hatua ya |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | iliyofikiwa katika Ofisi ya Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi | | | | kumtafuta mshauri elekezi |
| | Asilimia ya ukarabati iliyofikiwa katika Jengo la Ushindani Halali wa Biashara | 100 | 90 | 90 | Ujenzi katika katika hatua ya upakaji wa rangi, ufungaji wa taa na uwekaji wa viyoyozi (AC) |
| | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa katika Ofisi ya Maafa na Ghala | 100 | 10 | 10 | Ujenzi upo katika hatua ya msingi na uchimbaji wa kisima |
| | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa katika Ofisi ya Nyaraka | 100 | 40 | 40 | Ujenzi upo katika hatua ya umwagaji zege katika ghorofa ya tatu sambamba na upigaji wa plasta katika ya kwanza na ya pili |
| | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa katika Ofisi ya Jengo la Ushirika | 100 | 2 | 2 | Hatua ya ujenzi iliyofikiwa ni kumtafuta Mkandarasi kwa kuanza ujenzi |
| | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa katika Ofisi ya Jengo la Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji | 100 | 2 | 2 | Ujenzi upo katika hatua ya kuweka sawa ardhi (*landscaping*) |
| | Asilimia ya ujenzi wa nyumba za Shirika la Nyumba iliofikiwa | 100 | 100 | 100 | Ujenzi umeshakamililika |
| Ujenzi wa Mji wa Serikali katika eneo la Kisakasaka | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 2 | 2 | Jumla ya Kampuni saba (7) zimejitokeza kuingia ubia na Serikali kwa ajili ya ujenzi wa mji wa Serikali ambapo kampuni |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | tano (6) zimeshafanya mazungumzo na kampuni mbili (2) zinaendelea na mazungumzo. |

### ii. Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG-Z)

Programu hii imeanzishwa kwa lengo la kuimarisha miundombinu na huduma za msingi pamoja na kuimarisha haiba ya Miji ya Zanzibar. Kwa mwaka 2024/2025, Programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 32.00 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya TZS 17.6 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha TZS 18.98 sawa na asilimia 108 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kujenga na kukarabati mitaro ya maji ya mvua yenye urefu wa kilomita 4.76 katika maeneo ya Sebleni, Meya, Magomeni na mtaro wa mfumo C (Shehia ya Amani-Shehia ya Shauri Moyo) | Idadi ya kilomita za mitaro ya maji ya mvua iliyojengwa na kukarabatiwa | 4.76 km | 2.30 km | 48 | Ujenzi wa mitaro kuanzia eneo la Sebleni hadi Bwawa la Vijibwa umekamilika, ujenzi wa mitaro katika maeneo ya Sogea - danger- Magomeni Jitini, Mtaro wa pembezoni mwa barabara kwa Mchina Mwanzo hadi Magereza (Jan'gombe green corridor), Magomeni kwa Najim hadi Kwaboko Magazeti ujenzi unaendelea |
| Kufanya ukarabati wa vitatu vya mpira katika maeneo ya Magomeni Mzalendo, Machicha na Mbarawa | Idadi ya viwanja vya vya | 3 | 0 | 0 | Mkandarasi amewasilisha umeidhinishwa kwa ajili ya ukarabati wa viwanja vya michezo na anategemea kuanza ujenzi mwezi wa Mei 2025 |
| Ujenzi wa barabara za ndani zenye urefu wa kilomita 9.14 na uwekaji | Idadi ya urefu wa kilomita ya barabara zilizojengwa | 9.14 km | 2.026 km | 22 | Ujenzi umefika katika hatua ya uwekaji wa lami kwa barabara ya |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| wa taa zinazotumia nguvu za jua katika maeneo ya Sebleni kwa Wazee, Meya, Magomeni na Nyerere | | | | | Jang’ombe km 2.026, na kwa barabara za kwaboko - magazeti, Sogea-Danger na Magomeni – Kwa Najim – Mosi. Wandarasi wapo katika hatua ya uwekaji wa Kalvat na uchimbaji wa mitaro ya maji ya mvua katikakati ya barabara, pamoja na ukamilishaji wa barabara baada ya uwekaji wa mitaro hiyo |
| Kujenga soko moja la wajasiriamali katika eneo la Meya | Asilimia ya ujenzi wa soko iliyofikiwa | 100 | 0 | 0 | Serikali ipo katika utafutaji wa eneo muwafaka kwa ajili ya kuanza ujenzi |
| Ununuzi wa vifaa vya usafi (magari ya taka, makontena ya kuwekea taka na gari la kusafishia barabara) kwa Mabaraza ya Miji na Manispaa za | Asilimia ya manunuzi iliyofikiwa. | 100 | 90 | 90 | Vifaa vimeshanunuliwa vikiwemo, magari mawili ya kubebea taka (Hooklift track), makontena kumi na vikapu ishirini |
| Unguja na Pemba | | | | | |
| Kufanya Upembuzi Yakinifu wa mradi wa Mji Salama kwa | Asilimia ya Upembuzi Yakinifu uliofanyika | 100 | 67 | 67 | Upembuzi yakinifu umeshakamilika kwa Lot 1; hatua ya iliyofikiwa kwa |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| watembea kwa miguu katika maeneo ya Mji Mkongwe | | | | | Lot 2, Mshauri Elekezi anafanyia kazi maoni ya wadau baada ya kuwasilisha rasimu ya pili ya Upembuzi Yakinifu na kwa Lot 3, Mshauri Elekezi ameshawasilisha Michoro ya awali na anafanyia kazi maoni ya wadau. |
| Kuzijengea uwezo Taasisi za Serikali zinazosimamia maendeleo ya Miji, ikiwemo kuwapatia mafunzo ya muda mfupi watendaji wa Taasisi hizo pamoja na ununuzi wa vitendea kazi | Idadi ya maafisa waliojengewa uwezo | 238 | 121 | 51 | Jumla ya maafisa 121 wamejengewa uwezo juu ya usimamizi wa miradi, ununuzi na ugavi, mafunzo ya ukutubi pamoja mbinu bora za usimamizi wa Mikataba |
| Kuandaa Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi kwa upande wa Pemba | Asilimia ya matayarisho iliyofikiwa | 100 | 60 | 60 | Hatua zilizofikiwa timu ya mradi imeshafanya makubaliano na Mshauri Elekezi aliyeshinda zabuni pamoja na kupata idhini ya Mwanasheria Mkuu |
| Kufanya Upembuzi | Asilimia ya usarifu wa | 100 | 100 | 100 | Ripoti ya mwisho ya |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Yakinifu, usanifu wa michoro na kuandaa nyaraka za zabuni kwa mradi wa kuimarisha Miji ya Pemba na mradi wa kuendeleza maeneo ya utalii ya Nungwi, Chwaka na Makunduchi. | michoro na uandaaji wa nyaraka za zabuni iliyofikiwa kwa Pemba | | | | michoro imeshakamilika |
| | Asilimia ya Upembuzi Yakinifu na uandaji wa Zabuni iliyofikiwa | 100 | 50 | 50 | Ripoti ya Upembuzi Yakinifu na usanifu wa Michoro imeshaandaliwa hatua iliyofikiwa ni kuandaa zabuni |
| Kufanya Upembuzi Yakinifu, usanifu wa michoro na kuandaa nyaraka za zabuni kwa mradi wa usimamizi wa ujenzi wa vituo vya kusafirishia taka | Asilimia ya Upembuzi Yakinifu na uandaji wa Zabuni iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Usanifu wa michoro na nyaraka za zabuni za ujenzi wa vituo viwili vya kusafirishia taka kwa muda vinavyotajiwa kujengwa Pwani Mchangani na Fuoni Chunga umekamilika na hatua inayofuata ni kuandaa zabuni |
| Kufanya Upembuzi Yakinifu, usanifu wa michoro na kuandaa nyaraka za zabuni kwa mradi wa mradi wa usimamizi wa ujenzi wa vituo vya kukusanyia taka | Asilimia ya Upembuzi Yakinifu na uandaji wa Zabuni iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Upembuzi Yakinifu umekamilika na hatua inayofuata ni Usanifu wa michoro na nyaraka za zabuni za ujenzi wa vizimba vya kukusanyia taka vitakavyojengwa Unguja na Pemba. |

### iii. Programu ya Mageuzi katika Usimamizi wa Fedha (PFMRP – VI)

Programu hii imeanzishwa kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa fedha za umma katika utoaji wa huduma bora kwa wananchi. Kwa mwaka 2024/2025, Programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 4.45 bilioni (TZS 400.00 milioni kutoka Serikalini na TZS 4.46 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 2.67 bilioni (TZS 220 milioni kutoka Serikalini na TZS 2.45 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha TZS 1.85 bilioni (TZS 352 milioni sawa na asilimia 160 kutoka Serikalini na TZS 1.5 bilioni sawa na asilimia 61 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) kwa fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya uratibu wa Programu Zanzibar | Asilimia ya uratibu uliofanyika | 100 | 95 | 95 | Ofisi imefanya uratibu wa mradi kwa kufanya mafunzo kwa Kamati za nidhamu na maadili kwa wanufaika wa mradi na kushiriki katika vikao vya kupitia Mpango wa Manunuzi kwa upande wa Zanzibar pamoja na kufanya mafunzo ya “E-Waste Managenment and Cyber Security” |
| Kuimarisha Mifumo saba (7) iliyopangwa kuandaliwa. | Idadi ya mifumo iliyoandaliwa | 7 | 0 | 0 | Vikao vya kujadili mahitaji ya mifumo vimeshafanyika. Hatua inayoendelea ni kuwasilisha hadidu rejea zao katika Kamati za Uongozi |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | pamoja na Wakala wa Serikali mtandao kwa kupata idhini ili waweze kuendelea na hatua nyengine. |
| Kuimarisha na kuanzisha mifumo inayohusiana na usimamizi wa kodi, ukaguzi pamoja na usimamizi wa mipango na bajeti | Idadi ya mifumo iliyoanzishwa na kuimarishwa | 7 | 1 | 14 | Hadi sasa mfumo umeshaandaliwa uko katika majaribio na mfumo mmoja uko katika hatua ya matayarisho |
| Kufanya mapitio na kutoa miongozo inayohisuana na Sheria mbali mbali za mapato, matumizi, udhibiti na ukaguzi | Idadi ya Sheria na miongozo iliyopitiwa | 15 | 9 | 60 | Miongozo na mikakati mbali mbali imeandaliwa ikiwemo<br><br>Mpango Mkakati wa Ofisi ya Msajili wa Hazina (*Treasury Registrer* (TR) |
| Kufanya utafiti kuhusu athari za uchumi wa kidijitali kwa uchumi wa Zanzibar | Asilimia ya utafiti iliyofanyika | 100 | 5 | 5 | Mshauri elekezi ameshapatikana na kazi inaendelea |
| Kuandaa muongozo wa utayarishaji wa Upembuzi Yakinifu kwa miradi ya maendeleo | Asilimia ya muongozo ulioandaliwa | 100 | 5 | 5 | Mshauri elekezi ameshapatikana na kazi inaendelea |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuwajengea uwezo watumishi mbali mbali kuhusiana na mipango, bajeti, udhibiti, ukaguzi na usimamizi wa fedha za umma | Idadi ya watumishi waliojengewa uwezo | 368 | 219 | 60 | Maafisa wamejengewa uwezo katika fani tofauti zikiwemo mipango, bajeti, uthibiti, ukaguzi na usimamizi wa fedha za umma |
| Kufanya ziara za kujifunza ili kuongeza uwelewa juu ya usimamizi wa fedha za umma na udhibiti | Idadi ya ziara zilizofanyika | 3 | 3 | 100 | Maafisa kutoka Taasisi tofauti walishiriki ziara za kujifunza ili kuongeza uelewa katika maswali ya usimamizi wa fedha za umma na udhibiti. |

**a.Mradi wa Uimarishaji Rasilimali za ndani na Usimamizi wa Maliasili (ISP-DRMNRG)**

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha rasilimali za ndani na usimamizi wa maliasili kwa kuhakikisha usimamizi wa rasilimali na maliasili zote zinasimamiwa kupitia Sera na Sheria stahiki. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 1.06 bilioni (TZS 78.50 milioni kutoka Serikalini na TZS 986.9 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 585.9 milioni (TZS 44 milioni kutoka Serikalini na TZS 542 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha TZS 78.5 milioni sawa na asilimia 182 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kutoa huduma za uratibu na usimamizi wa miradi. | Asilimia ya huduma za uratibu zilizotolewa | 100 | 75 | 75 | Kazi za uratibu zinaendelea. |
| Kuandaa Sheria na miongozo ya madini | Asilimia ya muongozo iliyofikiwa | 100 | 80 | 80 | Mkataba wa kazi ya kuandaa Sheria tayari umeshasainiwa na kwa sasa ameshawasilisha ripoti ya awali |
| Kufanya warsha juu ya Sheria na miongozo ya madini | Idadi ya maafisa walioshiriki | 60 | 0 | 0 | Utekelezaji wa shughuli hii unategemea ukamilishwaji wa Sheria na Muongozo wa madini |
| Kuandaa Sheria ya Kodi na faida ya Mafuta na Gesi Asilia | Asilimia ya kazi ya uandaaji iliyofikiwa | 100 | 85 | 85 | Mkataba wa kazi tayari umeshasainiwa na kwa sasa ameshawasilisha ripoti ya awali (Inception Report) |
| Kufanya warsha juu ya Sheria ya kodi na Faida ya Mafuta na Gesi Asilia | Idadi ya maafisa walioshiriki | 60 | 0 | 0 | Utekelezaji wa shughuli hii unategemea ukamilishwaji wa sheria ya kodi na Faida ya Mafuta na Gesi Asilia |

### 11.2.3.1 Tume ya Mipango Zanzibar

Tume ya Mipango ni Taasisi inayoratibu Mipango ya Maendeleo ya kiuchumi na kijamii ikijumuisha kuandaa mipango ya muda mrefu, muda wa kati na muda mfupi, ufuatiliaji na tathmini, kuratibu uandaaji wa tafiti pamoja na masuala ya idadi ya watu na usimamizi wa Uchumi wa Zanzibar. Aidha, Tume inaratibu na kupanga Vipaumbele vya nchi na kutoa Miongozo ya kuimarisha uchumi na ustawi wa wananchi. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Tume ya Mipango imepanga kutekeleza programu moja na mradi mmoja wa maendeleo.

**i.Uratibu wa Programu ya Urasimishaji Ardhi na Biashara Zanzibar**

Programu hii imeanzishwa kwa lengo la kukuza mitaji kupitia urasimishaji wa ardhi na biashara ili ziweze kutumika kama dhamana. Kwa mwaka 2024/2025, Programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 3.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 1.65 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha TZS 1.67 bilioni sawa na asilimia 101 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya Utafiti wa Ajira na Mapato kwa mwaka 2023/24 | Asilimia ya utafiti iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Matokeo ya utafiti yameshatolewa |
| Kufanya Sensa ya Uzalishaji Mali Viwandani ya Mwaka 2023 | Asilimia ya Sensa iliyofikiwa | 100 | 25 | 25 | Kazi ya ukusanyaji wa taarifa imeanza |
| Kufanya Utafiti wa Kilimo wa Mwaka 2024 | Asilimia ya utafiti wa kilimo iliyofikiwa | 100 | 95 | 95 | Ripoti tayari imeshakamilika |
| Kuanza Utafiti wa Watu Wenye Uwezo wa Kufanya Kazi (ILFS) wa Mwaka 2023/2024 | Asilimia ya utafiti iliyofikiwa | 100 | 70 | 70 | Uandishi wa ripoti unaendelea baada ya kukamilika kwa zoezi la ukusanyaji wa taarifa na data |
| Kuanza Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya (HBS) 2024/2025 | Asilimia ya utafiti iliyofikiwa | 100 | 35 | 35 | Ukusanyaji wa taarifa unaendelea |
| Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Pemba | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Mkandarasi ameshapatikana kwa kuanza kazi ya ujenzi |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa Masjala ya Ardhi Chake Chake Pemba | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Tathmini ya kumpata Mkandarasi inaendelea |

**a. Mradi wa Kuimarisha Ufanisi katika Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa**

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2024/25 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2026/27. Mradi una lengo la kuimarisha uratibu, usimamizi, ufuatiliaji na tathmini wa utekelezaji wa Mipango, Sera na Mikakati ya Kisekta, Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ikiwemo Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021-2026, Ajenda ya Afrika 2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) 2030. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 2.30 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 1.27 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha TZS 440 milioni sawa na asilimia 35 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuandaa mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021 – 2026 na kuifanyia uchambuzi ripoti ya mapitio | Asilimia ya mapitio ya utekelezaji wa mpango iliyofikiwa | 100 | 95 | 95 | Rasimu ya mapitio ya utekelezaji wa ZADEPimekamilika. Hatua iliyopo ni kuwasilishwa kwa sekta kabla ya kuidhinishwa na Tume ya Mipango |
| Kufanya uhakiki wa miradi na programu za maendeleo | Idadi ya miradi na programu za maendeleo zilizohakikiwa | 97 | 97 | 100 | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya tathmini ya Programu na Miradi ya Maendeleo | Asilimia ya programu na miradi iliyofanyiwa tathmini | 50 | 5 | 10 | Kikosi kazi cha kufanya tathmini kwa miradi iliyokamilika imeanza |
| Kuanzisha mfumo wa kijiditali wa uandaaji na usimamizi wa Mipango na Miradi ya Maendeleo (ZiPS) | Asilimia ya uanzishwaji wa mfumo iliyofikiwa | 100 | 80 | 80 | Mfumo umeanzishwa kwa mashirikiano na maoni kutoka katika sekta zote za Serikali. Kwa sasa upo katika hatua za majaribio. |
| Kuanza maandalizi ya uwandaaji wa Mpango mpya wa Muda wa Kati baada ya kukamilika utekelezaji wa ZADEP | Asilimia ya maandalizi iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Hatua za awali zimekamilika za kuandika Andiko la awali na Hadidu rejea kwa kumpata Mshauri Elekezi. |

#### 2.11.3.2 Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali

Ofisi ina jukumu la kutoa, kukusanya, kuchambua, kuchapisha, kuhifadhi na kusambaza taarifa na takwimu zilizo rasmi, kutoa takwimu na taarifa zenye ubora na kuhamasisha matumizi ya takwimu katika mipango ya maendeleo, kufanya maamuzi katika masuala ya utawala na uendeshaji pamoja na ufuatiliaji na tathmini kwa shughuli za kiuchumi na kijamii. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisi imepanga kutekeleza Programu moja na mradi mmoja wa maendeleo.

**i. Programu ya Uimarishaji Takwimu Tanzania Awamu ya Pili (TSMP II)**

Programu hii imeanzishwa kwa lengo la kuimarisha shughuli za kitakwimu Zanzibar kwa kuwezesha ukusanyaji, upatikanaji na utoaji wa takwimu za kawaida (routine data) kwa wakati, kuweka mazingira mazuri ya kuratibu upatikanaji wa takwimu za Kiuchumi na Kijamii kupitia takwimu za kawaida, sensa na tafiti. Aidha, inalenga kuwezesha uzalishaji na usimamizi wa takwimu na uimarishaji wa mifumo ya kitakwimu na miundombinu, maendeleo ya rasilimali watu kwa Taasisi za Serikali kupitia Mfumo wa Takwimu Zanzibar ili kusaidia uimarishaji na upatikanaji wa takwimu rasmi. Kwa mwaka 2024/2025, Programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 8.32 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), programu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 4.58 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha TZS 3.45 bilioni sawa na asilimia 75 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya Utafiti wa Ajira na Mapato kwa mwaka 2023/24 | Asilimia ya utafiti iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Matokeo ya utafiti yameshatolewa |
| Kufanya Sensa ya Uzalishaji Mali Viwandani ya Mwaka 2023 | Asilimia ya Sensa iliyofikiwa | 100 | 25 | 25 | Kazi ya ukusanyaji wa taarifa imeanza |
| Kufanya Utafiti wa Kilimo wa Mwaka 2024 | Asilimia ya utafiti wa kilimo iliyofikiwa | 100 | 95 | 95 | Ripoti tayari imeshakamilika |
| Kuanza Utafiti wa Watu Wenye Uwezo wa Kufanya Kazi (ILFS) wa Mwaka 2023/2024 | Asilimia ya utafiti iliyofikiwa | 100 | 70 | 70 | Uandishi wa ripoti unaendelea baada ya kukamilika kwa zoezi la ukusanyaji wa taarifa na data |
| Kuanza Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya (HBS) 2024/2025 | Asilimia ya utafiti iliyofikiwa | 100 | 35 | 35 | Ukusanyaji wa taarifa unaendelea |
| Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Pemba | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Mkandarasi ameshapatikana kwa kuanza kazi ya ujenzi |

**a.Mradi wa Uimarishaji Takwimu za Jinsia**

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha uzalishaji na matumizi ya takwimu za jinsia ambazo husaidia katika kubuni sera na mipango ya kijamii, kiuchumi, na kisiasa ambayo inazingatia mahitaji na haki za kila jinsia hasa katika masuala ya elimu, afya, ajira na haki za kijamii. Vile vile, kutoa elimu ya dhana ya za udhalilishaji wa kijinsia na aina zake, kutambua makundi au maeneo ambayo yako katika hatari kubwa ya udhalilishaji wa kijinsia. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 343.24 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 189 milioni. Hadi kufikia Machi 2025, hakuna fedha iliyotumika.

### 2.11.4 Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora

Ofisi ina lengo la kuwa na Utumishi wa Umma wenye ujuzi utakaotoa huduma nzuri kwa jamii zenye kuzingatia misingi ya haki, Sheria na demokrasia, ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma zinazofuata misingi ya haki za kibinadamu. Aidha, Ofisi inasimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na miongozo ya masuala ya misingi yanayotokana na utawala bora kwa jamii ya Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisi imepanga kutekeleza Program mbili na mradi mmoja wa maendeleo.

**i. Programu ya Mageuzi ya Utumishi wa Umma Awamu ya II**

Programu hii imeanzishwa kwa lengo la kuimarisha utendaji wa watumishi wa umma Zanzibar katika utoaji wa huduma stahiki kwa jamii. Kwa mwaka 2024/2025, Programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 1.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), programu ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 550 milioni. Hadi kufikia Machi 2025, Jumla ya TZS 215 milioni sawa na asilimia 39 (TZS 106 milioni kutoka Serikalini na TZS 109 milioni kutoka Washirika wa Maendeleo) ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuimarisha Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili wa Taarifa za Mali na Madeni ya Viongozi wa Umma | Asilimia ya uimarishaji wa mfumo iliyofikiwa | 100 | 20 | 20 | Mfumo umekamilika katika hatua ya pili ripoti za utengenezaji wa mfumo (System Specification Na Software Design Documents Reports) zimewasilishwa |

### ii. Programu ya Mageuzi ya Sekta ya Sheria

Programu hii imeanzishwa mwaka 2022/23 na inatarajiwa kukamilika mwaka 2027/2028 Programu ina lengo la kuimarisha upatikanaji wa haki pamoja na kuimarisha uwezeshaji wa wananchi katika masuala ya sheria. Kwa mwaka 2024/2025, Programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 1.66 bilioni (TZS 500.00 milioni kutoka Serikalini na 1.16 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), programu ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 917 milioni (TZS 275 milioni kutoka Serikalini na TZS 642 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2025, shughuli zifuatazo zimetekelezwa: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuimarisha mifumo na uwezo wa Taasisi za Sheria na rasilimali watu | Idadi ya Miongozo iliyotayarishwa | 1 | 1 | 100 | |
| | Idadi ya Mitaala iliyotayarishwa | 1 | 1 | 100 | Mtaala wa Mafunzo unalengo la kuwasaidia wanafunzi waliokuwepo vizuizini kuendelea na |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | mafunzo watakapoachiwa huru |
| | Idadi ya sheria zilizofanyiwa mapitio | 2 | 2 | 100 | Sheria mbili zimefanyiwa mapitio, Sheria ya Madai na Mwenendo wa Makosa ya Jinai kwa ajili ya kupendekeza vipengele vya Sheria hizo kubadilika na kutunga upya Sheria inayokwenda na wakati |
| | Idadi ya tafiti zilizofanyika | 1 | 1 | 100 | Utafiti ulihusu Athari za makosa ya udhalilishaji umefanyika |
| Kuziwezesha Asasi za Kiraia kutoa msaada wa kisheria na kuhamasisha jamii juu ya haki za kisheria na za kibinadamu kwa makundi hatarishi | Idadi ya wanajamii waliopatiwa msaada wa kisheria | 4,000 | 3,439 | 86 | Shughuli hii ni endelevu |
| | Idadi ya wanajamii waliopatiwa mafunzo ya kisheria | 14 | 14 | 100 | Wanajamii 14 wamepatiwa mafunzo ya sheria, utengezaji wa sabuni pamoja na kuanzisha kampuni ya kuendesha biashara ndogo ndogo |
| | Idadi ya asasi za kiraia zilizowezeshwa kutoa msaada wa kisheria kwa makundi hatarishi | 6 | 6 | 100 | Asasi za kiraia zilizowezeshwa kutoa msaada wa kisheria kwa makundi hatarishi ni ZAFELA, WEPO, NAPAC, SOPAU, MDIPAO na PACSO |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuanzisha utaratibu wa kuelimisha jamii juu ya huduma ya haki katika kesi za unyayasaji wa kijinsia. | Idadi ya wanajamii waliopatiwa mafunzo ya kisheria | 260 | 260 | 100 | |
| | Idadi ya wanafunzi wa Vyuo waliopatiwa msaada wa kisheria. | 200 | 200 | 100 | |
| | Idadi ya wasaidizi wa Sheria walioajiriwa kutoa msaada wa kisheria kwa makundi hatarishi. | 32 | 32 | 100 | Jumla ya Wasaidizi wa Sheria 32 (20 Wanawake na 12 Wanaume) wameajiriwa kutoa msaada wa kisheria kwa makundi hatarishi. |

**a. Mradi wa Utoaji wa Huduma za Haki kwa Wanawake na watoto katika Kukabiliana na Kesi za Ukatili wa Kijinsia Zanzibar**

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2023/2024 na kumalizika 2024/2025. Mradi una lengo la kupunguza vitendo vya udhalilishaji kwa vijana, wanawake na watoto Zanzibar. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 350 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (UN-WOMEN). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 193 milioni. Hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha TZS 137 milioni sawa na asilimia 71 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuimarisha uratibu na taratibu za usimamizi wa kesi katika ngazi ya kitaifa kupitia mikutano kati ya polisi, mahakama na Mkurugenzi wa Mashtaka | Idadi ya Mikutano iliofanyika | 4 | 4 | 100 | Vikao vinne vya kila robo mwaka vya utekelezaji vimekamilika ambapo hujumuisha wahusika wakiwemo Jeshi la Polisi, Mahkama na Ofisi ya |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| (Case Management Coordination Meeting) | | | | | Mkurugenzi wa Mashataka |
| Kuandaa Muongozo wa Hukumu wa Kimahakama | Asilimia ya maandalizi ya muongozo iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Mwongozo umeandaliwa |
| Kusaidia programu ya kuifikia jamii (support community outreach program) ili kuongeza ufahamu wa umma juu ya kuripoti kesi pamoja na kushirikiana na Mkurugenzi wa Mashtaka juu ya kutoa ushahidi kwa kesi za Udhalilishaji na Ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto | Idadi ya watu waliofikiwa na kupatiwa elimu | 100 | 187 | 187 | Shughuli imevuka shabaha iliopangwa kutokana na muamko wa jamii katika kuhudhuria mikutano ya hadhara, ambapo Elimu kuhusu kuripoti na kutoa ushahidi juu ya kesi za udhalilishaji kwa wanawake na watoto kwa Unguja na Pemba |
| Kufanya Mkutano wa Wadau (Unguja na Pemba) kwa ajili ya kukusanya maoni juu ya Rasimu ya Jukwaa la Taifa la Haki za Wanawake na Wasichana | Asilimia ya uandaaji wa Jukwaa iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Muongozo wa uandaaji wa jukwaa la Taifa la Haki za Wanawake na Wasichana umefanyika |
| Kutoa elimu kwa jamii juu ya uwezeshaji wa Wanawake kumiliki Ardhi, stadi za maisha pamoja na haki za Wanawake na wasichana kupitia vipindi vya Habari Redio na Televisheni | Idadi ya vipindi vya redio na televisheni vilivyorushwa hewani. | 3 | 3 | 100 | Vipindi 3 vyenye maudhui ya uwezeshaji wa Wanawake katika masuala ya kumiliki ardhi, stadi za maisha pamoja na haki za Wanawake na wasichana vimerushwa hewani kupitia ZBC |

#### 11.2.4.1 Mahakama Kuu

Ofisi ina jukumu la kupokea, kusikiliza na kuyatolea maamuzi madai ya wananchi yanayowasilishwa mahakamani kwa lengo la upatikanaji wa haki kwa jamii ndani ya muda uliowekwa. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisi imepanga kutekeleza miradi minne ya maendeleo.

**a. Mradi wa Ujenzi wa Mahakama za Wilaya na Mikoa**

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2023/2024 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2024/2025 Mradi una lengo la kujenga majengo mapya ya Mahakama ambayo yatakuwa na mazingira bora na yatakayoongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za kisheria na upatikanaji wa haki. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 24.9 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 13.6 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha TZS 8.6 bilioni sawa na asilimia 63 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kujenga Mahakama ya Mkoa wa Mjini Magharibi katika eneo la Mazizini- Unguja | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 94 | 94 | Ujenzi umekamilika uko katika hatua za kufanya majaribio ya mifumo ya umeme na TEHAMA na umalizaji wa sehemu za milango wa kuingia na kutoka |
| Kujenga Mahakama ya Wilaya ya Magharibi "B" katika eneo la Kisakasaka- Unguja | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 93 | 93 | Ujenzi umekamilika hatua zinazoendelea ni kufanya majaribio ya mifumo ya umeme na TEHAMA |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kujenga Mahakama ya Mkoa wa Kaskazini katika eneo la Pale | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 93 | 93 | Ujenzi umekamilika hatua zinazoendelea ni pamoja na kufanya majaribio ya mifumo ya umeme na TEHAMA, umalizaji wa vibanda vya walinzi, kibanda cha jenereta na matengenezo ya eneo la nje |
| Kujenga Mahakama ya Mkoa wa Kusini Unguja katika eneo la Tunguu/Binguni | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 96 | 96 | Ujenzi umekamilika hatua zinazoendelea ni kufanya majaribio ya mifumo ya umeme na TEHAMA na umalizaji wa sehemu za milango wa kuingia na kutoka |
| Kujenga Mahakama ya Mkoa wa Kaskazini Pemba katika eneo la Kinyasini | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 77 | 77 | Ujenzi unaendelea kwa hatua za umalizaji wa vibanda vitatu vya Walinzi, uchimbaji wa mashimo ya choo, uwekaji wa sakafu ya kuzuia maji katika ghorofa ya juu na ujenzi wa sakafu kwa kuweka tiles |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kujenga Mahakama ya Wilaya ya Micheweni Pemba katika eneo la Konde | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 70 | 70 | Hatua zinazoendelea ni uwekaji wa madirisha, kuskimu kwa ukuta wa nje, uwekaji miundombinu ya maji na umeme pamoja ujenzi wa tiles. |
| Kujenga Mahakama ya Mkoa wa Kusini Pemba katika eneo la Changaweni | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 62 | 62 | Ujenzi unaendelea na hatua ya kuweka *landscaping*, uwekaji wa maru maru, pamoja na chumba cha jenereta |

**b. Mradi wa Uimarishaji Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Taarifa za Kesi**

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2023/2024 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2024/2025. Mradi una lengo la kuimarisha mifumo ya Mahakama katika uendeshaji wa kesi kwa njia ya kielektroniki ambao utaimarisha utendaji na ufanisi wa kazi katika utoaji wa huduma kwa wananchi. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 500.00 milioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 275 milioni. Hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha TZS 349 sawa na asilimia 127 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

### c. Mradi wa Kuimarisha Mahakama

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha Mahakama katika kuwezesha upatikanaji wa haki, kuongeza ufanisi wa utendaji kazi kwa watumishi wa Mahakama pamoja na kuimarisha mashirikiano na wadau ili kufikisha huduma kwa wananchi. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 26.1 bilioni (TZS 600.00 milioni kutoka Serikalini na TZS 25.5 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 14.4 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha TZS 7.1 bilioni sawa na asilimia 49 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ununuzi wa samani kwa majengo ya Mahakama | Asilimia ya ununuzi wa thamani iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | |
| Ununuzi wa kompyuta na vifaa vyake | Asilimia ya ununuzi iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Hatua za kumtafuta mzabuni zinaendelea |
| Ununuzi wa huduma za kimtandao | Asilimia ya ununuzi iliyofikiwa | 100 | 20 | 20 | Ununuzi wa leseni ya mfumo umeshakamilika kazi inayoendelea ni kuanza uandaaji wa mifumo |
| Ujenzi wa majengo ya Mahakama za Wilaya (Kijichi, Makunduchi, Chwaka, Kinduni na Kigunda) | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Tathmini ya udongo imeshafanyika ikiwa ni hatua ya awali. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Ukarabati wa majengo ya Mahakama ya Mahonda na Wete | Asilimia ya ukarabati iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Hatua iliyofikiwa ni kufanyika kwa tathmini ya Kijamii na Kimazingira imeshafanyika na kazi ya kuipitia tena michoro kwa ajili ya kuanza ukarabati inaendelea |
| Kulipa ada ya mshauri elekezi (Consultancy Fee) | Asilimia ya malipo iliyofikiwa | 100 | 70 | 70 | |
| Kufanya mafunzo ya utekelezaji na usimamiaji wa mradi kwa watumishi wa kitengo cha *Judiciary Reform Delivery Unit* | Idadi ya watumishi waliopatiwa mafunzo | 30 | 93 | 310 | Watumishi wamepatiwa mafunzo kwa mujibu wa kada na sehemu tofauti ikiwemo Kenya, Tanzania Bara |
| Ununuzi wa magari, gharama za Bima na Leseni za njia | Asilimia ya ununuzi iliyofikiwa | 100 | 70 | 70 | Malipo ya ununuzi wa magari 18 yameshakamilika na yanatarajiwa kupokelewa mwezi Juni 2025 |

**d. Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Mahakama Jumuishi (IJC)-Pemba**

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha majengo ya Mahakama ili kuwa na mazingira mazuri ya kazi na kuongeza ufanisi kwa watumishi wa Mahakama. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 3.00 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 1.7 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha TZS 1.25 bilioni sawa na asilimia 73 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa jengo la Mahakama Jumuishi katika eneo la Mfikiwa Pemba | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 30 | 30 | Ujenzi upo katika hatua ya uwekaji wa jamvi la ghorofa ya kwanza, uzio, kibanda cha umeme na ujenzi kwa jengo la kutoa huduma upo katika hatua ya linta |

### 11.2.5 Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ

Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ina jukumu la kutoa mwongozo na ushauri kwa Tawala za Mikoa katika kuratibu, kujenga mazingira mazuri na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ katika utoaji wa huduma na kuimarisha Utawala Bora. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisi imepanga kutekeleza miradi mitano ya maendeleo.

**a. Mradi wa Kuimarisha Ulinzi na Usalama Zanzibar.**

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2023/2024 na ni endelevu. Mradi una lengo la kuongeza ufanisi kwa Idara Maalum za SMZ katika kutekeleza majukumu yao ya kudumisha amani, utulivu na usalama nchini. Matokeo ya mradi huu ni pamoja na kupungua kwa matukio ya kihalifu katika jamii, kuongeza uwajibikaji na kuwa na miundombinu imara ya

ulinzi na usalama kwa wenyeji, wageni na wawekezaji. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 25.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 13.75 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha TZS 17.38 bilioni sawa na asilimia 126 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| **Shughuli Iliyopangwa** | **Kiashiria** | **Shabaha** | **Utekelezaji Halisi** | **Asilimia ya Utekelezaji** | **Maelezo** |
|---|---|---|---|---|---|
| Ununuzi wa vitendea kazi vya ulinzi | Asilimia ya vitendea kazi vilivyonunuliwa | 100 | 80 | 80 | Vitendea kazi vimenunulia kwa ajili ya matumizi ya Idara Maalum za SMZ ikiwemo sare za maafisa na wapiganaji. |
| Ununuzi na ufungaji wa vifaa vya mawasiliano ya ulinzi | Asilimia ya vifaa vya mawasiliano na ulinzi vilivyonunuliwa | 100 | 100 | 100 | Vifaa vimeshanunuliwa na tayari vimeshafungwa katika maeneo husika |
| Ununuzi wa magari maalum ya shughuli za kiulinzi | Asilimia ya manunuzi yaliofanyika | 100 | 100 | 100 | Gari zimeshanunuliwa |
| Kufanya matengenezo ya Mradi wa Mji Salama | Asilimia ya matengenezo yaliyofanyika | 100 | 5 | 5 | Wizara tayari imeingia mkataba na Kampuni ya ROM SOLUTION kwa ajili ya mategenezo ya mradi wa Mji salama |

**b. Mradi wa Ujenzi wa Ofisi za Masheha Zanzibar**

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha huduma za kijamii na kimaendeleo kwa wananchi, kuongezeka kwa ufanisi wa kiutendaji na upatikanaji wa huduma kwa jamii kupitia Shehia. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 3.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 1.65 bilioni Hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha TZS 516 milioni sawa na asilimia 31 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuanza na ujenzi wa Ofisi za Masheha kwa Shehia 48 Unguja na Pemba | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 90 | 90 | Nyumba 46 zimeshakamilika na 2 zinaendelea kwa hatua ya kuezekwa |
| Ununuzi wa samani za Ofisi za Masheha kwa Shehia 48 | Asilimia ya ununuzi samani iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Samani zimeshanunuliwa. |

**c. Mradi wa Kuimarisha Haki Jinai – Chuo cha Marekebisho ya Tabia**

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuwajengea uwezo waendesha mashtaka na wapelelezi katika masuala ya haki jinai. Mradi umedhamiria kuimarisha ushirikiano kati ya wadau wa haki jinai, kuongeza ufanisi na kasi ya upelelezi na uendeshaji wa mashtaka kwa utoaji haki kwa wananchi. Aidha, mradi unahusisha mafunzo kwa wanawake kuhusu kufahamu haki zao katika kesi za jinai na madai. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 22.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 12.1 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha TZS 6.6 bilioni sawa na asilimia 55 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo:

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuanza kwa ujenzi wa majengo mawili ya yenye vifaa vya kisasa ya Chuo cha kurekebisha tabia - Hanyegwa Mchana | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 20 | 20 | Ujenzi upo katika hatua ya kuchimba na kujenga misingi. |

**d. Mradi wa Ujenzi wa Kituo na Maegesho ya Vyombo Vya Usafiri katika Soko la Mwanakwerekwe**

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi na wafanyabiashara kwa kujenga kituo cha maegesho ya vyombo vya usafiri na huduma nyengine za usafiri katika soko la Mwanakwerekwe ili kuongeza ufanisi wa upatikanaji wa huduma kwa jamii, kupunguza msongamano wa vyombo na kuongeza mapato ya Serikali. Aidha, mradi utatunza mazingira katika eneo la bwawa la Mwanakwerekwe na kuleta mandhari nzuri. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 29.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 15.9 bilioni Hadi kufikia Machi 2025 hakuna fedha iliyoingizwa na shughuli zifuatazo zimetekelezwa: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa kituo cha Dalalada | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Hatua za awali za upembuzi yakinifu zinaendelea ikiwemo utafiti wa mazingira, sayansi ya udongo na umbile la eneo husika (Geotechnic Survey and Topography), pia Mkandarasi wa Ujenzi wa Mradi huo ameshapatikana ambaye ni CRJE kutoka China |
| Ujenzi wa eneo la maegesho ya vyombo vya usafiri katika eneo la Mwanakwerekwe | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | |

### e. Mradi wa Kijani -Pemba

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha miji inayoibuka kwa kutoa huduma za maji, usafishaji mazingira, usimamizi wa taka, kuweka mipango miji na kuwasaidia wajasiriamali, uwezeshaji wa wanawake na vijana. Vile vile, utasaidia katika Mkakati wa Taifa wa upandaji miti, uhifadhi wa mazingira ili kuimarisha ustawi wa misitu na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 11.12 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 6.1 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha TZS 1.7 bilioni sawa na asilimia 29 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya ukarabati na matengenezo ya mifumo ya maji na visima katika vituo vya afya, skuli na masoko kwa Mkoa wa Kusini na Kaskazini Pemba | Idadi ya visima vilivyokarabatiwa | 6 | 2 | 33 | Visima 2 vinavyohudumia Kizimabani na Weni vimekarabatiwa na kuwekewa *Solar Panel* na sasa vimeanza kufanya kazi |
| | Idadi ya mifumo ya maji ilivyokarabatiwa | 4 | 2 | 50 | Visima 2 vinavyohudumia Kizimbani na Weni vimewekewa mifumo ya *automatic* ya umeme wa jua na wa kawaida na kuwekewa uzio ili kulinda miundombinu hiyo |
| | Asilimia ya uwekaji miundombinu ya maji iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Maandalizi ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa kuunganishiwa *solar panel* kwa kisima kitachotoa huduma katika Zahanati ya |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Mzambarauni na Konde Mkoa wa Kaskazini Pemba kazi bado inaendelea |
| | Idadi ya masoko yaliyokarabatiwa | 2 | 2 | 100 | Soko la Kipitacho na Soko la Madungu |
| | idadi ya washiriki waliopatiwa mafunzo juu ya namna ya kutumia fursa za masoko | 1,000 | 300 | 30 | Wajasiriamali 300 wamepatiwa mafunzo juu ya fursa za kutumia masoko kwa kuongeza vipato vyao kwa Kaskazini Pemba. |
| | Idadi ya skuli zilizowekewa miundombinu ya maji | 9 | 7 | 78 | Skuli zimewekwa miundombinu ya huduma ya maji kwa kuunganishwa na *solar panel* (Shamiani Sekondari, Madungu Msingi, Ng'ombeni Msingi A&B) kwa upande wa Kusini na Kaskazini Pemba |
| Ujenzi wa kituo cha kusarifu taka na kujenga uwezo kwa vikundi vinavyojishughulisha na ukusanyaji wa taka taka katika jamii | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Eneo limeshapatikana na kuanza taratibu za ujenzi wa kituo |
| | Idadi ya vikundi vilivyojengewa uwezo | 100 | 30 | 30 | Vikundi vyenye idadi ya watu 20 vimejengewa uwezo kutoka Mkoa wa Kusini na Kaskazini Pemba |
| Kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji na vyoo kwenye vituo vya afya na skuli | Asilimia ya huduma ya maji iliyoimarishwa kwenye vituo vya afya | 100 | 5 | 5 | Maandalizi ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa kuunganisha *solar panel* kwa kisima kitakachotoa huduma ya |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | maji katika vituo 16 vya Afya ya jamii yanaendelea |
| | Asilimia ya huduma ya vyoo viliyoimarishwa kwenye vituo vya afya | 100 | 5 | 5 | Maandalizi ya ujenzi na ukarabati wa vyoo katika vituo 16 vya Afya vinanaendelea. |
| | Asilimia ya huduma ya maji iliyoimarishwa kwenye skuli | 100 | 5 | 5 | Maandalizi ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa kuunganisha *solar panel* kwa kisima kitachotoa huduma katika Skuli ya Msingi ya Madungu, Ng'ombeni A na Ng'ombeni B na Mkoani na Skuli za Sekondari za Shamiani na Chakechake ndizo ambazo zilizoguswa na mradi kwa upande wa Kusini na Kaskazini Pemba yanaendelea |
| | Asilimia ya huduma ya vyoo vilivyoimarishwa kwenye skuli | 100 | 30 | 30 | Ujenzi na ukarabati wa vyoo unaendelea katika Skuli ya Madungu, Ng'ombeni, Jadida na Micheweni kwa hatua za kujenga kuta |
| Kutoa mafunzo juu ya usimamizi wa maji, usarifu wa taka na kuzitumia katika njia mbadala pamoja na kuwapatia mafunzo | Idadi ya washiriki waliopatiwa mafunzo ya usimamizi wa maji na usarifu wa taka | 100 | 0 | 0 | Mchakato wa kuwapata washiriki wa mafunzo unaendelea katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Wakuu wa Wilaya |
| | Idadi ya vijana na wanawake waliopatiwa | 300 | 0 | 0 | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| vijana na wanawake juu ya upatikanaji wa masoko kwa bidhaa wanazozalisha | mafunzo ya upatikanaji wa masoko kwa bidhaa | | | | |
| Kufanya kampeni za uhamasishaji wa matumizi ya maji safi na usafi wa mazingira katika jamii | Idadi ya kampeni zilizofanyika | 2 | 1 | 50 | Kampeni moja imefanyika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ya kufanya usafi wa Mazingira na uhamasishaji wa matumizi ya maji safi ikijumuisha na Jamii |
| Kufanya ukarabati wa viwanja vya michezo na maeneo ya wazi ya jamii | Idadi ya viwanja vilivyokarabatiwa | 8 | 0 | 7 | Ukarabati umeanza kwa hatua za awali kwa viwanja vya michezo vinavyotumika katika maeneo mbali mbali |
| | Idadi ya maeneo ya wazi yaliyokarabatiwa | 1 | 0 | 0 | Hatua zimeanza ikiwemo kupata maeneo na kuyasafisha |
| Kuongeza uwezo wa kutumia rasilimali za misitu ili kutunza mazingira ya kijani | Idadi ya watu waliopatiwa mafunzo | 100 | 0 | 5 | Utekelezaji umeanza kwa kusaini Hati ya Makubaliano (MoU) baina watekelezaji wa mradi na Wizara ya Kilimo kupitia Idara ya Misitu, na mafunzo ya ukuzaji wa utunzaji wa Misitu kwa watendaji wa Serikali |
| Kuandaa ramani ya kijiditali itakayoonesha mipaka halisi ya maeneo | Asilimia ya uandaaji wa ramani iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Zoezi limekamilika na sasa mafunzo yanaendelea juu ya namna ya kutumia ramani na kuzitafsiri |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya utafiti juu ya athari za kimazingira, masoko na uwezo wa kiuchumi wa vikundi vya wanawake na vijana | Asilimia ya utafiti iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Utafiti umekamilika kwa sasa ni hatua za kuwafikishia jamii zinaendelea |
| Kuwajengea uwezo watoa huduma katika Taasisi za umma juu ya masuala ya utawala, usimamizi na uendeshaji | Idadi ya watoa huduma waliojengewa uwezo | 100 | 70 | 70 | Uwezo ulijengwa kwa walimu 22, watendaji wa ZAWA 7 na watumishi 41 wa Serikali |

### 11.2.5.1 Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar

Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar ina jukumu la kutoa huduma za usajili wa matukio ya kijamii yenye viwango kwa wananchi na wageni wanaoishi Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisi imepanga kutekeleza mradi mmoja wa maendeleo

**a. Mradi wa Kuimarisha Mfumo wa Usajili**

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha mifumo ya usajili wa matukio muhimu ya binadamu kama vile vizazi, vifo, ndoa, talaka na vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi. Vile vile, kuimarisha ubora wa takwimu za matukio ya kijamii, zichangie katika maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa nchini. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 1.90 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 1.0 bilioni Hadi kufikia Machi 2025, Jumla ya TZS 386 milioni sawa na asilimia 37 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuimarisha mfumo wa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi | Asilimia ya mfumo ulioimarishwa | 100 | 50 | 50 | Kazi hii ni endelevu |
| Kuimarisha mfumo wa usajili wa matukio ya kijamii na takwimu muhimu "Civil Registration and Vital Statistic" | Asilimia ya mfumo ulioimarishwa | 100 | 100 | 100 | Mfumo umekamilika na umeshaanza kufanya kazi |
| Kuweka mifumo ya kiusalama | Asilimia ya mifumo ya kiusalama iliyowekwa | 100 | 50 | 50 | Uwekaji wa mifumo ya kiusalama unaendelea kwa hatua tofauti |
| Kununua malighafi za kuchapishia vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi | Asilimia ya manunuzi yaliyofanyika | 100 | 100 | 100 | Ofisi tayari imeshapokea magamba 100,000 na malighafi za kuchapishia vitambulisho 37,000 |
| Kununua vifaa vya kielektroniki zikiwemo "computer" na mashine ya kuchapisha Vitambulisho | Asilimia ya ununuzi iliyofikiwa | 100 | 60 | 60 | Hatua za ununuzi wa printa na vifaa vya kielektroniki zimekamilika zitawasili Zanzibar ndani ya mwaka wa fedha 2024/25 |

### 11.2.5.2 Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM)

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kina lengo la kulinda usalama wa bahari na kuhakikisha kuwa Zanzibar inabaki salama na imara katika maeneo ya bahari ikiwa ni pamoja na kuzuia magendo na kupambana na uhalifu unaofanywa kupitia baharini. Kwa mwaka 2024/2025, Kikosi kimepanga kutekeleza miradi miwili ya maendeleo

**a. Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Kambi na Nyumba za KMKM**

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2016/17 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2024/25. Mradi una lengo la kutekeleza azma ya Serikali ya kuwawekea wafanyakazi wa Idara Maalum za SMZ mazingira bora ya kazi na makaazi yao. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 2.65 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 1.4 bilioni Hadi kufikia Machi 2025 hakuna fedha ilipatikana na maombi ya fedha tayari yameshapelekwa Tume ya Mipango kwa ajili ya malipo na shughuli zifuatazo zimetekelezwa: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Umalizaji wa kambi ya Kojani, Fundo na Kisiwapanza - Pemba | Asilimia ya umaliziaji iliyofikiwa | 100 | 15 | 15 | Mzabuni amepatikana na maombi ya fedha yameshawasilishwa Tume ya Mipango |
| Ununuzi wa Samani | Asilimia ya ununuzi yaliofanyika | 100 | 100 | 100 | Samani za ofisi kwa kambi 11 Unguja na Pemba zimenunuliwa |
| Ujenzi wa nyumba na kambi hanyegwa mchana | Asilimia ya ujenzi iliofanyika | 100 | 5 | 5 | Mradi upo katika hatua ya ujenzi wa misingi |
| Ununuzi wa Vifaa tiba | Asilimia ya vifaa vilivyonunuliwa | 100 | 100 | 100 | Vifaa vimeshanunuliwa |
| Ukarabati wa Kambi za KMKM | Asilimia ya ukarabati uliofikiwa | 100 | 10 | 10 | Kikosi kimekamilisha utayarisahji wa mkataba na |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | tayari kimeshawasilisha maombi ya fedha kwa ajili ya kuanza kazi ya utekelezaji wa mradi huo |

### b. Mradi wa Uzamiaji na Uokozi

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha huduma za uzamiaji na uokozi pale yanapotokezea maafa ya baharini yanayosababishwa na majanga ya kuzama kwa vyombo vya abiria, mizigo na vyombo vyengine vya usafiri wa baharini kwa Unguja na Pemba. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 2.46 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 1.3 bilioni Hadi kufikia Machi 2025 hakuna fedha iliyoingizwa na shughuli zifuatazo zimetekelezwa: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuvipeleka vyombo viwili (2) vikubwa chelezoni Mombasa | Asilimia ya upelekaji vyombo chelezoni iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Kikosi kimefanikisha utayarishaji wa Mkataba kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli |
| Ununuzi wa vipuri vya boti za KMKM | Asilimia ya manunuzi yaliyofanyika | 100 | 5 | 5 | Kikosi kimefanikisha utayarishaji wa Mkataba kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli |

### 11.2.5.3 Kikosi cha Valantia

Kikosi kina lengo la kudumisha amani, ulinzi na usalama katika Mikoa, Wilaya na Shehia. Kutoa huduma ya ulinzi kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Taasisi nyengine za ulinzi na usalama za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa mwaka 2024/2025, Kikosi kimepanga kutekeleza mradi mmoja wa maendeleo.

**a. Mradi wa Ujenzi wa Nyumba na Mahanga ya Maaskari**

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2018/2019 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2024/2025. Mradi unatekeleza azma ya Serikali ya kuwa na Idara Maalum za SMZ zenye majengo mazuri yatakayoimarisha utendaji wa kazi kwa wafanyakazi wake. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 8.72 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 4.8 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha TZS 8.1 bilioni sawa na asilimia 170 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa mahanga, ukarabati pamoja na uzio katika kambi ya KVZ Micheweni Pemba | Asilimia ya ujenzi uliofikiwa | 100 | 40 | 40 | Ujenzi wa hanga moja la kulala askari bado unaendelea na upo katika hatua ya kufunga mkanda wa kati, ambapo kwa upande wa uzio upo katika hatua ya uinuaji wa tofali, kwa upande mmoja, na Vile vile, umaliziaji wa ujenzi wa hanga moja la kulala askari upo katika hatua ya uwezekaji. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuendelea na ujenzi wa Mahanga (21), katika chuo cha KVZ Pangatupu | Asilimia ya ujenzi uliofikiwa | 100 | 35 | 35 | Ujenzi unaendelea na upo katika hatua za uwekaji wa zege ya juu (linter) kwa mahanga manne yaliyoanza kujengwa |
| Ujenzi wa kituo cha Afya, pamoja na uzio Katika kambi ya KVZ Ndugukitu Pemba | Asilimia ya ujenzi uliofikiwa | 100 | 30 | 30 | Ujenzi wa kituo cha afya upo katika hatua ya kumwaga zege kwa ajili ya ghorofa ya kwanza na uzio upo katika hatua ya kukamilisha kwa kufunga linta ya mwisho ya juu ya ukuta |
| Ujenzi wa ofisi, na mahanga 2, katika kambi ya KVZ Kiashange Unguja | Asilimia ya ujenzi uliofikiwa | 100 | 55 | 55 | Jengo la ofisi Kiashange lipo katika hatua ya umaliziaji wa upandishaji wa tofali za juu (ghorofa ya kwanza) na hanga lipo katika hatua ya upakaji rangi, utiaji wa madirisha, milango na maru maru |
| Ujenzi wa kituo cha afya katika kambi ya Makao Makuu Mtoni | Asilimia ya ujenzi wa kituo cha afya iliyofikiwa | 100 | 45 | 45 | Ujenzi upo katika hatua ya uwekaji wa jamvi kwa ajili ya ujenzi wa ghorofa ya kwanza |
| Kuanza ujenzi wa hanga moja katika kambi ya Kikungwi | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 60 | 60 | Ujenzi umefikia hatua ya ukamilishaji, kazi zilifanyika ni kuezeka, kuweka dari na kupiga plasta kazi zinazoendela ni kupaka rangi |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa Ofisi moja, hanga moja na nyumba ya Mkuu wa kambi katika kambi ya Pujini Pemba | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 57 | 57 | Ujenzi upo katika hatua tofauti:<br><br>Ofisi- uwekaji wa nguzo kwa ujenzi wa ghorofa ya kwanza,<br><br>Hanga- kazi zinazoendelea ni kuweka dari na<br><br>Nyumba ya Mkuu wa kambi - kazi zilizofanyika ni kupiga plasta, kueka dari pamoja na miundombinu ya maji na umeme. |

### 11.2.5.4 Chuo cha Mafunzo

Chuo cha Mafunzo kina lengo la kurekebisha tabia pamoja na kutoa huduma za ushauri nasaha kwa wanafunzi wa chuo wanapoingia na kutoka gerezani. Kutoa huduma zenye kuzingatia haki, kuongeza ubunifu katika urekebishaji wa tabia kwa kubuni programu zitakazoweza kuwasaidia wanafunzi kujiendeleza na kujitegemea wanaporejea katika jamii. Kwa mwaka 2024/2025, Kikosi kimepangiwa kutekeleza mradi mmoja wa maendeleo.

**a. Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Makaazi na Mahanga**

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2017/2018 na ulitakiwa kukamilika mwaka 2024/25. Mradi unatekeleza azma ya Serikali ya kuhakikisha watendaji wa Idara Maalum za SMZ wanafanya kazi zao katika mazingira mazuri. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 2.55 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 1.4 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha TZS 300 milioni sawa na asilimia 21 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa nyumba kambi hanyegwa mchana | Asilimia ya ujenzi iliofikiwa | 100 | 20 | 20 | Mradi upo katika hatua ya ujenzi wa msingi |
| Ujenzi wa hanga kambi ya Bumbwini | Asilimia ya ujenzi iliofikiwa | 100 | 40 | 40 | Mradi upo katika hatua ya ufungaji wa linta |
| Ununuzi wa vifaa vya TEHAMA kwa jengo la Ofisi ya Makao Makuu – Unguja | Asilimia ya ujenzi iliofikiwa | 100 | 100 | 100 | Vifaa vya TEHAMA vimesha nunuliwa na baadhi ya vifaa vimeshakabidhiwa na kuanza kutumika |

### 11.2.5.5 Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU)

Jeshi lina lengo la kuwafundisha vijana wa Zanzibar kulihudumia Taifa lao kwa kuwapatia mafunzo ya msingi ya kujiendeleza katika shughuli za kilimo, viwanda, uvuvi, ufundi na kazi za amali. Kuwafunza elimu ya uraia, kushiriki katika shughuli za maendeleo ya kijamii, utamaduni, pamoja na ulinzi wa Taifa kwa ujumla. Kwa mwaka 2024/2025 Kikosi kimepanga kutekeleza miradi miwili ya maendeleo.

**a. Mradi wa Ujenzi wa Nyumba na Mahanga ya Kambi za JKU**

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2023/2024 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2025/2026. Mradi una lengo la kuweka mazingira mazuri kwa Idara Maalum za SMZ kwa kuwapatia majengo yenye viwango ili kuimarisha utendaji wa kazi kwa wafanyakazi wake. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 1.64 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 902 milioni. Hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha TZS 1.64 bilioni sawa na asilimia 182 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa majengo mawili yenye ghorofa mbili kwa ajili ya Nyumba za maafisa na wapiganaji wa JKU Ng`ambwa | Asilimia ya ujenzi uliofikiwa | 100 | 40 | 40 | Ujenzi upo katika hatua ya kunyanyua nguzo na kuendelea na Ghorofa ya kwanza |

b. Mradi wa Ujenzi wa Dakhalia

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2023/24 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2025/26. Mradi una lengo la kuwapatia wanafunzi malazi wanaoishi mbali na Skuli na wanaotoka nje ya Zanzibar, kuwasaidia wanafunzi kwa kuwaweka pamoja na kuweza kujisomea. Uwepo wa dakhalia hii utasaidia kuleta mafanikio mazuri kwa wanafunzi na kuongeza ufaulu. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 1.50 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 825 milioni Hadi kufikia Machi 2025, shughuli zifuatazo zimefanyika: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuanza ujenzi wa jengo la ghorofa nne (4) katika kambi ya Mtoni | Asilimia ya ujenzi uliofikiwa | 100 | 5 | 5 | Ujenzi umeanza kwa hatua ya usafishaji wa eneo na upimaji na baadhi ya vifaa kama matufali na nondo zimeshapelekwa katika eneo la ujenzi kwa ajili ya kuanza ujenzi |

### 11.2.5.6 Kikosi cha Zimamoto na Uokozi

Kikosi kina jukumu la kusimamia na kuhakikisha kuwa huduma za zimamoto na uokozi zinapatikana katika maeneo yote ili kutoa huduma za dharura kwa wananchi itakapohitaji ikiwemo bandarini na viwanja vya ndege Unguja na Pemba. Kwa mwaka 2024/2025, Kikosi kimepanga kutekeleza miradi miwili ya maendeleo.

**a. Mradi wa Ujenzi wa Mahanga na Nyumba za Maaskari**

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha huduma ya makazi kwa watendaji wa Idara Maalum za SMZ ili kuweza kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 7.73 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 4.3 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha TZS 754 milioni sawa na asilimia 18 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuanza ujenzi wa vituo na mahanga ya askari katika kambi ya Kibuteni, Bwejuu, Mangapwani, Tumbatu kwa Unguja na Finya na Shamiani Muambe kwa Pemba | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 10 | 10 | Hatua ya ujenzi wa matofali imeanza katika kituo cha Bwejuu na Kibuteni, upimaji katika maeneo ya Tumbatu umeanza. Kikosi kimebadilisha eneo la ujenzi kutokana na uhitaji mkubwa zaidi kutoka Finya na kujenga Chamanangwe Pemba na kutoka Chuini na kujenga Tunguu Unguja. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuanza ujenzi wa nyumba za askari kambi ya Tasini Pemba | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 10 | 10 | Ujenzi unaendelea katika hatua ya msingi |
| Kuanza ujenzi wa Ofisi ya zoni kambi ya Mwanakwerekwe Unguja na Ofisi Kuu kambi ya Chanjaani Pemba | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa (Ofisi Kuu kambi ya Chanjaani Pemba) | 100 | 5 | 5 | Kuanza hatua za Maandalizi ya eneo la ujenzi |
| Ukarabati wa vituo vya Zimamoto katika kambi ya Kigunda, Marumbi, Kitogani kwa Unguja na ukarabati wa mahanga mawili kambi ya Chanjaani Pemba | Asilimia ya ukarabati iliyofikiwa | 100 | 70 | 70 | Ujenzi umefikia hatua tofauti ikiwemo kueka dari pamoja na kujenga sakafu |

### b. Mradi wa Ununuzi wa Magari na Vifaa vya Kuzimia Moto

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kukabiliana na maafa yanayosababishwa na majanga ya moto kwa wananchi na mali zao. Majanga pia yanayotokana na meli za abiria na mizigo na vyombo vyengine vya usafiri wa baharini na nchi kavu. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 29.64 (TZS 2.50 bilioni kutoka Serikalini na TZS 27.14 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 16.3 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha TZS 760 milioni sawa na asilimia 55 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa kutoka Serikalini na hakuna fedha iliyoingizwa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ununuzi wa gari za utoaji huduma ya uokozi na uzimaji moto. | Asilimia ya manunuzi ilofanyika | 100 | 40 | 40 | Asilimia 40 ya malipo ya awali yameshalipwa kwa mzabuni wa usambaji wa gari mbili za uzimaji moto na uokozi |
| Ununuzi wa magari 21 ya utoaji huduma za uokozi na uzimaji moto; | Asilimia ya manunuzi ilofanyika | 100 | 10 | 10 | Asilimia 22 ya malipo ya awali ya mkopo imeshalipwa matarajio Juni, 2025 kuwasili kwa gari kwa hatua ya kwanza. |

## 11.2.6 Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais

Ofisi hii imepewa dhamana ya kuratibu na kusimamia shughuli za sekta mtambuka zikiwemo Mazingira, Ukimwi, watu wenye mahitaji maalum na udhibiti wa madawa ya kulevya. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisi imepanga kutekeleza miradi minne (4) ya Maendeleo.

### a. Mradi wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi na Usimamizi wa Mazingira

Mradi huu unatekelezwa kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia 2024 – 2025. Mradi una lengo la kutathmini na kusaidia kupunguza athari za maeneo yaliyo hatarini kutokana na mabadiliko ya tabianchi na kuchukua hatua mahsusi ikiwa ni pamoja na kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika ukanda wa pwani, kujenga uwezo kwa wakulima wadogo wadogo jinsi ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa njia za vitendo na ubunifu ambazo zinatarajiwa kuwa na matokeo yenye tija. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 500.00 milioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 275 milioni. Hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha TZS 299 sawa na asilimia 109 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kujenga ukuta wenye urefu wa mita 70 katika eneo la Kisiwa panza - Pemba | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Ujenzi umekamilika |

### b. Mpango wa Kuirithisha Zanzibar Kijani

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2022/2023 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2026/2027 Mradi una lengo la kuimarisha hali ya uoto wa asili wa Zanzibar, kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kupanda, kuendeleza na kutunza miti ya misitu, matunda na mikoko kwa faida endelevu ya kimazingira, kiuchumi, kijamii na uhimili wa mabadiliko ya tabianchi. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 1.50 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 825 milioni. Hadi kufikia Machi 2025, shughuli zifuatazo zimetekelezwa:

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ununuzi wa miche milioni tatu na upandaji wa miti eneo la Donge, Chaani Masingini kwa Unguja na Pujini kwa Pemba na maeneo mengine yaliyoathirika na uchimbaji wa michanga na mawe | Idadi ya miche iliyonunuliwa na kupandwa | 3,000,000 | 30,536 | 1 | Miche hii imegawiwa katika maeneo husika |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Uchimbaji wa visima kwa ajili ya kusaidia vitalu vya miti | Idadi ya visima vilivyochimbwa | 2 | 2 | 100 | |
| Utoaji wa miche | Idadi ya miche iliyotolewa | 2,250,000 | 14,536 | 0.65 | Miche imetolewa kwa Taasisi za Serikali, Idara Maalum za SMZ na Jumuiya za kimazingira |
| Kuimarisha vitalu vya miti | Idadi ya miti iliyopandwa katika vitalu | 150 | 150 | 100 | |

### c. Mradi wa Ujenzi wa Nyumba ya Makamu wa Kwanza wa Rais

Mradi huu umeanza utekelezaji wake mwaka 2024/2025 na kutarajiwa kukamilika utekelezaji wake Juni 2025/2026. Mradi una lengo la kuimarisha mazingira ya makaazi kwa Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais na familia yake, ili kuendana na hadhi inayostahiki. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 1.50 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 825 milioni. Hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha TZS 55 milioni sawa na asilimia 7 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa nyumba ya Mheshimiwa Makamo wa Kwanza wa Rais Unguja | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Hatua za ufuatiliaji wa eneo la ujenzi wa nyumba hiyo zinaendelea kwa kushirikiana na WAMM, OMPR na OR-Ikulu |
| Ununuzi wa vifaa na samani | Asilimia ya ununuzi iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Hatua za manunuzi zinaendelea |

**d. Mradi wa Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa Kutumia Mfumo wa Ikolojia Vijijini – "Ecosystem-basedAdaptation for Rural Resilience" (EBARR)**

Mradi unatekelezwa kwa miaka sita, kuanzia mwaka 2018/19 hadi 2024/2025. Mradi una lengo la kusaidia uhimili wa mabadiliko ya tabianchi kwa kurejesha uoto wa asili kwa kutumia mifumo ya ikolojia, kutoa elimu ya kilimo chenye kustahamili athari za mabadiliko ya tabianchi na kuwajengea uwezo jamii juu ya njia mbadala za kujipatia kipato ambazo hazina athari za kimazingira. Mradi unagharimu jumla ya TZS 1.5 bilioni mpaka kumalizika kwake, na unatekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo kutoka United Nations Environment Programme (UNEP). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi kufikia Machi 2025), Jumla ya TZS 249.4 zimepatikana na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa mabanda ya kufugia kuku | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 90 | 90 | Mabanda matatu yamejengwa na ujenzi upo katika hatua ya kuweka milango na kuunga umeme |
| Ujenzi wa mabanda ya kufugia mbuzi | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 67 | 67 | Mabanda mawili (2) yamekamilika na ujenzi wa banda moja (1) unaendelea |
| Ununuzi wa mashine za kutotolea vifaranga – *Incubator* | Idadi ya mashine za kutotolea vifaranga | 3 | 3 | 100 | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kutoa Mafunzo ya ushoni wa vyerehani na upakasaji | Idadi ya washiriki waliopatiwa mafunzo | 45 | 77 | 171 | Mafunzo yamefanyika kwa Awamu ya Kwanza ambapo vikundi vitatu vya ushoni wa vyerehani na vikundi vya upakasaji kutoka Shehia za Matemwe Kijini, Mbuyutende na Jugakuu vimepatiwa mafunzo |
| Ununuzi wa vifaa vya kufugia nyuki kwa Shehia tatu | Asilimia ya manunuzi iliyofanyika | 60 | 60 | 100 | Ununuzi umekamilika na vifaa vimekabidhiwa kwa wahusika |

**e. Mradi wa Kuimarisha Mfumo wa Maji Machafu Chake Chake, Pemba**

Mradi huu umeanza utekelezaji wake mwaka 2021 na kutarajiwa kukamilika utekelezaji wake Juni 2025. Lengo la mradi ni kusafisha maji machafu yanayotoka katika makaazi ya watu kabla ya kuingia katika bahari na kusababisha uchafuzi wa mazingira na viumbe hai vilivyomo ndani yake. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 92.6 milioni Hadi kufikia Machi 2025, Jumla ya TZS 68.6 milioni sawa na asilimia 74 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuunganisha Kaya (nyumba) katika mfumo wa maji machafu | Idadi ya nyumba zilizounganishwa | 150 | 147 | 98 | Baadhi ya nyumba hazija unganishwa kutokana na kutokidhi vigezo vya kuunganishwa katika mfumo |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kupanda majani katika mabwawa ya kusafishia maji machafu | Asilimia ya upandaji wa majani iliyofikiwa | 100 | 20 | 20 | Jumla ya aina tatu za majani yalipandwa kwa majaribio na kubainika kuwa ni aina mbili tu za majani ndizo zilizoota |

### 11.2.6.1 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya

Mamlaka ina dhamana ya kusimamia mapambano dhidi ya biashara, usafirishaji na matumizi ya dawa za kulevya, kutoa taaluma kwa jamii juu ya athari za dawa za kulevya, kutoa tiba pamoja na ushauri nasaha kwa waathirika wa dawa za kulevya. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Mamlaka imepanga kutekeleza mradi mmoja wa Maendeleo.

**a. Mradi wa Kuimarisha Mamlaka ya Kupambana na Madawa ya Kulevya**

Mradi huu ni wa Awamu ya Pili umeanzishwa mwaka 2024/2025 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2025/2026 Mradi una lengo la kuimarisha kituo cha matibabu na kurekebisha tabia kwa watumiaji wa dawa za kulevya. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 2.55 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 1.4 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha TZS 250 milioni sawa na asilimia 18 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuanza ujenzi wa Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia Pemba. | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 15 | 15 | Mshauri Elekezi ameshatafutwa ambae ni ZBA, Rasimu ya Mkataba wa kampuni ya usanifu wa udongo tayari Mkataba umeshawasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu na matayarisho ya awali ya ujenzi yameshaanza. |
| Kukamilisha malipo ya ujenzi wa kituo cha tiba na marekebisho ya tabia Kidimni | Asilimia ya malipo iliyofikiwa | 100 | 20 | 20 | Hatua za malipo zinaendelea |

### 11.2.7 Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi

Ofisi ina dhamana ya kusimamia, kuratibu na kufuatilia shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ikiwa ni pamoja na kusimamia shughuli za Muungano (Zanzibar na Tanzania bara) kwa mujibu wa misingi ya Katiba na Sheria na kulinda haki za binadamu na ushirikishwaji kwa sekta husika. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisi imepanga kutekeleza programu moja na miradi miwili ya Maendeleo.

**i. Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini Awamu ya Tatu (TASAF III) Kipindi cha Pili**

Programu hii imeanzishwa mwaka 2020 na inatarajiwa kukamilika 2025. Programu ina lengo la kuziwezesha Kaya masikini ili waweze kuongeza kipato chao, fursa na uwezo wa kugharamia mahitaji muhimu ya kibinadamu hasa chakula, afya na elimu. Programu hii inakusudia kutekeleza miradi iliyoibuliwa na wananchi katika maeneo ya elimu,

afya, ufugaji na kupatikana kwa ajira za muda. Kwa mwaka 2024/2025, Programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 30.32 bilioni (TZS 100.00 milioni kutoka Serikalini na TZS 30.22 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 16.67 bilioni (TZS 55 milioni kutoka serikalini na 16.62 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha TZS 3.71 bilioni sawa na asilimia 22 (TZS 50 milioni kutoka Serikalini na 3.66 bilioni kutoka Washirika wa Maendeleo) ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Uhaulishaji wa Fedha kwa Kaya za Walengwa wa Mpango. | Idadi ya Kaya zilizohaulishiwa fedha | 36,430 | 36,401 | 99.9 | Kwa Kaya zilizohudhuria. |
| Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi wa Miundombinu ya Elimu na Afya. | Idadi ya Miradi iliyotekelezwa. | 10 | 10 | 100 | Miradi imeendelea kutekelezwa kupitia sekta za afya na elimu. Kati ya miradi 10 iliyopangwa kutekelezwa miradi sita (6) imekamilika na kukabidhiwa sekta husika kwa matumizi na miradi minne (4) inaendelea na utekelezaji. |
| Tathmini ya vikundi vya kuweka akiba na | Idadi ya Vikundi vilivyofanyiwa tathmini. | 1,147 | 1,138 | 99 | Tathmini imetekelezwa kwa lengo la kujua uhai wa vikundi, hali ya |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| kukuza uchumi wa kaya kwa Shehia 126 za Unguja. | | | | | huduma za kibenki, hali ya uwekaji wa Akiba na utoaji wa Mikopo kwa wanavikundi pamoja na hali ya usajili wa vikundi kwa Mamlaka husika. |
| Utoaji wa Ruzuku za uzalishaji kwa Kaya za walengwa waliokidhi vigezo. | Idadi ya Kaya zilizopatiwa ruzuku za uzalishaji. | 1,716 | 1,716 | 100 | |
| Kuratibu ziara na vikao kwa wadau wa mpango katika kufuatilia utekelezaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini. | Idadi ya ziara na vikao vilivyoratibiwa | 4 | 6 | 150 | Ziara na vikao hivi vilijumuisha Wadau wakiwemo wa Kimataifa |

**a. Mradi wa ujenzi wa Nyumba ya Makamu wa Pili wa Rais**

Mradi umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha na kuweka mazingira mazuri ya makaazi ya Mheshimiwa Makamo wa Pili wa Rais ili kuendana na hadhi inayostahiki. Kwa mwaka 2024/2025, mradi umepangiwa jumla ya TZS 4.50 bilioni. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 2.47 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha TZS 943 milioni sawa na asilimia 38 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuanza hatua ya ununuzi kwa kupata Mkandarasi na Mshauri elekezi wa mradi | Asilimia ya manunuzi iliyofanyika | 100 | 100 | 100 | |
| Ujenzi wa nyumba ya Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Maandalizi ya ujenzi yameanza kwa kufanya majaribio ya udongo pamoja na kutengeneza michoro ya jengo |
| Ujenzi wa nyumba ya Makamo wa pili wa Rais katika eneo la Osterbay Dar es Salaam | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 83 | 83 | Ujenzi upo katika hatua ya ukamilishaji kwa kuweka madirisha, milango, taa, kupaka rangi pamoja na *landscaping* |

### ii. Proramu ya Kukabiliana na Maafa

Programu hii imeanzishwa mwaka 2024/2025 na inatarajiwa kukamilika mwaka 2025/2026. Program ina lengo la kujenga uelewa wa jamii ili kusaidia kupunguza athari za majanga/maafa kwa kujiandaa, kujikinga, kukabiliana endapo yatatokea na kurejesha hali baada ya maafa kutokea. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 130 milioni kutoka Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 71.5 milioni Hadi kufikia Machi 2025, Jumla ya TZS 130 milioni sawa na asilimia 181.8 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya vikao cha robo mwaka cha wadau wa masuala ya maafa | Idadi ya vikao vilivyofanyika | 4 | 2 | 50 | Jumla ya wadau 46 kutoka sekta mbali mbali walishiriki katika vikao hivyo. |
| Kuimarisha mifumo ya Taarifa ya Kukabiliana na Maafa (ZDMIS) | Idadi ya mifumo iliyoimarishwa | 2 | 1 | 50 | Mfumo umekamilika kwa hatua ya awali kwa 50% |
| Kufanya mapitio ya Mpango Mkakati wa Kamisheni ya kukabiliana na maafa wa mwaka 2019-2025 | Asilimia ya mapitio iliyofanyika | 100 | 5 | 5 | Kazi imeanza kwa hatua za awali za kuandaa Hadudi Rejea, Mkataba pamoja na kikao cha kwanza na wadau |
| Kutoa mafunzo ya kukabiliana na maafa kwa wanafunzi wa skuli za msingi za Serikali na Binafsi kwa Unguja na Pemba | Idadi ya wanafunzi Waliopatiwa mafunzo | 5,500 | 5,500 | 100 | Wanafunzi wa skuli 55 (3,500 katika skuli 35 za Unguja na 2,000 katika skuli 20 za Pemba) wamepatiwa mafunzo |
| Kufanya ufuatiliajiwa robo mwaka wa mfumo wa uwekaji wa taarifa za kukabiliana na maafa | Idadi ya ziara za ufuatiliaji zilizofanyika | 4 | 4 | 100 | Ufuatiliaji na usimamizi ulifanyika kwa Wilaya zote za Unguja na Pemba. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuwapatia mafunzo ya kupunguza athari za maafa watendaji wa masuala ya kukabiliana na maafa | Idadi ya watendaji waliopatiwa mafunzo | 12 | 12 | 100 | |

### 11.2.8 Wizara ya Afya

Wizara ina jukumu la kusimamia afya za wananchi wa Zanzibar ili waweze kushiriki katika shughuli za ujenzi wa Taifa na kuleta maendeleo endelevu. Sekta hii inatekeleza ujenzi wa miundombinu na mifumo ya utowaji wa huduma za afya pamoja na kuimarisha uwezo wa sekta katika utoaji wa huduma za afya zilizobora kwa wananchi. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara imepanga kutekeleza programu saba na miradi miwili ya maendeleo.

**i. Programu ya Kumaliza Malaria Zanzibar**

Programu hii imeanzishwa kwa lengo la kutokomeza maradhi ya malaria kwa kuhakikisha kwamba maradhi haya yanamalizika hapa Zanzibar. Kwa mwaka 2024/2025, Programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 7.93 bilioni (TZS 645.00 milioni kutoka Serikalini na TZS 7.29 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 4.4 bilioni (TZS 354.7 kutoka Serikalini na TZS 4 bilioni kutoka kwa Washirika wa Mawendeleo). Hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha TZS 1.9 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo sawa na asilimia 44 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Uchunguzi na utibabu wa ugonjwa wa malaria | Idadi ya watu waliofanyiwa uchunguzi | 9,269 | 9,167 | 98.9 | Wagonjwa waliogunduliwa na vimelea vya malaria walipatiwa tiba stahiki |
| Upigaji dawa kwenye maeneo yenye maambukizi | Idadi ya nyumba zilizopigwa dawa | 6,554 | 6,139 | 94 | |
| Ufuatiliaji wa mwenendo wa ugonjwa wa malaria | Idadi ya wagonjwa walio fuatiliwa | 8,977 | 6,969 | 78 | |
| Kukusanya sampuli | Idadi ya sampuli zilizokusanywa | 9,269 | 9,167 | 99 | |

### ii. Programu Shirikishi ya UKIMWI, Homa ya Ini, Kifua Kikuu na Ukoma

Programu hii imeanzishwa kwa lengo la kupambana na maradhi ya Ukimwi, Homa ya Ini, Kifua Kikuu na Ukoma, kupunguza kasi ya maambukizi ya virusi vya Ukimwi, kupunguza vifo vitokanavyo na maradhi ya Kifua Kikuu, Homa ya Ini na kupunguza maambukizi ya ukoma. Kwa mwaka 2024/2025, Programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 4.45 bilioni (TZS 380.00 milioni kutoka Serikalini na TZS 4.06 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 2.4 bilioni (TZS 209 milioni kutoka Serikalini na TZS 2.2 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha TZS 3.8 bilioni sawa na asilimia 156 (TZS 952 milioni kutoka Serikalini na bilioni 2.86 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuendelea kuimarisha huduma za "Care Treatment Clinic" (CTC) kwa watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi (VVU) | Idadi ya watu wanaoishi na VVU waliopatiwa ARVs | 11,078 | 9,529 | 86 | |
| Kuendelea kupima VVU, Kifua Kikuu na Homa ya Ini kwa makundi yote katika jamii | Idadi ya watu waliopimwa VVU | 1,389,128 | 118,803 | 8.60% | |
| | Idadi ya wagonjwa wa kifua kikuu waliopimwa na kupatiwa matibabu sahihi | 1,230 | 561 | 45.60% | |
| | Idadi ya watu waliogundulika na virusi vya homa ya ini B na kuanza matibabu | 0 | 381 | | Wagonjwa wa homa ya ini B waligunduliwa na kuanza matibabu |

**iii. Programu Shirikishi ya Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto**

Programu hii imeanzishwa kwa lengo la kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi pamoja na vifo vya watoto walio chini ya umri wa miaka mitano. Kwa mwaka 2024/2025, Programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 6.19 bilioni (TZS 1.0 bilioni kutoka Serikalini na TZS 5.19 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 3.4 bilioni (TZS 550 milioni kutoka Serikalini na TZS 2.85 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha TZS 478 milioni sawa na asilimia 14 (TZS 297 milioni kutoka Serikalini na TZS 181 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ununuzi wa chanjo, dawa na vifaa tiba | Asilimia ya manunuzi yaliofanyika | 100 | 100 | 100 | Watoto waliopatiwa chanjo ya *Penta 3* chini ya mwaka mmoja 48,364 (Unguja 32,175 na Pemba ni 16,189) kwa kipindi cha Julai 24 - Machi 2025. |
| Kufanya ufuatiliaji wa utoaji wa huduma katika vituo na hospitali zinazotoa huduma za afya ya mama na mtoto | Idadi ya mama wajawazito waliohudhuria kliniki angalau mara moja | 61,461 | 54,546 | 89 | Kina mama **54,546** (Unguja **38,863** na Pemba **15,683**) walihudhuria kliniki |
| | Idadi ya vifo vya kina mama vitokanavyo na uzazi vilivyohakikiwa | 38 | 33 | 87 | |
| | Idadi ya kina mama waliojifungulia kwenye vituo na hospitali. | 42,152 | 36,166 | 86 | Kina mama **36,166** (Unguja 25,364 na Pemba 10,802) walijifungulia katika hospitali na vituo vya Afya |
| Kuimarisha utoaji wa huduma za afya ya uzazi na kupunguza matatizo na vifo vya mama na mtoto | Idadi ya akina mama waaliopata huduma ya afya ndani ya masaa 48 baada ya kujifungua | 39,094 | 37,491 | 96 | Kina mama 37,491 (Unguja 25,941 na Pemba 11,550) walipatiwa huduma |
| | Idadi ya wateja wapya wanaotumia njia za kisasa za uzazi wa mpango | 389,996 | 27,005 | 7 | Wateja wapya 27,005 (Unguja 18,850 na Pemba 8,155) walijiunga |

### iv. Programu ya Jamii ni Afya

Programu hii imeanzishwa kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya ili ziwe karibu na wananchi kwa kuwapelekea wahudumu wa afya katika ngazi ya Shehia waweze kusaidia kutoa huduma za awali wanapopata matatizo ya kiafya katika jamii. Kwa mwaka 2024/2025, Programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 1.50 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 825 milioni. Hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha TZS 560 milioni sawa na asilimia 68 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuwezesha wahudumu wa afya katika ngazi ya Jamii kutekeleza majukumu yao | Idadi ya wafanyakazi waliowezeshwa | 2,222 | 1,334 | 60 | |
| Kuwajengea uwezo wahudumu wa afya katika ngazi ya Jamii. | Idadi ya wafanyakazi waliojengewa uwezo | 1,200 | 1,242 | 104 | |

### v. Programu ya Ukarabati na Ujenzi wa Vituo vya Afya ya Msingi

Programu hii imeanzishwa kwa lengo kuimarisha afya ya msingi kwa kuimarisha miundombinu ya vituo vya afya ya msingi ili viweze kutoa huduma za afya ya msingi zenye kiwango na kuimarisha afya ya jamii. Kwa mwaka 2024/2025, Programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 35.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 19.2 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha TZS 17.8 bilioni sawa na asilimia 92 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa vituo vya afya (health care center) kumi (10) | Asilimia ya ujenzi iliofikiwa | 100 | 75 | 75 | Ujenzi unaendelea hatua mbali mbali za ukamilishaji kwa baadhi ya vituo, ujenzi wa kuta, |
| Ujenzi wa Kituo cha Afya Nungwi | Asilimia ya ujenzi iliofikiwa | 100 | 26 | 26 | Ujenzi wa tofali katika ghorofa ya kwanza unaendelea |
| Ujenzi wa Kituo cha Afya Tunguu | | | 70 | 70 | Hatua ya ujenzi iliyofikiwa ni kuezeka, kuweka frame za milango na kupiga plasta |
| Ujenzi wa Kituo cha Afya Sebleni | | | 55 | 55 | Ujenzi upo katika hatua za ukamilishaji wa jengo (finishing). |
| Ujenzi wa Kituo cha Afya Magomeni Wandaras | | | 70 | 70 | Ujenzi upo katika hatua za ukamilishaji wa jengo (finishing). |
| Ujenzi wa Kituo cha Afya Konde | | | 22 | 22 | Ujenzi upo katika hatua ya matayarisho ya kuweka jamvi kwa ajili ya kujenga ghorofa ya kwanza |
| Ujenzi wa Kituo cha Afya Jadida | | | 58 | 58 | Ujenzi upo katika hatua za ukamilishaji wa jengo (finishing).Kazi zinazoendelea ni uwekaji wa tarazo, upigaji wa plasta nje na ndani kwa jengo la pili, umwagaji wa zege kwa ajili ya njia za wenye mahitaji maalum, uwekaji wa mifumo ya umeme, maji na kipoza hewa |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa Kituo cha Afya Chonga | | | 35 | 35 | Ujenzi upo katika hatua ya kuweka jamvi kwa kuendelea na ghorofa ya kwanza |
| Ujenzi wa Kituo cha Afya Mahonda | | | 50 | 50 | Ujenzi unaendelea katika hatua ya uwekaji paa, tarazo na plasta kwa upande wa nje wa ghorofa ya kwanza. |
| Ujenzi wa Kituo cha Afya Mtambile | | | 22 | 10 | Ujenzi upo katika hatua ya kuweka msingi |
| Ujenzi wa Kituo cha Afya Kiuyu Minungwini | | | 10 | 10 | Ujenzi upo katika hatua ya kuweka msingi |

### vi. Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Afya

Programu hii imeanzishwa kwa lengo la kuimarisha miundombinu itakayosaidia katika utoaji wa huduma za afya zenye ubora na viwango vinavyokubalika Kitaifa na Kimataifa. Kwa mwaka 2024/2025, Programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 27.50 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 15.1 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha TZS 11.98 bilioni sawa na asilimia 79 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo:

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa Bohari Kuu ya Dawa – Unguja | Asilimia ya Ujenzi iliofikiwa | 100 | 7 | 7 | Mshauri Elekazi na Mkandarasi wameshapatikana. |
| Ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Kaskazini Unguja (Mahonda) | Asilimia ya ujenzi iliofikiwa | 100 | 10 | 10 | Ujenzi upo katika hatua ya msingi |
| Kuanza ujenzi wa Ofisi ya Wizara ya Afya Pemba | Asilimia ya ujenzi iliofikiwa | 100 | 5 | 5 | Michoro imeshakamilika. |

**vii. Programu ya Kusaidia Watu Wasiojiweza Kujiunga na Mfuko wa Huduma za Afya – Zanzibar**

Programu hii imeanzishwa kwa lengo kuwasaidia wananchi wasiojiweza na makundi maalum ikiwemo wazee kuanzia miaka 65, mama wajawazito, watoto chini ya umri wa miaka 5 na masikini, ili waweze kupata huduma za afya kupitia Mfuko wa Huduma za Afya ya Zanzibar kuhakikisha kuwa hakuna mwananchi anayekosa huduma za afya anapohitajia. Kwa mwaka 2024/2025, Programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 500.00 milioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 275 milioni. Hadi kufikia Machi 2025, hakuna fedha iliyopatikana na kazi ya uhakiki na usajili wa watu wasiojiweza na makundi maalumu kwenye jamii umeshafanyika.

**a. Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Wafanyakazi katika Hospitali za Wilaya**

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha makaazi kwa wafanyakazi ili waweze kufanya kazi kwa utulivu zaidi, kuongeza ufanisi na kupatikana muda wote itakapotokea dharura. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 6.48 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 3.56 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha TZS 8.3 bilioni sawa na asilimia 234 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuendelea na ujenzi wa nyumba za wafanyakazi katika Hospitali ya Pangatupu, Kitogani, Mwera Pongwe, Vitongoji na Kinyasini | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 95 | 95 | |
| Ujenzi wa nyumba ya Pangatupu | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 93 | 93 | Ujenzi upo katika hatua ya ukamilishaji kwa kazi za uwekaji Viyoyozi, makabati, rangi kumalizia kazi za nje |
| Ujenzi wa nyumba Kitogani | | | 95 | 95 | Jengo limeshakamilika, kwa sasa hatua za umaliziaji zinaendelea. |
| Ujenzi wa nyumba Mwera Pongwe | | | 99 | 99 | Ujenzi wa jengo umekamilika hatua iliyobakia ni uwekaji wa *lift* na jenereta. |
| Ujenzi wa nyumba kinyasini Pemba | | | 95 | 95 | Ujenzi upo katika hatua ya uwekaji wa mfumo wa maji na umeme na kumalizia kazi za nje. |
| Ujenzi wa nyumba Vitongoji | | | 91 | 91 | Ujenzi upo katika hatua ya uwekaji mfumo wa maji na umeme na kumalizia kazi za nje |

**b.Mradi wa Ukarabati na Utanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja.**

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha huduma katika hospitali ya Mnazi Mmoja kwa kuimarisha miundombinu ya utoaji wa huduma za afya na ununuzi wa vifaa tiba vya kisasa. Kupitia mradi huu Serikali imepanga kufanya ukarabati mkubwa katika hospitali ya Mnazi Mmoja ili kuiwezesha kutoa huduma nzuri na zenye kukidhi mahitaji. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 23.00 bilioni (TZS 2.00 kutoka Serikalini na TZS 21.00 bilioni kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 11.55 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2025, Jumla ya TZS 90.2 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo sawa na asilimia 1 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutumika kwa ajili ya mishahara na uendeshaji wa mradi na ununuzi wa gari moja kwa ajili ya shughuli za mradi.

**c. Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa – Binguni**

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha huduma za Afya kwa wananchi wa Zanzibar na wageni kutoka katika nchi ikiwemo watalii wanaotembelea Zanzibar. Mradi utahusisha ujenzi wa Hospital ya kisasa itakayoweza kutoa huduma za kitaalamu ambazo zitapunguza usafirishaji wa wagonjwa nje ya nchi, Mradi unatarajiwa kujengwa kupitia mkopo nafuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa Korea. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 30.57 bilioni. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 16.8 bilioni. Hatua zinazoendelea ni Upembuzi Yakinifu unaofanywa na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa Korea ili ujenzi uanze ukiwa ni utaratibu wa kawaida kwa miradi ya Serikali ya Jamhuri ya Watu wa Korea.

### 11.2.9 Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi

Wizara ina jukumu la kuweka mipango mizuri ya matumizi ya ardhi ambayo itasaidia kugawanya matumzi ya ardhi kulingana na shughuli mbalimbali zinazoendelea kutekelezwa nchini, ikiwemo uwekezaji, michezo, biashara, viwanda, kilimo na makaazi. Vile vile, Wizara ina jukumu la kusimamia upangaji na matumizi bora ya rasilimali ardhi kupitia

programu mbali mbali. Wizara hutumia wadau wakiwemo Shirika la Nyumba, Mabenki na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili kurahisisha upatikanaji wa makaazi yaliyobora na ya kisasa. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara imepanga kutekeleza mradi mmoja wa maendeleo kama ifuatavyo:

**a. Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Maendeleo**

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2024/2025 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2026/2027 Mradi una lengo la kuweka mazingira mazuri ya makaazi kwa wananchi pamoja na kuweka haiba nzuri katika mandhari ya mji wa Zanzibar. Mradi unakusudia kuwapatia wananchi wa Zanzibar makaazi yaliyobora na kwa gharama nafuu. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 40.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 22 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, Jumla ya TZS 22.65 bilioni sawa na asilimia 103 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuanza ujenzi wa nyumba za gharama nafuu 1,000 katika eneo la Chumbuni. | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 15 | 15 | Ujenzi upo katika hatua ya msingi ya umwagaji wa zege kwa block mbili (2) |

### 11.2.10 Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda

Wizara ina lengo la kukuza viwanda vidogo na vya kati sambamba na kuimarisha mazingira ya ufanyaji biashara kwa lengo la kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara imetekeleza programu moja (1) na mradi mmoja (1) wa maendeleo kama ifuatavyo:

**a. Mradi wa Kuendeleza Vituo vya Biashara na Maonyesho Zanzibar**

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2021/2022 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2026/2027. Mradi una lengo la kutoa huduma za kuimarisha sekta ya biashara na viwanda kwa kutoa msaada kwa wafanyabiashara wadogo wadogo na wa

kati. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 10.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 5.5 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha TZS 349 milioni sawa na asilimia 6 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| **Shughuli Iliyopangwa** | **Kiashiria** | **Shabaha** | **Utekelezaji Halisi** | **Asilimia ya Utekelezaji** | **Maelezo** |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuendelea na ujenzi wa jengo la utawala, vibaraza vya kuweka mashamiana na eneo la kuhifadhia vifaa vya maonyesho pamoja na kuimarisha ukumbi wa Mikutano wa Dkt. Hussein Mwinyi katika eneo la Nyamanzi | Asilimia ya ujenzi wa jengo la utawala iliyofikiwa | 100 | 20 | 20 | Hatua ilofikia ni uwekaji wa nondo kwa ajili ujenzi wa nguzo za kusimamishia tofali kwa sehemu ya chini (ground floor) |
| | Asilimia ya ujenzi wa eneo la kuhifadhia vifaa vya maonesho iliyofikiwa. | 100 | 5 | 5 | Kazi ya mchoro wa eneo la kuhifadhia vifaa vya maonesho inaendelea |
| | Asilimia ya kazi ya kuimarisha ukumbi iliyofikiwa | 100 | 95 | 95 | Kazi ya uwekaji wa vioo vya madirisha katika ukumbi wa Dkt. Hussein Mwinyi inaendelea |
| Kuimarisha mifumo ya umeme katika kituo cha maonesho pamoja na kuweka mfumo wa umeme wa jua | Asilimia ya kazi ya uimarishaji iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Kazi ya ujenzi wa (Power house) imeanza pamoja na ununuzi wa vifaa vya umeme kwa ajili ya kuimarisha huduma ya umeme |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuimarisha ulinzi kwa kuweka senyenge, kufunga kamera za CCTV na *scanner* pamoja na kuweka mfumo wa mawasiliano ya mtandao *"internet"* | Asilimia ya kazi ya ufungaji kamera za CCTV iliyofikiwa | 100 | 45 | 45 | CCTV kamera zimefungwa katika ukumbi wa Dr. Hussein Ali Mwinyi |

**b. Mradi wa kuanzisha na kuendeleza Maeneo Maalum ya Viwanda (Industrial Park)**

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha maeneo tengefu ya viwanda ili kurahisisha viwanda vidogo vidogo na vya kati ili viwe katika maeneo maalum yatakayosaidia kukuza uchumi na kutoa ajira kwa wajasiriamali. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 40.32 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 22.17 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha TZS 3.77 bilioni sawa na asilimia 17 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa ukuta wa uzio na mabanda ya viwanda (Industrial Shed steel-fabricated) katika eneo la Dunga na Chamanangwe | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa katika eneo la Dunga | 100 | 15 | 15 | Hadidu rejea ya kazi ya ujenzi na michoro ya ujenzi ya mabanda imekamilika na mchakato wa kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa mabanda hayo unaendelea. |
| | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa katika eneo la Chamanangwe | 100 | 15 | 15 | |
| Kuandaa Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi, Upembuzi Yakinifu pamoja na "topographic survey" katika eneo la Pangatupu | Asilimia ya uandaaji wa Mpango Mkuu wa matumizi ya ardhi iliyofikiwa | 100 | 15 | 15 | Hadidu rejea ya kazi ya ujenzi imeandaliwa. Aidha, Wizara inasubiri kupatiwa hati ya umiliki wa eneo hilo ili iweze kuendelea na utekelezaji wa kazi hiyo. |
| | Asilimia ya kazi ya ufanyaji wa survey iliyofikiwa. | 100 | 50 | 50 | Upimaji wa udongo umefanyika kwa ajili ya kuanza ujenzi |
| Ujenzi wa miundombinu ya maji na barabara za ndani katika eneo la viwanda Chamanangwe | Asilimia ya ujenzi wa miundombinu ya maji iliyofikiwa | 100 | 15 | 15 | Hadidu rejea ya kazi ya ujenzi na michoro ya ujenzi wa miundombinu ya maji imekamilika na mchakato wa kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa miondombinu hiyo unaendelea |
| Ujenzi wa miundombinu ya umeme katika eneo la viwanda Dunga na Chamanangwe. | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa – Dunga | 100 | 5 | 5 | Wizara imewaandikia Shirika la Umeme Zanzibar juu ya kufanyiwa tathmini ya uwekaji wa miundombinu ya umeme katika eneo la viwanda la Dunga na Chamanangwe. |
| | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa – Chamanangwe. | 100 | 5 | 5 | |

### 11.2.11 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

Wizara hii ina jukumu la kuleta maendeleo ya Taifa, kwani Elimu ni Sekta Mama katika kuleta maendeleo ya Taifa lolote hapa duniani. Sekta hii hujenga maarifa na ujuzi ambao huweza kutumika kama dira katika kufikia malengo ya nchi kwa kutumia rasilimali watu. Kwa mwaka 2024/2025, Wizara hii imepanga kutekeleza programu mbili na mradi mmoja wa maendeleo

**i. Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Elimu**

Programu hii imeanzishwa kwa lengo la kuimarisha miundombinu ya sekta ya elimu kiujumla ili kuwawezesha wananchi kupata elimu bora na viwango vya ufanisi. Kwa mwaka 2024/2025, Programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 391.57 bilioni (TZS 234.39 bilioni kutoka Serikalini na TZS 183.13 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 229.6 bilioni (TZS 128.9 bilioni kutoka Serikalini na TZS 100.7 bilioni kutoka kwa Washirika wa MAendeleo). Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 147.8 bilioni (TZS 94.4 bilioni kutoka Serikalini na TZS 53.4 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) sawa na asilimia 64 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kujenga madarasa 840 kupitia ujenzi wa skuli 20 za ghorofa (15 za msingi na 5 za sekondari) zikiwemo skuli 2 za ufundi | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 10 | 10 | Maandalizi ya ujenzi kwa skuli sita (6) yameanza kwa hatua ya kuzungushia uzio wa mabati kwenye maeneo husika.<br><br>Orodha ya Skuli zitakazojengwa<br><br>Skuli za Msingi (15): Magogoni, Kihinani, Chunga, Uzi Mjini, Fuoni Kibondeni, Shaurimoyo, Jumbi, Chaani, Minungwini, Mchanga Mdogo, Micheweni, Chanjamjawiri, Uondwe, Jadida, na Ng'ombeni.<br><br>Skuli za Sekondari (5): Kitope, Bambi, Dunga, Kengeja na Shamiani. |
| Kujenga madarasa 420 mapya (120 ya Sekondari na 300 ya Msingi) ya skuli za chini | Idadi ya madarasa yaliyojengwa | 420 | 298 | 71 | Jumla ya madarasa 298 yamekamilika kujengwa na 122 yanaendelea na ujenzi.<br><br>Skuli ambazo madarasa hayo yamejengwa ni: Wingwi, Kizimbani, Cheju, Kijundu, Kiboje, Mgogoni, Mjini Kiuyu, Pondeani, Kukuu, Makombeni, Makoongwe, Mtangani, Ukutini, Chanjaani, Kilindi, Ndagoni, Pujini, Michenzani, Mizingani, Wambaa, Chwale, Vitongoji, Tasini, Furaha, Ziwani, Chwaka, Kiungoni, Pandani na Mtambile. (Kiuyu, Zawiyani, Kipangani, Makongeni, Koani na Mjini wingwi). Kibuyuni, Kibeni, Mgambo, Kisiwa panza, Chambani, Kiwani, Msuka, Ghana, Mjimbini, Kangani, Simai, Jojo, Maziwa ngombe, Mtemani, Micheweni, Shumba, Tumbe B, Kangani, na Chokocho. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kukamilisha madarasa 170 yaliyoanzishwa na wananchi (100 Msingi na 70 Sekondari); | Idadi ya madarasa yaliyokamilishwa | 170 | 125 | 74 | Jumla ya madarasa 125 yamekamilika na 192 yanaendelea na ujenzi katika hatua mbalimbali za utekelezaji, ikiwa ni pamoja na kumalizia sakafu, kuezeka paa, kupiga plasta na kupaka rangi. Shughuli hizi zinaendelea katika skuli za Mfenesini, Dimani, Ubago Uzini, Unguja Ukuu, Kibele, Koani, Uchukuni, Kiboje, Ndijani, Ndijani sekondari, Binguni, Kitogani, Miza wa Miza, Muungoni, Kinowe sekondari, Kiuyu sekondari, Shumba sekondari, Tumbe sekondari, Tumbe Magharibi, Karume, Maziwangombe, Mnarani, Kipange, Kinowe, Chimba, Matangatuwani, Mijileni, Msuka, Kilindini, Mabandani tutu, Uwandani, Pembeni, Kilindi, Pujini Wesha , Vikunguni ,Wawi, Mavungwa, M/michungwani, M/kibokoni, Tutu Matuleni, Wawi mgogoni, Jambangome, Kisiwa panza, Ng'ombeni "B", Shidi, Mahduthi, Chwale chambani, Tironi, Andikoni, Mkanyageni msingi, Michenzani hostel, Chambani holi, Chokocho, Mtambile, Kandwi, Bilindi, Bwereu, Kigunda, Potoa, Mbuyutende, Mlimboni, Mtowa pwani, Kinyasini, Tumbatu A, Mbuyu maji, Kidoti,<br><br>Kilindi, Nungwi, Kitope msingi, Mahonda , Kinduni, Mgambo, Mahonda, Mahonda Ambasha ms, Jadida ms, Mzambarau Takao, Shengejuu, Minungwini, Bwagamoyo, Mwane, Tungamaa, Kidundo maandalizi (TUTU), Jitenge maandalizi(TUTU), Pandani kilimani, Mchangamdogo sekondari na Kivumoni Mtambwe. |
| Ujenzi wa Karakana za ufundi katika skuli 33 za sekondari (skuli 3 kila Wilaya) | Idadi ya Karakana zilizojengwa | 33 | 0 | 10 | Maeneo yamepatikana na hatua ya kuandaa michoro (design) ya karakana inaendelea. |
| Kujenga Maktaba Kuu ya Kisasa | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 7 | 7 | Hatua ya manunuzi kwa ajili ya kumpata mshauri elekezi inaendelea. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa dakhalia ya wanafunzi 500 wanawake katika eneo la Tunguu - SUZA | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 15 | 15 | Ujenzi upo katika hatua ya uchimbaji wa misingi |
| Ujenzi wa Chuo cha Ubaharia | Asilimia ya ujenzi uliofikiwa | 100 | 8 | 8 | Mshauri elekezi ameshawasilisha michoro ya ujenzi kwa hatua ya kumtafuta mkandarasi. |
| Utanuzi wa Chuo Cha KIST | Asilimia ya ujenzi uliofikiwa | 100 | 8 | 8 | Mshauri elekezi ameshawasilisha michoro ya ujenzi kwa hatua ya kumtafuta mkandarasi. |
| Kuendelea na ujenzi wa vyuo vitano (5) vya Amali | Idadi ya vyuo vilivyojengwa | 5 | 0 | 6 | Hatua inayoendelea kwa sasa ni upitiaji wa mwisho wa michoro kwa ajili ya kumtafuta mkandarasi |
| Kujenga Chuo Kipya cha Ualimu na kuvifanyia ukarabati vyuo viwili na vituo vya Ualimu (TCs) | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Hati miliki tayari imepatikana kwa ajili ya ujenzi wa chuo kipya cha Ualimu katika eneo la Dole. |
| | Idadi ya vyuo na vituo vya ualimu vilivyokarabatiwa | 2 | 0 | 8 | Hatua inayoendelea ni tathmini ya wakandarasi waliofanya maombi. |
| | Asilimia ya ukarabati vituo vya ualimu iliyofikiwa | 100 | 8 | 8 | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Idadi ya nyumba za walimu wa Sekondari zilizojengwa | 8 | 0 | 5 | |
| Kujenga dakhalia katika skuli 11 | Idadi ya Dakhalia zilizojengwa | 11 | 8 | 73 | Ujenzi wa dakhalia unaendelea kwa hatua mbali mbali kama ifuatavyo: -<br><br>Lumumba, Misufini, Kiwani, Mikindani na Paje Mtule (finishing), Fidel Castro, Maziwa Ng'ombe, Chwaka Tumbe (kuezeka). |
| Kujenga karakana ya magari katika Chuo cha Amali Mkokotoni; | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | |
| Kujenga Ofisi za Elimu za Wilaya katika Wilaya za Kusini, Kaskazini "B", Magharibi "A" kwa Unguja na Micheweni kwa Pemba | Idadi ya Ofisi zilizojengwa | 4 | 2 | 50 | Ujenzi wa ofisi unaendelea kwa hatua mbali mbali kama ifuatavyo: -<br><br>Wilaya ya Kusini na Micheweni (maandalizi ya ujenzi), Kaskazini "B" (msingi), Magharibi "A" (kuezeka) |
| Kujenga viwanja vitatu (03) vya kisasa vya michezo (3 in 1) ambapo kiwanja | Idadi ya viwanja vilivyojengwa | 3 | 0 | 10 | Maombi ya ujenzi wa viwanja vitatu vya michezo yamewasilishwa |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| kimoja (01) Wilaya ya Magharibi “B”, kimoja (01) Wilaya ya Kusini Unguja na kiwanja kimoja (01) Pemba Wilaya ya Chakechake pamoja na kukarabati kiwanja kimoja (01) cha michezo Wilaya ya Mjini Unguja. | Asilimia ya ukarabati iliyofikiwa | 100 | 25 | 25 | Kiwanja kilichokarabatiwa ni kiwanja cha mchezo wa Volleyball |
| Kukamilisha ujenzi wa uzio wa Chuo cha Mafunzo ya Amali Vitongoji | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 10 | 10 | Hatua ya kupitia na kuboresha mchoro inaendelea. |
| Kuyafanyia ukarabati majengo ya Ofisi | Asilimia ya ukarabati iliyofikiwa | 100 | 25 | 25 | Ukarabati wa majengo ya Ofisi Unguja unaendelea, na kwa Pemba bado haujaanza. |
| Kuanza ujenzi wa skuli ya meno na kliniki yake katika eneo la Tunguu - SUZA | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 7 | 7 | Kazi ya uandaaji wa michoro kwa skuli hizo imekamilika aidha taratibu za zabuni kwa ajili ya mkataba wa ujenzi zinaendelea |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya ukarabati wa skuli 100 (70 za msingi na 30 za sekondari) | Idadi ya skuli zilizofanyi wa ukarabati | 100 | 16 | 16 | Ukarabati wa skuli 16 umekamilika na unaendelea kwa skuli zifuatazo:<br><br>Uroa, Bambi, Uzini, Mwera, Charawe, Ukongoroni, Jendele, Chwaka, Ndijani, Kikungwi, Kiboje, Dunga, Ndijani Kikungwi, Kajengwa, Bwejuu, Kijigoni, Paje, Michamvi, Jambiani, Kikadini, Kitogani, Kiongoni, Paje Jambiani, Fukuchani, Kijini, Gamba, Nungwi, Potoa, Chaani, Tumbatu Jongowe, Pwani Mchangani, Mfurumatonga, Mkwajuni, Gamba Secondary,Matemwe Secondary,Tumbatu Secondary, Potoa, Mkwajuni, Kijini Secondary, Upenja, Fujoni, Donge Karange, Donge, Donge Munadhamati Ya Kiislam, Kiwengwa, Fujoni, Kinowe, Kiuyu, Konde "A", Konde "B", Makangale, Maziwang'ombe, Micheweni "A", Micheweni "B", Mkiangoombe, Mnarani, Mtemani, Shumba, Wingwi, Msuka, Wingwi, Bopwe, Chwale, Fundo, Gando, Jadida, Kizimbani, Limbani Mchangamdogo, Mjini Kiuyu, Pandani, Shengejuu, Uondwe, Bububu, Mwenge, Kizimbani, Bububu Kihinani, Mbuzini, Kama, Chunga, Kibweni, Kidichi, Kisiwa Panza, Kangani, Kengeja, Mizingani,<br><br>Mjimbini, Mtambile, Mtangani, Mtuhaliwa, Ng'ombeni "A", Ng'ombeni "B", Ngwachani, Wambaa, Kisiwandui, Kidongochekundu, Chanjaani, Ndagoni, Ngomeni, Pembeni, Pujini, Vitongoji, Wawi, Ziwani, Birikau, Chanjamjawiri, Fidel-Castro, Furaha, Kilindi, Ng'ambwa, Pondeani, Shamiani, Uwandani, Chwaka, Kangani, Kengeja Ufundi, Kengeja, Kisiwa Panza, Makombeni Makoongwe, Mizingani, Mkanyageni, Mtambile, Mtangani, Wambaa, Fundo, Gando, Kinyasini Mabatini, Mitiulaya, Pandani, Uondwe, Utaani na Uvinje. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kujenga jengo la Ofisi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa Unguja na Kuendelea na Ujenzi wa Jengo la Ofisi Kuu Pemba | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa (Unguja) | 100 | 12 | 12 | Ripoti ya thathmini imeshawasilishwa na hatua inayofuata ni kumkabidhi Mkandarasi kwa kuanza kazi |
| | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa (Pemba) | 100 | 40 | 40 | Ujenzi upo katika hatua ya kumwaga zege kwa ghorofa ya tatu (3) |
| Kuendelea na ujenzi wa skuli tatu (3) zenye dakhalia kwa mashirikiano na BADEA | Idadi ya Skuli zilizojengwa | 3 | 3 | 95 | Ujenzi upo katika hatua za kumalizia kwa<br><br>Skuli zote ambazo ni Kifundi, Gamba na Mfenesini |
| Ujenzi wa karakana za Uhandisi Mitambo, Uhandisi ujenzi na magari – KIST | Idadi ya karakana zilizojengwa | 3 | 0 | 7 | Zabuni za kumpata Mkandarasi wa ujenzi zinaendelea. |
| Ukarabati wa Karakana na Maabara (Drawing, Aviation, Chemistry na Physics) – KIST | Asilimia ya Ukarabati uliofikiwa | 100 | 7 | 7 | Zabuni za kumpata Mkandarasi wa ujenzi zinaendelea. |
| Ujenzi wa jengo la skuli ya kilimo na jengo la maabara ya sayansi ya kisasa katika kampasi ya Tunguu – SUZA | Asilimia ya Ujenzi iliyofikiwa | 100 | 25 | 25 | Kazi zinazoendelea kwa sasa ni umwagaji zege ya jamvi na usimamishaji nguzo za chini (ground floor) |

**ii.Programu ya Uimarishaji Ubora wa Elimu**

Programu ina lengo la kuimarisha utoaji wa elimu katika ngazi zote kwa kuwapatia walimu na wanafunzi vifaa vya kujifunzia na kufundishia, pamoja na mafunzo ya walimu na matumizi ya TEHAMA. Kwa mwaka 2024/2025, Programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 75.54 bilioni (TZS 49.41 bilioni kutoka Serikalini na TZS 26.13 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 41.55 bilioni (TZS 27.17 bilioni kutoka Serikalini na 14.37 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 11.79 bilioni (TZS 83 milioni kutoka Serikalini na 11.70 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) sawa na asilimia 28 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuzipatia skuli za sekondari vifaa kwa ajili ya masomo ya fani za ujuzi wa amali na ufundi | Asilimia ya skuli za sekondari zilizopatiwa vifaa | 100 | 10 | 10 | Baadhi ya vifaa vipo katika hatua ya manunuzi na vyengine vinaendelea kuratibiwa kwa ajili ya kupata mahitaji halisi. |
| Kuzipatia skuli vifaa vya kujifunzia na kufundishia masomo ya ufundi na amali | Asilimia ya skuli zilizopatiwa vifaa | 100 | 10 | 10 | Baadhi ya vifaa vipo katika hatua ya manunuzi na vyengine vinaendelea kuratibiwa kwa ajili ya kupata mahitaji halisi |
| Kuzipatia skuli vifaa vya michezo (mpira wa miguu, wavu, mikono na vifaa vya kuogelea) | Asilimia ya skuli zilizopatiwa vifaa | 40 | 10 | 10 | Mipira ya mchezo wa mpira wa miguu (football) imeanza kutolewa maskulini na vifaa vyengine vya mpira wa wavu, mikono na vifaa vya kuogelea vinaendelea kuratibiwa. Jumla ya Skuli 127 zilipatiwa mipira ya miguu (Unguja 62 na Pemba 65) |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa jengo la Ofisi, skuli ya elimu na lugha za kigeni, nyumba za wafanyakazi na kiwanja cha michezo. | Asilimia ya Ujenzi iliyofikiwa | 100 | 9 | 9 | Tathmini ya kumtafuta mshauri elekezi wa kutayarisha michoro na usimamizi wa ujenzi kwa hatua ya pili (technical and financial evaluation) zimekamilika na kuwasilishwa BADEA kwa kupata ridhaa (No Objection). |
| Ujenzi wa skuli 22 za Maandalizi za chini | Asilimia ya ujenzi uliofikiwa | 100 | 50 | 50 | Ujenzi wa skuli upo katika hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na ujenzi wa kuta na uwezekaji. |
| Ujenzi wa skuli 17 za Msingi | Asilimia ya ujenzi uliofikiwa | 100 | 65 | 65 | Ujenzi unaendelea kwa hatua ya plasta na uwezekaji kwa skuli zifuatazo: -<br><br>Mwera Mtufaani, , Potoa Msingi, Vuga Mkadini, Kiuyu, Maziwang'ombe, Tumbe "A", Wingwi, Kiungoni, Kizimbani, Madungu, Mbuzini, Vitongoji, Dodo, Kengeja, Ndagoni na Michenzani. |
| Ujenzi wa skuli 15 za Sekondari | Asilimia ya ujenzi uliofikiwa | 100 | 67 | 67 | Ujenzi unaendelea kwa hatua za msingi, kuta, uwezekaji na plasta kwa skuli zifuatazo: -<br><br>Mwenge, Kama, Chuini, Mbuzini,<br><br>Kisauni,Tunguu, Koani, Karume, Kinowe, Sizini, Simai, Mtemani, Finya, Vikunguni na Furaha. |
| Kuzipatia skuli vifaa vya TEHAMA vikiwemo *Computer Desktop 500, Laptop 100 na Projector* | Asilimia ya skuli zilizopatiwa vifaa vya TEHAMA | 100 | 10 | 10 | Hatua za manunuzi zinaendelea kwa vifaa vya<br><br>*Computer Desktop 500, Laptop 100 na Projector 100* |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuzipatia skuli vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalum (miwani, shime sikio, fimbo nyeupe) | Asilimia ya skuli zilizopatiwa vifaa | 100 | 25 | 25 | Vifaa (miwani, shime sikio, fimbo nyeupe) tayari vimenunuliwa vinasubiria kufanyiwa uhakiki na uthibitisho ( wanafunzi 87 kati ya 207 watapatiwa vifaa) |
| Kuimarisha huduma za maktaba kwa kuanzisha "e-library" | Asilimia ya uanzishwaji wa e-library | 100 | 5 | 5 | Hatua ya manunuzi ya kumtafuta Mshauri elekezi inaendelea. |
| Kuwaandaa walimu wa mafunzo ya fani za amali na ufundi kwa kuwapatia mafunzo. | Idadi ya walimu waliopatiwa mafunzo | 40 | 102 | 255 | Mafunzo hayo ni *water treatment; Standalone solar system; small boat handling* na *aluminium work.* Uelewa wa matumizi ya *multimedia* katika kufundishia pamoja na Mafunzo ya zana za ufundishaji (*log book*) |
| Kuimarisha upatikanaji wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia kwa elimu ya maandalizi, msingi na sekondari | Idadi ya skuli zilizopatiwa vifaa | 622 | 622 | 100 | Skuli 222 za Sekondari zimepatiwa vifaa kama<br><br>Madaftari, vifaa vya maabara, chaki, mafolda na madaftari ya mahudhurio.<br><br>Skuli 400 za Maandalizi na Msingi zimepatiwa madaftari na chaki boksi 1000. |
| Kuendelea na ujenzi wa vyuo vitano vya mafunzo ya Amali | Idadi ya vyuo vilivyojengwa | 5 | 0 | 6 | Hatua inayoendelea kwa sasa ni upitiaji wa mwisho wa michoro kwa ajili ya kumtafuta mkandarasi |
| Kuwapatia walimu wa maandalizi, | Idadi ya walimu waliopatiwa | 450 | 360 | 80 | Walimu waliobakia watafanyiwa mafunzo |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| msingi na sekondari mafunzo ya utekelezaji wa Mtaala wa Umahiri | mafunzo | | | | |
| Kuimarisha mafunzo ya walimu kazini katika ngazi ya skuli (SBI) | Idadi ya walimu waliopata mafunzo | 720 | 988 | 137.2 | Walimu waliopatiwa mafunzo ni kutoka katika Wilaya za majaribio (Magharibi A, Kusini na Wete) |
| Kuziunganisha skuli 230 za Sekondari na Mkonga wa Taifa | Idadi ya Skuli za Sekondari zilizounganishwa | 230 | 68 | 32.8 | Skuli 68 tayari zimelazwa mkonga, 49 Unguja na 19 Pemba. Skuli 10 za Unguja tayari zimeshaunganishwa |
| Kuimarisha ufundishaji kwa njia ya mtandao *(virtual learning)* | Asilimia ya uimarishaji iliyofikiwa | 100 | 7 | 7 | Kwa sasa hatua za manunuzi ya kumpata Mshauri elekezi kwa ajili ya kuandaa maudhui ya masomo (*content development and curation*) zinaendelea. |

### a. Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Juu

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuongeza idadi ya wataalamu wazalendo katika visiwa vya Zanzibar. Kwa mwaka 2024/2025, mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 25.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 13.75 bilioni kutoka Serikalini. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 17.03 bilioni (TZS 11.07 bilioni kutoka Serikalini na 5.96 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) sawa na asilimia 124 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo:

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuwapatia mikopo wanafunzi wa elimu ya juu Zanzibar. | Idadi ya wanafunzi waliopatiwa mikopo | 7,367 (wapya 3,070 na wanaoendelea 4,297) | 8,867 | 120 | Jumla ya Wanafunzi wapya 4,623 waliteuliwa kupata mikopo (3,457 ni shahada ya kwanza, pili na tatu; na 1,166 ni Diploma). Vile vile, wanafunzi wanaoendelea 4,244 walifunga Mkataba wa kuendelea na mkopo |

## 11.2.12 Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo

Wizara hii ina jukumu la utoaji uhakiki na utoaji wa Habari na kupokelewa kwa wasikilizaji na watazamaji kwa kutumia Magazeti, TV na Redio kwa usahihi na kwa wakati, kuwawezesha vijana kwa kuwatafutia fursa za ajira, kudumisha utamaduni na kuimarisha michezo. Kwa mwaka 2024/2025, Wizara imepanga kutekeleza programu moja na miradi miwili ya maendeleo.

### i. Programu ya Kuendeleza Viwanja vya Michezo

Programu hii imeanzishwa mwaka 2023/2024 na inatarajiwa kukamilika mwaka 2025/2026, Programu ina lengo la kuiwezesha sekta ya michezo kwa kujenga na kuimarisha miundombinu ya michezo Zanzibar itakayokidhi viwango vya Kitaifa na Kimataifa. Kwa mwaka 2024/2025, Programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 60.63 bilioni (TZS 60.00 bilioni kutoka Serikalini na TZS 633.98 milioni kutoka Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), programu ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 33.35 bilioni (TZS 33.00 bilioni kutoka Serikalini na 348 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 57. 58 bilioni (TZS 55.45 bilioni kutoka Serikalini na 2.13 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) sawa na asilimia 173 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| **Shughuli Iliyopangwa** | **Kiashiria** | **Shabaha** | **Utekelezaji Halisi** | **Asilimia ya Utekelezaji** | **Maelezo** |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa viwanja vya Wilaya Unguja na Pemba | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa. | 100 | 30 | 30 | Shughuli za ujenzi wa viwanja vya Wilaya na Mikoa zinaendelea ambapo Mkandarasi amekamilisha ujenzi wa majengo yanayojumuisha Ofisi, vyumba vya kubadilishia nguo wachezaji na vyoo vyake; uzio na taa katika viwanja, kazi zinazoendelea ni ujenzi katika eneo la kucheza (Pitch). Maeneo yaliyoanza kujengwa ni Chake chake (Gombani) na Kishindeni Mkoa wa Kaskazini Pemba. Kwa upande wa Unguja ni Maisara, *Breeze* na Kitope. Hadi kufikia Machi jumla ya viwanja vinne (4) vimeshawekwa nyasi bandia.<br><br>Viwanja vya *four in one* vya Maisara vimekamilika na kwa upande wa Kilimani *Breeze* vipo katika hatua za mwisho kukamilika. |
| Ujenzi wa viwanja na uzio katika Uwanja wa Gombani | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 95 | 95 | Uzio wa Uwanja wa Gombani umeshakamilika zimebaki kazi ndogo ndogo za uwekaji sawa ardhi katika eneo la kuingilia ndani. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya Ukarabati na Uboreshaji wa kiwanja cha michezo Gombani | Asilimia ya ukarabati na marekebisho yaliyofanyika | 100 | 70 | 70 | Mkandarasi amekamilisha ujenzi wa vikalio (base) pamoja na kuweka nguzo za kufunikia paa la uwanja wote, Ujenzi wa vyumba vya kubadilishia nguo wachezaji na vyoo vyake, uwekaji wa viti katika majukwaa ya watazamaji (Mashabiki) na eneo la Viongozi Mashuhuri. Aidha, anaendelea na kukamilisha mapaa (Roof) pamoja na maegesho ya magari. |
| Ukarabati wa viwanja vya Mao Ze Dong. | Asilimia ya ukarabati ilyofikiwa. | 100 | 70 | 70 | Shughuli zilizokamilika ni uwekaji wa nyasi bandia, taa, viti, kujenga vyumba vya kubadilishia nguo kwa wachezaji pamoja na kujenga vyoo. Hatua zilizobakia ni upakaji wa rangi na kueka umeme. |
| Ujenzi wa viwanja vinne *(4 in 1)* Unguja na Pemba; | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa. | 100 | 57 | 57 | Shughuli zote za utekelezaji wa mradi zinafanywa na Shirika la Maendeleo la Ujerumani *(GIZ)*. Ujenzi wa viwanja vyote vinne unaendelea katika hatua mbali mbali ikiwemo kujenga majengo yanayojumuisha ofisi, vyoo na vyumba vya kubadilishia nguo wachezaji na kuweka zege (base) katika eneo la uwanja kwa viwanja vyote vinne ambavyo ni Tumbatu, Mkokotoni, Kangani na Mchangamdogo. |
| Ukarabati Viwanja viwili vya michezo midogo midogo *(4 in 1)* | Asilimia ya ukarabati iliyofikiwa | 100 | 57 | 57 | Hatua iliyofikiwa katika ukarabati ni kuwekwa zege (base), mifumo ya umeme pamoja na maji. kujengwa kwa vyumba vya wachezaji, vyoo kwa viwanja vyote viwili (Mwera Regeza Mwendo Unguja na Polisi Tennis Chake chake Pemba) hatua za ujenzi bado zinaendelea. |

### a. Mradi wa Vituo vya Mafunzo kwa Vijana Awamu ya Pili

Mradi huu umeanzishwa kwa kuwajengea uwezo vijana kwa kuwapatia mafunzo ya stadi za Maisha na Ufundi. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 4.59 bilioni (TZS 4.50 bilioni kutoka Serikalini na TZS 90.00 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 2.80 bilioni (TZS 2.75 bilioni kutoka Serikalini na 50 milioni kutoka kwa

Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 199 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo sawa na asilimia 7 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi (utanuzi) wa vituo vya mafunzo Pangeni Unguja na Mjini Ole Pemba; | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 2 | 2 | Utaratibu wa kumtafuta Mshauri Elekezi umeshaanza. |
| Ununuzi wa vifaa kama vile vyerahani kwa ajili ya vijana wajasiriamali. | Asilimia ya manunuzi iliyofanyika | 100 | 2 | 2 | Utaratibu wa kumtafuta Mshauri Elekezi umeshaanza. |
| Kuratibu programu za mafunzo ikiwemo mafunzo ya Uongozi, Ujasiriamali na Taaluma za Maisha *(life skills)* | Idadi ya programu zilizoratibiwa | 3 | 0 | 0 | |

**b. Mradi wa Ujenzi wa Chuo cha Sanaa na Utamaduni**

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2024/2025 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2025/2026. Mradi una lengo la kuweka miundombinu kwa ajili ya mafunzo na utaalamu wa Sanaa katika tasnia ya Sanaa ikiwemo kuibua, kukuza na kuhuisha vipaji kwa vijana ili kukuza ajira na vipato vyao. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 5.09 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 2.75 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 1.29 bilioni sawa na asilimia 47 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa Chuo cha Sanaa na Utamaduni Unguja | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 65 | 65 | ujenzi upo katika hatua za *skimming* na kumalizia *fitting* ya umeme na maji |
| Ununuzi wa samani na vifaa vya Ofisi. | Asilimia ya manunuzi iliyofikiwa. | 100 | 0 | 0 | Mchakato wa manunuzi unasubiri kukamilika kwa jengo. |

### 11.2.13 Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo

Wizara hii ina jukumu la kusaidia upatikanaji wa pembejeo za kilimo na utoaji wa mafunzo kwa wakulima na wafugaji. Wizara inafanya kazi kwa kushirikiana na sekta nyengine katika ukuzaji uchumi kwa kutoa mchango wa moja kwa moja kwa wananchi katika kupambana na umasikini, uzalishaji mashambani, utoaji wa ajira pamoja na kuimarisha huduma za kilimo. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara imepanga kutekeleza programu tatu (3) na miradi mitano (5) ya maendeleo kama ifuatavyo:-

#### i. Programu ya Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji

Programu imeanza mwaka 2022/2023 na umekamilika mwaka 2024/2025. Programu ina lengo la kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji ili kuongeza uzalishaji wa zao la mpunga pamoja na kuwawezesha wakulima kwa kuwajengea uwezo wa uzalishaji wenye tija zaidi kwa kutumia pembejeo za kilimo. Kwa mwaka 2024/2025, Programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 24.00 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), programu ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 13.20 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 13.63 bilioni (TZS 13.27 bilioni kutoka Serikalini na 364 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) sawa na asilimia 103 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kujenga na kusimamia miundombinu ya umwagiliaji yenye ukubwa wa eneo la hekta 131 katika bonde la Cheju "B" | Idadi ya kilomita za barabara zilizojengwa | 10 | 10 | 100 | Kazi zote za ujenzi wa miundombinu katika bonde la Cheju B zimekamilika. |
| | Idadi ya hekta zilizojengwa | 131 | 131 | 100 | |
| Kujenga na kusimamia kazi ya ujenzi wa misingi ya maji (drainage canals) bonde la Cheju B | Idadi ya kilomita za misingi zilizojengwa | 5 | 5 | 100 | Kazi za uchimbaji wa misingi mikubwa na midogo ya kutolea maji *(Primary, Secondary and Tertiary Drainage Canals*) katika bonde la Cheju B zimekamilika. |
| Ujenzi wa mitaro midogo yenye urefu wa kilomita 20 kwa kiwango cha saruji katika mabonde ya Kilombero, Cheju na Kinyasini | Idadi ya kilomita za mitaro zilizojengwa | 20 | 20 | 100 | Kazi hii imekamilika katika mabonde yote |
| Kazi ya Uwekaji sawa konde (Leveling) katika bonde la Cheju B | Idadi ya hekta zilizowekwa sawa | 130 | 130 | 100 | Kazi za Uwekaji sawa wa ploti *(Land Leveling)* kwa eneo lote la bonde la Cheju B zimekamilika. |
| Kujenga na kusimamia kazi ya ujenzi wa misingi ya ndani ya saruji *(Tertiary Irrigation canals)* katika | Idadi ya kilomita za misingi zilizojengwa | 15 | 20 | 133 | Kazi za ujenzi wa misingi ya ndani ya saruji (Tertiary Irrigation canals) katika mabonde yote ya Mradi |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| mabonde ya Cheju A, Kilombero, Mlemele, Kibokwa, Kinyasini, Chaani na Cheju B | | | | | imekamilika. |
| Kujenga uzio (fence) kwenye bwawa la Kinyasini na Chaani | Idadi ya mita za uzio zilizojengwa | 300 | 300 | 100 | Kazi za ujenzi wa uzio katika mabwawa ya Chaani na Kinyasini zimekamilika |
| Kujenga na kusimamia kazi ya ujenzi wa ofisi | Asilimia ya ujenzi wa ofisi iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Ujenzi wa Ofisi katika mabonde 6 ya Mradi (Cheju, Kilombero, Mlemele, Kibokwa, Kinyasini na Chaani) zimekamilika. |
| Kusimamia kazi ya Uchimbaji wa Visima katika bonde la Cheju B | Idadi ya visima vilivyochimbwa | 8 | 8 | 100 | Visima vyote vilivyochimbwa vimewekewa pampu |
| Kufanya vikao kwa ajili ya mafunzo ya usimamizi maeneo yaliyojengwa miundombinu ya umwagiliaji maji | Idadi ya vikao vilivyofanyika | 24 | 6 | 25 | Kazi hii ni endelevu katika mabonde yote, hufanyika kabla na baada ya msimu wa ukulima wa mpunga na mbogamboga |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kazi ya Uungaji wa umeme mkubwa *(high tension)* kwa visima 14 katika bonde la cheju B | Idadi ya visima vilivyoungwa umeme | 14 | 0 | 0 | Kazi ya Uungaji wa umeme ni jukumu ya Serikali kutokana Mkataba wa mradi huu. Kazi hii imeanza na inaendelea katika bonde la Cheju B |

**ii.Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo na Mifugo**

Programu hii imeanzishwa kwa lengo la kuimarisha na kuinua sekta ya kilimo na mifugo kwa wakulima na wafugaji wadogo wadogo Zanzibar. Kwa mwaka 2024/2025, Programu inatarajiwa kutekeleza miradi mitatu (3). Nayo ni:-

**a. Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Mifugo**

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2023/2024 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2025/2026. Mradi una lengo la kuwa na miundombinu yenye viwango vya kukidhi udhibiti wa maradhi ya mifugo na kusaidia kupata wanyama. Mradi utawezesha kupata ng'ombe bora wa kisasa, kuongeza uzalishaji wa mifugo na mazao yake pamoja na kusimamia, kuratibu tafiti za mifugo kwa kuimarisha miundombinu ya Taasisi za utafiti. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 2.50 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 1.38 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, shughuli zifuatazo zimetekelezwa: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ununuzi wa mtambo wa kuzalisha gesi ya Nitrogen ili kuhifadhia mbegu za madume kwa ajili ya kupandishia ng'ombe kwa njia ya sindano | Asilimia ya manunuzi iliyofikiwa | 100 | 10 | 10 | Taratibu za kununua mtambo zimekamilika fedha za Awamu ya Kwanza asilimia 20 kwaajili ya kununua mtambo huo tayari zimeombwa. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kukarabati na kujenga miundombinu ya karantini ya Kisakasaka – Unguja na Gando Nziwengi – Pemba | Idadi ya miundombinu iliyokarabatiwa | 2 | 0 | 0 | Zabuni ya Ujenzi wa Miundombinu hiyo imeshatangazwa na wakandarasi wamejitokeza na wanafanyiwa tathmini ili kupatikana wakandarasi watakaokidhi vigezo vya kujenga miundo mbinu hiyo. |
| Ujenzi wa miundombinu ya utafiti Kizimbani – maabara na mabanda ya mbuzi | Asilimia ya ujenzi wa maabara iliyofikiwa | 100 | 15 | 15 | Mkandarasi wa ujenzi wa miundombinu ameshapatikana, Mkataba wa ujenzi tayari umeshapita kwa Mwanasheria Mkuu kwa kuidhinishwa. |
| | Asilimia ya ujenzi wa mabanda ya mbuzi iliyofikiwa | 100 | 50 | 50 | Ujenzi wa mabanda ya utafiti wa mbuzi na kondoo Unguja unaendelea na umefikia hatua ya linta. Kwa Pemba uko katika hatua ya kutayarisha michoro |
| Ujenzi wa mabanda ya utafiti wa kuku | Asilimia ya ujenzi wa mabanda ya utafiti wa kuku iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Ujenzi wa banda la utafiti wa kuku Pemba uko katika hatua ya kutayarisha michoro |

### b. Mradi wa Kuendeleza Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Nyuki (BEVAC)

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2022/2023 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2026/2027. Mradi una lengo la kuimarisha sekta ya ufugaji nyuki katika ukuaji wa uchumi shirikishi nchini Tanzania na kuweza kuvuna asali kwa njia endelevu na mazingira mazuri ili iweze kuingia katika masoko ya ndani na nje ya nchi. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 500.00 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 275 milioni. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 56 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo sawa na asilimia 20 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuendelea na tafiti za nyuki | Asilimia ya utafiti iliyofikiwa | 100 | 20 | 20 | Timu ya watafiti 6 ikiongozwa na watafiti kutoka TAFORI wamekutana na kupitia maandiko ya kitafiti (Literature Review) kwa ajili ya maandalizi ya ukusanyaji wa taarifa za nyuki wadogo |
| Kufanya Mapitio ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali Misitu (1996) | Asilimia ya mapitio ya Sheria iliyofikiwa | 100 | 30 | 30 | Rasimu ya Sheria ya Usimamizi na Uhifadhi wa Rasilimali Misitu (2025) imetengenezwa na wataalamu wa sekta ya Maliasili kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Rasimu hii inategemewa kupata maoni ya wadau baada ya kutafsiriwa mwezi Aprili 2025. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kujenga na Kuimarisha Skuli ya Kilimo (SOA) ili kuweza kutoa mafunzo ya vitendo ya uzalishaji wa asali na upatikanaji wa masoko | Idadi ya skuli ya kilimo iliyojengwa | 1 | 1 | 100 | Shamba darasa (Manzuki) kwa ajili ya mafunzo ya ufugaji nyuki limejengwa na kuanza kutumika katika Skuli ya Kilimo – Kizimbani. Hii ni muendelezo wa kuimarisha taasisi za elimu na utoaji wa elimu ya ugani kwa wafugaji nyuki wa Zanzibar |
| Kutayarisha Muongozo wa Ufundishaji (Training Manual) wa Somo la Ufugaji Nyuki (PS 2406) | Asilimia ya utayarishaji wa muongozo wa Ufundishaji iliyofikiwa | 100 | 25 | 25 | Muongozo wa Ufundishaji (Training Manual) wa Somo la Ufugaji Nyuki (Principles of Beekeeping - PS 2406) umetayarishwa na kuwasilishwa katika Kamati ya Uongozi ya Chuo |
| Kuandaa Makala (Video Documentary) kwa ajili ya Kuendeleza uwekaji na usambazaji wa taarifa za utekelezaji wa mradi | Idadi ya Makala iliyoandaliwa | 1 | 1 | 100 | Makala ya kazi za mradi katika maeneo na wadau wa mradi imeandaliwa. |
| Kutoa mafunzo ya ufugaji bora wa nyuki | Idadi ya wafugaji nyuki waliopatiwa mafunzo | 1000 | 400 | 40 | Wafugaji nyuki wamepatiwa mafunzo ya ufugaji nyuki bora kutoka kwa maafisa misitu wa Wilaya 4 za Pemba. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kutoa mafunzo kwa mafundi nguo juu ya ushonaji wa mavazi kinga ya nyuki | Idadi ya Mafundi nguo waliopatiwa mafunzo | 30 | 30 | 100 | Mafundi nguo 30 wamepatiwa mafunzo ya ushonaji mavazi kinga ya nyuki katika vituo vya Mafunzo ya Amali Daya na Vitongoji. |
| Ugawaji wa mizinga ya kisasa kwa wafugaji nyuki | Idadi ya Mizinga ya kufugia nyuki iliyotolewa | 200 | 200 | 100 | Mizinga ya kufugia nyuki 200 imetolewa kwa vikundi 23 vya wafugaji nyuki. Vikundi 6 Wete, 5 Micheweni, 7 Chake Chake na 5 Mkoani |
| BEVAC Kushiriki Maonesho ya Siku ya Chakula katika viwanja vya maonesho Chamanangwe Pemba | Idadi ya maonesho waliyoshiriki | 1 | 1 | 100 | BEVAC ikishirikiana na Idara ya Misitu Pemba na Jumuiya ya Wafugaji Nyuki Pemba (PEBA) ilishiriki katika maonesho ya Siku ya Chakula Duniani yaliyofanyika viwanja vya Chamanangwe wilaya ya Wete tarehe 07-16/10/2024. |
| Kutayarisha Mikataba ya makubaliano ya matumizi ya Misitu ya Jamii Kuanzisha Hifadhi za Nyuki katika Misitu ya Jamii | Idadi ya Mikataba iliyotayarishwa | 7 | 5 | 71 | Mikataba ya makubaliano mitano (5) kati ya saba (7) kwa Misitu ya Jamii imetayarishwa kwa ajili ya hatua za kisheria. Misitu hiyo ya jamii ni Mwambe Chaleni, Mjini Wingwi, Shanake, Mtambwe, Kiungoni, Wambaa na Vikunguni. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya Mapitio ya Sera ya Rasilimali Misitu | Asilimia ya mapitio iliyofanyika | 100 | 70 | 70 | Rasimu ya Sera ya Rasilimali Misitu imetengenezwa na kutafsiriwa kwa Kiswahili. Rasimu hii imeshapitiwa na wadau wa Sekta ya Misitu wa Unguja na Pemba Pamoja na Kamati ya Wataalamu na Uongozi wa Wizara. |
| Kutoa muongozo wa ufundishaji wa masomo ya ufugaji nyuki | Asilimia ya utayarishaji wa muongozo iliyofikiwa | 100 | 90 | 90 | Muongozo wa Ufundishaji (Training Manual) wa Somo la Ufugaji Nyuki (Principles of Beekeeping - PS 2406) umetayarishwa na kuwasilishwa katika Kamati ya Uongozi ya Chuo kwa mapendekezo |

**c. Mradi wa Kilimo Tija**

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuendeleza fursa za kiuchumi na kuimarisha mifumo ya masoko kwa mazao ya mboga mboga na matunda, hasa kwa vijana ili kuongeza fursa za ajira. Mradi unahamasisha wajasiriamali kutumia teknolojia za kilimo zinazozingatia mabadiliko ya mazingira na tabianchi. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 3.44 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 1.9 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 949 milioni sawa na asilimia 50 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuimarisha uwezo wa mabwana shamba pamoja na kushajiisha wadau zaidi wa ugani | Idadi ya mabwanashamba waliopatiwa mafunzo | 180 | 169 | 93.8 | Maafisa ugani wa Serikali walinufaika na mfunzo haya |
| Kuhimiza upatikanaji na matumizi ya teknolojia za kilimo zinazozingatia mabadiliko ya tabianchi na kuongeza tija ili kuhakikisha kuwepo kwa uzalishaji wa mazao mwaka mzima huku ikisaidia wakulima kufikia masoko | Idadi ya washiriki waliopatiwa mafunzo ya teknolojia | 4,000 | 3,489 | 87.2 | Mafunzo ya Mabadiliko tabianchi yametolewa. |
| Kuwajengea uwezo mabaraza ya vijana katika ngazi ya Wilaya juu ya uzalishaji wa mazao ya kilimo pamoja na kuendeleza biashara katika minyororo ya thamani. | Idadi ya vijana waliopatiwa mafunzo | 1,590 | 1,447 | 91 | Kuwaimarisha vijana katika maeneo tofauti ikiwepo ajira, usimamizi wa fedha, uwekezaji, mauzo pamoja na kuwainua vijana walioko kwenye mnyororo wa thamani kwenye kilimo cha mboga mboga na matunda |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kusaidia jitihada za sekta binafsi katika kuwawezesha wakulima na wadau wengine katika mnyororo wa thamani kufikia mitaji itakayosaidia biashara zao | Idadi ya wanufaika waliopata mitaji | 185 | 181 | 97.8 | Jumla ya Mikopo 181 yenye thamani ya TZS 325.66 milioni imetolewa |
| Kushirikiana na sekta binafsi katika kusaidia kuandaa ramani ya udongo ya Zanzibar na kuwawezesha wakulima na wadau wengine katika mnyororo wa thamani kufikia mitaji itakayosaidia biashara zao | Idadi ya ramani zilizoandaliwa | 3 | 3 | 100 | |
| Kusaidia kuimarisha vikundi vya ushirika vya mboga na matunda Zanzibar katika maeneo ya uzalishaji, utawala bora na upatikanaji wa mitaji | Idadi ya vikundi vya ushirika vilivyoimarishwa | 30 | 51 | 170 | |

### iii. Programu ya Kudhibiti Maradhi na Upotevu wa Mazao

Programu hii imeanzishwa kwa lengo la kupunguza upotevu wa mazao ya kilimo ili kuongeza upatikanaji wa chakula kwa wakulima na wananchi nchini. Kwa mwaka 2024/2025, Programu inatarajiwa kutekeleza miradi mitatu (3) nayo ni:

#### a) Mradi wa Kupambana na Sumu Kuvu Tanzania (TANIPAC)

Mradi umeanza mwaka 2019 na unatarajia kukamilika 2025, Mradi una lengo la kupunguza athari zinazotokana na sumukuvu katika mahindi na njugu nyasa. Mradi umepanga kutoa taaluma na kuimarisha miundombinu na teknolojia ya uhifadhi kabla na baada ya mavuno. Mradi unatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Zanzibar na Tanzania Bara. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 203.09 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 111 milioni. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 119 sawa na asilimia 107 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuendelea na udhamini wa wanafunzi wa Shahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamivu | Idadi ya wanafunzi waliodhaminiwa | 3 | 3 | 100 | Wanafunzi wanarajiwa kuhitimu mwaka 2024/25 |
| Kuendelea na shughuli za kutoa elimu ya sumu kuvu kwa wadau | Idadi ya makundi yaliyopatiwa elimu ya sumukuvu | 3 | 3 | 100 | Elimu imetolewa kwa wakulima, wafanyabiashara na wataalamu wengine wa Kilimo |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kushiriki katika maonesho ya Kitaifa | Idadi ya maonesho waliyoshiriki | 2 | 2 | 100 | Mradi uliwezesha ushiriki katika maonesho ya Kilimo Nane nane Kizimbani Unguja na maonesho ya siku ya chakula Duniani Chamanangwe Pemba |
| Ununuzi wa vifaa kwa ajili ya maghala Kizimbani Unguja na Ole Dodeani Pemba | Idadi ya vifaa vilivyonunuliwa | 12 | 12 | 100 | |
| Kuandaa ripoti juu ya Usimamizi na Uendeshaji wa mradi | Idadi ya Ripoti zilizoandaliwa | 2 | 2 | 100 | |

**b) Mradi wa Kuimarisha Huduma za Afya ya Mimea kwa Usalama wa Chakula (Strengthen Plant Heath Service in Tanzania)**

Mradi huu umeanzishwa mwaka Novemba 2021na unatarajiwa kukamilika mwaka 2024/2025. Mradi una lengo la kuimarisha mfumo wa udhibiti uingizaji na usafirishaji wa mazao ya kilimo kwa kuongeza upatikanaji wa mazao ya kilimo yanayokidhi viwango vya Kitaifa na Kimataifa pamoja na afya ya mimea. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 4.08 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 2.24 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 941 milioni sawa na asilimia 42 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya ukarabati wa majengo ya maabara za ZARI zilizopo Kizimbani kwa Unguja na Matangatuani kwa Pemba | Asilimia ya ukarabati uliofanyika | 100 | 5 | 5 | Mshauri elekezi ameanza kazi ya kusarifu michoro ya majengo ya maabara hizo. |
| Kuwajengea uwezo wakulima juu ya njia za kilimo kwa kutumia teknolojia ya kilimo biashara na udhibiti wa upotevu wa mazao baada ya mavuno | Idadi ya wakulima waliojengewa uwezo | 400 | 400 | 100 | Shughuli hii imetekelezwa kwa mafunzo ya mbinu bora za uzalishaji, na teknolojia ya Kilimo Shadidi cha Mpunga (System of Rice Intensification). |
| Kufanya ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji kwa kutumia njia zilizochimbwa kutokea katika visima katika eneo la hekari 434 kwa mabonde ya Bumbwisudi, Mtwango, Kibokwa, Mwera kwa Unguja na Makombeni, Weni, Saninga na Kinyakuzi kwa Pemba; na | Asilimia ya ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji iliofikiwa | 100 | 5 | 5 | Utaratibu wa kumpata Mshauri Elekezi wa michoro unaendelea. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kukarabati maabara za wadudu na kuwajengea uwezo wataalamu watakaoendesha shughuli za maabara Unguja na Pemba | Idadi ya maabara zilizokarabatiwa. | 5 | 0 | 0 | Mchakato wa ukarabati wa maabara umeshaanza kwa kutoa zabuni kwa wakandarasi. |
| | Idadi ya wataalamu wa maabara waliopatiwa mafunzo | 10 | 5 | 50 | Mafunzo ya siku tano juu ya Viwango vya Kimataifa vya Usalama wa Chakula yalifanyika |

### c) Mradi wa Kuwaunganisha Wakulima wa Mboga na Matunda (AGRICONNECT)

Mradi huu umeanza mwaka 2019/20 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2024/2025. Mradi una lengo la kusaidia upatikanaji wa Sera zitakazoweka mazingira wezeshi na kuongeza uwekezaji wa Sekta Binafsi, kukuza minyororo ya thamani kwa kuongeza uzalishaji, usindikaji, uuzaji na kuwaunganisha wakulima na masoko. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 2.83 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 1.56 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 1.57 bilioni sawa na asilimia 101 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuwajengea uwezo wakulima hasa wanawake kupata na kutumia vyakula vyenye lishe bora ambavyo vinazingatia mfumo wa kilimo kinachoendana na mabadiliko ya tabia ya nchi | Idadi ya wakulima waliojengewa uwezo | 400 | 302 | 75.5 | Wizara ilitembelea maeneo mbali mbali ya kilimo cha mbogamboga, Matunda na Viungo mbalimbali pamoja na kutembelea miundombinu ambayo imejengwa na mradi kama vikaushio vya kutumia jua, *cold room* na wakulima ambao walifikishiwa miundo mbinu ya maji. |
| Kugawa mifuko ya kuhifadhia mazao *(Purdue Improved Crop Storages*) kwa wakulima na vikundi vya wakulima kwa ajili ya kupunguza uharibifu baada ya kuvuna | Idadi ya wakulima waliopatiwa vihifadhia mazao | 116 | 116 | 100 | Vikundi 10 vya wakulima wa mazao ya viungo na mboga mboga walipatiwa vihifadhia mazao |
| Kuwapatia mitaji wajasiriamali na wakulima wadogo wadogo wa vikundi 45 ili kuendeleza miradi ya kilimo cha mboga mboga (horticulture) pamoja na usindikaji | Idadi ya wajasiriamali waliopatiwa mitaji | 200 | 62 | 31 | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuendeleza mifumo ya kusambaza taarifa za masoko na elimu kwa wadau wa mazao ya bustani. | Idadi ya mifumo ya usambazaji wa taarifa iliyokamilishwa | 3 | 3 | 100 | |

### a. Mradi wa Ukarabati wa Maghala na Uhifadhi wa Chakula

Mradi huu umeanza mwaka 2023/2024 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2025/2026, una lengo la kuwezesha upatikanaji wa chakula katika ngazi ya Kaya na Taifa kwa kuimarisha maghala ya uhifadhi wa chakula. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 27.50 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 15.13 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 330 milioni sawa na asilimia 2 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuanza ujenzi wa maghala ya kuhifadhia chakula (silos) eneo la Bungi kwa Unguja na Chamanangwe kwa Pemba | Asilimia ya ujenzi iliofikiwa | 100 | 5 | 5 | **Ujenzi uko hatua za kukamilisha nyaraka za kumpata Mkandarasi** |
| Ukarabati wa maghala tisa (9) Saateni, Kilombero na Donge kwa Unguja Dodeani, Weni, Mkoani, Kizimbani (2) na Wete kwa Pemba. | Idadi ya maghala yaliokarabatiwa | 9 | 9 | 100 | Ukarabati wa Maghala unaendelea kwa hatua tofauti |
| Kununua chakula cha akiba. | Idadi ya tani za Mpunga zilizonunuliwa | 100,000 | 0 | 0 | Mkataba wa Makubaliano baina ya Wizara na Wakala wa Uhifadhi wa Chakula (*National Food Reserve Agency)* kwa ajili ya ununuzi wa nafaka tayari umesainiwa. Mchakato wa kufanya makubaliano ya ununuaji wa mpunga kutoka Tanzania Bara yamefikiwa. |
| | Idadi ya tani za Mahindi zilizonunuliwa | 30,000 | 0 | 0 | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa vihenge Unguja na Pemba. | Asilimia ya ujenzi iliofikiwa | 100 | 5 | 5 | Mkandarasi wa kujenga Vihenge vyenye ujazo wa tani 40,000 MT kwa Unguja na 20,000 MT kwa Pemba amepatikana. |

**b.Mradi wa Mageuzi ya Uzalishaji wa Maziwa kwa Wafugaji Wadogo Unaozingatia Mabadiliko ya Tabianchi (C-STDTP)**

Mradi umeanzishwa kwa lengo la kuleta mageuzi kwenye mnyororo wa thamani wa uzalishaji wa maziwa kwa ajili ya kukuza hali ya maisha kwa jamii, kuongeza uhakika wa chakula. Mradi unatekelezwa kwa kuzingatia athari za mabadiliko ya tabia nchi katika sekta ya ufugaji wa ng'ombe wa maziwa. Mradi utasaidia kukuza kipato, kuongeza lishe kwa wazalishaji wadogo wadogo wa maziwa na uhimilivu wa tabianchi. Kwa mwaka 2024/2025 mradi umepangiwa jumla ya TZS 7.5 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (IFAD/OPEC). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 4.13 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, hakuna fedha iliyotolewa.

**c. Mradi wa Uhimilivu wa Mifumo ya Chakula Tanzania (TFSRP)**

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2023/24 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2027/28. Mradi una lengo la kupata uhimilivu wa mfumo wa chakula kwa kuimarisha utoaji wa huduma za kilimo, kupitisha teknolojia za kilimo zinazohimili mabadiliko ya tabianchi pamoja na kujenga uwezo wa uhimilivu katika mazao ya chakula. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 18.75 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 10.31 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 10.19 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo sawa na asilimia 99 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya ukarabati wa majengo ya maabara za ZARI zilizopo Kizimbani kwa Unguja na Matangatuani kwa Pemba | Asilimia ya ukarabati uliofanyika | 100 | 5 | 5 | Mshauri elekezi ameanza kazi ya kusarifu michoro ya majengo ya maabara hizo. |
| Kuwajengea uwezo wakulima juu ya njia za kilimo kwa kutumia teknolojia ya kilimo biashara na udhibiti wa upotevu wa mazao baada ya mavuno | Idadi ya wakulima waliojengewa uwezo | 400 | 400 | 100 | Shughuli hii imetekelezwa kwa mafunzo ya mbinu bora za uzalishaji, na teknolojia ya Kilimo Shadidi cha Mpunga (System of Rice Intensification). |
| Kufanya ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji kwa kutumia njia zilizochimbwa kutokea katika visima katika eneo la hekari 434 kwa mabonde ya Bumbwisudi, Mtwango, Kibokwa, Mwera kwa Unguja na Makombeni, Weni, Saninga na Kinyakuzi kwa Pemba; na | Asilimia ya ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji iliofikiwa | 100 | 5 | 5 | Utaratibu wa kumpata Mshauri Elekezi wa michoro unaendelea. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Ununuzi wa vifaa kwa ajili ya kuwafundishia vijana kutoa huduma mashambani, ikiwemo trekta ndogo ndogo za kulimia, kupandia, kupalilia na kuvunia | Asilimia ya manunuzi iliofikiwa | 100 | 5 | 5 | Utaratibu wa kumpata Mshauri elekezi unaendelea baada ya kupokea na kuyafanyia kazi maoni ya Mwanasheria Mkuu |

**d. Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Chakula kwa Kuongeza Tija na Uzalishaji Kupitia Huduma za Kisasa za Kilimo Katika Umwagiliaji**

Mradi umeanzishwa kwa lengo la kuchangia uimarishaji wa uhakika wa chakula na kuongeza kiwango cha kipato kwa wakulima wa mpunga Zanzibar pamoja na kuongeza tija ya mpunga katika mashamba ya umwagiliaji. Kwa mwaka 2024/2025, mradi umepangiwa jumla ya TZS 1.50 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 825 milioni. Hadi kufikia Machi 2025, hakuna fedha iliyoingizwa.

**e. Mradi wa Kuendeleza Mifumo ya Chakula, Matumizi na Urejesheaji wa Ardhi**

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2024/25 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2027/28. Mradi una lengo la kurejeshea uoto wa asili katika maeneo yaliyochimbwa maliasili zisizorejesheka. Pia unajikita katika kuhifadhi misitu katika maeneo ya Kaskazini ‘A’ na ‘B’, kushirikisha sekta za kilimo, mazingira, ardhi na sekta nyengine zenye mnasaba pamoja na uhifadhi wa misitu na kusimamia rasilimali hiyo.

Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 682.80 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 375 milioni. Hadi kufikia Machi 2025, Jumla ya TZS 52 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo sawa na asilimia 14 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kukarabati majengo ya vituo vya wakulima Kaskazini Unguja | Asilimia ya ukarabati iliofikiwa | 100 | 15 | 15 | Kazi ya ukarabati inaendelea |
| Kuhamasisha juu ya kutunza mazingira, kupanda miti, uoto wa kuzuia uharibifu wa mazingira kwa jamii zinazozunguka Wilaya za Kaskazini A na B | Asilimia ya kazi ya uhamasishwaji iliofikiwa | 100 | 0 | 0 | |
| Kutoa elimu juu ya uhifadhi wa misitu | Idadi ya vikundi vilivyoelimishwa | 40 | 10 | 25 | |

### 11.2.14 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

Wizara hii imeanzishwa kwa lengo la kuimarisha ustawi wa jamii kwa kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za jamii, wazee na watoto ili kuwa na Maisha ya staha, sambamba na kushughulikia maendeleo ya kijamii na kuleta usawa wa kijinsia. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara imepanga kutekeleza miradi minne ya maendeleo.

**a. Mradi wa Hifadhi ya Wazee**

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2023/24 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2024/25 Mradi una lengo la kukuza ustawi wa wazee kwa kuimarisha usalama wao, kuhakikisha wanaishi katika makaazi mazuri na wanapata huduma zao za msingi. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 4.50 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025 mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 2.48 bilioni kutoka Serikalini. Hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya TZS 1.56 bilioni sawa na asilimia 63 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa jiko katika nyumba za wazee Sebleni na Limbani | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa kwa jiko la Limbani. | 100 | 70 | 70 | Ujenzi unaendelea |
| | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa kwa jiko la Sebleni. | 100 | 10 | 10 | Hatua za maandalizi ya awali zimekamilika na kazi ya ujenzi inategemewa kuanza robo ya nne |
| Ujenzi wa ukuta wa nyumba za wazee Limbani | Asilimia ya ujenzi uliyofikiwa | 100 | 95 | 95 | Ujenzi wa ukuta umeshamaliza na hatua iliyobakia ni waya wa ulinzi (electric fence) na kuweka geti |
| Kufanya ukarabati katika makaazi ya wazee Limbani – Pemba na Sebleni – Unguja | Asilimia ya ukarabati iliyofanyika-Limbani | 100 | 80 | 80 | Hatua ya umaliziaji inaendelea kwa kuweka milango na kupaka rangi |
| | Asilimia ya ukarabati iliyofanyika –Sebleni | 100 | 98 | 98 | Ukarabati umekamilika kazi inayoendelea ni kazi ya usafi kwa ajili ya kusafisha jengo |
| Ununuzi wa vifaa na samani. | Asilimia ya manunuzi iliyofikiwa. | 100 | 50 | 50 | Hatua za kumtafuta mzabuni wa ununuzi wa samani zimekamilika |

**b. Mapambano Dhidi ya Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji kwa Wanawake na Wasichana**

Mradi huu umeanzishwa mwaka na 2023/2024 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2028/2029. Mradi una lengo la kumaliza vitendo vya udhalilishaji kwa wanawake na wasichana. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 536.00 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 294 milioni. Hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya TZS 103 milioni sawa na asilimia 35 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi cha robo ya kwanza imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo:

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuandaa Sera ya Maendeleo ya Jamii | Asilimia ya sera iliyoandaliwa | 100 | 75 | 75 | Rasimu ya awali ya sera ya maendeleo ya Jamii imeshatayarishwa |
| Kuandaa Mpango Mkakati wa kupambana na ukatili na udhalilishaji | Asilimia ya mpango Mkakati uliyoandaliwa | 100 | 100 | 100 | Mpango wa Kitaifa wa kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji umekamilika na kuzinduliwa |
| Kufanya uhamasishaji wa Vikundi vya Wanajamii vinavyojishughulisha na mapambano dhidi ya Vitendo vya Udhalilishaji | Idadi ya vikundi vilivyohamasishwa | 57 | 26 | 46 | Vikundi hivyo vipo katika Wilaya ya Kusini Unguja na Mkoani Pemba Wilaya ambazo zinanufaika na mradi huo. |

### c. Mradi wa Kusimamia Sheria ya Jinsia na Sera

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2002 na una lengo la kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji kwa wanawake na Watoto ni mradi endelevu. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 208.00 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025 mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 114 milioni. Hadi kufikia Machi, 2025 hakuna fedha iliyoingizwa, hata hivyo shughuli zifuatazo zimefanyika: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya tathmini ya vituo vya mkono kwa mkono | Asilimia ya tathmini iliyofanyika | 100 | 100 | 100 | Mkutano wa kupokea taarifa ya Awali iliyowasilishwa na Mshauri Elekezi umefanyika. Tathmini imekamilika |
| Kuandaa mkutano wa kuhamasisha wanawake juu ya haki na wajibu wao. | Idadi ya mikutano ya uhamasishaji iliyofanyika | 2 | 2 | 100 | Mikutano 2 iliyofanyika kwa Unguja na Pemba ambapo wanawake, wasichana na watu wenye ulemavu walipata nafasi ya kufahamu haki zao pamoja na Sheria zitakazowasaidia kufanya kazi zao kwa uweledi zaidi |

**d.Mradi wa Hifadhi ya Mtoto**

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2010 kwa lengo la kuimarisha Mfumo wa hifadhi ya mtoto katika maeneo ya Mazingira wezeshi (enabling environment), kinga (prevention) na muitiko (reaction) katika masuala yote ya hifadhi ya mtoto. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya 536.00 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 294.8 milioni. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 57 milioni sawa na asilimia 19 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya kikao cha wataalamu kutoka taasisi zinazoshughulikia watoto kupitia zana za kufundishia watoto, wazazi na walimu kuhusu udhalilishaji wa watoto kwa njia ya mtandao. | Idadi ya zana zilizopitiwa | 1 | 1 | 100 | Ujumbe kuhusu udhalilishaji wa watoto kupitia mtandao ulitengenezwa na timu ya wadau kwa ajili ya kusambazwa kwa watoto na jamii. Jumla ya wadau 20 kutoka taasisi za serikali na binafsi walishiriki kwenye mapitio ya dhana hii kwa ajili ya watoto na kwa ajili ya wazazi na walimu |
| | Idadi ya vikao vilivyofanyika | 1 | 1 | 100 | |
| | Idadi ya washiriki walioshiriki | 20 | 20 | 100 | |
| Kuwajengea uwezo maafisa ustawi wa jamii wa mpango wa marekebisho ya tabia, wanasihi wa kituo cha elimu mbadala na maofisa wa Mahkama | Idadi ya maafisa waliojengewa uwezo | 10 | 10 | 100 | Maofisa ustawi wa jamii wawili wanaosimamia mpango na wanasihi (counsellor) watano kutoka kituo cha elimu Mbadala Rahaleo wanaosaidia kurekebisha tabia za watoto |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| kuhusu mpango wa marekebisho ya tabia kwa watoto wanaokinzana na Sheria | | | | | wanaokinzana na Sheria na maafisa 3 wanaotoa huduma ya kiustawi kwenye Mahkama za watoto walishiriki mafunzo hayo |
| Kufanya mafunzo ya hifadhi ya mtoto na mradi wa kurekebisha tabia kwa uongozi na walimu wanaotoa ujuzi kwa watoto wanaokinzana na | Idadi ya walimu na viongozi waliopatiwa mafunzo | 29 | 29 | 100 | Viongozi na walimu 29 wa kituo cha Elimu mbadala cha Rahaleo walijengewa uwezo kuhusu mpango wa kurekebisha tabia kutokana na ushiriki wao katika kuwapokea watoto hao na |
| Sheria wa Kituo cha Elimu mbadala Rahaleo | | | | | kuwapatia ujuzi ukiwemo wa lugha, kompyuta na huduma ya unasihi. Viongozi na walimu 29 kutoka kituo cha elimu Mbadala Rahaleo wanaosaidia kurekebisha tabia za watoto wanaokinzana na Sheria walishiriki mafunzo hayo |
| Kuandaa kikao cha taasisi za rufaa za watoto wanaokinzana na Sheria kwenye mpango wa kurekebisha tabia | Idadi ya washiriki waliohudhuria kikao | 25 | 25 | 100 | Jumla ya washiriki 25 kutoka Mahkama za watoto kwa Mikoa mitatu ya Unguja, Madawati ya Polisi ya Mikoa, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, maofisa |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ustawi wa Jamii na taasisi za msaada wa kisheria walishiriki kikao hicho. |
| Kufanya mafunzo ya mpango wa marekebisho ya tabia kwa maofisa ustawi wa jamii wa ngazi ya Taifa na Mikoa ya Unguja | Idadi ya maofisa wa ustawi wa jamii walioshiriki mafunzo | 21 | 21 | 100 | Jumla ya maofisa ustawi wa jamii 21 wa Mikoa na Taifa walipatiwa mafunzo kuhusu watoto wanaokinzana na Sheria na mpango wa marekebisho ya tabia na utekelezaji wake pamoja na majukumu yao Maofisa wa mikoa mitatu ya Unguja na maofisa ustawi wa jamii wa Idara ya Ustawi wa Jamii walishiriki mafunzo hayo. |
| Kufanya mafunzo ya mpango wa marekebisho ya tabia kwa maofisa ustawi wa jamii wa ngazi ya Wilaya kwa Wilaya zote za Unguja | Idadi ya maafisa ustawi wa jamii wa Wilaya waliopatiwa mafunzo. | 28 | 28 | 100 | Jumla ya Maofisa 28 wa ustawi wa jamii na Maendeleo ya jamii katika Wilaya 7 za Unguja walipatiwa mafunzo kuhusu watoto wanaokinzana na Sheria na mpango wa marekebisho ya tabia na utekelezaji wake pamoja na majukumu yake. . Maofisa ustawi wa jamii na maendeleo ya Jamii wa |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Wilaya ambao wanafanya tathmini za watoto wanaokinzana na Sheria wanapokamatwa polisi kabla ya kufikishwa mahkamani |
| Kufanya mafunzo ya wakufunzi wa Kitini cha hifadhi ya Mtoto | Idadi ya wakufunzi waliopatiwa mafunzo | 17 | 17 | 100 | Wakufunzi 17 kutoka Idara ya Ustawi wa Jamii walipatiwa mafunzo juu ya kitini na moduli zake kitakachotumika kufundishia wadau wanaohusika na watoto |
| Kufanya mafunzo ya hifadhi ya mtoto kwa maofisa ustawi wa Jamii wa Wilaya na | Idadi ya maofisa wa ustawi wa jamii na maendeleo waliopatiwa mafunzo | 30 | 30 | 100 | Maafisa ustawi wa jamii na maafisa maendeleo ya jamii 30 kutoka Wilaya zote za Unguja walipatiwa mafunzo |
| ngazi ya Taifa kwa kutumia kitini cha hifadhi ya mtoto. | | | | | ya hifadhi ya mtoto kwa kutumia kitini. Mafunzo hayo yalijumuisha ujuzi wa msingi katika kushughulika na masuala ya hifadhi ya mtoto pamoja na usimamizi wa mashauri ya yanayohusu ukiukwaji wa haki za mtoto na jinsi ya kushughulikia mashauri hayo. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuandaa kikao cha kufanya mapitio ya mwisho ya makubaliano ya kushughulikia kesi za watoto baina ya Idara ya Ustawi wa Jamii na Polisi | Idadi ya washiriki walihudhuria | 17 | 17 | 100 | Washiriki 17 kutoka makao makuu ya polisi, Mahakimu wa Mahkama za Watoto Unguja na Pemba, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashataka na maofisa ustawi wa Jamii walishiriki kupitia makubaliano hayo ambayo utekelezaji wake unategemeana baina ya polisi na taasisi nyengine za mfumo wa haki jinai |
| Kuandaa kikao cha robo mwaka cha maafisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya na Mikoa kujadili maendeleo ya utekelezaji wa mfumo wa kuhifadhia taarifa wa hifadhi ya mtoto wa PRIMERO | Idadi ya washiriki waliohudhuria | 33 | 33 | 100 | Washiriki 33 wakiwemo maafisa Ustawi wa jamii, maofisa maendeleo ya jamii wanaosimamia kesi za watoto kutoka Wilaya 7 za Unguja, maafisa kutoka Idara ya Ustawi wa Jamii na wasimamizi wa mfumo wa PRIMERO (IT) kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii walishiriki kikao hicho. Kikao cha kujadili maendeleo ya mfumo wa PRIMERO, na changamoto kinafanyika kila robo mwaka |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | kwa wasimamizi wa mashauri na watiaji wa taarifa kwenye mfumo. |
| Kuandaa kikao cha robo Mwaka cha wasimamizi wa mfumo wa kuhifadhia taarifa za watoto Wilaya na Mikoa kujadili maendeleo ya utekelezaji wa mfumo wa kuhifadhia taarifa za mtoto wa PRIMERO | Idadi ya washiriki waliohudhuria | 35 | 35 | 100 | Jumla ya wanakamati 35 kutoka taasisi zinazosimamia mifumo ya serikali na wadau wa watoto walishiriki kikao hicho cha robo mwaka ili kupokea taarifa ya maendeleo na utekelezaji wa mfumo wa hifadhi ya mtoto wa PRIMERO.<br><br>Washiriki wa Kamati hiyo ni wa ngazi ya Wakurugenzi na Viongozi wengine |

### 11.2.15 Wizara ya Maji, Nishati na Madini

Wizara hii inajumuisha sekta kuu tatu ambazo ni sekta ya Maji, Nishati na Madini, sekta zote hizi ni nyenzo muhimu katika maendeleo ya nchi na wananchi wa Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara imepanga kutekeleza programu mbili zitazogharimu kiasi cha TZS 365.88 bilioni (TZS 80.50 bilioni kutoka Serikalini na TZS 285.38 bilioni ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

**a.Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar**

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha miundombinu ya usambazaji maji safi na salama katika maeneo ya Wilaya ya Magharibi "A", (Mfenesini, Masingini na Kizimbani) Magharibi "B" (Dimani na Kidutani) na Wilaya ya Kati (Jumbi- Mkorogo) pamoja na ujenzi wa jengo jipya la Ofisi ya Mamlaka ya Maji Zanzibar. Vile vile, kusaidia kuondoa tatizo la maji na wananchi kupata maji safi na salama. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 33.20 bilioni (TZS 10.15 bilioni kutoka Serikalini na TZS 23.05 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 18.26 bilioni (TZS 5.58 bilioni kutoka Serikalini na TZS 12.67 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 21.46 bilioni (TZS 3.33 bilioni kutoka Serikalini na TZS 18.12 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) sawa na asilimia 118 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuratibu vikao vya Kamati Kiongozi na Kamati ya Wataalamu. | Idadi ya vikao vilivyoratibiwa | 9 | 9 | 100 | |
| Malipo kwa ajili ya uangalizi wa mradi (*Defect Liability Period*). | Asilimia ya malipo iliyofanyika | 100 | 90 | 90 | |

**b.Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji Huduma za Usambazaji Maji Safi na Usafi wa Mazingira Zanzibar**

Mradi una lengo la kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama Zanzibar ili kufanikisha malengo yalioainishwa katika mikakati ya Serikali. Utekelezaji wa shughuli za mradi huu utahusisha Serikali pamoja na Washirika wa Maendeleo. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa jumla ya TZS 16.32 bilioni (TZS 2.85 bilioni kutoka Serikalini na TZS 13.46 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 8.97 bilioni (TZS 1.56 bilioni kutoka Serikalini na TZS 7.40 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 2.60 bilioni kutoka Serikalini sawa na asilimia 29 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na shughuli iliofanyika ni kumtafuta Mshauri Elekezi kwa ajili ya uratibu wa mradi.

**c. Mradi wa Uimarishaji wa Huduma za Usambazaji Maji Safi na Salama Zanzibar**

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha miundombinu ya maji kwa kufanya usambazaji na uzalishaji wa maji safi na salama katika maeneo ya visiwa vya Zanzibar. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 30.50 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 16.77 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 2.46 bilioni sawa na asilimia 14 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ulipaji wa fidia za vipando na majengo katika maeneo ya uimarishaji wa miundombinu ya maji (Maeneo yenye visima vya Ras al- Khaimah) | Asilimia ya kazi ya ulipaji fidia iliofikiwa | 100 | 5 | 5 | Uhakiki wa malipo ya fidia kwa maeneo haya umekamilka. |

**d.Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maji Mkoa wa Mjini Magharibi (ZUWDIFP)**

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa maji katika maeneo ya Mkoa wa Mjini Magharibi ili kupunguza changamoto za upatikanaji wa huduma hiyo. Mradi utatekelezwa katika maeneo ya Welezo juu, Welezo Magharibi na Migombani. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 3.37 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 1.85 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 1.37 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo sawa na asilimia 74 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuandaa taarifa ya kina ya kitaalamu (details design) ya mradi | Asilimia ya taarifa iliyoandaliwa | 100 | 90 | 90 | Taarifa ya Kitaalamu imekamilika na kuwasilishwa Mamlaka ya Maji |
| Kuandaa mpango na utaratibu wa manunuzi kwa ajli ya kupata Mkandarasi | Asilimia ya mpango na utaratibu wa manunuzi ulioandaliwa | 100 | 50 | 50 | Kazi ya utaratibu wa manunuzi kwa ajili ya kupata Mkandarasi inaendelea. |
| Kufanya tathmini kwa ajili ya kumtafuta Mkandarasi | Asilimia ya tathmini iliyofanyika | 100 | 0 | 0 | Kazi itafanyika baada ya kumpata Mkandarasi |
| Kuandaa Mikataba kwa ajili ya Mkandarasi | Asilimia ya Mikataba iliyoandaliwa | 100 | 50 | 50 | Andiko la zabuni limeshaandaliwa na kuwasilishwa JICA kwa mapendekezo ya kuandaa Mkataba |

**e.Mradi wa Usalama wa Maji na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi Mijini**

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuijengea uwezo sekta ya maji juu ya usimamiaji wa usalama na upatikanaji wa maji nchini. Vile vile, umelenga kutekeleza maeneo makuu matatu (3) ambayo ni kusaidia Wizara ya Maji, Nishati na Madini katika usimamizi wa mikakati na miongozo ya mageuzi, kuanzisha mfumo jumuishi wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na uchafuzi wa kimazingira na kuijengea uwezo Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) ili iweze kujiendesha kibiashara. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 2.67 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 39.15 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, shughuli zifuatazo zimetekekelezwa: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kusimamia na kuandaa utekelezaji wa Sera na Miongozo inayohusiana na sekta ya maji safi na usafi wa mazingira | Asilimia ya Sera na miongozo iliyoandaliwa | 100 | 10 | 10 | Hatua ya kumpata Mshauri elekezi kwa ajili ya kuandaa mikakati ya utekelezaji wa sera, miongozo inayohusiana na sekta ya maji safi na usafi wa mazingira zinaendelea |
| Kuanzisha mifumo ya ukusanyaji, uchambuzi na ufuatiliaji wa taarifa zinazohusiana na rasilimali maji iliyopo chini ya ardhi | Asilimia ya mifumo iliyoanzishwa | 100 | 10 | 10 | Hatua zinazoendelea ni Zabuni ya kumpata Mshauri Elekezi kufanya kazi hiyo. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya Upembuzi Yakinifu kuweza kuvuna maji ya mvua kama chanzo mbadala cha maji | Asilimia ya Upembuzi Yakinifu iliyofanyika | 100 | 10 | 10 | Kazi itafanywa na Mshauri elekezi ambaye anatafutwa. |
| Kuratibu ujumuishaji wa masuala ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi na jinsia katika usimamizi wa rasilimali maji | Asilimia ya uratibu iliyofikiwa | 100 | 10 | 10 | Kazi itafanywa na Mshauri elekezi ambaye anatafutwa. |
| Kuandaa mipaka katika maeneo ya vyanzo na vianzio vya maji. | Asilimia ya mipaka iliyoandaliwa | 100 | 10 | 10 | Kazi itafanywa na Mshauri elekezi ambaye anatafutwa. |

**f. Mradi wa Ununuzi wa Chlorine, Usimamizi na Ungalizi Bora wa Maji**

Programu hii inatekelezwa kwa pamoja baina ya Mamlaka ya Maji Zanzibar na Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia Watoto Duniani (UNICEF). Lengo kuu la programu hii ni kutambua idadi ya visima binafsi pamoja na kutibu maji. Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 programu hii ilipangiwa kutumia TZS 40.0 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 81.4 milioni zilipatikana kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na kutumika kwa kazi ya ununuzi wa dawa ya kutibu Maji.

**g.Mradi wa Uhuwishaji na Uboreshaji wa Huduma ya Maji Safi na Salama Mkoa wa Kaskazini kupitia Kampuni ya (NEC)**

Mradi huu unatekelezwa ndani ya Mkoa wa kaskazini Unguja katika skimu ya Mahonda, Nungwi na Kiwengwa pia sehemu ya Mkoa wa Kusini Unguja katika skimu ya Machui. Mradi huu ni wa mwaka mmoja kuanzia mwaka 2024/25 kwa hatua ya ujenzi pamoja na usimamiaji kwa kipindi cha miaka mitano. Mradi utagharimu jumla ya dola za kimarekani milioni ishirini na tano (mill.25 USD) ambapo mpaka sasa Mkandarasi hajaanza kulipwa gharama kwa mujibu wa makubaliano ya mradi.

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa Matangi 3 Kilindi, Nungwi na Mahonda | Asilimia ya Ujenzi iliyofikiwa | 100 | 15 | 15 | Kazi zinazoendelea ni uchimbaji wa misingi kwa matangi ya Kilindi na Nungwi |
| Uchimbaji wa visima 2 kwa skimu ya Mahonda | Idadi ya visima vilivyochimbwa | 2 | 1 | 50 | Kisima kilichochimbwa kipo katika hatua ya majaribio na kilichobaki hakijaanza kuchimbwa |
| Ujenzi na matengenezo ya vibanda 49 vya kuhifadhia mashine | Idadi ya vibanda vilivyojengwa | 49 | 14 | 29 | Ujezi wa vibanda 14 vimeanza msingi na kusimamishwa nguzo |
| Ununuzi na ufungaji wa pampu za nishati ya jua | Asilimia ya manunuzi iliofikiwa | 100 | 30 | 30 | Pampu 49 zimeshaagizwa na kukaguliwa |
| Ulipaji wa fidia | Asilimia ya kazi ya ulipaji wa fidia | 100 | 15 | 15 | Mthamini ameshafanya tathmini skimu ya Machui na Mahonda maandalizi ya ripoti yanaendelea |
| Ununuzi wa mita za maji 10,000 | Asilimia ya manunuzi iliofikiwa | 100 | 20 | 20 | Mita zimeshaagizwa kutoka kwa Mzabuni |

h. **Mradi wa Usalama wa Maji (Water Security Project)**

Mradi huu unatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW). Mradi umepangiwa kutumia EURO Milioni 25 kwa kazi za Uimarishaji wa Miundombinu ya Maji Kisiwani Pemba. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi,2025, mradi umepangiwa kutumia TZS 34.29 bilioni kwa ajili ya malipo ya Mshauri elekezi na Mkandarasi. Hadi kufikia Machi, 2025 hakuna fedha zilizopatikana kupitia Mradi huu hata hivyo shughuli ifuatayo imetekelezwa: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kumtafuta mshauri Elekezi | Asilimia ya manunuzi iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Taratibu za kumtafuta Mshauri elekezi zinaendelea kwa hatua ya tathmini |

i. **Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Umeme**

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha huduma za umeme katika vijiji 305 (180 Unguja na 125 Pemba) ili kupata huduma ya umeme salama na ya uhakika. Kukamilika kwa mradi huu kutapunguza changamoto ya upungufu wa umeme katika maeneo tofauti ya Zanzibar. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 33.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 18.15 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 15.96 bilioni sawa na asilimia 85 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Usambazi wa umeme katika vijiji vya Unguja na Pemba | Asilimia ya usambazaji iliyofikiwa | 100 | 85 | 85 | Usambazaji wa umeme unaendelea kwa vijiji vyenye uhitaji wa umeme kwa Unguja na Pemba |
| Ununuzi wa nguzo na vifaa vya umeme | Asilimia ya ununuzi uliofanyika | 100 | 70 | 70 | Vifaa vilivyonunuliwa ikiwemo nguzo, *transformer, standby genarator* na *connector*. |
| Uvutaji wa njia mpya za umeme | Asilimia ya njia ya umeme iliyovutwa | 100 | 50 | 50 | Njia mpya za umeme zimevutwa katika makaazi ya watu katika vijiji vinavyokuwa kwa haraka. |

**j.Mradi wa Kuifanyia Mabadiliko Sekta ya Nishati (ZESTA)**

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha miundombinu ya umeme na kuzijengea uwezo Taasisi zinazoshughulikia masuala ya nishati ili ziweze kuimarisha utoaji wa huduma za usambazaji wa umeme katika maeneo tofauti ya visiwa vya Unguja na Pemba. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 178.26 bilioni (TZS 4.00 bilioni kutoka Serikalini na TZS 174.26 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 98.04 bilioni (TZS 2.2 bilioni kutoka Serikalini na TZS 95.84 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 79.46 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo sawa na asilimia 81 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ulipaji wa fidia katika maeneo yatakayoathirika na mradi | Idadi ya watu waliolipwa fidia | 1,510 | 1,354 | 90 | Ulipaji wa fidia unaendelea |
| Utoaji wa mafunzo ya shughuli za uhamishaji wa wananchi katika maeneo ya mradi | Asilimia ya utoaji wa mafunzo iliofikiwa | 100 | 100 | 100 | Utoaji wa mafunzo umekamilika katika maeneo ya mradi |
| Kuandaa Mpango wa uhamishaji wakaazi katika maeneo yaliaothirika na mradi. | Asilimia ya mpango iliyoandaliwa | 100 | 80 | 80 | Mpango upo katika hatua ya kupata maoni kutoka kwa wadau |
| Kuendelea na ujenzi wa laini kubwa ya umeme yenye uwezo wa kilovoti 132 pamoja na kufanya malipo kwa Mshauri Elekezi; | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 20 | 20 | Mkandarasi anaendelea na usanifu wa njia ya umeme na usafishaji wa maeneo ya ujenzi |
| | Asilimia ya malipo ya Mshauri Elekezi yaliyofanyika | 100 | 100 | 100 | |
| Kuanza ujenzi wa miundombinu ya umeme wa jua | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 30 | 30 | Kazi zilizofanyika ni utafiti wa kijiografia na udongo (*geotechnical* na *topographic*), kusafisha eneo pamoja na ujenzi wa barabara (*access road*) |

### 11.2.16 Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi

Lengo kuu la Wizara hii ni kuona sekta hii inachangia zaidi ukuaji wa uchumi wa Zanzibar kwa kuimarisha sekta zinazohusiana na uchumi wa buluu ikiwemo uvuvi wa bahari kuu, kilimo cha bahari, ufugaji wa mazao baharini, utalii wa baharini na fukwe, utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia sambamba na uratibu wa utawala na mazingira ya baharini. Wizara imedhamiria kuwawezesha wajasiriamali katika kukuza ubunifu, uwezo wa kupata zana, mitaji na masoko, pamoja na kuchangia katika sekta ya biashara na viwanda ambazo zitasaidia upatikanaji wa ajira na masoko kwa vijana. Kwa mwaka 2024/2025, Wizara imepanga kutekeleza jumla ya programu mbili (2) na miradi mitano (5) ya maendeleo.

i. **Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo na Uvuvi-AFD**

Programu hii imeanzishwa mwaka 2020/21 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2025/27. Programu ina lengo la kuongeza tija endelevu, faida kwa biashara ya mbegu za mazao, uvuvi na ufugaji wa samaki kwa kutilia mkazo uwezeshaji wa wanawake na ushiriki wa vijana. Programu inatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Tanzania Bara na Zanzibar kwa kutumia fedha za Washirika wa Maendeleo pekee. Kwa mwaka 2024/2025, Programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 13.35 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 7.34 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, hakuna fedha iliyopatikana, hata hivyo shughuli zifuatazo zimetekelezwa: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ununuzi wa meli yenye mita 26 ya uvuvi wa bahari kuu | Asilimia ya ununuzi wa meli uliofikiwa | 100 | 5 | 5 | Kazi ya kutafuta mzabuni wa ununuzi wa meli inaendelea na zabuni imetangazwa upya kutokana na kukosekana kwa mzabuni aliyekidhi vigezo |
| Ujenzi wa kiwanda kimoja mjumuishi cha uchakataji wa samaki pamoja na mitambo baridi ya kuhifadhia samaki – Fungurefu Mkokotoni | Asilimia ya ujenzi wa kiwanda uliofikiwa | 100 | 7 | 7 | Kazi ipo katika hatua ya ujenzi wa misingi (foundation) |
| Kuandaa Modeli ya Mashirikiano baina ya sekta ya Umma na sekta binafsi (PPP model) ya kiwanda | Asilimia ya uandaaji wa *PPP model* iliyofikiwa | 100 | 15 | 15 | Modeli ya *PPP* imekamilika |
| Ununuzi wa lori la jokofu tani 10 | Asilimia ya ununuzi wa lori uliofikiwa | 100 | 5 | 5 | Kazi ya kutafuta mzabuni wa ununuzi wa meli inaendelea na zabuni imetangazwa upya kutokana na kukosekana kwa mzabuni aliyekidhi vigezo |
| Ujenzi wa mitambo minne ya kukaushia mwani na dagaa inayotumia nguvu za jua, 2 Unguja na 2 Pemba, kwa matumizi ya jamii | Idadi ya mitambo ya kukaushia mwani na dagaa iliyojengwa | 4 | 3 | 75 | Mitambo 3 iliyokamilika ni Kiuyu Micheweni – Pemba (2) na Muungoni – Unguja (1) |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa maabara ya uzalishaji wa mbegu bora za mwani | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | |
| Ununuzi wa vifaa vya maabara | Asilimia ya manunuzi iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Vifaa vimeshafungwa tayari kwa matumizi |
| Kufanya utafiti wa uzalishaji na ukuzaji wa aina tatu za samaki (majongoo bahari, kaa na *milk fish*) | Asilimia ya utafiti iliyofikiwa | 100 | 50 | 50 | Utafiti upo katika hatua ya uchambuzi |
| Kuanzisha ujenzi wa mashamba darasa mawili ya ufugaji wa samaki (kwa kutumia mabwawa na matangi) pamoja na karakana kwa ajili ya matengenezo ya vifaa na mitambo Unguja na Pemba; (Fisher Field School) | Asilimia ya ujenzi uliofikiwa | 100 | 20 | 20 | Ripoti ya tathmini ya kumpata Mshauri elekezi imeshawasilishwa IFAD kwa ajili ya kupata ridhaa (no objection) na tayari imeshapatikana |

**a.Mradi wa Kuanzisha Kituo cha Taifa cha Uhifadhi wa Taarifa za Mafuta na Gesi Asilia (NDR)**

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2022/23 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2026/27. Mradi una lengo la kujenga kituo cha uhifadhi wa taarifa za mafuta na gesi asilia. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 4.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 2.2 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 1.77 bilioni sawa na asilimia 80 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo:

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kukamilisha ununuzi wa vitendea kazi kwa ajili ya kituo cha muda cha uhifadhi wa Taarifa | Asilimia ya manunuzi iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | |
| Kuajiri Mshauri Elekezi kwa ajili ya kutoa huduma za kitaalamu za ujenzi zikiwemo usanifu na uchoraji ramani wa jengo la kudumu la Kituo cha Kuhifadhi Taarifa | Asilimia ya kazi iliyofanyika ya kumuajiri Mshauri Elekezi | 100 | 100 | 100 | |
| Kuanza ujenzi wa kituo kipya cha uhifadhi taarifa | Asilimia ya ujenzi iliofikiwa | 100 | 5 | 5 | Kazi hii imesimama kutokana na eneo lililotegemewa kujengwa kituo hicho kuwa na changamoto |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kukamilisha ujenzi wa chumba cha kukagulia data za Mafuta na Gesi Asilia *(Data Viewing Room)* | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | |

**b.Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kuhifadhia Bidhaa za Petroli Iliyosafishwa na Usambazaji (bulk storage facility)**

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuwepo kwa bohari ya uhifadhi wa mafuta na kufanya biashara ya mafuta Zanzibar katika eneo la Mangapwani. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 4.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 2.2 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, hakuna fedha iliyotolewa.

**c.Mradi wa Ujenzi wa Madiko na Masoko ya Samaki ya Kisasa**

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2024/2025 kwa lengo la kuwawezesha wavuvi kuweza kupata huduma za msingi za bandari na masoko kwa kuwajengea madiko na masoko ya kuhifadhia na kuuzia samaki yenye hadhi ya kisasa katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 27.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 14.85 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 12.71 bilioni sawa na asilimia 86 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuandaa Upembuzi Yakinifu kwa madiko mapya | Asilimia ya maandalizi iloyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Kazi hii imekamilika |
| Ujenzi wa diko na soko la kisasa la samaki (Fungurefu mkokotoni) Unguja | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Ujenzi upo katika hatua ya uchimbaji wa misingi |
| Ujenzi wa diko na soko la kisasa la samaki- Mkoani Pemba | Asilimia ya ujenzi uliokamilika | 100 | 60 | 60 | Ujenzi upo hatua ya kuezeka |

**d.Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maabara ya Uthamini wa Ubora wa Bidhaa za Baharini**

Mradi umeanzishwa mwaka 2023/24 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2024/25. Mradi una lengo la kuimarisha miundombinu ya maabara ya uthamini wa ubora wa bidhaa za baharini. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 4.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 2.2 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 728 milioni sawa na asilimia 33 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ununuzi wa vifaa vya maabara vya uthamini wa bidhaa za baharini | Asilimia ya ununuzi wa vifaa iliyofikiwa. | 100 | 100 | 100 | Mzabuni anaendelea na ufungaji wa vifaa |
| Ujenzi wa uzio katika jengo la maabara - Maruhubi | Asilimia ya ununuzi wa vifaa iliyofikiwa | 100 | 70 | 70 | Maombi ya fedha yameshawasilishwa kwa ajili ya ujenzi wa Awamu ya Pili |

**e.Mradi Jumuishi wa Uwezeshaji wa Wanawake katika Ufugaji wa Mazao ya Baharini**

Mradi umeanza mwaka 2023/24 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2027/28. Mradi una lengo la kuwawezesha wakulima na wasindikaji wa mazao ya baharini kufikia maendeleo endelevu kwa kuwa na mnyororo wa thamani. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 2.40 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 1.32 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 108 milioni sawa na asilimia 8 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo:

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuanzisha mashamba manne ya majaribio ya mwani/majongoo bahari | Asilimia ya kazi iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Kazi ya ununuzi wa vifaa kwa ajili ya ujenzi wa mashamba ya majaribio inaendelea ambapo hatua iliyopo ni kumpata mzabuni atakayesambaza vifaa hivyo |
| Ujenzi wa kiwanda cha kusarifu mwani Chokocho Pemba | Asilimia ya ujenzi wa kiwanda iliyofikiwa | 100 | 15 | 15 | Kazi ya kuandaa michoro kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda imekamilika na tayari rasimu ya mwanzo imepatikana |
| Kuanzisha vitalu viwili vya mwani na majongoo bahari | Asilimia ya uanzishaji wa Vitalu iliyofikiwa | 100 | 0 | 5 | Kazi hii ipo katika hatua za manunuzi |
| Utoaji wa vifaa kwa wakulima wa mwani na wafugaji wa mazao ya baharini | Asilimia ya utekelezaji iliyofikiwa | 100 | 0 | 5 | Kazi hii ipo katika hatua za manunuzi |

**f.Mradi wa Utafiti wa Usalama wa Chakula na Maisha Endelevu kwa Jamii**

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2021/22 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2026/27. Mradi una lengo la kujenga uelewa na kutoa ufadhili wa elimu ya juu mbinu za kiuchumi, usalama wa chakula na maisha endelevu. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 41.07 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 22 milioni. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 62 milioni sawa na asilimia 278 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya utafiti wa kuimarisha sekta ya uvuvi kupitia wavuvi wadogo wadogo | Idadi ya tafiti zilizofanyika | 4 | 2 | 60 | Kazi ya uchakataji wa taarifa za tafiti zilizokusanywa na uandishi wa ripoti ya tafiti hizo inaendelea. |
| Kutoa udhamini wa masomo ya elimu ya juu | Idadi ya watendaji waliopatiwa udhamini | 5 | 1 | 20 | Malipo ya masomo kwa ngazi ya uzamili yamefanyika. |

### g.Mradi wa Tathmini wa Ubora wa Maji ya Bahari

Programu ya kufanya tathmini ubora wa maji ya bahari Zanzibar imeanzishwa kwa lengo la kupata tathmini na taarifa juu ya ubora wa maji ya mwambao wa bahari ya Zanzibar na kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji wa ubora wa maji ya baharini. Mradi huu unatekelezwa kwa kipindi cha miezi kumi (10) na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kupitia Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Bahari Zanzibar (ZAFIRI), ambao unadhaminiwa na Shirika la Usimamizi wa Mazingira la Umoja wa Mataifa UNEP kupitia Nairobi Convention. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 279 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo

Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 131 milioni. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 469 milioni sawa na asilimia 356 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya tathmini ya vyanzo vya uchafuzi wa mazingira ya bahari vilivyopo ardhini na maeneo ya ukanda wa pwani wa Zanzibar | Asilimia ya tathmini iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Tathmini imefanyika katika Wilaya zifuatazo: Kaskazini A, Kaskazini B, Mjini, Magharibi A, Magharibi B, Kati na Wilaya ya Kusini ikijumuisha Shehia 145. |
| Uanzishaji wa Kanzi Data (database) kwa ajili ya uhifadhi wa taarifa za ubora wa maji ya bahari ya Zanzibar | Asilimia ya uanzishaji wa Kanzi Data iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Taarifa za ubora wa maji ya Bahari ya Zanzibar zimeanza kuingizwa kwenye Kanzi Data kwa ajili ya kuzihifadhi |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuanzisha mfumo wa kielektroniki wa ufuatiliaji wa ubora wa maji ya Bahari ya Zanzibar | Asilimia ya uanzishaji wa mfumo iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Uandaaji wa mfumo umekamilika na kwa sasa taarifa za awali kuhusu ubora wa maji ya Bahari ya zimeshaanza kuingizwa |
| Kufanya tathmini ya takataka za baharini katika fukwe za Bahari ya Zanzibar | Idadi ya tathmini zilizofanyika | 3 | 2 | 66 | Ukusanyaji wa taarifa (sampuli) za takataka za baharini katika fukwe 16 kwenye maeneo ya Hifadhi za Bahari za Zanzibar ikiwemo: Kizingo, Ngazi mia, Bububu, Maruhubi, Fumba, Unguja Ukuu, Kizimkazi, Jambiani, Marumbi, Pongwe, Kiwengwa, Nungwi, Fukuchani, Mizingani na Fungurefu umefanyika. |
| Kufanya tathmini ya uchafuzi wa maji ya baharini unaotokana na takataka za aina ya kemia na kibiolojia, katika ukanda wa maji ya pwani wa Zanzibar | Idadi ya tathmini zilizofanyika | 3 | 1 | 33 | Ukusanyaji wa sampuli za maji na udongo katika baadhi ya maeneo ya Hifadhi za Bahari umefanyika ikiwemo: CHABAMCA, MBCA, TUMCA na MIMCA.<br><br>Uchakataji wa taarifa umekamilika na hatua ya uandishi wa ripoti inaendelea. |

### 11.2.17 Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi

Wizara ina lengo la kuimarisha miundombinu wezeshi itakayochochea ukuaji wa Uchumi. Wizara imepanga kutekeleza programu tano (5) na miradi mitatu (3) ya maendeleo.

**i.Programu ya Ujenzi wa Barabara Kuu**

Programu hii imeanzishwa kwa lengo la kuunganisha miji mikubwa ya Zanzibar kwa lengo la kuhuisha uchumi na uwekezaji. Barabara hizi ni kiunganishi cha miji na maeneo mengine ya kiuchumi ikiwemo viwanja vya ndege na bandari. Kwa mwaka 2024/2025, Programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 311.77 bilioni (TZS 115.54 bilioni kutoka Serikalini na TZS 196.23 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 171.47 bilioni (TZS 63.54 bilioni kutoka Serikalini na TZS 107.92 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 11.90 bilioni (TZS 3.01 bilioni na TZS 8.89 bilioni kutoka Washirika wa Maendeleo) sawa na asilimia 7 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ulipaji wa fidia kwa vipando na nyumba katika maeneo wananchi waliopisha na ujenzi wa barabara | Idadi ya wananchi waliolipwa fidia | 100 | 0 | 0 | Uhakiki kwa ajili ya malipo ya fidia umekamilka upo katika hatua za taratibu za malipo. |
| Ujenzi wa barabara ya Wete – Chake Chake kwa uwekaji wa lami km 22.1 | Idadi ya kilomita za barabara zilizowekwa lami | 22.1 | 16 | 72 | Kazi ya Uwekaji wa lami imekamilika kuanzia Meli tano hadi Machengwe |
| | Idadi ya km zilizowekwa fusi | 6.1 | 2.7 | 44 | Kazi ya uwekaji wa tabaka la mwisho la kifusi imekamilika katika maeneo ya Weni hadi Limbani na kazi ilobakia ni km 3.4 ambayo ujenzi haujaanza unasubiri kukamilika kwa hatua za ulipaji fidia kutoka Limbani hadi Bandarini |
| Ujenzi wa barabara ya Tunguu-Makunduchi km 53, Chake Chake-Mkoani km 43.5 na Fumba - Kisauni km 12 | Idadi ya km za barabara zilizojengwa | 108.5 | 0 | 0 | Taratibu za kuanza ujenzi zimekamilika na ujenzi unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2024/25 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Ukamilishaji wa barabara kwa kiwango cha lami km 42.95, ambazo ni barabara ya Jozani – Charewe – Ukongoroni – Bwejuu km 23.3, Fuoni – Tunguu km 5.8, Barabara ya Bungi km 0.5, Barabara za Nungwi km 13.35 | Idadi ya km zilojengwa | 42.95 km | 42.95 km | 100 | |

**ii.Programu ya Ujenzi wa Barabara za Ndani**

Programu hii imeanzishwa kwa lengo la kujenga barabara za ndani zenye urefu wa kilomita 275.9 katika maeneo ya mijini na vijijini Unguja na Pemba. Programu itaunganisha mitaa na maeneo mengine ikiwemo barabara kuu. Aidha, kukamilika kwa programu hii kutasaidia kupunguza msongamano katika barabara kuu pamoja na kuongeza haiba ya kupendezesha miji na mitaa katika maeneo ya Zanzibar. Kwa mwaka 2024/2025, Programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 45.60 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), Programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 25.08 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 102.57 sawa na asilimia 409 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya tathmini na ulipaji wa fidia za nyumba na vipando vitakavyoathiriwa na ujenzi wa barabara | Idadi ya wananchi waliofanyiwa tathmini | 50 | 50 | 100 | Uhakiki kwa ajili ya malipo ya fidia unaendelea kwa hatua za uandishi wa ripoti na kuzikabidhi kwa hatua za malipo |
| | Idadi ya Wananchi waliolipwa fidia | 50 | 2 | 4 | Wananchi hao wamelipwa fidia kutokana na malalamiko yao ya muda mrefu. Wananchi waliobakia wanaendelea kulipwa |
| Usafishaji uwekaji wa kifusi kwa tabaka mbali mbali | Idadi ya km za barabara zilizowekwa kifusi | 89.65 | 57.49 | 64 | Kazi ya uwekaji wa kifusi kwa tabaka mbali mbali zinaendelea kwa barabara ya Masingini-Kijichi (8.0km), Kilindini - Kilimajuu (1.44km) na Kilimajuu-Kigomani (4.0 km).<br><br>Kwa Pemba ni barabara ya Chanjamjawiri – Pujini(Matale) km 4.65, Finyakicha km 8.93, Mgagadu – Kwautao km 5.6, Mzambarau Takao- |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Mchangamdogo Km 6.13, Konde-Msuka Km 4.1, Pembeni-Pandani Km 3.34, Kengeja-Shamiani+Kiimbini Spar Km 4.85 na Wawi Mesi-Mzambaraumboko Km 6.4. | | | | | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa mitaro na uwekaji wa lami kwa baadhi ya barabara zilizoanza kujengwa | Idadi ya km zilizowekwa lami | 128 km | 38.35 | 30 | Kazi ya uwekaji lami kwa tabaka mbali mbali upande wa Unguja zimefanyika kwa barabara ya Kichakani (Ghana)-Kichaka Mapundi (0.5km), Ussi Kombo-Daniel Ali-Mnarani (2.52km), Mto wa Pwani-Fungurefu (2.0 km), Bwekunduni-Soko la Samaki (2.66km), Kitaruni - Kichaka - Mabundi - Mkarafuu Pakacha (2.14km), Mfurumatonga-Mlilie Skuli (2.84 km), Mfurumatonga-Mbuyu Popo (3.35km), Donge Mbiji-Chechele (2.0km) na Mwakaje-Mwachealale-Bumbwisudi (5.13km).<br><br>Na kwa upande wa Pemba ni barabara ya Micheweni-Shumba Mjini-Bandarini (2.99km), Ukutini-Mtangani-Bandarini (4.65km) na Micheweni-Kiuyu-Maziwa Ng'ombe (7.57km) |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| (Roundabout) ya Mwanakwerekwe na Amani | (Mwanakwerekwe) | | | | upande wa kuelekea Kiembe Samaki |
| | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa (Amani) | 100 | 65 | 65 | Kazi zinazoendelea sasa ni ujenzi wa mzunguko |

### iii Programu ya Matengenezo ya Barabara za Mjini

Programu hii imeanzishwa kwa lengo la kuimarisha haiba ya mji wa Zanzibar kwa ujenzi wa barabara katika maeneo ya mjini. Programu inahusu ujenzi wa kilomita 100.9 za barabara za mjini na uimarishaji wa barabara katika maeneo ya Mkoa wa Mjini Magharibi. Kukamilika kwa programu hii kutaongeza haiba na kupendezesha Mji wa Zanzibar na kusaidia kuimarika kwa baadhi ya sekta ikiwemo sekta ya usafirishaji, utalii na biashara. Kwa mwaka 2024/2025, Programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 112.09 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 61.65 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 42.85 bilioni sawa na asilimia 70 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa barabara kuu za njia mbili (Two lanes dual) ikiwemo barabara ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume –Kiinua Miguu (5.2 km), Kiembesamaki Amani-Mtoni (Mkapa road) km 8.8, Kariakoo – Magomeni Mwanakwerekwe Sokoni km 2.9, Kinazini (Benki Kuu) - Mtoni km 3.5, Amani Round about-Mikunguni- Kwabizredi km 2.6 | Idadi ya km za barabara zilizojengwa | 23 km | 8.52 km | 37 | Kazi zilizofanyika ni ujenzi wa barabara katika maeneo hayo |
| Ujenzi wa barabara za njia moja (single carriage way) zikiwemo barabara ya 0.68 km, Mwembe Makumbi - Basra - Karakana - Mtopepo skuli 1.6 km | Idadi ya km za barabara | 0.93 km | 0.33 km | 35 | Ujenzi wa barabara iliyokamilika kwa kiwango cha |
| Kuendelea kwa ujenzi wa barabara ndogo ikiwemo barabara ya Mpendae planned area 5.765 km, Chukwani mwisho – Buyu 3.45 km, Kilimani bar – Jangombe 0.47 km, Kwakira -kituo kipya Uwanja wa Ndege 0.153 km, Mbweni afya - Madina-Mbweni matrekta 2.071 km, ZSSF Mbweni Estate - Mbweni Ruins - Mbweni BOT quater - Kiembe Samaki 0.9 km, Baraza la Wawakilishi Chukwani - Makamo wa Kwanza wa Rais 0.4 km, | Idadi ya km za barabara zilizojengwa | 29.42 km | 22.89 km | 77.8 km | Barabara zilizojengwa zilizokamilika kwa hatua ya kiwango cha zege na lami na nyengine zinaendelea na ujenzi |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| River Tiba - Chukwani Tuta 1.519 km, Rahaleo ZBC - Bizred -Michenzani ring roads 3.07 km, Faraja Skuli – Mboriborini 2.07 km, Makadara Mfereji wa Wima & Associate 0.48 km, Darajabovu Mboriborini, Magazeti Press-Mkele 0.35 km, Msikiti Shurba - Mshelishelini Matarumbeta 0.61 km, Muungano Muembe Mkali 0.6 km , Muungano – Sogea 0.684 km, Mnara wa Mbao - Migombani Garden and Walkways in Garden 0.29 km | | | | | |
| Kuendelea na ujenzi wa njia za juu (flyover) katika mzunguko (Roundabout) ya Mwanakwerekwe na Amani | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa (Mwanakwerekwe) | 100 | 90 | 90 | Kazi inayoendelea kwa sasa ni ujenzi wa mzunguko kwa upande wa kuelekea Kiembe Samaki |
| | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa (Amani) | 100 | 65 | 65 | Kazi zinazoendelea sasa ni ujenzi wa mzunguko |

### iv.Programu ya Kuimarisha Viwanja vya Ndege

Programu hii imeanzishwa kwa lengo la kuimarisha miundombinu ya usafirishaji wa abiria na mizigo kwa njia ya anga ili iweze kuwa katika viwango vya Kimataifa. Programu itahusisha ujenzi wa uwanja wa ndege wa Pemba ikiwemo maegesho ya ndege, njia za kupitia ndege pamoja na sehemu za kukaa abiria. Kwa mwaka 2024/2025, Programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 182.77 (TZS 35.50 bilioni kutoka Serikalini na TZS 147.27 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 100.53 bilioni (TZS 19.52 bilioni kutoka Serikalini na TZS 81.00 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 22.20 bilioni (TZS 11.51 bilioni kutoka Serikalini na TZS 10.68 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) sawa na asilimia 22 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuendelea na ujenzi wa jengo la Abiria Terminal II (AAKIA) | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 50 | 50 | Kazi zinazoendelea ni uwekaji wa miundombinu ya maji na umeme katika jengo la abiria terminal II |
| Kukamilisha tathmini pamoja na kulipa fidia kwa maeneo yatakayoathirika wakati wa ujenzi wa uwanja wa ndege wa Pemba | Idadi ya wananchi waliofanyiwa tathmini | 818 | 818 | 100 | Tathmini imekamilika |
| | Idadi ya Wananchi waliolipwa fidia | 818 | 727 | 89 | Kazi za ulipaji wa fidia kwa wananchi waliobaki inaendelea |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuanza kwa hatua za awali za ujenzi wa uwanja wa ndege wa Pemba | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Mkandarasi ameshaanza kazi za *mobilization* ya vifaa vya ujenzi na maabara na wataalam. Pia Mkandarasi anaendelea na kazi za usanifu wa michoro ambapo tayari ameshawasilisha *Inception report* kwa Wizara |

**a. Mradi wa Ujenzi wa Bandari Jumuishi ya Mangapwani**

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kujenga bandari jumuishi ya kisasa (Multipurpose Port) ambayo itajumuisha ujenzi wa gati ya mizigo eneo la ushushaji na upakiaji wa mafuta, bandari ya uvuvi, na chelezo cha kukarabati meli. Kukamilika kwa bandari hii kutasaidia kupunguza msongamano uliopo katika bandari ya Malindi, upatikanaji wa ajira na kuongezeka kwa mapato ya Serikali. Serikali inatarajia kushirikiana na sekta binafsi katika ujenzi wa bandari hii. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 257.54 bilioni (TZS 157.54 bilioni kutoka Serikalini na TZS 100.00 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 141.64 bilioni (TZS 86.64 bilioni kutoka Serikalini na TZS 55.00 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 155.68 bilioni kutoka Serikalini sawa na asilimia 110 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa nyumba 370 za wananchi za fidia Mangapwani | Idadi ya nyumba zilizojengwa | 370 | 247 | 66.75 | Ujenzi wa nyumba unaendelea katika hatua mbalimbali ambapo, Nyumba 38 ziko katika hatua za ujenzi wa Awali |
| Ujenzi wa miundombinu ya barabara (Ringroads) katika eneo la bandari Mangapwani | Idadi ya kilomita zilizojengwa | 12.6 | 5.8 | 46 | Ujenzi wa barabara umeanza hata hivyo, ujenzi umesita kutokana na changamoto za fidia katika baadhi ya maeneo. Uhakiki unaendelea ili kufahamu thamani ya mali za wananchi wanaopisha mradi. |
| Kufanya tathmini pamoja na kulipa fidia kwa maeneo yatakayoathirika wakati wa ujenzi | Idadi ya wananchi waliofanyiwa tathmini | 603 | 600 | 99.5 | Tathmini ya malipo ya fidia imekamilika iko katika hatua za malipo |
| | Idadi ya wananchi watakaolipwa fidia | 603 | 100 | 17 | |
| Kuendelea na shughuli za upelekaji wa miundombinu ya maji, umeme katika eneo la bandari | Asilimia ya kazi iliyofanyika | 100 | 100 | 100 | Kazi hii imekamilika |
| Ujenzi wa bandari kwa Awamu ya kwanza | Asilimia ya ujenzi wa bandari iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Mkandarasi Kampuni ya CHEC ya nchini CHINA imekabidhiwa eneo la ujenzi na kazi za utafiti wa udongo na bahari zinaendelea kabla ya kuanza ujenzi. |

### b. Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Abiria Maruhubi

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha huduma ya usafirishaji wa abiria na mizigo katika visiwa vya Unguja na Pemba na maeneo mengine, mradi utahusisha ujenzi wa gati ya abiria na gati ya mizigo (roro) katika eneo hilo. Mradi unatarajiwa kutekelezwa baina ya Serikali na Kampuni ya ZF DEVCO na unatarajiwa kutekelezwa kwa muda wa miezi thelathini na sita kuanzia mwaka 2024/25. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 127.50 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 70.12 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, shughuli zifuatazo zimetekelezwa:

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kukamilisha hatua za awali za mradi ikiwemo kupima udongo pamoja na utafiti | Asilimia ya kazi iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Kazi ya upimaji wa udongo na utafiti imekamilika |
| Kuanza hatua za kufukia bahari (Reclaimation) katika eneo la Maruhubi | Asilimia ya kazi iliyofikiwa | 30 | 5 | 17 | Mkandarasi anaendelea na hatua ya *mobilization* ya vifaa. Aidha kazi ya ufukiaji wa eneo la juu la bahari imeanza ili kuweka usawa *(level)* |

### c. Mradi wa Uboreshaji wa Mfumo wa Mawasiliano

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha mifumo ya mawasiliano ambayo itarahisisha utoaji wa huduma za kimtandao na utoaji wa huduma Serikalini. Mradi huu utahusisha mifumo mbali mbali ya Serikalini inayotumika katika utoaji wa huduma zenye ufanisi zaidi za mawasiliano na kuongeza ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia TZS 6.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi ulipangiwa kutumia TZS 3.30 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 3.48 sawa na asilimia 106 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo:

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya matengenezo na uwekaji wa mkonga wa mawasiliano katika maeneo yanayojengwa miundombinu ya barabara | Idadi ya km za uwekaji wa mkonga iliyofikiwa | 120 km | 74 km | 61.7 | Barabara iliyotekelezwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa mradi husika ni Kwa Mndo kizimbani yenye kilomita 2.5, Maeneo ya barabara ya Chukwani – Mombasa – Mazizini km 24, pamoja na barabara ya Tunguu - Makunduchi km 38. Kwa mwaka huu wa fedha mradi umeendelea kwa barabara za ndani ambazo mkonga umepita.<br><br>Mradi huu bado unaendelea kwa mwaka wa fedha 2025/2026. |

### d.Mradi wa Matengenezo ya Boti Mpya za Abiria

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha usafirishaji wa abiria na mizigo kwa wananchi wa visiwa vya Unguja na Pemba ili kupunguza changamoto za usafiri zinazoikabili Zanzibar. Mradi utasaidia kuimarika kwa shughuli za biashara na usafirishaji wa abiria na mizigo. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 26.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi ulipangiwa kutumia TZS 14.30 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, TZS 2.85 bilioni sawa na asilimia 20 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| **Shughuli Iliyopangwa** | **Kiashiria** | **Shabaha** | **Utekelezaji Halisi** | **Asilimia ya Utekelezaji** | **Maelezo** |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuandaa michoro *(detailed design)* kwa boti za abiria. | Asilimia ya uandaaji wa michoro iliyofikiwa | 100 | 90 | 90 | Michoro imeandaliwa na tayari imewasilishwa kwa Kampuni ya RINA- Classification Society ya nchini Italy kwa ajili ya kuthibitishwa (Approval). |
| Kuanza matengenezo ya boti mpya mbili za mwendo kasi kwa ajili ya abiria na mizigo. | Asilimia ya ujenzi ilipofikia. | 100 | 5 | 5 | Kwa sasa Mjenzi anakusanya vifaa *(Mobilisation of equipment)*. |

### 11.2.18 Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale

Wizara ina jukumu la kusimamia utalii na mambo ya kale kwa kuibua na kuongeza vivutio vipya vya utalii na kuendelea kuitangaza Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara imepanga kutekeleza programu moja na miradi miwili ya maendeleo.

#### i. Programu ya Kuimarisha Maeneo ya Kihistoria

Programu hii imeanzishwa mwaka 2017/2018 na inatarajiwa kukamilika mwaka 2024/2025 Programu ina lengo la kuendeleza Sekta ya Utalii kwa kuimarisha maeneo ya kihistoria na kukuza utalii kwa kuongeza fursa za ajira, vivutio vya utalii na kuongeza Pato la Taifa. Kwa mwaka 2024/2025, Programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 15.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 8.25 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 889 milioni sawa na asilimia 11 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuimarisha maeneo ya kihistoria Fufuni na Kichokochwe Pemba; | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 2 | 2 | Maeneo ya kihistoria ya Fufuni na Kichokochwe yapo katika hatua za manunuzi. |
| Kuimarisha eneo la kihistoria la Kasri ya Mtoni | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 2 | 2 | Eneo la Kasri ya Mtoni, mradi huu utatekelezwa kwa mashirikiano na Sekta Binafsi ambapo tayari Mkataba baina ya Wizara na Kampuni ya Infinity umesainiwa. |
| Kufanya marekebisho ya eneo la bandari ya Majahazi iliopo Chake Chake Pemba | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 2 | 2 | Eneo la Bandari ya Majahazi lipo katika hatua za manunuzi. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuimarisha Pango la Pete | Asilimia ya uimarishaji iliyofikiwa | 100 | 2 | 2 | Eneo la Pango la Pete lipo katika hatua za manunuzi. |
| Ujenzi wa uzio katika maeneo ya kihistoria | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 2 | 2 | Kazi ya kuweka uzio kwa baadhi ya maeneo ya kihistoria ipo katika hatua za kumpata Mkandarasi atakaejenga uzio katika maeneo hayo. |
| Ununuzi wa vifaa vya makumbusho | Asilimia ya manunuzi iliyofikiwa | 100 | 2 | 2 | Kazi ya ununuzi wa vifaa vya Makumbusho ipo katika hatua za manunuzi |
| Kuimarisha eneo la kihistoria la Ras Mkumbuu | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 65 | 65 | Ujenzi wa Duka (shop building), Mkahawa (Restaurant), Sehemu ya mapumziko (lounge) na Ofisi unaendelea na uko karibu kumalizika. Kisima cha maji kimekamilika kinatoa maji ya kutosha na usambaji wa maji kwenda kwenye maeneo husika ushafanyika. Hodhi na mnara wa maji uko katika hatua ya kukamilika. Utengenezaji wa njia za kupita na sehemu ya maegesho ya vyombo vya moto pamoja na upandaji wa bustani ujenzi unaendelea. |
| Kufanya matengenezo eneo la Ngomekongwe | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 85 | 85 | Kazi zinazoendelea ni pamoja na kufanya matengenezo ya theatre, matengenezo ya vibaraza na bustani, kusafisha kuta za ndani na kuzifanyia matengenezo |
| Kufanya matengenezo mahamam ya Forodhani na Hamamni | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 77 | 77 | Kwa upande wa Hamam la Forodhani halijaanza matengenezo na upande wa Hamam la Hamamni |

**a. Mradi wa ukarabati wa majengo ya Mji Mkongwe**

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2023/24 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2026/27. Mradi una lengo la kuimarisha majengo yaliyo katika hali mbaya ya uchakavu katika maeneo ya Mji Mkongwe ili kubaki kuwa ni ukumbusho wa Hisotia ya Zanzibar kwa kuyahifadhi na kuyalinda. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 9.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 4.95 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, shughuli zifuatazo zimefanyika: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ukarabati wa majengo kumi (10) ya Mji Mkongwe. | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 14 | 14 | Majengo yalifanyiwa ukarabati ni pamoja na<br><br>Jengo namba 2312 lililopo Vuga - Ujenzi wa jengo hili umefikia asilimia 70% ambapo kazi zilizofanyika ni kurekebisha paa, dari, kuweka plasta na umeme. Jengo namba 1196/97 lililopo Malindi - Ujenzi wa jengo hili umefikia asilimia 25 ambapo kazi zilizofanyika ni kutia boriti na kugonga kuta. Jengo namba 1065 lililopo Malindi Funguni - Ujenzi wa jengo hili umefikia asilimia 40 ambapo kazi zilizofanyika ni kulikarabati lisibomoke nje na ndani, kugonga kuta, kupiga plasta, kuezeka, kurekebisha dari. Aidha, jengo namba F06A limefikia asilimia 10, kazi zilizofanyika ni pamoja |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | na kurekebisha paa, dari, kufanya "fitting" ya umeme, kuanza ukarabati wa madirisha na milango ya ghorofa ya pili, kuanza kupaka rangi katika kuta za nje na kukarabati bustani.<br><br>Jengo namba 2515-17 Mkandarasi ameshasaini Mkataba lakini wanasubiri Shirika la nyumba kuhamisha wapangaji wake. |

**b. Mradi wa Ukarabati wa Jengo la Beit el Ajaib**

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2023/24 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2026/27 Mradi una lengo la kulihami jengo na kulirejeshea haiba yake kwa kuzingatia kuwa Beit El Ajaib ni alama ya Sura ya Zanzibar pamoja na kudumisha historia ya jengo hilo lenye sifa za kipekee na urithi wa dunia. Kwa mwaka 2024/2025, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 15.02 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2024 hadi Machi 2025), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 8.26 bilioni. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 3.07 bilioni sawa na asilimia 37 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| **Shughuli Iliyopangwa** | **Kiashiria** | **Shabaha** | **Utekelezaji Halisi** | **Asilimia ya Utekelezaji** | **Maelezo** |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuendelea na ukarabati mkubwa wa nyumba ya ajabu (Beit el Ajaib). | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 38 | 38 | Utekelezaji wa Mradi huu umefikia **asilimia 38** ambapo kazi zilizofanyika kwa kipindi cha miezi tisa 2024/2025 ni kukamilisha uimarishaji wa msingi (foundation), kuta na kazi za mbao. Aidha vifaa kwa ajili ya ujenzi vimeanza kuwasili Zanzibar. |

| UPATIKANAJI WA FEDHA KWA PROGRAMU NA MIRADI YA KIMKAKATI KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA (JULAI 2024- MACHI,2025) ("000 TZS MILIONI") | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **WIZARA/TAASISI** | **KILICHOPANGWA** | | | **KILICHOTOKA** | | | **ASILIMIA** | | |
| **PROGRAMU/MIRADI** | **SMZ** | **WM** | **JUMLA** | **SMZ** | **WM** | **JUMLA** | **SMZ** | **WM** | **JUMLA** |
| **OFISI YA RAIS - IKULU** | | | | | | | | | |
| **i) Mradi wa Uimarishaji waMajengo ya Ikulu** | **1,375,000** | **0** | **1,375,000** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **ii) Mradi wa Uimarishaji Mfumo wa Ulinzi na Usalama katika Majengo ya Ikulu na Makaazi ya Mhe. Rais** | **880,000** | **0** | **880,000** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **iii) Mradi wa Kuimarisha Mawasiliano ya Mfumo wa Rais** | **220,000** | **0** | **220,000** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **JUMLA YA FUNGU** | **2,475,000** | **0** | **2,475,000** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **OFISI YA RAIS - UCHUMI NA UWEKEZAJI** | | | | | | | | | |
| **Programu ya Uimarishaji wa Maeneo Huru ya Uwekezaji** | **8,250,000** | **0** | **8,250,000** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **JUMLA YA FUNGU** | **8,250,000** | **0** | **8,250,000** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **WAKALA WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI** | | | | | | | | | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **i) Mradi wa Kuwasaidia Wajasiriamali Wadogo Wadogo, Wakati na Wakubwa** | **2,475,000** | **2,805,000** | **5,280,000** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **ii) Mradi wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi** | **17,600,000** | | **17,600,000** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **iii) Mradi Kukuza Usawa wa Kijinsia Tanzania (Pamoja)** | | **1,100,000** | **1,100,000** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **JUMLA YA FUNGU** | **20,075,000** | **3,905,000** | **23,980,000** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **OFISI YA RAIS - FEDHA NA MIPANGO** | | | | | | | | | |
| **Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali Zanzibar** | | | | | | | | | |
| **i) Ukamilishaji wa Ofisi za Serikali** | **44,143,653** | | **44,143,653** | **10,218,551** | | **10,218,551** | **23** | **0** | **23** |
| **ii)Ujenzi wa Mji wa Serikali** | **18,547,189** | **0** | **18,547,189** | **1,249,029** | **0** | **1,249,029** | **7** | **0** | **7** |
| **Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG-Z)** | | **17,600,000** | **17,600,000** | | **18,961,072** | **18,961,072** | **0** | **108** | **108** |
| **Programu ya Mageuzi Katika Usimamizi wa Fedha (PFMRP)** | **220,000** | **2,452,178** | **2,672,178** | **352,900** | **1,500,000** | **1,852,900** | **160** | **61** | **69** |
| **Mradi** | | | | | | | | | |
| **i) Uimarishaji wa Rasilimali za Ndani na Usimamizi wa Maliasili** | **43,175** | **542,783** | **585,958** | **78,500** | **0** | **78,500** | **182** | **0** | **13** |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ii) Ulipaji wa Madeni kwa miradi ya Maendeleo | 171,600,000 | 0 | 171,600,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **234,554,016** | **20594961.2** | **255,148,978** | **11,898,980** | **20,461,072** | **32,360,052** | **7** | **0** | **13** |
| **TUME YA MIPANGO** | | | | | | | | | |
| Uratibu wa Programu ya Urasimishaji Ardhi na Biashara Zanzibar | 1,650,000 | 0 | 1,650,000 | 1,669,935 | 0 | 1,669,935 | 101 | 0 | 101 |
| Miradi | | | | | | | | | |
| i) Usimamizi, Kujenga Uwezo na Kuoanisha Mipango ya Kisekta, Kitaifa na Kimataifa (ZADEP, SDGs na African Agenda) | 1,265,000 | 0 | 1,265,000 | 439,595 | 0 | 439,595 | 35 | 0 | 35 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **2,915,000** | **0** | **2,915,000** | **2,109,530** | **0** | **2,109,530** | **72** | **0** | **72** |
| **OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI** | | | | | | | | | |
| i) Mpango Mkuu wa Uimarishaji Takwimu Tanzania Awamu ya Pili (TSMP II) | 0 | 4,575,519 | 4,575,519 | 0 | 3,446,231 | 3,446,231 | 0 | 75 | 75 |
| ii) Mradi wa Uimarishaji wa Takwimu za Jinsia | 0 | 188,783 | 188,783 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **0** | **4,764,302** | **4,764,302** | **0** | **3,446,231** | **3,446,231** | | **0** | **72** |
| **OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA** | | | | | | | | | |
| Programu ya Mageuzi ya Utumishi wa Umma | 550,000 | | 550,000 | 105,740 | 109,073 | 214,813 | 19 | 0 | 39 |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| (Phase II) | | | | | | | | | |
| Programu ya Mageuzi ya Sekta ya Sheria | 275,000 | 641,772 | 916,772 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Miradi | | | | | | | | | |
| i) Kusaidia Kukabiliana na Kesi za Ukatili kwa Utoaji wa Huduma ya Haki ya Masuala ya Kijinsia kwa Wanawake | 0 | 192,500 | 192,500 | 0 | 136,785 | 136,785 | 0 | 71 | 71 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **825,000** | **834,272** | **1,659,272** | **105,740** | **245,858** | **351,598** | **13** | **0** | **21** |
| MAHAKAMA KUUU | | | | | | | | | |
| i) Mradi wa Ujenzi wa Mahakama za Wilaya na Mikoa | 13,695,000 | 0 | 13,695,000 | 8,657,332 | 0 | 8,657,332 | 63 | 0 | 63 |
| ii) Mradi wa Kuanzisha Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Taarifa za Kesi *(ECMIS)* | 275,000 | | 275,000 | 349,419 | 0 | 349,419 | 127 | 0 | 127 |
| iii) Mradi wa Uboreshaji wa Mahkama | 330,000 | 14,025,000 | 14,355,000 | 0 | 7,068,295 | 7,068,295 | 0 | 50 | 49 |
| iv) Mradi wa Ujenzi wa Mahkama Jumuishi ( IJC) _ Pemba | 0 | 1,650,000 | 1,650,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **14,300,000** | **15,675,000** | **29,975,000** | **9,006,751** | **7,068,295** | **16,075,046** | **63** | **0** | **54** |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ** | | | | | | | | | |
| **i) Mradi wa Kuimarisha Ulinzi na Usalama** | **13,750,000** | **0** | **13,750,000** | **17,382,973** | **0** | **17,382,973** | **126** | **0** | **126** |
| **ii) Mradi wa Ujenzi wa Kituo na Maegesho ya Vyombo vya Usafiri Soko la Mwanakwerekwe** | **15,950,000** | **0** | **15,950,000** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **iii) Mradi wa Kuimarisha Haki Jinai Chuo cha Mafunzo** | **12,100,000** | **0** | **12,100,000** | **6,600,000** | **0** | **6,600,000** | **55** | **0** | **55** |
| **iv) Mradi wa Ujenzi wa Ofisi wa Masheha** | **1,650,000** | **0** | **1,650,000** | **515,704** | **0** | **515,704** | **31** | **0** | **31** |
| **v) Mradi wa Kijani - PEMBA** | | **6,116,174** | **6,116,174** | | **1,765,553** | **1,765,553** | **0** | **29** | **29** |
| **JUMLA YA FUNGU** | **43,450,000** | **6,116,174** | **49,566,174** | **24,498,677** | **1,765,553** | **26,264,230** | **56.38360715** | **0** | **53** |
| **WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII ZANZIBAR** | | | | | | | | | |
| **Mradi wa Kuimarisha Mfumo wa Usajili** | **1,045,000** | **0** | **1,045,000** | **386,030** | **0** | **386,030** | **37** | **0** | **37** |
| **JUMLA YA FUNGU** | **1,045,000** | **0** | **1,045,000** | **386,030** | **0** | **386030** | **37** | **0** | **36.940669856** |
| **KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO** | | | | | | | | | |
| **i) Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Kambi na Nyumba za KMKM** | **1,457,500** | **0** | **1,457,500** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **ii) Mradi wa Matengenezo ya Boti za Ulinzi na Uokozi** | **1,353,022** | **0** | **1,353,022** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **JUMLA YA FUNGU** | **2,810,522** | **0** | **2,810,522** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **KIKOSI CHA VALANTIA** | | | | | | | | | |
| **Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Mahanga ya KVZ** | **4,794,570** | **0** | **4,794,570** | **8,146,443** | **0** | **8,146,443** | **170** | **0** | **170** |
| **JUMLA YA FUNGU** | **4,794,570** | **0** | **4,794,570** | **8,146,443** | **0** | **8,146,443** | **170** | **0** | **170** |
| **CHUO CHA MAFUNZO** | | | | | | | | | |
| **Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Makaazi na Mahanga - Chuo Cha Mafunzo** | **1,402,500** | **0** | **1,402,500** | **300,000** | **0** | **300,000** | **21** | **0** | **21** |
| **JUMLA YA FUNGU** | **1,402,500** | **0** | **1,402,500** | **300,000** | **0** | **300,000** | **21** | **0** | **21** |
| **JESHI LA KUJENGA UCHUMI** | | | | | | | | | |
| **i) Mradi wa Ujenzi wa Nyumba na Mahanga ya Kambi za JKU** | **902,000** | **0** | **902,000** | **1,640,000** | **0** | **1,640,000** | **182** | **0** | **182** |
| **ii) Mradi wa Ujenzi wa Dakhalia** | **825,000** | **0** | **825,000** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **JUMLA YA FUNGU** | **1,727,000** | **0** | **1,727,000** | **1,640,000** | **0** | **1,640,000** | **95** | **0** | **95** |
| **KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI** | | | | | | | | | |
| **i) Mradi wa Ujenzi wa Mahanga na Nyumba za Maaskari - KZU** | **4,250,762** | **0** | **4,250,762** | **754,126** | **0** | **754,126** | **18** | **0** | **18** |
| **ii) Mradi wa Ununuzi wa Magari ya Zimamoto** | **1,375,000** | **14,927,000** | **16,302,000** | **759,981** | **0** | **759,981** | **55** | **0** | **5** |
| **JUMLA YA FUNGU** | **5,625,762** | **14,927,000** | **20,552,762** | **1,514,107** | **0** | **1,514,107** | **27** | **0** | **7** |
| **OFISI YA MAKAMO WA KWANZA WA RAIS** | | | | | | | | | |
| **i) Mradi wa kukabiliana** | **275,000** | **0** | **275,000** | **298,508** | **0** | **298,508** | **109** | **0** | **109** |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| na Mabadiliko ya Tabianchi na Usimamizi wa Mazingira | | | | | | | | | |
| ii) Mradi wa Kuirithisha Zanzibar Kijani | 825,000 | | 825,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| iii) Mradi wa Kuimarisha Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi wa Jamii ya Pwani | 0 | 300,896 | 300,896 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| iv) Ujenzi wa Nyumba za Makamu wa Kwanza wa Rais | 825,000 | 0 | 825,000 | 55,358 | 0 | 55,358 | 7 | 0 | 7 |
| JUMLA YA FUNGU | 1,925,000 | 300,896 | 2,225,896 | 353,866 | 0 | 353,866 | 18.38264935 | 0 | 16 |
| MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA MADAWA YA KULEVYA | | | | | | | | | |
| Mradi wa Kuimarisha Mamlaka ya Kupambana na Madawa ya Kulevya | 1,402,500 | 0 | 1,402,500 | 250,079 | 0 | 250,079 | 18 | 0 | 18 |
| JUMLA YA FUNGU | 1,402,500 | 0 | 1,402,500 | 250,079 | 0 | 250,079 | 18 | 0 | 18 |
| OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS, SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI | | | | | | | | | |
| Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini (TASAF III) | 55,000 | 16,621,059 | 16,676,059 | 50,000 | 3,665,011 | 3,715,011 | 91 | 22 | 22 |
| Miradi | | | | | | | | | |
| i) Ujenzi wa Nyumba za Makamu wa Pili wa Rais | 2,475,000 | 0 | 2,475,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| ii) Ukarabati wa Ofisi ya | 302,500 | 0 | 302,500 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |

322

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Uratibu Dar es Salaam | | | | | | | | | |
| **JUMLA YA FUNGU** | **2,832,500** | **16,621,059** | **19,453,559** | **50,000** | **3,665,011** | **3,715,011** | **2** | **22** | **19** |
| **WIZARA YA AFYA** | | | | | | | | | |
| **Programu ya Ukarabati na Ujenzi wa Vituo vya Afya ya Msingi** | **19,250,000** | **0** | **19,250,000** | **17,798,051** | **0** | **17,798,051** | **92** | **0** | **92** |
| **Programu ya Ujenzi wa Nyumba za Wafanyakazi Katika Hospitali za Wilaya na Mkoa** | **3,561,250** | | **3,561,250** | **8,330,337** | **0** | **8,330,337** | **234** | **0** | **234** |
| **Programu ya Kumaliza Malaria Zanzibar** | **354,750** | **4,007,516** | **4,362,266** | **0** | **1,914,533** | **1,914,533** | **0** | **48** | **44** |
| **Programu Shirikishi ya Afya ya Uzazi wa Mama na Mtoto** | **550,000** | **2,857,157** | **3,407,157** | **296,815** | **180,758** | **477,573** | **54** | **6** | **14** |
| **Programu ya Kudhibiti Maradhi ya Ukimwi, Homa ya Ini, Kifua Kikuu na Ukoma** | **209,000** | **2,236,111** | **2,445,111** | **951,733** | **2,869,348** | **3,821,081** | **455** | **128** | **156** |
| **Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Afya** | **15,125,000** | **0** | **15,125,000** | **11,986,472** | **0** | **11,986,472** | **79** | **0** | **79** |
| **Programu ya Kuimarisha huduma za Mama na Mtoto** | **0** | **4,941,444** | **4,941,444** | **0** | **606,658** | **606,658** | | **12** | **12** |
| **Programu ya Jamii ni Afya** | **825,000** | **0** | **825,000** | **560,173** | **0** | **560,173** | **68** | **0** | **68** |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Programu ya Kusaidia Watu Wasiojiweza Kujiunga na Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar | 275,000 | 0 | 275,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Miradi | | | | | | | | | |
| i) Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa Binguni | 0 | 16,816,828 | 16,816,828 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Matumizi kwa Miradi ya UVIKO-19 | 0 | 0 | 0 | 842,367 | 0 | 842,367 | 0 | 0 | 0 |
| JUMLA YA FUNGU | 40,150,000 | 30,859,056 | 71,009,056 | 40,765,948 | 5,571,297 | 46,337,245 | 102 | 18 | 65 |
| HOSPITALI YA MNAZI MMOJA | | | | | | | | | |
| i) Mradi wa Kuipandisha Hadhi Hospital ya Mnazi Mmoja | 1,100,000 | | 1,100,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| ii) Mradi wa Ukarabati na Utanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja | 0 | 11,550,000 | 11,550,000 | 0 | 90,249 | 90,249 | 0 | 1 | 1 |
| JUMLA YA FUNGU | 1,100,000 | 11,550,000 | 12,650,000 | 0 | 90,249 | 90,249 | 0 | 1 | 1 |
| WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI | | | | | | | | | |
| i) Ujenzi wa Nyumba za Maendeleo | 22,000,000 | 0 | 22,000,000 | 22,659,099 | 0 | 22,659,099 | 103 | | 103 |
| ii) Mfumo wa Usajili na Usimamizi wa Taarifa za Ardhi Zanzibar (LARIS) | 2,750,000 | 0 | 2,750,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| JUMLA YA FUNGU | 24,750,000 | 0 | 24,750,000 | 22,659,099 | 0 | 22,659,099 | 92 | 0 | 92 |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA** | | | | | | | | | |
| **Programu ya Kuendeleza Viwanda** | | | | | | | | | |
| **i) Mradi wa Kuanzisha na kuendeleza Maeneo Maalum ya Viwanda (Indurstrial Parks)** | **22,176,000** | **0** | **22,176,000** | **3,779,402** | **0** | **3,779,402** | **17** | **0** | **17** |
| **Miradi** | | | | | | | | | |
| **i) Mradi wa Kuendeleza Vituo vya Biashara na Maonyesho Zanzibar** | **5,500,000** | **0** | **5,500,000** | **348,568** | **0** | **348,568** | **6** | **0** | **6** |
| **JUMLA YA FUNGU** | **27,676,000** | **0** | **27,676,000** | **4,127,970** | **0** | **4,127,970** | **15** | **0** | **15** |
| **WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI** | | | | | | | | | |
| **Programu ya Uimarishaji wa Miundombinu ya Elimu** | **128,914,499** | **100,724,203** | **229,638,702** | **94,401,903** | **53,400,090** | **147,801,993** | **73** | **53** | **64** |
| **Programu ya Uimarishaji wa Ubora wa Elimu** | **27,172,750** | **14,374,250** | **41,547,000** | **83,731** | **11,702,639** | **11,786,370** | **0** | **81** | **28** |
| **Miradi** | | | | | | | | | |
| **i) Uimarishaji wa Elimu ya Juu** | **13,750,000** | **0** | **13,750,000** | **11,070,000** | **5,962,966** | **17,032,966** | **81** | **0** | **124** |
| **ii) Ukamilishaji wa Miradi ya UVIKO-19** | **0** | **0** | **0** | **645,858** | **0** | **645,858** | **0** | **0** | **0** |
| **JUMLA YA FUNGU** | **169,837,249** | **115,098,453** | **284,935,702** | **106,201,492** | **71,065,695** | **177,267,187** | **63** | **62** | **62** |
| **WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** | | | | | | | | | |
| **Programu ya Kuendeleza Viwanja** | **33,000,000** | **348,690** | **33,348,690** | **55,447,169** | **2,128,304** | **57,575,473** | **168** | **610** | **173** |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| vya Michezo | | | | | | | | | |
| Miradi | | | | | | | | | |
| i) Ujenzi wa Chuo cha Sanaa na Utamaduni | 2,750,000 | 0 | 2,750,000 | 1,288,073 | 0 | 1,288,073 | 47 | 0 | 47 |
| ii) Ujenzi wa Vituo vya Mafunzo kwa Vijana Awamu ya Pili | 2,750,000 | 49,500 | 2,799,500 | 0 | 198,578 | 198,578 | 0 | 401 | 7 |
| JUMLA YA FUNGU | 38,500,000 | 398,190 | 38,898,190 | 56,735,242 | 2,326,882 | 59,062,124 | 147 | 584 | 152 |
| WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO | | | | | | | | | |
| Programu ya Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji | 0 | 13,200,000 | 13,200,000 | 364,478 | 13,265,417 | 13,629,895 | 0 | 100 | 103 |
| Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo na Mifugo | | | | | | | | | |
| i) Kuendeleza Miundombinu ya Mifugo | 1,375,000 | 0 | 1,375,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| ii) Mradi wa Kuendeleza Mnyororo wa Thamani wa Bidhaa za Nyuki | 0 | 275,000 | 275,000 | 0 | 56,118 | 56,118 | 0 | 20 | 20 |
| iii) Mradi wa Kilimo Tija | 0 | 1,890,901 | 1,890,901 | 0 | 949,683 | 949,683 | 0 | 50 | 50 |
| Programu ya Kudhibiti Maradhi na Upotevu wa Mazao | | | | | | | | | |
| i) Kupambana na Sumukuvu Tanzania | 0 | 111,704 | 111,704 | 0 | 119,524 | 119,524 | 0 | 107 | 107 |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **(TANIPAC)** | | | | | | | | | |
| **ii) Kuimarisha Huduma za Afya ya Mimea na Kuhakikisha Usalama wa Chakula (STREPHIT)** | **0** | **2,244,000** | **2,244,000** | **0** | **941,626** | **941,626** | **0** | **42** | **42** |
| **iii) Kuwaunganisha Wakulima wa Mboga na Matunda** | **0** | **1,559,002** | **1,559,002** | **0** | **1,572,187** | **1,572,187** | **0** | **101** | **101** |
| **Miradi** | | | | | | | | | |
| **i) Ukarabati wa Maghala na Uhifadhi wa Chakula** | **15,125,000** | **0** | **15,125,000** | **330,346** | **0** | **330,346** | **2** | **0** | **2** |
| **ii) Mradi wa Mageuzi ya Uzalishaji wa Maziwa kwa Wafugaji Wadogo Unaozingatia Mabadiliko ya Tabianchi (C-SDTP)** | **0** | **4,125,000** | **4,125,000** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **iii) Uhimilivu wa Mifumo ya Chakula Tanzania (TFSRP)** | **0** | **10,312,500** | **10,312,500** | **0** | **10,189,125** | **10,189,125** | | **99** | **99** |
| **iv) Kuimarisha Mifumo ya Chakula kwa Kuongeza Tija na Uzalishaji Kupitia Huduma za Kisasa za Kilimo katika** | **0** | **825,000** | **825,000** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Umwagiliaji** | | | | | | | | | |
| **vi) Kuendeleza Mifumo ya Chakula, Matumizi na Urejeshaji wa Ardhi (FOLUR)** | **0** | **375,540** | **375,540** | **0** | **52,000** | **52,000** | **0** | **14** | **14** |
| **JUMLA YA FUNGU** | **16,500,000** | **34,918,648** | **51,418,648** | **694,824** | **27,145,679** | **27,840,502** | **4** | **78** | **54** |
| **WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,WAZEE NA WATOTO** | | | | | | | | | |
| **i) Mradi wa Hifadhi ya Wazee** | **2,475,000** | **0** | **2,475,000** | **1,560,047** | **0** | **1,560,047** | **63** | | **63** |
| **ii) Mradi wa Kutokomeza Udhalilishaji na Ukatili wa Kijinsia kwa Wanawake na Wasichana** | **0** | **294,800** | **294,800** | **0** | **103,534** | **103,534** | **0** | **35** | **35** |
| **iii) Mradi wa Kusimamia Sheria ya Jinsia na Sera** | **0** | **114,400** | **114,400** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **iv) Mradi Kukuza Usawa wa Kijinsia Tanzania (Pamoja)** | **0** | **4,461,394** | **4,461,394** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **JUMLA YA FUNGU** | **2,475,000** | **4870594.3** | **7,345,594** | **1,560,047** | **103,534** | **1,663,581** | **63** | **2** | **23** |
| **WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI** | | | | | | | | | |
| **Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo na Uvuvi** | **0** | **7,340,847** | **7,340,847** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Programu ya Kutengeneza Miundombinu ya Mafuta na Gesi Asilia** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **i) Ujenzi wa Kituo cha Kuhifadhi Taarifa za Mafuta na Gesi Asilia (NDR)** | **2,200,000** | **0** | **2,200,000** | **1,769,486** | **0** | **1,769,486** | **80** | **0** | **80** |
| **ii) Ujenzi wa Kituo cha Kuhifadhia Bidhaa za Petroli iliyosafishwa na Usambazaji** | **2,200,000** | **0** | **2,200,000** | **0** | **0** | **0** | **-** | **0** | **0** |
| **Miradi** | | | | | | | | | |
| **i) Uanzishwaji wa Kuimarisha Miundombinu ya Maabara Uthamini wa Ubora wa Mazao ya Baharini** | **2,200,000** | **0** | **2,200,000** | **728,472** | **0** | **728,472** | **33** | **0** | **33** |
| **ii) Ujenzi wa Madiko na Masoko ya Kisasa ya Samaki** | **14,850,000** | **0** | **14,850,000** | **12,710,587** | **0** | **12,710,587** | **86** | **0** | **86** |
| **iii) Mradi Jumuishi wa Uwezeshaji wa Wanawake katika Ufugaji wa Mazao ya Baharini** | **0** | **1,320,000** | **1,320,000** | **0** | **108,000** | **108,000** | **0** | **8** | **8** |
| **iv) Utafiti wa Usalama wa Chakula na Maisha** | **0** | **22,590** | **22,590** | **0** | **62,802** | **62,802** | **0** | **278** | **278** |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Endelevu kwa Jamii** | | | | | | | | | |
| **v) Mradi wa Tathmini ya Ubora wa Maji ya Bahari** | **0** | **131,835** | **131,835** | **0** | **469,060** | **469,060** | **0** | **356** | **356** |
| **JUMLA YA FUNGU** | **21,450,000** | **8,815,271** | **30,265,271** | **15,208,545** | **639,862** | **15,848,407** | **71** | **7** | **52** |
| **WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI** | | | | | | | | | |
| **Program ya Kuimarisha Huduma za Usambazaji Maji Safi na Salama Zanzibar** | | | | | | | | | |
| **i) Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar (INDIA)** | **5,585,230** | **12,674,750** | **18,259,980** | **3,334,066** | **18,126,218** | **21,460,284** | **60** | **143** | **118** |
| **ii) Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji Huduma za Usambazaji Maji Safi na Usafi wa Mazingira Zanzibar** | **1,567,500** | **7,407,114** | **8,974,614** | **4,337,228** | **0** | **4,337,228** | **277** | **0** | **48** |
| **iii) Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Maji Mkoa wa Mjini Magharibi (ZUWDFIP)** | **0** | **1,856,619** | **1,856,619** | **0** | **1,376,094** | **1,376,094** | **0** | **74** | **74** |
| **iv) Kuendeleza Miundombinu ya Uimarishaji wa Huduma za Usambazaji** | **16,775,000** | **0** | **16,775,000** | **2,465,244** | **0** | **2,465,244** | **0** | **0** | **0** |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Maji Safi na Salama Zanzibar | | | | | | | | | |
| v) Mradi wa Kuimarisha Usalama wa Maji na Uhimili wa Tabianchi katika Maeneo ya Mijini | 0 | 39,157,027 | 39,157,027 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| vi) Mradi wa Ununuzi wa Chlorine, Usimamizi na Ungalizi Bora wa Maji | 0 | 22,000 | 22,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Umeme Zanzibar | | | | | | | | | |
| i) Kuimarisha Miundombinu ya Umeme | 18,150,000 | 0 | 18,150,000 | 15,958,401 | 0 | 15,958,401 | 88 | 0 | 88 |
| ii) Kuifanyia Mabadiliko Sekta ya Nishati (ZESTA) | 2,200,000 | 95,840,728 | 98,040,728 | 0 | 79,461,510 | 79,461,510 | 0 | 83 | 81 |
| JUMLA YA FUNGU | 44,277,730 | 156,958,237 | 201,235,967 | 26,094,939 | 98,963,822 | 125,058,761 | 59 | 63 | 62 |
| WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI | | | | | | | | | |
| Programu ya Ujenzi wa Barabara Kuu | 63,547,072 | 107,924,312 | 171,471,384 | 3,013,584 | 8,887,175 | 11,900,759 | 5 | 0 | 7 |
| Programu ya Ujenzi wa Barabara za Ndani | 25,080,000 | 0 | 25,080,000 | 102,568,538 | 0 | 102,568,538 | 409 | 0 | 409 |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Programu ya Matengenezo ya Barabara za Mjini** | **61,650,600** | **0** | **61,650,600** | **42,851,244** | **0** | **42,851,244** | **70** | **0** | **70** |
| **Programu ya Kuimarisha Viwanja vya Ndege** | | | | | | | | | |
| **i) Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba** | **5,225,000** | **50,540,132** | **55,765,132** | **2,526,525** | **10,685,143** | **13,211,668** | **48** | **21** | **24** |
| **ii) Ujenzi wa Jengo la Abiria Terminal II AAKIA** | **14,300,000** | | **14,300,000** | **8,988,693** | **0** | **8,988,693** | **0** | **0** | **0** |
| **iii) Ujenzi wa Jengo la Abiria Terminal IV AAKIA** | **0** | **30,461,640** | **30,461,640** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **Programu ya Kuimarisha Bandari** | | | | | | | | | |
| **ii) Ujenzi wa Bandari Jumuishi - Mangapwani** | **86,646,978** | **55,000,000** | **141,646,978** | **155,682,271** | **0** | **155,682,271** | **180** | **0** | **110** |
| **iii) Ujenzi wa Bandari ya Maruhubi** | **0** | **70,125,000** | **70,125,000** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **Miradi** | | | | | | | | | |
| **i) Uboreshaji wa Mifumo ya Mawasiliano (Connectivity)** | **3,300,000** | **0** | **3,300,000** | **3,484,761** | **0** | **3,484,761** | **106** | **0** | **106** |
| **ii) Kuimarisha Mfumo wa Usafiri wa Umma Zanzibar** | **0** | **1,067,942** | **1,067,942** | **0** | **1,252,248** | **1,252,248** | **0** | **0** | **117** |
| **iii) Ununuzi wa Boti mbili za Serikali** | **14,300,000** | **0** | **14,300,000** | **2,856,178** | **0** | **2,856,178** | **20** | **0** | **20** |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **JUMLA YA FUNGU** | **274,049,650** | **315,119,026** | **589,168,676** | **321,971,794** | **20,824,566** | **342,796,360** | **117** | **7** | **58** |
| **WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE** | | | | | | | | | |
| **Programu ya Kuimarisha Maeneo ya Kihistoria katika Maeneo ya Fukwe** | **8,250,000** | **0** | **8,250,000** | **889,356** | **0** | **889,356** | **11** | **0** | **11** |
| **Miradi** | | | | | | | | | |
| **i) Ukarabati wa Majengo ya Mji Mkongwe** | **4,950,000** | **0** | **4,950,000** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **ii) Ukarabati wa Jengo la Beit Al Ajaib** | **0** | **8,264,202** | **8,264,202** | **0** | **3,074,991** | **3,074,991** | **0** | **37** | **37** |
| **JUMLA YA FUNGU** | **13,200,000** | **8,264,202** | **21,464,202** | **889,356** | **3,074,991** | **3,964,347** | **7** | **0** | **18** |
| **** Matumizi ya Kawaidia (Recurrent Activities)** | **0** | **0** | **0** | **0** | **10,915,222** | **10,915,222** | **0** | **0** | **0** |
| **JUMLA KUBWA** | **1,024,375,000** | **770,590,341** | **1,794,965,341** | **657,169,460** | **277,373,819** | **934,543,279** | **64** | **36** | **52** |